

# FAMILIA YA KIKRISTO

Shepherds Global Classroom ipo kwa ajili ya kuujenga mwili wa Kristo kwa kutoa mtaala kwa ajili ya kuwaendeleza viongozi wa Kikristo duniani kote. Tunalenga kuongeza programu za mafunzo ya asili kwa kuweka chombo cha mtaala wa kozi 20 mikononi mwa viongozi wa kiroho wanaotoa mafunzo katika kila nchi duniani.

Kitabu hiki kinapatikana bure kwa njia ya kupakua kutoka katika <https://www.shepherdsglobal.org/courses>

Mwandishi Mkuu: Dr. Stephen K. Gibson

Hakimiliki © 2023 Shepherds Global Classroom

Toleo la kwanza.

Haki zote zimehifadhiwa.

Nyenzo za wahusika wengine zilizotumika ni hakimiliki ya wamiliki husika ambazo zimeshirikishwa na kutumika humu chini ya leseni mbalimbali.

Tafsiri ya Maandiko “yaliyonukuliwa” kutoka chapisho la Kiingereza kwa ajili ya chapisho hili la Kiswahili yanatoka katika Biblia Takatifu ya Kiswahili, “Swahili Union Version Bible” (SUVB®).” Yametumika kwa kibali. Haki zote zimehifadhiwa.

#### **Taarifa kuhusu vibali:**

Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa na kutawanywa bure kikiwa kimechapishwa na katika mifumo ya kidigitali chini ya miongozo ifuatayo: (1) Maudhui yaliyoko kwenye kitabu hiki hayawezi kubadilishwa kwa namna yeyote ile; (2) Nakala zinazopatikana haziwezi zikauzwa kwa ajili ya kupata faida; (3) Taasisi za elimu zina uhuru wa kutumia na kukinakili kitabu hiki, hata kama wanalipisha ada za masomo ya ziada; na (4) Kitabu hiki hakiwezi kufanyiwa tafsiri pasipokuwepo na kibali na usimamizi wa Shepherds Global Classroom.

Tafsiri ya chapisho la Kiingereza kwenda katika Kiswahili imefanywa na:

Askofu Wilbert Alfayo Ngowi,  
Arusha, Tanzania, East Africa.

E-mail: [revwangowi@gmail.com](mailto:revwangowi@gmail.com)

Uhariri umefanywa na John Tuu.

# Yaliyomo

Mtazamo wa Kozi .....	5
(1) Kuumbwa kwa ajili ya Mahusiano .....	7
(2) Familia ya Kibiblia .....	17
(3) Dhana ya Biblia kuhusu Ndoa .....	31
(4) Masuala ya Kujamiiiana .....	43
(5) Useja .....	65
(6) Maandalizi kwa ajili ya Ndoa .....	79
(7) Kustawisha Ndoa iliyo Imara .....	93
(8) Lugha Tano za Upendo – Sehemu ya 1 .....	105
(9) Lugha Tano za Upendo – Sehemu ya 2 .....	119
(10) Suala la Kutokuwa na Mtoto .....	137
(11) Maendeleo na Utunzaji wa Mtoto .....	149
(12) Kuwalea Watoto Kwa Makusudi .....	159
(13) Mambo Yanayohusu Kulea Mtoto .....	173
(14) Malezi wakati wa Ujana .....	187
(15) Kijana Aliyekomaa .....	199
Heshima kwa Wanawake .....	211
Kudhibiti Uzazi .....	215
Vyanzo Vilivyopendekezwa .....	219
Kumbukumbu ya kazi zilizofanywa .....	221



# Mtazamo wa Kozi

## Ufafanuzi kuhusiana na Kozi

Kozi hii inafundisha kanuni za Mungu kwa ajili ya hatua mbalimbali za kimaisha na mahusiano ya kifamilia, hasa ndoa na ukuzaji wa watoto. Kupitia mafundisho haya, wanafunzi watakuwa wamewezeshwa katika kumheshimu Mungu katika hatua yao ya sasa ya maisha na katika mahusiano yao. Watakuwa tayari kufundisha wengine kuhusu kanuni za kibiblia na jinsi ya kuwa na matumizi ya kanuni hizo. Wanafunzi watakuwa wamehamasishwa kujihusisha na kanisa lao katika kuleta mguso wa utauwa kwenye familia zilizoko kwenye ushirika wao na jamii zao.

Pamoja na mambo mengine, wanafunzi watakuwa wanajifunza kuhusu kufanya uanafunzi kwa watoto na vijana katika familia. Somo la 12, na Kazi ya kufanya ya 3 inatoa maelekezo kwa wazazi ambao wanachukua kozi hii kuwa na mpangilio wa kila siku wa kuwa na nyakati za kufanya ibada kwa ajili ya familia zao. Shepherds Global Classroom wametoa kitabu cha kufanya uanafunzi kwa familia, kiitwacho *Zana za Mafundisho kwa Familia* ambacho wazazi watapenda kukitumia wakati wa ibada zao za kuabudu. Kitabu hiki kiko tayari kwa ajili ya kupakuliwa kutoka [shepherdsglobal.org](http://shepherdsglobal.org).

## Maelekezo kwa Viongozi wa Madarasa

**Maswali ya kujadiliana na shughuli za ndani ya darasa** zinaonyeshwa kwa alama ya ►. Kwa ajili ya maswali ya kujadiliana, kiongozi wa darasa atapaswa kuuliza swali na kuruhusu wanafunzi kujibu. Siyo lazima kwamba swali lijibiwe kwa usahihi sana wakati wa majadiliano. Mafundisho yaliyoko kwenye somo yatajibu swali hilo. Kama mwanafunzi mmoja ndiye kwa kawaida huwa anaanza kujibu kwanza, na wanafunzi wengine huwa hawajibu, kiongozi anaweza akaelekeza swali kwa mmoja wao: "Igor, ni kwa jinsi gani utaweza kujibu swali hili?"

Kila somo linamalizika kwa kuwepo na maswali mbadala ya hiari kwa ajili ya majadiliano ya kikundi. Kiongozi wa darasa anaweza akachagua ni swali gani linaloweza kujadiliwa na kikundi.

**Maandiko** mengi yametumiwa katika kozi hii. Vifungu ambavyo vinapaswa visomwe kwa nguvu katika darasa vinaonyeshwa kwa njia ya alama za mchoro za mshale. Kila mtu katika kikundi atapaswa alitizame andiko, wakati mwanafunzi mwingine akiwa analisoma kwa sauti. Wakati mwingine, marejeo ya Maandiko hutolewa kwenye mabano katika kifungu hicho. Kwa mfano: (Waefeso 6:1). Marejeo hayo ni kwa ajili ya kuunga mkono taarifa zilizoko kwenye maandishio. Sio lazima kusoma vifungu vilivyoko kwenye mabano kila wakati.

Majadiliano mafupi kuhusiana na mada mbili maalumu yanajumuishwa mwishoni mwa kozi hii. Mada hizi hazina uhusiano kabisa na masomo mengine yeyote na siyo masomo kamili

yaliyokamilika yenyewe. Hata hivyo, ni mada muhimu kuzielewa kutokana na mtazamo wa Kikristo. Darasa linapaswa kujifunza na kujadili Kiambatanisho A kinachofuata Somo la 3 na linapaswa pia kujifunza Kiambatanisho B kufuatia Somo la 10. Mambo ya kukumbuka yametolewa mwishoni mwa masomo hayo mawili.

Kila somo linamalizikia na **kazi za kufanya**. Kazi za kufanya zinapaswa zimalizike na kuwakilishwa kabla ya muda wa kuanza somo linalofuata. Kama mwanafunzi hatakamilisha kazi ya kufanya, anaweza akaifanya kwa wakati mwingine. Hata hivyo, kiongozi atapaswa kuwahamasisha wanafunzi kutunza na kuendana na wakati ili waweze kujifunza zaidi kutoka darasani. Pamoja na kukamilisha kazi za kufanya kwa kila somo, wanafunzi watapaswa wasome somo linalofuata kwa ajili ya maandalizi ya darasa litakalofuata.

Kama mwanafunzi atahitaji kupata **cheti cha kufuzu mafunzo kutoka Shepherds Global Classroom**, atapaswa ahudhurie vipindi vyote vya darasa na amalize kufanya kazi zote zilizotolewa. Fomu imetolewa mwisho wa kozi hii kwa ajili ya kuweka kumbukumbu ya kazi za kufanya zilizomalizika.

# Somo la 1

## Kuumbwa kwa ajili ya Mahusiano

### Malengo ya Somo

Hadi kufikia mwishoni mwa somo hili, mwanafunzi atapaswa:

- (1) Atambue na athamini uhusiano ambao Mungu anataka awe nao Pamoja nasi.
- (2) Aelewe na athamini sura ya Mungu kwa kila mtu.
- (3) Atambue kwamba sisi tunawajibika kwa Mungu kwa ajili ya chaguzi mbalimbali tunazozifanya katika mahusiano yetu.
- (4) Afahamu kwamba Biblia ndiyo mwongozo wetu kwa ajili ya mahusiano ya kimungu, na kwamba tunapaswa tumtafakari Mungu katika mahusiano yetu.

### Mahusiano na Mungu

Kwenye Maandiko, tunajifunza kwamba Mungu ni Mungu aliye na nafsi, mwenye mahusiano na anayewasiliana na wengine (Waebrania 1:1-2). Maandiko yanatuonyesha kwamba Mungu Baba, Mungu Mwana, na Mungu Roho Mtakatifu wamekuwa kwenye uhusiano kati yao kwa umilele wote.<sup>1</sup>

Mungu aliziumba mbingu, nchi, bahari na vyote vilivyomo. (Kutoka 20:11). Zaburi 8:3-8 inatuonyesha kwamba ubinadamu ulikuwa ndio uumbaji uliokuwa bora na muhimu Zaidi. Mungu aliumba watu kama viumbe vya uhusiano, kama yeye alivyo ni kiumbe wa uhusiano.

Katika Maandiko yote, Mungu huwaalika watu kwenye mahusiano ya maisha ya uzima pamoja na yeye mwenyewe.<sup>2</sup>

Ni ajabu gani kutambua kwamba Mungu, aliye Muumbaji wa ulimwengu, anatamani awe na uhusiano na wewe pamoja na mimi!

► Mwanafunzi anapaswa asome Mwanzo 3:8-9 kwa ajili ya kikundi.

Hebu jaribu kutulia kwa muda, funga macho yako, kisha uwazie tukio ambalo umesoma hapa hivi punde. Tumia mawazo yako kufanya Aya hizi ziwe halisia hai. Ukiwa umesimama kwenye bustani nzuri zaidi sana katika sehemu yenye baridi ya siku, jisikie upepo wa

---

<sup>1</sup> Kwa mfano, maandiko haya yanaonyesha mahusiano kati ya Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu: Yohana 17:22-24; Yohana 14:16, 26; na Yohana 15:26. Ingawaje aya hizo hazizungumzii ni kwa jinsi gani Roho Mtakatifu ni wa milele, tunajua kutokana na aya nyingine, kama vile Waebrania 9:14, kwamba yeye pia ni wa milele.

<sup>2</sup> Kwa mfano, ona Isaya 55:3, Yohana 1:12-13, Yohana 3:36, Yohana 17:3, 2 Wakorintho 6:16-18, 1 Yohana 1:3, Ufunuo 3:20.

kupendeza ukikupulizia usoni mwako. Sikiliza sauti ya nyayo za Mungu na usikie mwitikio wa kimya wa viumbe wake wawili wapendwa; kisha swali la Mungu, “Uko wapi?”

Je, unaweza kufikiria wakati huo ulikuwaje, wakati Mungu akiita kwa ajili ya kuwa na ushirika na mwanamume na mwanamke? Tulia tena katika kuutafakari moyo wa Mungu. Mungu anatamani na anatafuta kuwa na ushirika kati yake na Adamu na Hawa, pamoja na wewe, na mimi!

Ingawaje tumejitenga sisi wenyewe kutoka kwa Mungu kwa kutokumtii kwetu (Isaya 59:2), Mungu bado anatamani kuwepo na uhusiano na kila mtu anayeishi. Luka 19:10 anatuonyesha kwamba Mungu anamtafuta kila mwenye dhambi. Mungu angali bado anauliza, “Uko wapi?” Kwa kuwa Yesu alikufa kwa ajili yetu, tunaweza tukarejea tena kwenye uhusiano sahihi na yeye (Waefeso 2:13, 19). Wewe na mimi tumeumbwa kwa ajili ya uhusiano na Mungu.

### **Muundo wa Muumbaji Wetu**

Wale watu ambao hawaamini katika uumbaji wenye upendo na kusudi la Mungu, wanajitahidi kuunda utambulisho wao na kusudi lao wenyewe. Ni vigumu kabisa kuelewa kwa usahihi ubinadamu kama siyo kutokana na uhusiano na Mungu. Mtu anayeishi kwa ushauri wa kutafuta hekima ya kidunia iliyoelekezwa katika kufuatilia furaha, - hawezi kuyaelewa Maisha kwa usahihi.

Ili kuelewa kwa ukweli utambulisho wetu (kwamba sisi ni nani), kusudi letu (kwa nini tunaishi), na jinsi tulivyotumbwa, ni lazima tulijue kusudi la Muumba wetu, ambalo linapatikana kutoka katika Biblia Takatifu, Mungu tayari alishatengeneza utambulisho wetu; sio jambo ambalo tunazua. Ametuumba kwa ajili ya kusudi na ametutengeneza kimakusudi. Ni pale tu tunapokuwa tumelewa mpango wake juu ya maisha yetu pamoja na mahusiano yetu ndipo tutakapoweza kutegemewa tuwe kama tunavyotakiwa tuwe na tutakapoweza kukamilisha kusudi lake kwa ajili ya kuwepo kwetu.

Kuumbwa katika sura ya Mungu kunamaanisha kwamba watu waliumbwa kwa ajili ya kuwa na uhusiano wa kipekee. Kama vile Mungu alivyo kwenye uhusiano, aliwafanya watu nao wawe viumbe vyenye uhai. Mungu aliumba nafsi, roho na mwili wa kila mtu kwa ajili ya uhusiano na Mungu na pamoja na watu wengine.

### **Mwongozo Wetu kwa ajili ya Mahusiano ya Kibinadamu**

Ukweli kwamba Mungu aliumba watu kwa ajili ya uhusiano unadhihirisha kwamba anazo kanuni na miongozo kwa ajili ya mahusiano yetu. Mtengenezaji wa bidhaa huandika mwongozo kuhusiana na ile bidhaa ambao unaelezea jinsi ile bidhaa ilivyotengenezwa na jinsi ya kuitumia. Vivyo hivyo, Mungu ametupa Neno lake Biblia, ambayo inaelezea muundo wetu na jinsi maisha na mahusiano yetu vinavyoweza kufanya kazi kwa njia nzuri kabisa.

Biblia inaelezea kwa uwazi majukumu ambayo Mungu ameweka kwa ajili ya mahusiano ya kibinadamu. Inashughulikia majukumu ya waume na wake; wababa, wamama, na watoto;



wakaka na wadada; mababu na mabibi; marafiki; maadui; majirani; serikali na raia; waajiri na waajiriwa. Kanuni za Neno la Mungu zinatufundisha muundo wake kwa ajili yetu, haijalishi hali au mazingira yetu. Biblia inatufundisha mapenzi ya Mungu kwetu katika kila hatua ya maisha.

Jamii na tamaduni za kibinadamu zinaonyesha muundo wa Mungu, ingawaje siyo kwa ukamilifu sana. Tamaduni huelezea tabia ya kawaida ya kibinadamu kwenye mahusiano na hali za aina zote. Kila utamaduni una njia zake za kukuza watoto na kudumisha uhusiano wa ndoa. Tamaduni zinaonyesha tofauti kubwa katika mila, mazingira, maumbile, na matukio muhimu, lakini kila utamaduni unashiriki maadili ya msingi. Kwa mfano, kila utamaduni una aina yake ya ndoa.

Hata hivyo, tabia zote zinapaswa zifanyiwe tathmini na kanuni za kibiblia, na siyo kwa kanuni za kitamaduni. Biblia ni mamlaka yetu; lakini siyo utamaduni (Warumi 12:2).

Maelezo ya kina ya kitamaduni siyo lazima yafungamane na upande wowote, na hatupaswi kutegemea iwe hivyo (Waefeso 2:2). Tamaduni huwa zinakuzwa na watu walioanguka ambao huchochewa na tamaa mbaya na ubinafsi. Jamii inaweza ikawa na ujuzi fulani wa ukweli wa kibiblia, lakini bado hakuna jamii inayofuata mara kwa mara viwango vya Mungu vya mema na mabaya. Hakuna kitu chochote kinachostahili kuhesabiwa haki kwa sababu tu ni cha kitamaduni. Biblia peke yake kwa ukamilifu wake ndiyo inayotonyesha kiwango cha Mungu (Zaburi 19:7-11).

Kama ukiweza kuitembelea nchi ya Libya na ukashuhudia jinsi ambavyo Walibya wanavyoendesha magari bila kujali usalama, unaweza ukafikiri kwamba, "Huo ni utamaduni wao tu; mtindo wao wa uendeshaji unafaa kwa ajili yao." Ni ukweli kwamba Libya ina kiwango kikubwa cha vifo vya ajali mbaya za magari duniani. Kiwango chao ni mara mbili ya nchi ambayo ina kiwango cha pili cha vifo vya magari duniani. Kwa uhakika, utamaduni wao haujaweza kujenga mtindo mzuri wa kuendesha magari.

Mungu anajua ni kwa jinsi gani maisha yanavyopaswa kufanya kazi na ametupa sisi sheria. Hatupaswi tu kufanya majaribio na kuchunguza. Hatupaswi tu kufanya kile ambacho kinachoonekana kwamba kitatupatia kile tunachotaka. Hatupaswi tu kufikiria kupata kile tunachofikiria kwamba kitakuwa cha maisha ya furaha. Ni lazima tufuate mpango wa Mungu wa mahusiano.

Jambo zuri ni kwamba uaminifu kwenye maelekezo ya mambo ya Mungu ni jambo jema kwetu. Mungu ametupa amri kwa sababu anatupenda sisi (Kumbukumbu la Torati 6:24). Kwa kuzishika amri hizo, tunafurahia matokeo mazuri na tunalindwa dhidi ya matukio mengi mabaya. Mbunifu wetu anajua ni nini kilicho kizuri kwa ajili yetu, na tunapofuata mpangilio wake, tunabarikiwa.

### **Kuwajibika kwa Mungu katika Mahusiano**

► Je, ni kwa jinsi gani mwenendo wetu dhidi ya watu wengine unaathiri mahusiano yetu na Mungu?

► Wanafunzi wanapaswa wasome kila moja ya vifungu vifuatavyo kwa ajili ya kikundi. Jadili kwa ufupi kile ambacho Mungu anataka katika mahusiano haya ya kibinadamu, na jinsi utii unavyoathiri uhusiano wetu na Mungu.

<b>Mahusiano yetu na Mungu na Mahusiano yetu na Wanadamu.</b>			
<b>Kifungu cha Maandiko</b>	<b>Mtu/ Jukumu</b>	<b>Anachokihitaji Mungu kwenye Mahusiano ya Mwanadamu</b>	<b>Athari kwenye uhusiano na Mungu</b>
1 Petro 3:7	Mume	Kuwa na ufahamu na heshima kwa mke.	Maombi ya mume hayazuiliki.
Waefeso 5:22, 24, 33; 1 Petro 3:1-6	Mke	Kuwa mtiifu kwa mume.	Hivyo ndivyo mke anapokuwa mtiifu kwa Mungu. Mungu anathamini mtazamo huu na tabia hii ndani yake.
Wakolosai 3:20	Mtoto	Waheshimu wazazi katika mambo yote.	Tabia hii inampendeza Mungu.
Mathayo 6:12-15	Kila mtu	Kusamehe wale wote wanatenda dhambi kinyume chetu	Mungu anaweza kutusamehe.
Warumi 13:1-5	Kila mtu	Kutii mamlaka za kidunia	Ni kwa namna tunavyomtii Mungu.
1 Petro 2:18-20	Mtumishi	Vumilia kwa subira mambo unayotendewa yasiyokuwa ya haki.	Watumishi hupata kibali kutoka kwa Mungu.

Sisi ni viumbe wenye maadili, ikimaanisha kwamba tunaielewa kwamba matendo mengine ni mabaya na mengine ni mema, na tunawajibika kwa Mungu kwa chaguzi zetu tunazofanya. Hii inatupa uwezo na wajibu mkubwa.

Uchaguzi wetu unaathiri mahusiano yetu na Mungu. Utii kwenye maagizo ya Mungu kuhusiana na mahusiano siyo tu jambo lenye kutumika tu la jinsi tunavyoweza kuwa na furaha na kupata kile kilicho bora zaidi katika maisha. Tunawajibika kwa Mungu kwa maamuzi yetu na tabia zetu katika mahusiano (Warumi 14:10, 12).

Mungu ametuita sisi kuwatendea wengine haki, na kufanya kwa upendo na rehema (Mika 6:8). Tatizo ni kwamba, kwa sababu ya dhambi ya Adamu, wazao wake wote waliomfuata wanazaliwa katika hali ya dhambi (Warumi 5:12, 19). Kwa sababu hiyo, hatuwezi kutenda mema mara kwa mara kwa upendo, rehema, na njia za haki (Warumi 7:15-24). Lakini

neema ya Mungu inatubadilisha tunapozaliwa mara ya pili. Roho Mtakatifu hutuwezesha kutimiza matakwa ya Mungu (Warumi 8:3-4).

### **Thamani ya Kila Mtu**

► Wanafunzi wanapaswa wasome Isaya 44:24, Zaburi 139:13-16, Mwanzo 9:6, na Yakobo 3:9 kwa ajili ya kikundi. Je, Maandiko haya yanatueleza nini kuhusu thamani ya kila maisha? Je, Ni kitu gani kinachompa mtu thamani?

Ili kuwa na uhusiano mzuri wenye nguvu pamoja na watu wengine, ni lazima tuwathamini watu kama vile ambavyo Mungu anavyowathamini. Kila mtu ameumbwa kwa sura ya Mungu na ni wa thamani kwa sababu hiyo tu. Kila mtu kwa binafsi yake ni kiumbe pekee cha Mungu. aidha awe mwanamume au mwanamke, mwenye afya njema au mgonjwa, mzima au kilema, kijana au mzee, tajiri au maskini (Mithali 14:31), ambaye tayari ameshazaliwa au ambaye bado yuko kwenye tumbo la mama yake bado kuzaliwa, chochote kilicho kivuli cha ngozi zao; na bila kujali uwezo wao wa kiakili au kimwili au mapungufu (Kutoka 4:11).

Kuna tamaduni ambazo wazee husahaulika, wanawake huchukuliwa kwamba ni duni kuliko wanaume, au watoto huchukuliwa kuwa kero. Kwenye baadhi ya tamaduni, vilema huchukuliwa kama ni waliolaaniwa na hufichwa au kukataliwa kutoka kwa jamii. Duniani kote ubaguzi wa rangi umekuwa ni jambo la kawaida: Kabila moja au kikundi fulani cha ukoo kinajiona na kujichukulia chenyewe kama kilicho bora zaidi kuliko wengine na kuwatendea wengine mambo ya aibu.

Kila moja ya vitendo hivi vinashusha thamani ya watu, ambao ni wa thamani zaidi ya uumbaji wote wa Mungu. Ili kuwa na mahusiano yenye afya, yanayomheshimu Mungu, ni lazima kwanza tufikirie watu wote jinsi walivyo—wachukuaji sura ya Mungu.

### **Kuumbwa kwa ajili ya Mungu, Kuumbwa kwa ajili ya watu wengine.**

Ufunuo 4:11 inatueleza kwamba Mungu aliviumba vitu vyote kwa ajili yake mwenyewe. Hii kwa uhakika inahusisha ubinadamu. Tumeumbwa na Mungu, kwa ajili ya Mungu. Tunachotakiwa kufanya, tunatakiwa tufanye kwa ajili ya utukufu wa Mungu (1 Wakorintho 10:31, 1 Petro 2:12). Tumeumbwa pia kwa ajili ya kuwa faida kwa ajili ya watu wengine.

**Tuliumbwa ili tufanye kazi na watu wengine katika kukamilisha makusudi ya Mungu.** Ndoa ni mfano mmojawapo wa muundo wa Mungu kwa ajili ya kufanya kazi pamoja. Mara tu baada ya kuumbwa kwa binadamu wa kwanza, Mungu alisema, "Si vema huyo mtu awe peke yake, nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye (Mwanzo 2:18). Mwanamke ni sawa na mwanamume katika njia nyingi muhimu, lakini tofauti katika njia nyingine muhimu. Kwa pamoja wanaweza kukamilisha makusudi ya Mungu kwa ajili ya uwepo wao. Mungu aliwapa -kwa pamoja- kazi ambayo wangepaswa kuifanya (Mwanzo 1:26-28).

Kanisa ni mfano mwingine wa mpango wa Mungu kwa watu kufanya kazi kwa pamoja. Mtume Paulo alitumia kielelezo cha sehemu za mwili (1 Wakorintho 12:12-26). Mtu hapaswi

kufikiri kwamba anaweza kutimiza kusudi la Mungu akifanya kazi peke yake au kwamba hahitaji watu wengine. Ndoa na Kanisa ni mifano miwili tu kati ya mifano mingi ya mpango wa Mungu kwa ajili ya watu kufanya kazi kwa pamoja.

**Tuliumbwa kwa ajili ya kutumikia watu wengine** (Wagalatia 5:13-14). Tumeumbwa kwa ajili ya mahusiano yenye upendo na wengine, ambamo tunajitoa ili kuwanufaisha wengine.

► Wanafunzi wanapaswa wasome Mithali 17:17, Wagalatia 6:2, na Wafilipi 2:4 kwa ajili ya kikundi.

Tuliumbwa kwa ajili ya Mungu na kwa ajili ya watu wengine. Kila hitaji ambalo Mungu hutufanya katika Neno lake Linahusiana na aidha uhusiano wetu Naye, uhusiano wetu na wengine, au mahusiano yote mawili. Kwa hakika, Yesu alisema kwamba kila jambo ambalo Mungu anataka tufanye linaweza kufupishwa kwa amri za kumpenda Mungu kwa moyo wetu wote, nafsi yetu yote, na akili yetu yote na kuwapenda watu wengine kama tunavyojipenda wenyewe.

► Mwanafunzi anapaswa asome Mathayo 22:36-39 kwa ajili ya kikundi.

Tuliumbwa kwa ajili ya Mungu na kwa ajili ya watu wengine; mambo haya mawili yanahusiana kwa karibu sana. Mojawapo ya maeneo ya msingi ambayo tunamtukuza nayo Mungu na kuonyesha mfano wake ni katika mawasiliano yetu na wengine. Tabia na matendo ya Mungu yanatuwajibisha kuwa kama yeye (1 Petro 1:16, Mathayo 5:48). Watu wote wameumbwa katika sura ya Mungu, lakini sisi huonyesha asili na tabia ya Mungu tunapotenda kama yeye anavyotenda.

Mtu anapoonyesha kuwa mwenye huruma kwa wahitaji, huruma yake ni mfano wa huruma ya Mungu, na tendo lake la huruma ni kuiga kazi ya Mungu. Jambo hili ni la ukweli bila kujali kama anayeonyesha huruma ni mtu aliyeokoka au ambaye hajawahi kuokoka kabisa. Hata hivyo, tunamuiga Mungu vizuri zaidi tunapokuwa tumepatanishwa naye na Roho wake kufanya kazi ndani yetu.

► Mwanafunzi anapaswa asome 2 Petro 1:2-11 kwa ajili ya kikundi.

Kifungu hiki kinaelezea mpango wa ajabu wa Mungu kwa ajili ya kila mfuasi wa Kristo. Kutokana na kifungu hiki tunajifunza kwamba:

1. Kwa utukufu na wema wake, Yesu kwa pamoja ametuita na kutupa sisi ahadi nzuri za ajabu (Aya ya 3-4).
2. Kupitia ahadi hizi nzuri za ajabu, wale ambao miongoni mwetu wanamjua Kristo tunaweza tukawa na asili ya kiungu ya Mungu ndani yetu (Aya ya 4).
3. Kupitia uhusiano wetu na Mungu aliye Baba na Yesu, tuna kila kitu tunachohitaji kwa ajili ya maisha na utauwa (Aya ya 3).

4. Kwa sababu ya mambo haya yote, tunaweza tukaishi kama Yesu alivyoishi na kama alivyotuita sisi tuishi (Aya ya 5-8).

- Ni kwa jinsi gani inawezekana kuakisi tabia na asili ya Mungu katika mahusiano yetu?
- Mwanafunzi anapaswa asome 2 Wakorintho 4:4 kwa ajili ya kikundi. Ni nani aliye picha kamilifu kwa ajili ya Mungu?
- Mwanafunzi anapaswa asome 2 Wakorintho 3:18 kwa ajili ya kikundi.

Roho Mtakatifu huwabadilisha waumini ili wazidi kuakisi utukufu kwa ajili ya Bwana. Kwa kumwangukia Yesu, tunafanywa kuwa zaidi na zaidi kama yeye katika mitazamo na tabia zetu. Huu ndio uzuri wa Injili. Kupitia nguvu za Mungu Baba, Yesu na Roho Mtakatifu, tunaweza kutafakari na kuiga tabia ya Mungu.

Kwenye mahusiano yetu na watu wengine, Mungu anatutaka tumwige (Waefeso 5:1). Kama vile ambavyo mtoto anavyomtamaza na kumwiga mzazi wake, ndugu, au dada yake mkubwa, tunapaswa tuangalie kutoka katika mfano wa Yesu kisha tuige tabia zake, mitazamo yake, na matendo yake tunapokuwa tunashirikiana na watu wengine (Wafilipi 2:5-7, Waefeso 5:2).

► Wanafunzi wanapaswa wasome vifungu vifuatavyo kwa ajili ya kikundi. Zingatia: (1) Tabia au kazi ya Mungu, na (2) Matarajio ya Mungu kwa ajili yetu. (Maelezo ya vifungu viwili vya kwanza tayari yameandikwa kama mfano. Mwishoni mwa somo hili, Kazi ya kufanya ya 2 ni mwendelezo wa fundisho hili.)

<b>Jinsi Mahusiano ya Wanadamu Yanavyoakisi Utukufu wa Mungu</b>		
<b>Andiko</b>	<b>Anachokifanya Mungu/ Alichokifanya Kristo</b>	<b>Kitendo Chetu kinachomwakisi Mungu</b>
Wafilipi 2:3-8	Aliachilia haki zake. Alifanyika kuwa mtumwa. Alijinyenyekeza kabisa akawa mtiifu.	Kuacha haki zetu. kujali maslahi ya wengine. Kuwa mnyenyekevu.
Yohana 13:3-5, 12-15	Aliwahudumia wanafunzi wake, katika mahitaji yao halisia.	Kuwahudumia waumini wengine.
Waefeso 4:32-5:2		

Kwa asili, hakuna hata mmoja wetu ambaye anaonyesha upendo wa Mungu kwa sababu tumezaliwa tukiwa na asili ya ubinafsi. Mungu hutupa neema ya kuturejesha tena kwenye

mpango wake kwa ajili yetu. Sala ya unyenyekevu ya kujisalimisha inaweza ikampeleka mtu kupita katika mabadiliko haya.

### **Hitimisho**

Biblia inafunua kwamba Mungu kwa upendo wake aliwaumba watu kwa ajili ya mahusiano; uhusiano pamoja naye na mahusiano na watu wengine.

Kwa kuwa Mungu ndiye Muumbaji wa watu wote na Mbunifu wa mahusiano ni lazima:

1. Kupata mtazamo wake juu ya uhusiano wetu wa kibinadamu.
2. Kutambua uwajibikaji wetu kwake kwa ajili ya chaguzi mbalimbali tunazofanya katika mahusiano.
3. Kukubali na kufuata mpango wake kwetu kwa ajili ya mahusiano yetu.

Kozi hii ya mafunzo mahususi itakusaidia wewe kufanya mambo haya na itakutayarisha katika kufundisha wengine mapenzi ya Mungu kwa ajili ya mahusiano ya kibinadamu.

### **Kwa ajili ya Majadiliano ya Kikundi**

► Je, kwa nini utamaduni hautoshi kuwa ni mwongozo kwa ajili wa mahusiano ya kibinadamu?

► Je, umepata dhana gani mpya kwako kutokana na somo hili? Kwa nini ni muhimu? Je, kwa kuielewa dhana hii, itakusaidiaje katika mahusiano yako? Kwa kuielewa dhana hii, itaathiri vipi huduma yako?

► Je, ni kwa jinsi gani unatarajia kwamba utakua kwa sababu ya kusoma kozi hii?

### **Maombi**

Baba wa Mbinguni,

Asante kwa kuniumba katika sura yako pamoja na kusudi kwa ajili ya maisha yangu.

Asante kwa kuniumba mimi katika sura yako ili niweze kuwa katika uhusiano na wewe na kufanya iwezekane kupitia kifo cha Yesu kwa ajili ya dhambi zangu.

Asante kwa hazina ya Neno lako, ambayo inanifundisha jinsi ya kuhusiana nawe, na jinsi ya kukutukuza wewe kwenye mahusiano yangu na watu wengine.

Kwa kupitia Neno lako na Roho Mtakatifu wako, nifundishe kuyashikilia maisha uliyoyapanga kwa ajili yangu.

Nisaidie mimi katika kukudhihirisha wewe kwa usahihi kwa kila mtu anayenizunguka, ili kwamba na wengine waweze kuja kukujua wewe.

Ameni

## Kazi za kufanya

(1) Elezea jinsi ukweli juu ya uumbaji katika sura ya Mungu unavyompa kila mtu uthamani na jinsi ambavyo kukataliwa kwa uumbaji kunavyoondoa thamani ya ubinadamu.

(2) Soma kila moja ya Maandiko yafuatayo. Zingatia: (1) Tabia ya Mungu au kazi zake, na (2) Matarajio ya Mungu kwa ajili yetu.

<b>Jinsi Mahusiano ya Wanadamu Yanavyoakisi Utukufu wa Mungu</b>		
<b>Andiko</b>	<b>Kile anachokifanya Mungu/ Alichokifanya Kristo</b>	<b>Kitendo Chetu kinachomwakisi Mungu</b>
Zaburi 68:5; Yakobo 1:27		
2 Petro 3:9; Tito 3:1-5		
Mathayo 5:43-48, 1 Wathesalonike 5:14-15		
Yohana 13:1, 34; 1 Yohana 4:7-8, 1 Yohana 4:11-12		

(3) Ukiangalia Jedwali kutoka kwenye Kazi ya kufanya 2, na hili lililotolewa hapa mwishoni mwa somo, chukua muda wa kuchunguza maisha yako:

- Je, kwa sasa unaakisi sura ya Mungu katika njia ambayo inamletea heshima na kumtukuza Yeye?
- Je, kuna namna yeyote ile ya kutokutii ambayo ni lazima kutubu ili kwamba maisha yako yawe yanaenda kwa uwazi na kwa nguvu katika kusudi la Mungu kwenye maisha yako?
- Je, ni hatua gani ambazo Mungu anakutaka wewe uchukue ili kukufanya wewe ufanane zaidi na Yesu?

Andika aya moja ya maombi kuhusiana na fundisho hili. (Hailazimiki kushirikishana andiko hili na kiongozi wako wa darasa lakini unaweza tu kutoa taarifa kwamba ulishakamilisha Kazi ya kufanya.)





# Somo la 2

## Familia ya Kibiblia

### Malengo ya Somo

Hadi kufikia mwishoni mwa somo hili, mwanafunzi atapaswa:

- (1) Kuelewa jinsi ndoa inavyotakiwa kuakisi mahusiano yaliyoko katika Utatu Mtakatifu wa Mungu.
- (2) Akubaliane na mpango wa Mungu kuhusu kupata watoto.
- (3) Kuelewa jinsi Anguko la mwanadamu lilivyoathiri ndoa na mahusiano ya kifamilia.
- (4) Athamini jinsi mapenzi ya Mungu yanavyokuwa yanatekelezwa licha ya kasoro za kibinadamu zilizopo.
- (5) Atambue kwamba utiifu kwenye mpango wa Mungu unaweza ukaisaidia familia yeyote kuwa familia ya ukombozi.

### Matokeo ya Mahusiano ya Kifamilia

Katika kozi hii, tutajifunza zaidi kuhusu familia inayoishi pamoja kwenye eneo moja la kuishi. Michanganyiko mingi tofauti ya watu huunda vikundi vinavyoishi katika nyumba pamoja na huitwa familia. Kuna familia ambazo zina mzazi mmoja, kuna familia ambazo zimegawanyika kwa kupeana talaka, Kuna familia zilizo na mzazi mmoja, familia zilizogawanyika kwa sababu ya talaka, familia zilizounganishwa na ndoa ya pili, familia ambazo zimeasili watoto, familia zenye vizazi vingi, na familia ambazo zinazohudumia watoto au watu wazima kwa muda.

Kila mmoja wetu ana dhana ya kiakili ya nini maana ya familia. Majadiliano kuhusu familia huunda hisia tofauti ndani yetu, kulingana na uzoefu wetu wa kibinafsi.

### Jinsi Utoto Unavyotuathiri

Labda una kumbukumbu nzuri za utoto wako, au labda unapambana na hasira kwa sababu ya mambo uliyokutana nayo wakati wa utoto. Labda wanafamilia wako mara nyingi husaidiana na kutiana moyo, au yumkini wanakwepana kila mmoja na mwenzake na wana migogoro kila wanapokuwa pamoja. Unaweza kuhisi kuwa familia yako imekuwa msingi na msaada mkubwa kwa maisha yako, au labda nyumba yako ilikuwa kama jela, ikiwa na mazingira machungu yaliyoleta hamu ya kutoroka. Labda unapona familia zinazoonekana kuwa bora zaidi kuliko zako, unahisi kwamba familia yako haikukufanikisha.

Uelewa wetu wa familia zetu ni muhimu kwa sababu unaathiri uelewa wetu wa maisha na ufahamu wetu kuhusu Mungu ni nani. Biblia inazungumza juu ya Mungu kuwa Baba wa watu

wake. Mahusiano yetu na wazazi wetu – hasa baba zetu – huunda na kutengeneza dhana yetu juu ya Baba yetu wa Mbinguni. Ikiwa baba yetu wa kibinadamu alikuwa hayupo, mwenye lugha chafu, asiyejali, mwenye kudai, mwenye hila, mwenye kukaa tu bila hisia, au mwenye kuumiza kwa njia yeyote ile, dhana yetu ya Mungu kuwa Baba ingeweza kuharibiwa. Hadi pale tutakapomjua Mungu kupitia Neno Lake, kupitia maisha ya Yesu, na kupitia kutembea kwetu kibinafsi pamoja naye, tunaweza tukapata ugumu wa kumwona yeye kama Baba **mzuri**. Kwa kweli yeye ni baba mzuri ambaye huwalinda na kuwaandalia watoto wake kwa vitendo. Yeye husikiliza na kuzungumza na watoto wake, huwaongoza, na hufurahia hali zao njema. Mungu anaweza kutusaidia kutengeneza kwa upya tena uelewa wetu kumhusu Yeye kwa kadri tutakavyoweza kumjua Yeye.<sup>3</sup>

### **Jinsi Tofauti za Kiroho Zinavyotuathiri**

Baadhi yetu tumekataliwa na familia zetu kwa sababu ya kuamua kumfuata Kristo. Yesu alisema kwamba tunapaswa kutarajia mateso kutoka kwa wanafamilia ambao hawajaamini kwa sababu ya kujitoa kwetu kwa ajili yake. Katika maeneo mengi waumini wanasalitiwa, wanaaibishwa, wanapuuzwa, wananyanyaswa, na wanauawa na wanafamilia wao wenyewe ambao wamekataa kumkubali Kristo.

► Mwanafunzi anapaswa asome Mathayo 10:21-22, 28, 32-39. Baada ya kuzisoma hizi aya, yajadili maswali yafuatayo:

- Kwa mujibu wa aya hii, je, waumini wanapaswa kutarajia nini?
- Ni ahadi gani zinazotolewa hapa?
- Ni kwa jinsi gani waumini wanapaswa kufikiria kuhusu mateso?

Watu wengine miongoni mwetu wanaweza wasipatwe na matatizo kutoka katika familia zao lakini wanaweza kupatwa na changamoto za mahusiano kwa sababu ya imani yetu. Inawezekana mahusiano ya familia zetu yana shida, ni ya Umbali, ni madogo, kwa sababu kama waumini maisha yetu yako tofauti sana na maisha waliyo nayo wanafamilia wetu. Tunaweza tusieleweke au tusipewe heshima zinazostahili. Huenda watu wa familia wakajaribu kuzuia huduma zetu. Hata Yesu mwenyewe alikutana na magumu haya (Marko 3:21, Yohana 7:3, 5), kwa hiyo hatupaswi kushangaa tukifanyiwa hivyo pia.

### **Wewe na Familia yako**

Kwa dakika chache, utajitambulisha kwa wanafunzi wenzako, lakini hutataja tu jina lako, bali pia utashirikisha wewe ni nani katika muktadha wa familia yako.

Kwanza fikiria kuhusu nyadhifa zako zote ulizo nazo katika familia yako, kama vile mtoto wa kiume au wakike, mume au mke, mjomba au shangazi, au kama ni bibi au babu. Je, unaweza ukafikiria kuhusu vyeo vingine vya ziada? Inawezekana una vyeo vingine kadhaa.

---

<sup>3</sup> Ili kujifunza jinsi ya kufanya upya uelewa wako kuhusu Mungu ni nani, ona Somo la 4 la *Malezi ya Kiroho* kutoka Shepherds Global Classroom.

Je, una majukumu gani mengine au nafasi gani nyingine katika familia yako? Wewe ndiyo mkubwa au ni mdogo zaidi? Wewe ni mtoaji wa fedha? Wewe ni mtu uliye na jukumu la kuitunza nyumba yako? Je, wewe unalo jukumu la kuwatunza wazee na watu wasiojiweza? Jaribu kufikiria tena majukumu mengine uliyo nayo ndani ya familia yako.

► Jitambulisha kwa wanafunzi wenzako, ukiorodhesha baadhi ya vyeo na majukumu yako ndani ya familia yako.

► Sasa, chukua muda wa kufikiri kuhusu jinsi ambavyo vyeo vyako na majukumu yako yanavyoshawishi: (1) Mtazamo wako juu yako mwenyewe, na (2) Jinsi unavyowaona wengine ndani ya familia yako.

Licha ya jinsi unavyoweza kuhisi kuhusu wanafamilia wako wa karibu au wa mbali, wao ni wako. pengine familia yako imevunjika, ina alama za maumivu na huzuni. Au labda watu wanakuonea wivu kwasababu familia yako inaonekana kuwa kamilifu: una ndoa nzuri, watoto wenye akili na afya njema, na nyumba iliyojaa upendo, amani na kicheko.

**Aidha iwe familia yako inaonekana kuwa dhaifu au yenye nguvu, Mungu anapendezwa na anahusika kikamilifu na familia yako. Anao mpango kwa ajili ya familia yako.**

► Orodhesha majina ya wanafamilia wako (angalao vizazi 3-4 vya wanafamilia). Kwa mfano, majina ya babu zako (kizazi cha 1), majina ya wazazi wako (kizazi cha 2), jina lako na ndugu zako (kizazi cha 3), majina ya watoto wako au wapwa - *watoto wa kike au wa kiume wa kaka /dada* - (kizazi cha 4).

Chora nyota kando ya majina ya wale ambao una mahusiano ya karibu na yaliyo mazuri. Chora alama ya pembetatu mbele ya majina ambayo una mahusiano madogo sana nao, na chora alama ya pembe mraba mbele ya wale ambao hamhusiani kabisa katika jambo lolote kwa sababu iwayo yeyote ile.

Je, wako watu ambao unawachukulia kama ni sehemu ya familia yako, ingawaje kwa uhakika siyo wenye kuwa na mahusiano na wewe: watu ambao wanahudhuria katika makutaniko na sherehe mbalimbali kana kwamba ni wanafamilia? Waandike na yawekee alama ya mviringo majina yao.

## **Familia ya Kwanza ya Kibinadamu**

► Fungua Biblia yako katika kitabu cha Mwanzo tunapojifunza maisha ya Adamu na Hawa, na Ibrahimu na Sara.

### **Harusi ya Kwanza**

Adamu na Hawa ilikuwa familia ya kwanza ya kibinadamu: mume mmoja na mke mmoja, mwanamume mmoja na mwanamke mmoja wakiunganishwa pamoja katika ndoa. Katika harusi ya kwanza, Adamu alisema, "Sasa huyu ni mfupa katika mifupa yangu, na nyama

katika nyama yangu, basi ataitwa mwanamke, kwa maana ametwaliwa katika mwanamume” (Mwanzo 2:23).

Aya inayofuata inatoa ufafanuzi wa kibiblia kuhusu ndoa:

“Kwa hiyo mwanamume atamwacha baba yake na mama yake naye ataambatana na mkewe, nao watakuwa mwili mmoja” (Mwanzo 2:24).

Ufafanuzi huu wa kufanana umerudiwa tena katika Agano Jipya kwenye Mathayo 19:5 na Waefeso 5:31. **Muunganiko wa mwili mmoja wa mwanamume na mwanamke ni wajibu usiokuwa na masharti, ahadi mbele ya Mungu na mwanadamu kwamba itakuwa ni ya kudumu kwa maisha yote.**

Ndoa ni muujiza ulioko wa aina tatu. Ni muujiza wa kibiolojia ambao katika huo watu wawili wanafanyika hasa kuwa mwili mmoja; ni muujiza wa kijamii ambao kupitia huo, familia mbili tofauti hupandikizwa kuwa familia moja; ni muujiza wa kiroho ambao kwao uhusiano wa ndoa unatoa picha inayofananishwa na muunganiko wa Kristo na Bibi Harusi wake, yaani Kanisa.<sup>4</sup>

### **Ndoa inaakisi Mahusiano yaliyoko kwenye Utatu Mtakatifu wa Mungu**

Ndoa imekusudiwa kuakisi tabia ya Mungu na mahusiano yake. Mungu Baba, Mungu Mwana, Mungu Roho Mtakatifu kwa wakati wote wamekuwa na siku zote wataendelea kuwa kwenye uhusiano na kila mmoja. Kila mmoja ni wa kipekee kwenye jukumu lake, lakini nafsi zote tatu ni za kudumu na zenye asili moja. Kwenye uhusiano kati ya nafsi tatu za Utatu Mtakatifu wa Mungu, tunaona umoja, ukaribu, uaminifu, na upendo thabiti. Ndoa ya Kibiblia imeundwa baada ya uhusiano huu wa kushangaza. Mpango wa Mungu ni kwa kila mume na mke kuwa safi katika upendo wao na kila mmoja kujitolea kwa ajili ya mwingine kwa maisha yake yote.

“Ndoa ni...

Udhihirisho wa tabia ya Mungu kama mfanyaji wa agano mkuu na mshikaji wa agano. Katika agano, vipengele muhimu ni uaminifu, na uadilifu, na siyo mhemuko.”

- Robertson McQuilkin,  
Utangulizi wa Biblia kuhusu Maadili  
(*An Introduction to Biblical Ethics*)

Uhusiano wa ndoa ya kibinadamu unapaswa uakisi mahusiano yaliyoko ndani ya Utatu Mtakatifu wa Mungu kwa njia hizi:

1. Ndoa inapaswa isiwe na masharti, yenye ahadi ya kipekee kwa mwingine.
2. Ndoa ni kuwa na uhusiano wa upendo wa kujitoa mwenyewe.
3. Ndoa inapaswa iwe na uhusiano unaotoa matunda.

---

<sup>4</sup> Biblia ya Mafunzo kwa Mwanamke (*The Woman's Study Bible*), (Thomas Nelson, Inc., 1995), 9.

## Agizo la Kwanza

Wakati wa harusi ya kwanza, ambayo ilifanywa na Mungu mwenyewe,

Mungu akawabarikia, Mungu akawaambia, Zaeni, mkaongezeke, mkaijaze nchi, na kuitiisha; mkatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na kila kiumbe chenye uhai kiendacho juu ya nchi” (Mwanzo 1:28).

Kuzaa na kuongezeka ni agizo la kwanza ambalo Mungu alilitoa ndani ya Biblia. **Ndoa imeundwa ili kuwa na uhusiano unaotoa matunda kwa upendo wa kujitoa mwenyewe.** Uzazi ndani ya ndoa unamtukuza Muumbaji, kwa kuwa mume na mke kwa pamoja humletea Mungu utukufu kwenye kazi yake ya uumbaji na huwaleta watu wengi zaidi kwenye uhusiano wa kifamilia.

Huu ni upendeleo na uwajibikaji!

► Mwanafunzi anapaswa asome Zaburi 127:3-5 kwa ajili ya kikundi.

Kifungu hiki kinatumia picha za maneno kuelezea watoto. Picha za maneno ni nini? Kulingana na picha hizi za maneno, je, tunapaswa kuwafikiriaje watoto wetu?

Biblia inatuonyesha kwamba watoto ni zawadi, ni mali ya thamani sana ya kuwa nayo. Hawapaswi kufikiriwa tu kwamba ni matokeo ya mahusiano ya tendo la ndoa. Iwe au isiwe kwamba mazingira yanayohusika ya utungwaji wa mimba wa mtoto ni wa kutaka au wa haki, Mpaji wa Uhai anakuwa na makusudi wakati wa kutungwa kwa mimba na kuzaliwa kwa kila mtoto, ikiwa ni pamoja na wewe na mimi. Mungu analo kusudi na kila mtu bila kujali mazingira ya kuzaliwa kwake.

Hakika, watoto ni zawadi kutoka kwa Mungu, lakini pia ni zawadi ya wazazi kwa Mungu.

Hakuna mtu mmoja aliyetenda hivi, ambaye alikuwa na ufahamu kidogo. Au je! Kuna mtu mmoja atafutaye mzao mwenye kumcha Mungu? Kwa hiyo jihadharini roho zenu; mtu awaye yote asimtende mke wa ujana wake mambo ya hiana” (Malaki 2:15).

Watoto ni amana takatifu. Mungu anatarajia wazazi wawalee watoto wao kwa ili kutimiza makusudi yake mwenyewe.

Mungu anataka awatumie watoto wetu kwa ajili ya kuuendeleza ufalme wake (Mwanzo 18:19). Mungu ametuamini kuwatayarisha watoto wetu kwa ajili ya maisha ya kumtumikia yeye (Kumbukumbu la Torati 6:2). Hatuwalei ili watutumikie au kutimiza ndoto zetu. Tunapaswa tuwaone watoto kama mishale ya kurushwa nje ili kupiga shabaha ambayo Mungu anayo kwa ajili yao.

## Anguko na Kuvunjika kwa Familia ya Kibinadamu

Katika Mwanzo 3, familia peke yake ambayo ni kamilifu kuwahi kuwepo ilianguka katika hali ya kuvunjika na kuhitaji Mkombozi. Adamu na Hawa walitenda dhambi, na laana ya kifo

ikawaangukia wanadamu wote. Uhusiano kati ya Adamu na Hawa uliharibika kabisa, nao walitengwa na Mungu.

Kwa pamoja mwanamume na mwanamke walipata laana zaidi.

- Kuzaa kutakuwa kwa uchungu.
- Waume watatumia mamlaka yao vibaya.
- Wake watakuwa wakaidi na wasio na heshima.
- Kazi zitakuwa za kukatisha tamaa na zilizo ngumu.<sup>5</sup>

Mpango wa Mungu ulio mkamilifu kwa ajili ya familia ulivurugwa kwa sababu watu walikubaliana na uongo wa Shetani.

Mwanzo 4 panaendelea kudhihirisha kuvunjika kwa familia ya kibinadamu iliyoanguka.

Angalia taarifa iliyoko katika Mwanzo 4:1, kuhusu mimba ya kwanza na kuzaliwa. Aya hii inahusu muda wa miezi tisa – kipindi kati ya kutungwa kwa mimba ya mtoto hadi kuzaliwa kwa mtoto. Jaribu kujituliza kidogo ufikirie kuhusu hiyo miezi tisa ya uja uzito ilivyopaswa kuwa kwa Hawa, wakati akijaribu kushirikishana kuhusu mashaka na furaha yake pamoja na Adamu.

Hakukuwa na mtu wa kumpa ushauri, wala mtu wa kujibu maswali yake. Tumbo lake lililokuwa likiongezeka, mateke ya mtoto wake, na mchakato wa kujifungua akiwa na mivutano mbalimbali mwilini pamoja na maumivu vyote vilikuwa ni uzoefu wa mara ya kwanza kwa mwanamke yeyote wa kibinadamu.

Hakuna mashaka kwamba Hawa alisema kuhusu kuzaliwa kwa Kaini, “Nimepata mtoto mwanamume kwa Bwana” (Mwanzo 4:1).

Muda ulipita, na katika aya inayofuata, tunajifunza kuhusu mimba ya uzazi wa pili. Sasa Adamu na Hawa wana familia ya watu wanne. Katika nusu ya sehemu ya pili ya Aya hiyo hiyo ni muhtasari wa taaluma za watoto wao. Kufikia Aya ya 3, wavulana hao tayari ni watu wazima na katika Aya inayofuata tunasoma hadithi ya kutisha ya mauaji ya kwanza. Mtoto mkubwa wa Adamu na Hawa alimuua ndugu yake kwenye tendo la hasira na wivu. Je, unaweza kufikiria kuhusu mshtuko huo, huzuni, maswali, uchungu na maumivu?

Jibu lako katika maswali hayo linaweza kuwa “Ndiyo! Ninaweza nikafikiria hivyo. Kwa uhakika, mimi nimewahi kupata uzoefu unaofanana na hali hiyo. Acha nikutie moyo: Hauko peke yako. Familia yako inaweza kukombolewa. Kuna habari njema kwa kila familia.

Gordon Wenham anaandika,

---

<sup>5</sup> Ni muhimu kutaja hapa kwamba **uzazi wa mtoto** haukuwahi kuwa sehemu ya laana.

Maumivu wakati wa uzazi wa mtoto ni matokeo ya laana, lakini uzazi wa mtoto siku zote umekuwa ni mpango wa Mungu wa ajabu wa kuzalisha kizazi kijacho. Aidha kazi haikuwa laana, bali ugumu wa kazi ndiyo uliokuwa laana. Kwa hakika, kwenye maagizo mengine ambayo alimpa Adamu na Hawa katika Mwanzo 1:28 zinaonyesha kwamba tumeumbwa kwa ajili ya kazi! Kazi ni mojawapo ya njia tunazoakisi sura ya Mungu.

...Ujumbe wa kitabu cha Mwanzo...Ni hadithi ya ushindi wa neema, licha ya dhambi ya mwanadamu, ya ushindi wa neema hata katika familia ambazo zimevunjika kutokana na dhambi. Kitabu hiki kinaanza na dokezo la hali ya juu ya uumbaji wa ulimwengu likimalizia na uumbaji wa mwanadamu katika sura ya Mungu na Mungu akitangaza kwamba kila kitu alichokifanya na alichokiumba vilikuwa vizuri sana...Ni katika sura ya 3 tu ndipo tunapoona mambo yakianza kwenda vibaya, ikiwa ni pamoja na kutotii [migogoro], na kifo kikichukua nafasi ya utii, upatanifu, na uhai. Mambo yanaendelea kuwa mabaya zaidi katika sura ya 4...na kufikia katika [kiwango cha chini sana] katika sura ambako dunia inasemekana kuwa katika hali kamili ya vurugu (Mwanzo 6:11, 13).<sup>6</sup>

### **Uvunjikaji katika Familia ya Ibrahimu**

Ukiendelea zaidi katika kitabu cha Mwanzo, tunasoma kuhusu Ibrahimu, baba wa taifa la Waebrania (Mwanzo 11:27-25:11).<sup>7</sup> Ilikuwa ni kupitia katika familia ya Ibrahimu kwamba Mungu angemleta Mkombozi kwenye familia ya kibinadamu.

#### **Utasa<sup>8</sup>**

Mwanzo 11 inaorodhesha ukoo wa Abram, ambaye alikuwa ni uzao wa Shemu mwana wa Nuhu. Mwanzo 11:30 tunaelezwa kwamba Sarai mke wa Abram hakuwa amejaliwa kupata watoto. Aya hiyo ni ya machozi, uchungu, huzuni, kuchanganyikiwa, ubatili, hasira na masikitiko kwa wengi watakaokuwa wanaisoma. Kama utaweza kuliweka jina lako kwenye Aya hii likawepo badala ya Sarai, tambua kwamba hauko peke yako.

Kwa wale ambao wangependa kuwa na watoto, lakini wanapitia katika hali ya utasa, kusoma vifungu kama vile Mwanzo 1:28 na Zaburi 127:3-5 kunasababisha maumivu makali na huzuni. Ni hali ya kawaida kujihihi kwamba kukosa mtoto ni adhabu au laana.

Ukweli ni kwamba, wewe siyo mtu usiyekuwa wa muhimu kwa Mungu kwa sababu ya kutokuwa na watoto. Hujasahaulika. Utasa wako haimaanishi kuwa familia yako ni familia yenye kasoro. Wako watu wengine ambao walishakutana na kadhia hii ya majuto makali inayofanana na hii.

Jinsi wanandoa wanavyoshughulika kwenye kupitia utasa, wote kwa pamoja na kama mtu binafsi, ni muhimu sana. Maamuzi yasiyo na busara yanaweza kusababisha matatizo zaidi, kama tutakavyoona kwenye maisha ya Abram na Sarai.

---

<sup>6</sup> Gordon Wenham akiandika katika Familia ndani ya Biblia (*Family in the Bible*), na kuhaririwa na Richard S. Hess na M. Daniel Carroll R., Grand Rapids, MI: Baker Academic, 2003, 29

<sup>7</sup> Mungu alibadilisha majina ya Abram na Sarai kuwa Abrahamu na Sara katika Mwanzo 17:5, 15.

<sup>8</sup> Ona Somo la 10 kwa ajili ya mambo mengi zaidi katika mada hii..

## Kusubiria Ahadi

Kufuatia kifo cha baba yake, Abram ukaawa baba wa ukoo wa familia yake. Mungu aliahidi kumfanya Abram kuwa taifa kubwa (Mwanzo 12:2) na aliahidi kuwapa wazao wa Abram nchi ya Kanaani (Mwanzo 12:7). Abram sasa alikuwa na umri wa miaka 75 (Mwanzo 12:4) na Sarai mdogo miaka kumi (Mwanzo 17:17). Sarai alikuwa mwanamke mrembo isivyo kawaida mwenye umri wa miaka 65 (Mwanzo 12:11), bado akiwa tasa, na tayari alikuwa ameshapitiliza miaka yake ya kawaida ya kuweza kuzaa.

Miaka iliendelea kupita, na bado akawa hajakapata mtoto, ingawaje ahadi ya Mungu ilikuwa imefanywa upya katika Mwanzo 13:14-17. Abram alionekana amekataa tamaa ya kuwa baba wa mtoto wake mwenyewe, kwa sababu katika Mwanzo 15:2-3 anaonekana akimwambia Mungu kwamba mtumishi wake ndiye atakayekuwa mmiliki wa nyumba yake. Bwana alimjibu, "Huyu hatakurithi, bali atakayetoka katika viuno vyako ndiye atakayekurithi (Mwanzo 15:4). Kisha Mungu akampa Abram picha ya pili ya ahadi ya uzao usiokuwa na hesabu, na Abram akamwamini Bwana (Mwanzo 15:6).

Mungu anafanya kazi ya kutufanya sisi tumfananie Yesu. Wakati mwingine Mungu anatufanya tuwe na subira, kwa sababu kupitia kipindi cha kusubiri anaweza kufanya kazi ndani ya mioyo yetu ambapo kwa vinginevyo haingewezekana.

Jaribu kufikiria ni kwa jinsi gani miaka hii yote ya kusubiria ingekuwaje kwa Sarai.

Kama vile maumivu ya hukumu ya wengine ingeweza kuwa imefanyika kwa Sarai, ilikuwa ni ukatishwaji tamaa (mkali) ambao ulikuwa umemuumiza zaidi. Pengine hakuwa ametamani tu sana utimizwaji wa ahadi ya kuwa mama bali pia kwa ajili ya heshima na stahiki inayopewa kwa wamama wazazi katika jamii ambayo wanawake hawakuwa na lolote la kuhesabika wa maana badala yake. Tunajua kwamba utasa wa kiume unaweza kuwa sababu ya mwanamke kutobeba mimba lakini hakukuwepo na ujuzi huo wa kibiolojia wakati wa ulimwengu wa Sarai. Utambulisho wa Sarai kama mwanamke, na kama mtu wa thamani, ulitegemea aweze kuzaa na kunyonyesha watoto. Hakuweza kupata thamani machoni pa wanaume kwa kuwa kiumbe mwenye haki na mwaminifu, ila kwa kuzaa watoto wa kiume ambao wangukuwa warithi kwa mume wake. Tumbo tupu lilimaanisha maisha matupu.<sup>9</sup>

---

<sup>9</sup> David na Diana Garland, *Flawed Families of the Bible*, Grand Rapids, MI: Brazos Press, 2007, 21-22



## Suluhisho la Kibinadamu na Matokeo Yenye Maumivu

Abramu alipokuwa wa umri wa miaka 85, Sarai alikuwa na wazo – suluhisho kwa jinsi gani Abramu atakavyoweza kupata mtoto. Mjakazi wa kike wa Sarai angeweza akawa mzazi wa mtoto wao (Mwanzo 16:1-4). Lakini kile ambacho Abramu na Sarai walikuwa wamedhamiria kwamba kingekuwa ndicho suluhisho sahihi na kiliharibu amani katika nyumba yao Hajiri alipobeba mimba. Kilichoonekana kuwa ni kizuri sana kimekuwa ni kibaya sana. Jaribio lao la kumsaidia Mungu kutimiza ahadi yake lilisababisha tu ugomvi na mafarakano. Watu wanaposhindwa kuamini mpango na wakati wa Mungu, matokeo yake ya kawaida ni mahusiano kuvunjika na hisia za kuumiza.

Katika miaka iliyofuata, mivutano, maumivu, kutoelewana, matatizo ya mawasiliano, hasira, utelekezaji, na kukataa tamaa viliongezeka (Mwanzo 16-21), siyo tu kwenye nyumba ya Abramu na Sarai, lakini pia kwenye familia ya mpwa wao Lutu.

“Mungu anazo sababu takatifu za kusubiria wakati tunapokuwa tu wahitaji, kama alivyokuwa amefanya kwa Elizabethi (Luka 1:7, 13), na kuendelea hata zaidi kabla hatujawa tayari, kama alivyofanya kwa Mariamu. (Luka 1:34).

Tunapokuwa tunamtii na kumwabudu Yeye, anatuelekeza, anaelimisha, na anatoa kwa ajili ya mpango wake, ambao hauzuiliki kamwe na kile ambacho hatuwezi kufikiria.”

- Nukuu kutoka kwa Shauna Letellier,  
*Remarkable Advent*

## Familia zenye mapungufu

Abramu alikuwa amechaguliwa na Mungu kuwa baba wa taifa kubwa, ukoo ambao Yesu angezaliwa kupitia humo. Inaonekana kama Abramu alikuwa anaharibu mpango wa Mungu, kama walivyokuwa wanafanya watu wengine wa familia yake. Kwao ilikuwa ni mfano wa familia zilizokuwa na mapungufu sana.

Katika Mwanzo 49:33, Abrahamu na Sara, Isaka na Rebeka, Yakobo na wake zake walikuwa wote wamekufa. Pamoja na watoto wa Yakobo, walikuwa familia yenye kushindwa katika mambo mengi sana. Mapigano, mabishano, upendeleo, udanganyifu, utelekezaji, mashindano baina ya wanandugu, ubakaji, na zinaa ya kifamilia vote vilikuwa sehemu ya hadithi ya familia yao. Hakuna hata neno moja kati ya maneno hayo linalofafanua familia yenye kustawi na amani.

Jambo la kusikitisha ni kwamba, hadithi hii inaweza kurudiwa katika Biblia yote na katika dunia yote kwa karne zote zilizopita. Bila shaka, hata katika familia hizi kulikuwa na nyakati za furaha, hadithi nzuri za upendo, na hata wanaume wachache waadilifu.

Katika kupitia haya yote, Mungu kamwe hakusitisha mpango wake wa kuwakomboa wanadamu. Na hakubadili kusudi lake kwa ajili ya familia. Ukiendelea kusoma Agano la Kale, utagundua mada nzuri sana ya ukombozi kupitia taarifa ya familia ya Kiebrania. Matukio mengi yameelekezwa kwa Yesu kwa siku za mbele. Sadaka ya Ibrahimu ya Isaka, Pasaka na kuondolewa kwa Waisraeli katika utumwa wa Misri; kukombolewa kwa Rahabu

kutokana na hukumu na kujumuishwa kwake kwenye kundi la watu wa Mungu; na matukio mengine mengi ambayo yameeleza kwa uzuri sana ahadi kwamba Mkombozi angekuja na kuwakomboa wanadamu.

### **Kazi ya Ukombozi wa Mungu kwenye Familia**

Katika Waefeso 5 tunaelezwa kwamba Mungu aliitengeneza ndoa ili iwe picha ya uhusiano Kati ya Kristo na bibi harusi, yaani Kanisa. Kama vile Kristo aliye kichwa anavyojitoa mwenyewe kwa ajili ya Kanisa, vivyo hivyo kila mume, kama kichwa kwa mke wake, anapaswa ajitoe mwenyewe kwa ajili yake. Vilevile, kila mke anapaswa afuate mfano wa Kanisa. Kama ambavyo Kanisa limejitoa kwa ajili ya Kristo, kila mke anapaswa ajitiishe kwa mume wake.

Anguko la mwanadamu liliharibu mpango wa awali wa Mungu uliokuwa umeandaliwa kwa ajili ya familia za wanadamu na kusababisha madhara katika mahusiano ya ndoa. Kila familia inakabiliwa na madhara ya kuanguka kwa mwanadamu katika dhambi. Hata hivyo,

Yesu alikuja kwa ajili ya ukombozi wa mambo yote, ikiwa ni pamoja na ndoa. Alikuwa kukomboa na kurejesha mambo yote ambayo dhambi iliharibu na kuharibiwa. Mahali ambapo hatukuweza kuishi kutokana na mpango wa Mungu wa ndoa, Yesu alikamilisha viwango vyote vya Mungu kwa ukamilifu. Yesu alilipenda Kanisa kiasi cha kufa kwa ajili yake. Alijitiisha kikamilifu kwa mpango wa Mungu Baba. Yesu ndiye utimilifu kamili na mkamilifu wa mpango wa Mungu na wa kile ambacho ndoa zetu hushindwa kufanya: upendo na utii.<sup>10</sup>

► Yesu ni mfano wa mtazamo wa tabia gani ambao mtu aliyeoa anapaswa kuwa nao?

Yesu sio tu kwamba anatimiza mapenzi ya Mungu katika kujitiisha kwake kikamilifu na kwa upendo wake mkamilifu, bali anawawezesha waume na wake kushinda katika mielekeo yenye uharibifu ambayo ni asili ya ubinadamu ulioanguka. Kwa neema yake, waume kwa wake wanaweza kutimiza mpango wa Mungu kwa ajili ya ndoa wanapoiishi kwa nguvu ya Roho Mtakatifu wa Mungu (Waefeso 5:18).

Hakuna familia iliyokamilika, lakini Mungu anatamani aiokoe kila familia. Neema ya Mungu inaweza kufanya kazi ndani ya familia ikiwezesha watu binafsi wawe kama ambavyo Mungu alikuwa amewakusudia wawe tangu mwanzo.

Kama ambavyo watu binafsi katika familia huchagua kutii maagizo ya Mungu, utii wao husaidia kushinda baadhi ya kasoro na mapungufu ambayo ni ya asili kwa kila familia. Matokeo ya Anguko ambayo yanaathiri mahusiano ya kibinadamu yanapungua wakati tunapokuwa tumejisalimisha kwenye mapenzi ya Mungu.

---

<sup>10</sup> Christina Fox, "Redeeming Marriage." Imepatikana kutoka katika <https://cbmw.org/2013/08/29/redeeming-marriage/> November 29, 2022.

Kwa mfano, mume mcha Mungu anapotii maagizo ya Mungu kwake kwenye Waefeso 5, anakuwa ameshinda mwelekeo wake wa asili wa matumizi mabaya ya mamlaka yake dhidi ya mke wake. Utiifu wake kwa Mungu ni wa ukombozi kwa sababu anapunguza madhara ya Anguko. Utii huu ungeweza pia ukamchochea mke wake kujisalimisha mwenyewe kwake.

Inapotokea mke anapotii kwa mume wake katika kutii agizo la Mungu (Waefeso 5:24), anakuwa akishinda mwelekeo wake wa asili wa dhambi wa kuzuia mamlaka ya mume wake. Utii wake kwa Mungu ni ukombozi, unaosaidia uhusiano wao uwe wa kufanana zaidi kama Mungu alivyokusudia ndoa iwe (1 Wakorintho 11:3, 1 Petro 3:1-7).

Mungu ametoa maelekezo ya ukombozi kwa familia za Kikristo ikituonyesha sisi kwamba mahusiano ya familia ni ya muhimu sana kwa Mungu.

## **Wajibu wa Kibiblia wa Familia**

### **Majukumu ya Wazazi na Mababu**

Kuna vifungu vingi katika Maandiko ambavyo vinazungumzia kuhusu hitaji la wazazi na mababu kuwafundisha watoto na wajukuu zao njia za Mungu.

Tutaziangalia tatu kwa kifupi:

► Mwanafunzi anapaswa asome Waefeso 6:4 kwa ajili ya kikundi.

Aya hii inamaanisha nini?

Ni mpango wa Mungu kwa wazazi kuwafundisha watoto wao kumjua na kumtii Mungu. Njia ambayo wazazi wanaitumia kuongoza, kuelekeza, kusahihisha, na kufundisha watoto wao inapaswa kuakisi njia ambayo Mungu hufanya mambo haya kwa ajili ya watoto wake.

► Mwanafunzi anapaswa asome Zaburi 78:1-8 kwa ajili ya kikundi.

Jibu maswali yafuatayo:

- Ni, vizazi vingapi vya familia vimetajwa katika kifungu hiki?
- Kila kizazi kina wajibu gani?
- Ni mambo gani wazee wanapaswa kufundisha vijana?

Zaburi ya 78 imefurika kwa neema na rehema za Mungu za ajabu. Inaelezea kazi zake katika familia ya wana wa Israeli tangu walipotoka Misri hadi kwenye utawala wa mfalme Daudi. Zaburi hii inapaswa kuwapa wasomaji matumaini kwa ajili ya hali zilizopo kwenye familia zao.

► Mwanafunzi anapaswa asome Kumbukumbu la Torati 6:1-9 kwa ajili ya kikundi.

Kwa kuangalia kifungu hiki, Je, ni mambo gani ambayo sisi kama watu wa Mungu tunapaswa tuyafanye?

Andiko hili ni sehemu ya hotuba ya Musa kwa wana wa Israeli, kabla tu hawajaingia kwenye nchi ya ahadi ambayo Mungu alikuwa anawapatia. Walikuwa wanajifunza jinsi ya kuwa watu wa Mungu na kwamba ilimaanisha nini kuwa mali ya Mungu. Ukweli katika Aya hizi bado ni msingi wa kuishi kama watoto wa Mungu.

Mungu anatuamuru sisi kuwa watiifu katika kulisikia Neno Lake – na kufanya kila ambacho anakihitaji kutoka kwetu (Aya ya 3-4).

Tunatakiwa tufanye yafuatayo:

1. Kumpenda Bwana kwa moyo wote, kwa roho yote, na kwa nguvu zote (Aya ya 5).
2. Kuyaweka maneno ya Mungu katika mioyo yetu wenyewe (Aya ya 6).
3. Kuwafundisha watoto wetu kwa bidii jinsi ya kufuata Neno la (Aya ya 7).
4. Kuyaweka maneno ya Mungu kwenye fahamu zetu na yawe mbele yetu mara kwa mara (Aya ya 8-9).

Tambua kwamba amri hizi ni kwa kila kizazi (Aya ya 2). Mungu huwajibisha wazazi, mababu na mabibi kufundisha watoto wao na wajukuu wao kuishi kwa ajili yake. Kwa muda gani? Siku zote za maisha yao (Aya ya 2). Mungu anatuambia kwamba wazazi wanapaswa kuwafundisha watoto wao njia zake kwa siku nzima, kila siku, kila mahali waendapo, na katika kila jambo wanalofanya (Aya ya 7-9).

Elimu ya kiroho kwa ajili ya watoto ilikuwa ni jukumu la mzazi. Mafundisho hayo yangefanyika kila siku kupitia kielelezo cha wazazi na vilevile kurudiwa kwa sheria. Umuhimu wa amri hii unaonekana katika kiwango ambacho wazazi walipaswa kwenda ili kuwafundisha watoto wao. Hii ilikuwa ni zaidi ya kufundisha mambo ya hakika ya sheria; ilikuwa ni udhihirishwaji wa mtindo wa maisha uliokuwa umesukiwa kwenye kitambaa kilichofumwa cha maisha ya kila siku. Ubunifu ulikuwa unahitajika katika kuwafundisha maadili ya Mungu wakati wakiwa wanajishughulisha na mambo ya kawaida kabisa ya nyumbani.<sup>11</sup>

Wazazi hawapaswi kufundisha tu akili za watoto wao, lakini pia na mioyo yao. Wanapaswa kuwafundisha watoto wao siyo tu ukweli kuhusu Mungu, bali pia matumizi ya vitendo vya jinsi ya kuishi kwenye uhusiano na Mungu na katika kumtii Yeye. Wazazi hufundisha watoto wao kwa maelekezo ya maneno na mfano wa maisha yao. Kwa pamoja vyote hivi ni vya muhimu.

Kifungu hiki kinaweza kuonekana kuwa rahisi, lakini pia ni cha muhimu sana. Kweli hizi na amri hutoa madhumuni na mwelekeo kwa watu binafsi na kwa familia. Jinsi wazazi ambavyo watakuwa wanaendelea kumtafuta Mungu vizuri zaidi na kumtii kikamilifu katika mambo yote, wanakuwa wanawafundisha watoto wao kufanya kama wao wanavyofanya. Wazazi

---

<sup>11</sup> *The Woman's Study Bible*, Thomas Nelson, Inc. 1995, 292

wanapaswa kuwa na mtazamo wa maisha ya muda mrefu wa kujifunza na kutii. Huu ni mfano kwa watoto wao, na huwapa watoto kuwa na njaa kwa ajili ya Mungu.

► Je, ni njia zipi zinazofaa ambazo wazazi wanaweza kuwafunza watoto wao kila siku?

### **Uwanja wa Mafunzo ya Familia kwa ajili ya Kuwapenda Watu Wengine**

► Mwanafunzi anapaswa asome 1 Yohana 4:7-13, 19 kwa ajili ya kikundi.

Mada ya kifungu hiki ni upendo. Ili tuweze kumjua Mungu katika utajiri wake kwamba ni nani, ni lazima tupendane. Hii ni pamoja na familia zetu. Moja ya sababu ambazo Mungu ametupatia familia ni ili tujifunze jinsi ya kuwapenda watu wengine. Tunapojifunza kuonyesha upendo kwa wanafamilia wetu (hata katika wakati ambapo ni mgumu), tunafanana zaidi na Mungu – kwa sababu Mungu ni wa upendo! (Aya ya 8).

Wakati wanafamilia – aidha wawe wa kiroho au wa kimwili – wanapoonyesha kupendana, wanathibitisha kwamba wamezaliwa na Mungu (Aya ya 7). Wanapokuwa mmoja anampenda mwenzake, upendo wa Mungu unakamilishwa ndani yao (Aya ya 12).

Mungu hapendi tu tuwapende watu wengine, yeye kwanza alitupenda (Aya ya 9-11, 19). Alitupenda kwa kumtuma Yesu kuwa dhabihu kwa ajili ya dhambi zetu (Aya ya 10). Upendo wa Mungu kwetu sisi ni motisha kwa upendo wetu kwa ajili yawatu wengine (Aya ya 11).

Kupenda familia zetu kunaweza kuwa rahisi kwa wengine, na kwa wengine ikawa ni vigumu sana, lakini wote kwa pamoja tunaweza kuwa na kile tunachohitaji ili kutii maagizo ya Mungu – Mungu akikaa ndani yetu kupitia Roho Mtakatifu (Aya ya 12-13).

Mungu anatuita tupendane sisi kwa sisi, ikiwa ni pamoja na wazazi wetu, wenzi wetu, na watoto. Kuipenda familia yetu haimaanishi ni kuidhinisha ubaya au uovu. Haimaanishi kwamba hatuhitaji uwajibikaji. Inamaanisha kwamba tunataka kile ambacho ni kizuri zaidi kwa ajili ya wanafamilia wetu na kwamba kwa hiari tuko tayari kujitoa kwa ajili ya manufaa yao.

### **Kwa ajili ya Majadiliano ya Kikundi**

► Kwa maneno yako mwenyewe, elezea baadhi ya njia ambazo ndoa huakisi mahusiano yaliyoko kwenye Utatu Mtakatifu wa Mungu.

► Elezea ni kwa jinsi gani Mungu alivyoikomboa ndoa iliyokuwa imeharibiwa na dhambi.

► Toa ufafanuzi ni kwa nini maagizo ya Mungu kwenye ndoa ni ya ukombozi.

### **Maombi**

Chukua muda wa kuomba na mshukuru Mungu kwa ajili ya familia yako. Ombea familia yako. Omba kuhusu maumivu na kushindwa, sherehe na furaha. Yatafakari maneno yaliyoko katika Kumbukumbu la Torati 6:4-9, ukiyaweka kwenye maombi ya kunyenyekea na dua.

## Kazi za Kufanya

(1) Kariri akilini Kumbukumbu la Torati 6:4-9. Mwanzoni mwa kipindi cha darasa kinachofuata, andika au simulia hicho kifungu kutoka kichwani bila ya kunukuu popote.

(2) Kwenye Kumbukumbu la Torati 6:1-9, Mungu anatutaka sisi katika mambo manne. Kwa maombi na kwa uaminifu jitathmini mwenyewe katika haya maeneo manne.

Tunatakiwa tufanye yafuatayo:

- Kumpenda Bwana kwa moyo wote, kwa roho yote, na kwa nguvu zote (Aya ya 5).
- Kuyaweka maneno ya Mungu katika mioyo yetu wenyewe (Aya ya 6).
- Kuwafundisha watoto wetu kwa bidii jinsi ya kufuata Neno la Mungu (Aya ya 7).
- Kuyaweka maneno ya Mungu kwenye fahamu zetu na yawe mbele yetu mara kwa mara (Aya ya 8-9).

Andika kifungu kimoja cha maombi kwa kila kipengele. (Hutakiwi kushirikisha andiko hili kwa kiongozi wako wa darasa lakini unapaswa umpe taarifa kwamba ulishaifanya kazi hiyo.)

(3) Kutokana na maisha ya Abrahamu na Sara tunajifunza kuhusu nyakati zinazoongezeka kwa ajili ya kusubiria. Fikiria kuhusu maswali haya:

- Je, ni lini umewahi kungoja wakati wa Mungu? Umejifunza nini kutoka kwa nyakati hizi za kungoja?
- Je, ni kwa vizuri kiasi gani unaamini ahadi zilizoko kwenye Neno la Mungu? Je, kwa wakati huu unapambana na ahadi? Je, kupambana huko kunaathiri familia yako? Kwa vipi
- Je, ulishawahi kufanya jambo lolote wewe mwenyewe au kwa ajili ya familia yako bila ya kumtumainia Mungu? Matokeo yalikuwa ni nini?
- Je, ni kwa jinsi gani subira na ukosefu wa imani kwa njia hasi vimeathiri familia?

Andika jumla ya vifungu vitatu kwa ajili ya kujibu mada hii. (Hutakiwi kushirikisha andiko hili kwa kiongozi wako wa darasa lakini unapaswa umpe taarifa kwamba ulishaifanya kazi hiyo.)

# Somo la 3

## Dhana ya Biblia kuhusu Ndoa

### Malengo ya Somo

Hadi kufikia mwishoni mwa somo hili, mwanafunzi atapaswa:

- (1) Kujitoa kwa ajili ya mpango na makusudi ya Mungu kwenye ndoa.
- (2) Kujitoa kwa utii wa kibinafsi kwa kanuni za Mungu kwa ajili ya ndoa ya Kikristo.
- (3) Atakuwa amewezeshwa kwa ajili ya kufundisha watu wengine kuhusu ndoa ya kibiblia.

### Robertson McQuilkin, Mtunza Ahadi

Dr. Robertson McQuilkin alitumika kama mmishenari huko Japani kwa kipindi cha miaka 12. Baadaye akawa raisi wa Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Columbia. Alijulikana sana kama mwandishi, mzungumzaji, na mwalimu. Mkewe Muriel aliugua ugonjwa wa ubongo unaoathiri uwezo wa mtu wa kufikiri, kukumbuka na kuwasiliana. Wakati ugonjwa ulivyozidi kuendelea hadi kufikia kwenye hali ambayo Muriel alihitaji awe chini ya uangalizi wa mara kwa mara, Dr. McQuilkin alijiuzulu kutoka kwenye uraisi wa chuo ili aweze kumhudumia mke wake. Alisema kwamba alikuwa anatimiza ahadi yake waliyowekeana wakati walipooana. Aliamini kwamba kwa kutunza mke wake lilikuwa jambo la maana zaidi kuliko kuendelea kutunza nafasi ya raisi katika chuo kikuu.

### Taasisi ya Mungu ya Ndoa.

Ndoa ilisimikwa na Mungu kwa ajili ya mwanamume na mwanamke wa kwanza aliokuwa amewaumba. Ndoa iliundwa na Mungu kuwa kitu ambacho watu walihitaji. Iliundwa haswa kwa ajili ya asili ya mwanadamu. Katika kila kitu ambacho Mungu huumba na katika kila kitu anachokihitaji, kila siku anatumia kilicho chema zaidi (Kumbukumbu la Torati 6:24). Mungu alikusudia kwamba mpango wake wa ndoa umpe kila mwenzi wa ndoa hali bora ya hisia, ya kimahusiano na hali bora ya kiroho.

Mungu alisema kwamba katika ndoa mwanamume na mwanamke huachana na wazazi wao na kuungana pamoja. Ndoa huwaweka watu kwenye urafiki na uhusiano ulio na nguvu na ukaribu zaidi kuliko uhusiano wowote wa kibinadamu. Ndoa siyo tu kwa ajili ya watu wawili kwenye uhusiano mdogo. Maisha yao yameunganishwa ili kwa maana fulani wawe kama mtu mmoja. Hii haina maana kwamba haiba zao binafsi zinafutika, lakini ni umoja wa aina yake.

### Ndoa ya Kibiblia

Ndoa ya Kibiblia ni kitu kizuri sana. Lakini wanandoa wanaotaka kuona uzuri wake na kuonja wema wake lazima wachunguze kile ambacho maandiko yanafundisha kuhusiana nacho, na

kisha waendeleze utii katika kile watakachojifunza. Ndoa yenye kuridhisha inahitaji juhudi na kujitoa dhabihu.

### **Ndoa ya Kibiblia ni kwa ajili ya Ushirika**

Kitabu cha Mwanzo kinaelezea uumbaji wa Mungu wa ndoa. Kila sehemu ya maelezo inatoa heshima kwa ndoa.

Bwana Mungu akasema, Si vema huyo mtu awe peke yake, nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye” (Mwanzo 2:18).

Kama vile ambavyo Mungu ni Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu walivyo katika ushirika, Mungu alitufanya sisi tuwe jamii. Alitufanya kwa ajili ya kuwasiliana. Alituumba kwa ajili ya urafiki wa karibu sana na ushirika wa pamoja. Mungu alisema haifai mtu kuwa peke yake!

Mungu aliuchukua ubavu kutoka kwa mwanamume na kuufanya kuwa mwanamke mzuri sana, mtu mwingine – aliyeumbwa kuwa sawa na sura ya Mungu, mwenye usawa katika thamani, lakini aliye kiumbe tofauti katika kutengenezwa – ambaye alimkamilisha mwanamume. Huyo mwanamke “huletwa kwa heshima maalumu kwa mwanamume kama uumbaji wa mwisho na mkamilifu zaidi wa Muumba.”<sup>12</sup>

### **Ndoa inapaswa kuwa muungano wenye furaha.**

Wakati Adamu aliposema, “Sasa huyu ni mfupa katika mifupa yangu” (Mwanzo 2:23) alikuwa akionyesha heshima na furaha. Adamu hakusema, “Hatimaye, nimepata mtumwa! Sasa ni mtu wa kunifulia nguo, kupika chakula changu, kukanda mgongo wangu, na kufanya kazi zangu!” Hapana, Adamu alisema, “Mwishowe, nimempata msaidizi anayenikamilisha mimi!”

### **Ndoa inapaswa kuwa muungano wa wenza walio sawa.**

... msaidizi wa kufanana naye (Mwanzo 2:18).

Mungu alimuumba mwanamke wa kumfanania na kumkamilisha mwanamume.

Mathayo Henry anatukumbusha kwamba, “Mwanamke aliumbwa kutoka katika ubavu uliotoka kwa Adamu; siyo kutoka kichwani kwake kusudi amtawale, wala kutoka katika miguu yake ili kukanyagwa naye, bali nje ya ubavu wake ili awe sawa na yeye, awe chini ya mkono wake kwa ajili ya kulindwa, na awe karibu na moyo wake kwa ajili ya kupendwa.”<sup>13</sup> Mwanamke hakuwa duni wala bora zaidi kuliko mwanamume, lakini alifananishwa na yeye.

---

<sup>12</sup> Charles Ellicot, ed., *Ellicot's Commentary for English Readers*. (Maelezo katika Mwanzo 2:22). Yamepakuliwa kutoka <https://biblehub.com/genesis/2-22.htm#commentary> Desemba 29, 2020.

<sup>13</sup> Mathayo Henry, *Mathayo Henry's Commentary on the Whole Bible*. (Maelezo katika Mwanzo 2:21-25). Yamepakuliwa kutoka <https://studylight.org/commentaries/eng/mhbm/Mwanzo-2.html> Julai 31, 2023.



### ***Ndoa inapaswa iwe muungano wa agano.***

Kwa hiyo mwanamume atamwacha baba yake na mama yake naye ataambatana na mkewe, nao watakuwa mwili mmoja (Mwanzo 2:24).

Ndoa zenye nguvu hazitegemei hisia za kimapenzi za siku zote (hisia siyo za siku zote), au raha, (ingawa katika ndoa zenye afya huleta furaha), au utimilifu wa kibinafsi (ingawa katika ndoa imara huleta utimilifu). Faida nzuri za ndoa hazisababishi ndoa imara; ni matokeo ya ndoa imara. Ndoa imeanzishwa juu ya msingi usiotikisika wa agano – mume mmoja na mke mmoja wakiwa wamejitoe kipekee kila mmoja kwa mwingine kwa maisha yao yote.

Ndoa inatakiwa iwe ya wazi, ya kuaminika, na yenye uhusiano unaokubalika — “Nao walikuwa uchi wote wawili, Adamu na mkewe, wala hawakuona haya” (Mwanzo 2:25). Kwa kuwa dhambi ilikuwa bado haijaharibu kutokuwa na hatia kwa wanandoa wa kwanza, ndoa yao ilikuwa isiyo na hukumu, isiyo na aibu, na isiyo na hofu. Agano la Jipya linatueleza kwamba, “Ndoa na iheshimiwe na watu wote, na malazi yawe safi” (Waebrania 13:4).

Ndoa yenye imara haiwezi kuwepo mahali ambapo kuna ukosefu wa usalama, kutoaminiana, kutiliwa mashaka au woga, au ambapo wanandoa hawana uhakika wa kila mmoja kujitoe kwa ajili ya mwenzake katika ndoa hiyo. Ndoa imara huhitaji ahadi ambayo itaisha pale tu ambapo mwenzi mmoja atakuwa amefariki dunia (Warumi 7:1-2).

Kusudi la Mungu ni kwamba ndoa iwe ya agano la kudumu kati ya mwanamume mmoja na mwanamke mmoja (Mathayo 19:3-6). Paulo alisema kwamba waumini hawako chini ya kifungo wakati wake zao wasioamini wanapotengana nao. (1 Wakorintho 7:15), lakini mwenzi aliyeamini hapaswi kutaka kutengana na mwenzi asiyeamini (1 Wakorintho 7:12-14, 16). Hapo awali Paulo alikuwa ameandika kwamba Bwana alikuwa amesema jambo linalofanana: Watu walioamini hawapaswi kuchagua kuachana/kutengana kutoka kwa wenzi wao, lakini kama wakiamua kufanya hivyo, hawapaswi kuoa au kuolewa na mtu mwingine tena (1 Wakorintho 7:10-11, Mathayo 5:31-32, Mathayo 19:9).

Upendo wa agano ni wa kujitoe kabisa, ni wa heshima, na wenye kupendeza hata wakati ambapo uhusiano uko kwenye matatizo (1 Wakorintho 13). Ahadi dhaifu husababisha juhudi zisizo thabiti, kukosa muungano wa kihisia, kujiondoa, na majaribu.

Mume anaonyesha upendo wa agano anapokataa kukata tamaa kwa mke wake hata anapokuwa hajali, hana heshima, au anaumwa. Mke anaishi katika upendo wa agano wakati anapochagua kuheshimu na kumtii mumewe, kwa ajili ya Kristo, hata wakati ambapo mume wake hampendi.

Upendo wake unamfanya mkewe amuheshimu, na heshima yake inamfanya mumewe ampende zaidi. Kwa pamoja, wanazidi kuimarika na kukua katika uhusiano wao!

► Je, ni matatizo gani hutokea ikiwa watu watafunga ndoa huku wakiwa wanafikiria kwamba wanaweza kubadilisha maamuzi yao baadaye kama watakuwa hawana furaha na

ndoa yao? Je, kujitolea kwa ukamilifu kunaleta tofauti gani ikiwa mtu anaamini kwamba ndoa ni ya kudumu?

### **Ndoa Ya Kibiblia ni Mahali Pa Utimilifu wa Mapenzi na Kuzaa**

Mungu alifanya tendo la ndoa liwe la kufurahisha kabisa na lenye nguvu ya kipekee. Ni tendo linalokusudiwa kuleta umoja kimwili, kihisia, na kiroho. Maisha ya tendo la ndoa lenye afya siyo tu kuisimua na kuleta umoja, lakini linafanya uhusiano kunawiri. Kwa wale wanaotaka kufuata maadili ya kibiblia katika tendo la kujamiiana, tendo la ndoa ni zawadi kutoka kwa Mungu iliyotolewa kwa ajili ya kufurahia kikamilifu ndani ya ndoa.<sup>14</sup>

► Wanafunzi wanapaswa wasome 1 Wakorintho 7:1-5 na Waebrania 13:4 kwa ajili ya kikundi.

Kwenye aya za 1 Wakorintho tunaambiwa kwamba kusudi moja la ndoa ni kuridhishana katika matamano ya kujamiiana. Mume na mke kila mmoja amejitoa kwa ajili ya mwenzake na wameachana na madai yao ya umiliki wa miili yao kwamba ni mali yao wenyewe. Hiyo inamaanisha kwamba mtu aliyeko kwenye ndoa asitegemee kujihusisha na kujamiiana tu kwa wakati anaouchagua yeye lakini pia anatakiwa aweze kuitikia tamaa ya mwenzi wake wa ndoa. Mistari hiyo haifundishi kwamba mtu anaweza kulazimisha kutimiziwa mahitaji yake bila ridhaa ya mwenzi wake. Badala yake, inahimiza kila mmoja kuzingatia na kujibu mahitaji ya mwenzake kwa upendo na heshima.

Kifungu hiki kinatueleza kwamba watu walioko kwenye ndoa hawapaswi kumnyima mwenzake fadhila hii. Kipindi kifupi cha kuacha kujamiiana kukiambatana na kufunga kwa maombi ni halali, lakini utengano wa muda mrefu utasababisha majaribu kwa sababu ya matamano yasiyoridhika.

Wakati mwingine wanandoa huchagua wenyewe kutenganishwa kwa miezi kadhaa au zaidi kwa sababu mtu huenda kazini au kusoma mahali pa mbali. Kabla ya kufanya uamuzi kama huo, wanapaswa kuzingatia kama mpango wao huo unalingana na mpango wa Mungu au la. Wanaweza kupata matatizo kwa sababu ya kutengana kwao kwa muda mrefu.

Watu wengine huamua kuishi bila watoto, lakini Biblia inafundisha kwamba Mungu husherehekea wazazi wanapokuwa na watoto wanaomcha (Malaki 2:15). Ni jambo la muhimu kutambua kwamba siyo uzazi tu Mungu anaoutaka, bali watoto wanaomcha Mungu. Wazazi wameitwa na Mungu kuwafundisha watoto wao kumfuata Kristo.

---

<sup>14</sup> “Spiritual Health and Porn Addiction,” retrieved from <https://thefreedomfight.org/health/porn-addiction-and-spiritual-health/> on Julai 31, 2023.

## Ndoa ya Kikristo ni kwa ajili ya Kristo

► Wanafunzi wanapaswa wasome 1 Petro 3:1-7 na Waefeso 5:22-33 kwa ajili ya kikundi. Kikundi kitapaswa kiweke vifungu hivi wazi kwa ajili ya kuvifanyia kazi wakati wa majadiliano haya.

Katika Waefeso 5:30-32, Roho Mtakatifu wa Mungu anafunua kwa undani zaidi maana ya ndoa, iliyofichwa hadi Yesu atakapokuja. Ndoa ni kivuli cha kidunia – kuakisi – uhusiano kati ya Yesu Kristo na Kanisa.

Paulo anaanza sehemu hii kwa kuwahimiza waumini wajazwe na Roho (Waefeso 5:18). Ni katika muktadha huu ndipo anapotoa maelekezo yafuatayo kuhusiana na ndoa.

**Bibi-harusi aliyejazwa na Roho** atajinyenyekeza kwa bwana-harusi wake (“kichwa chake”) katika Bwana, kama jinsi ambavyo waumini hujinyenyekeza kwa Yesu (Waefeso 5:24, 32; ona pia 1 Petro 3:1). Hii ndiyo njia ambayo bibi-harusi anaweza kuonyesha heshima kwa Yesu na kwa mume wake. Mke anapaswa akubaliane na uongozi wa mume wake hata kama mume siyo mtu aliyeamini/aliyeokoka. Ikiwa atafanya hivyo, mume wake ambaye hajaokoka ana uwezekano mkubwa wa kuokoka.

Ni muhimu sana kwa kila mke kuwa na Bwana kwenye akili katika utii wake. Ni kwake na kwa ajili yake kwamba ananyenyekea na siyo kwa ajili ya mume wake. Jicho lake linamwangalia Yesu, ambaye peke hajawahi kuwa na makosa. Mke kujitiisha kwa hiari kwa ajili ya mume wake ni kitendo cha ibada kwa Yesu. Utii wa Kibiblia, kama vile upendo, hauwezi kuwa wa kulazimishwa (Waefeso 5:33). Utii wa Kibiblia ni zawadi ambayo wake huwapa waume zao kwa heshima kuu kama kwa Yesu.<sup>15</sup>

Kujitoa kwa mke kwa ajili ya mumewe ni tendo la heshima (Waefeso 5:33) kwake, kama sehemu ya maisha yaliojazwa na Roho (Waefeso 5:18-21). Heshima hii inayotoka katika roho ya upole na utulivu ni ya thamani sana mbele za Mungu (1 Petro 3:4).

**Bwana-harusi aliyejazwa na Roho** atampenda bibi-harusi wake kama vile Yesu alivyolipenda Kanisa lake (Waefeso 5:25). Bwana harusu ni lazima ampende mke wake kama anavyoupenda mwili wake mwenyewe (Waefeso 5:28-29). Ni lazima kujidhabihu kwa kujazwa na Roho kama vile Yesu alivyodhihirisha kwa kanisa lake wakati alipojitoa kwa ajili yake. Hiki ndicho kitendo chake cha kujisalimisha kwa Mungu (Waefeso 5:21).

Mtoa maoni mmoja aliliweka jambo hili kama ifuatavyo:

Kama Yesu alivyojitoa kufa msalabani ili kuokoa kanisa, vivyo hivyo tunapaswa kuwa tayari kujinyima na kuvumilia [kazi ngumu na matatizo], ili tuweze kuleta furaha kwa mke. Ni wajibu wa mume [kufanya kazi kwa bidii] kumuhudumia; kukidhi mahitaji yake; kujinyima raha na mapumziko, ikibidi, ili kumtunza anapokuwa

---

<sup>15</sup> Kwa ajili ya uchunguzi zaidi wa mada ya uwasilishaji wa Biblia, ona Somo la 10 la *Malezi ya Kiroho*, linalopatikana kutoka Shepherds Global Classroom.

mgonjwa; kumlinda mbele ya hatari; kumtetea anapokuwa [katika hali ya hatari]; kuvumilia tabia yake anapokuwa na hasira; kushikamana naye anapojaribu kumsukumia mbali; kuomba naye anapokuwa na matatizo ya kiroho; na kuwa tayari kufa ili kumuokoa. Kwa nini isiwe hivyo? Ikiwa watakuwa katika ajali ya meli, na kuna ubao mmoja tu wa kuokoa maisha, je, haipaswi awe tayari kumweka mke wake juu yake, na kuhakikisha usalama wake kwa gharama yoyote kwake mwenyewe? Lakini kuna zaidi... mume anapaswa kuhisi kuwa lengo kuu la maisha yake ni kutafuta wokovu wa mke wake. Anapaswa kumpatia yote anayohitaji kwa ajili ya roho yake... Na anapaswa kuwa mfano; kumpa ushauri ikiwa anahitaji ushauri; na kuifanya njia ya wokovu iwe rahisi kwake iwezekanavyo. Ikiwa mume ana Roho na kujikana nafsi kama Mwokozi, hataona dhabihu yoyote kuwa kubwa sana ikiwa inaweza kuendeleza wokovu wa familia yake.<sup>16</sup>

Bwana harusi anapaswa atafute usafi wa bibi harusi wake kama ambavyo Kristo alimtaka bibi harusi wake, yaani Kanisa (Waefeso 5:26-27).

Katika 1 Petro 3:7 panasema kwamba mume anapaswa aishi na mke wake kwa njia ya kuelewana, ikimaanisha kwamba atapaswa afanye kila linalowezekana katika kumwelewa mke wake. Anapaswa kumsoma ili aweze kuelewa mahitaji yake. Katika aya hii, mwanamke anaitwa "chombo kidhaifu." Mke anahitaji kuzingatiwa na mume wake. Anapaswa amlinde siyo tu kwenye madhara ya kimwili, lakini pia kutoka katika wasiwasi na mhemuko unaotokana na msongo wa mambo.

Mume anapaswa kutoa kila njia muhimu itakayohitajika kwa ajili ya kumstawisha mke wake; uaminifu, upendo usiokuwa na masharti, ufahamu/uelewa, ushauri, kufundisha, na huruma.

Inapotokea mume kutendea mke wake kwa upendo kama huu, atalipwa kwa furaha. Paulo anasema kwamba, "Ampendaye mkewe hujipenda mwenyewe" (Waefeso 5:28). Waume wanaowapenda wake zao kwa njia hii ya kujidhabihu watalipwa zaidi na Bwana, na uwezekano mkubwa ni kwa heshima, upendo na uaminifu wa mke wake.

► Je, ni mambo gani mahususi ambayo mume anapaswa kuyafanya ili kutoa msaada wa kiroho kwa mke wake?

Ni muhimu kukumbuka jinsi maagizo katika mistari hii yanavyotolewa. Mume hakuagizwa kutumia mamlaka kwa nguvu juu ya mke wake. Ingawa mke ameagizwa kumtii mumewe, mume hakuambiwa amfanye mkewe kumtii kwa kulazimisha.

---

<sup>16</sup> Albert Barnes, *Barnes' Notes on the Whole Bible*. (Notes on Waefeso 5:25). Retrieved from <https://studylight.org/commentaries/eng/bnb/Waefeso-5.html> on Julai 31, 2023.

Kipaumbele cha mume hakiswi kiwe ni kudumisha mamlaka yake bali kutoa utunzaji wa upendo. Kipaumbele cha mke hakiswi kiwe ni kudai matunzo kwa ajili yake mwenyewe bali kumheshimu mume wake.

Mtume Petro anamuonya mume kwamba maombi yake yatazuiliwa kama hatachukua jukumu la kumtunza mke wake inavyostahili. Kutokana na maneno ya Paulo na Petro, tunaweza kuona kwamba mume ambaye hamjali mke wake kama ambavyo ingetakiwa afanye atakuwa pia hampendi Mungu kama inavyotakiwa iwe. Mwanamke ambaye hawezi kumheshimu mume wake anakuwa pia hamheshimu Mungu kama ambavyo ingepaswa iwe.

**Tabia zetu kwenye ndoa zinaathiri uhusiano wetu na Mungu.**

### **Kudumu kwa Ndoa**

Mungu alipanga ndoa iwe kitu cha kudumu. Katika ndoa, mwanamume na mwanamke kila mmoja anatoa ahadi ya kuwa mwaminifu kwa mwenzake kwa muda wote watakaokuwa wanaishi pamoja wakiwa hai.

Biblia inarekodi maneno ya Yesu kuhusu ndoa aliyozungumza kwenye mahojiano yake na Mafarisayo.

► Mwanafunzi anapaswa asome Mathayo 19:3-8 kwa ajili ya kikundi.

Yesu alisema kwamba Mungu alikusudia ndoa iwe ya kudumu. Alisema kwamba talaka ilianzishwa kwa ajili ya watu wasiomfuata Mungu.

Kuna sababu nyingi ambazo zilimfanya Mungu apange ndoa iwe ya kudumu, na baadhi ya sababu hizo tulizizungumzia katika sehemu ya mwisho. Sababu nyingine ya ndoa kuwa ya kudumu ni kwa sababu ya watoto. Kutii mpango wa Mungu katika ndoa husababisha kuwepo na mazingira bora zaidi ya kulea watoto. Wazazi wanapomheshimu Mungu kwa Kutii kanuni zake katika ndoa na familia zao, wataweza kulea watoto wanaomcha Mungu (Malaki 2:15).

Mungu alipanga maisha ya mwanadamu kwa njia ambayo watoto huchukua miaka kadhaa ya kukua na kuwa watu wazima. Wakati wa kipindi hiki, watoto huwa ni tegemezi kwa wazazi wao kwa ajili ya ulinzi, kuwapatia mahitaji, na mafunzo. Hii ni tofauti na wanyama ambao hukua na kukomaa kwa kipindi kati ya mwaka mmoja au miwili tu. Watu wanahitaji muda zaidi ili kuweza kukuza tabia iliyokomaa. Mungu alipanga familia kama njia ya kulea watoto. Matatizo mengi katika jamii yanatokana na ukosefu wa familia zilizo na wazazi waaminifu.

Ndoa inahitaji watu kutoa ahadi ya kukabidhiana maisha yao yote. Kila tamaduni ina aina yake na sherehe ya kuonyesha kwamba ndoa ni ahadi nzito. Sherehe ni njia mojawapo ya mwanamume na mwanamke kuweza kutamka hadharani kwamba wanafanya ahadi hii ya maisha yao yote.

Serikali nyingi hutunza kumbukumbu za ndoa zilizofungwa. Sheria kuhusu ndoa zinagusa umiliki wa mali, utunzaji wa watoto, na urithi.

Huu hapa ni mfano wa viapo vya harusi ambavyo vimetumiwa katika harusi nyingi:

Mimi [...] ninakuchukua wewe kuwa [mume/mke] wangu wa ndoa, kuanzia siku hii na kuendelea, kuwa nawe na kukushikilia, kwa mema na mabaya, kwa utajiri na umasikini, katika ugonjwa na afya, kukupenda na kukuthamini, hadi kifo kitakapotutenganisha, kulingana na amri takatifu ya Mungu; na kwa hayo, najitoa kwako.

Hisia za mapenzi haziwezi kuwa za kudumu nyakati zote. Ndoa haiwezi kutegemea hisia za kibinafsi ambazo zinaweza zikabadilika. Viapo vya ndoa vinaamaanisha kwamba mwanamume na mwanamke wanaahidiana kuwa waaminifu kwa kila mmoja wao kwa muda wote ambao wote wawili watakuwa wanaishi, na kwamba ahadi hiyo haihusiani na masharti yoyote.

Kwa sababu ya kudumu kwa ndoa, wakristo hawapaswi kamwe kutoa kauli ambazo zinaonyesha kwamba wako tayari kuvunja ndoa zao kwa sababu za matatizo ya mahusiano. Mtu hatakiwi kusema, "Laiti nisingelikuoa wewe," au "Labda tuachane." Wakati mwingine, kauli hizo ni jaribio la kumshawishi mwenzi mwingine kuonyesha kwamba anajali ndoa. Mtu hufikiri kwamba mwenzi wake ataweza kujitahidi zaidi kumpendeza kwa sababu ya kauli hiyo kali, lakini mara nyingi hilo halitokei. Badala yake, mwenzi mwingine hujilinda kwa kusema, "Sawa, tunaweza kuachana kama unataka." Hivyo basi, wote wawili huonyesha kuwa wako tayari kumaliza ndoa kwa sababu ya matakwa yao binafsi, na mahusiano huwa mabaya zaidi.

- Je, kwa nini ndoa inaanza na viapo vya harusi na siyo tu tamko la upendo?
- Je, kuna mtu anataka kushirikisha jinsi ambavyo yeye ameingia kwenye ndoa akitegemea manufaa zaidi lakini bila ya kutambua kwamba dhamira ni muhimu?

### **Ndoa kama ushirika wa Kikristo**

- Mwanafunzi anapaswa asome 2 Wakorintho 6:14-18 kwenye kikundi.

Aya hizi zinatuambia kwamba kujitoa kwa muumini kunaweza kuzuiliwa ikiwa ameunganishwa kwa karibu sana na watu wasioamini. Kama vile ambavyo muumini hawezi kuabudu pamoja na mtu ambaye anamwabudu Shetani, hawezi kufuata mtindo wa maisha na vipaumbele vya watu wasioamini. Onyo hili linaweza kutumika kwenye aina kadhaa mbalimbali za mahusiano, ikiwa ni pamoja na ushirikiano wa kibiashara.

Ndoa ni uhusiano ulio wa karibu zaidi wa kibinadamu. Mtu aliyeokoka hapaswi kabisa kufikiria kuoa mtu ambaye siyo mtu aliyeokoka kwa kumaanisha (1 Wakorintho 7:39). Mtu aliyeokoka akiolewa na mtu ambaye hajaamini atapata huzuni nyingi na vikwazo vingi katika kulea watoto na hata katika kufanya maamuzi ya mfumo wa maisha.

Kama mume na mke wote wameokoka lakini wanatoka katika makanisa tofauti ya watu walioamini, lazima wahakikishe kwamba wanakuwa kwenye makubaliano kuhusiana na

masuala muhimu ya kiroho. Watatakiwa wapange kuwa sehemu ya kanisa moja la mtaa baada ya kuwa wameshaoana.

### **Njia Ambazo Wanandoa Wanaweza Kuimarisha Ndoa Yao**

#### **(1) Ni lazima washerehekee/wafurahie mpango wa Mungu wa asili wa uumbaji na kuthamini majukumu yao ya kipekee yaliyo ndani ya ndoa.**

Mume ni lazima akumbuke kwamba mke ni zawadi kutoka kwa Mungu, na ni msaidizi anayemkamilisha. Anapaswa atoe uhai wake kwa ajili ya usalama wake na kwa ajili ya hali yake ya kiroho, mihemuko, na ya kimwili.

Ni lazima achague kuwa mtu wa shukrani kwa ajili yake na kumpenda hata katika wakati ambapo yeye hastahili kabisa, akitambua wazi kwamba ni Mungu peke yake awezaye kubadilisha kile kinachotakiwa kabadilike ndani yake. Mungu ataheshimu utii na imani ya mume.

Mke anapaswa aheshimu chaguo la mume wake kuwa kichwa chake, anapaswa amheshimu katika kila njia atakayoweza. Ni lazima achague kuwa na unyenyekevu na heshima hata anapokuwa amefanya makosa na kutostahili kabisa, akiomba Mungu kwamba abadilishe kile kinachotakiwa kubadilishwa ndani yake. Mungu ataheshimu utii na imani ya mke.

#### **(2) Wanandoa waliooana ni lazima wastawishe urafiki wa karibu sana wa kiroho na kimwili.**

Ni lazima watafute kujuana wao wenyewe pasipo kuwepo na mashaka, lawama, ulinganifu na wengine, unyanyasaji, tamaa ya ubinafsi, au udhalilishaji. Ni lazima waishi katika hali ya uwazi na uadilifu mbele za Mungu na wao wenyewe.

#### **(3) Wanandoa waliooana ni lazima wafuate mfano wa neema ya Mungu wanaposhindwa kujipima.**

Wakati Adamu na Hawa walipoanguka katika dhambi na kujisikia wenye aibu na majuto, Mungu aliufunua uwezo wake kwa ajili ya kukomboa madhaifu yao. Mungu alimtoa mnyama akamfanya dhabihu na kutengeneza hapo makoti kwa ajili ya kuwafunika Adamu na Hawa wasitiri hali zao za kuwa uchi (Mwanzo 3:21). Kitendo hiki cha upendo kilichofanywa na Mungu kilikuwa ni picha ya neema na ya ahadi ya Mungu ya ukombozi kupitia Kristo. Kristo hutuwezesha sisi kusamehewa na kurejeshwa tena. Kupitia Kristo, wanandoa wanaweza kurudi katika hali ya kuwa na ukaribu bila aibu hata baada ya kushindwa.

### **Hitimisho**

Ndoa ni mpango wa Mungu wa uumbaji, na siyo wa mwanadamu. Kwa hiyo, ni lazima tumwendee Mungu kwa ajili ya maelekezo, na siyo kwenda kwa dunia au kwenye tamaduni zetu. Mungu peke yake ndiye anayejua jinsi ya kuzifanya ndoa zetu ziwe zenye nguvu, endelevu, na zenye thawabu. Lakini kamwe haitawezekana tuwe wanandoa tunaotaka tuwe pasipokuwepo na uwepo wa Roho Mtakatifu!

## **Kwa ajili ya Majadiliano ya Kikundi**

- Je, kuna ukweli gani katika ndoa ambao unaonekana kusahaulika na watu wengi?
- Elezea kanuni ambazo kanisa linapaswa kufundisha ili kuimarisha ndoa. Kuna uelewa gani ambao kipekee unakosekana kwenye mazingira yako?

## **Maombi**

Baba wa Mbinguni,

Asante kwa kutupa sisi zawadi nzuri ya ajabu ya ndoa. Asante kwa ajili ya njia nzuri uliyotumia kuiunda. Tusaidie sisi kujitoa kabisa kwa umuhimu wake kwa ajili yetu ili tuizoe ndoa katika njia ambayo uliipanga wewe.

Tusaidie katika kudhihirisha upendo ambao ni kama ule ulioko kati ya Kristo na Kanisa.

Tusaidie tuweze kwenda zaidi ya dhana za utamaduni wetu kwenye kuonyesha heshima kwa ajili ya mwingine.

Asante kwa ajili ya kazi ya Roho Mtakatifu ambaye hufanya mahusiano ya furaha na nguvu yawezekane.

Ameni

## **Kazi za Kufanya Mazoezi**

(1) Chagua kanuni mbili ambazo zilikuwa mpya kwako kutoka katika somo hili. Andika aya kwa kila kanuni ukielezea kwa maneno yako mwenyewe.

(2) Andaa wasilisho fupi kuhusiana na mada zilizoordheshwa hapa chini. (Kiongozi wa darasa atagawa mada kwa kila mwanafunzi.) Shirikisha wasilisho hili mwanzoni mwa kipindi cha darasa kitakachofuata. Mada hizo ni:

- Mpango wa Mungu wa muunganiko katika ndoa
- Madhumuni ya Biblia katika ndoa
- Majukumu yaliyotolewa na Mungu ndani ya ndoa na umuhimu wa kujazwa Roho Mtakatifu kwa ajili ya kutekeleza majukumu hayo
- Kudumu kwa ndoa

(3) Ikiwa bado hujaoa, lakini unapanga kuoa wakati ujao, andika vifungu viwili vya aya kuhusu ahadi ya kutii kanuni za Mungu kwa ajili ya ndoa yako wakati ujao. Ikiwa tayari ulishafunga ndoa, andika vifungu viwili vya aya kuhusu ahadi ya kutii kanuni za Mungu kwenye ndoa yako.



## **Heshima kwa Wanawake**

Kabla ya kuendelea na Somo la 4, darasa linapaswa **lijifunze na kujadili Kiambatanisho A**. Huu ni mjadala mfupi kwa ajili ya heshima kwa wanawake, na ni mada muhimu sana inayohusiana na ndoa na familia.



## Somo la 4

### Masuala ya Kujamiiana

#### Malengo ya Somo

Hadi kufikia mwishoni mwa somo hili, mwanafunzi atapaswa:

- (1) Aweze kuelezea ni kwa jinsi gani Anguko liliweza kuathiri asili ya mwanadamu na matamano ya kujamiiana.
- (2) Aweze kufafanua kuhusu utambulisho binafsi na jinsi unavyohusiana na maadili ya kibinafsi.
- (3) Kumbatia mtazamo wa kibiblia kuhusu uasili wa jinsia ya binadamu na kuepuka uasherati.
- (4) Kutafuta uhuru wa kutoka katika dhambi na kupata ushindi wakati wa majaribu ya uasherati.
- (5) Kuwa mtumishi uliyetayarishwa kuhudumia wengine wanaohitaji msaada na ushindi.

#### Christopher Yuan

Christopher alikulia kwenye familia moja ya Kiasia-Kimarekani nchini Marekani. Tangu wakati alipokuwa bado kijana mpevu alikuwa anavutiwa zaidi na wanaume kuliko wanawake. Wazazi wake walishtuka na kuona aibu kutokana na shauku ya kijana wao. Akiwa kijana mdogo alikuwa kwenye mfululizo wa mahusiano na wanaume. Alikuwa anategemea kupata upendo wa kweli na uwajibikaji, lakini kila uhusiano hatimaye ulishindwa. Kwa uzembe alianza kuwa na mahusiano yasiyo ya maadili na wanaume wengi. Alianza kuwa na mahusiano mabovu na wanaume wengi. Kila kitu kilianza kubadilika kwa Christopher wakati mama yake alipookoka na kumpa upendo na kukubalika ambapo alikuwa hajawahi kupata hapo nyuma. Alianza kutambua kwamba utambulisho wake wa msingi ni wa mtu aliye kwenye sura ya Mungu. Alitubu na kuwasilisha vipengele vyake vyote vya maisha yake kwa Mungu. Alipata ukamilifu na kusudio lake kwenye uhusiano wake na Mungu.

#### Asili ya Kibinadamu Iliyoanguka na Matamano ya Dhambi

Wakati Mungu alipomuumba Adamu na Hawa, aliwafanya watu walio wakamilifu katika maeneo yote, bila ya kasoro au mapungufu (Mwanzo 1:31). Asili zao zilitamani kile ambacho kilikuwa ni sahihi na kizuri. Fahamu zao na akili zao vyote vilifanya kazi kwa usahihi. Kisha Adamu akaamua kutokutii maagizo ya Mungu. Alipofanya hivyo, asili yake ya mwanadamu iliharibika (Warumi 8:20-23). Miili na akili za kibinadamu zilidhurika. Hata mtu mwenye afya

njema sana na akili nyingi hudhuriwa na matokeo ya dhambi. Dhambi iliharibu kabisa kile ambacho kilikuwa kikamilifu hadi hapo Kristo atakaporudi (1 Wakorintho 15).

Kwa uharibifu ambao umeshafanyika kwenye asili yetu ya ubinadamu na miili yetu ya asili, tusitegemee kwamba matamano yetu ya asili ya miili yetu siku zote yatakuwa sahihi. Ukweli ni kwamba tamaa zetu nyingi haziko sawa. Kwa kawaida watu hutamani yale mambo yaliyo mabaya. Yesu aliiona hali hiyo ya asili ya dhambi ya ubinadamu wakati alipoorodhesha aina zote za dhambi zinazotoka moyoni (Marko 7:21-22).

Katika somo hili tunazungumzia kuhusu masuala ya kujamiana. Kati ya matamano yote ya binadamu, matamano ya ngono yanaweza yakawa ndiyo yenye nguvu sana kuliko mengine yote.

Matamano mabaya ya ngono huonekana ni jambo la kawaida kwa yule mtu anayejisikia. Anaweza akafikiri kwamba hapaswi kulaumiwa kwa ajili ya kuwa kwenye matamano yake. Hata hivyo, kila mtu anapaswa ajizuie na mwelekeo wake wa asili kwa ajili ya kuweza kufanya yaliyo sahihi. Mtu anaweza kuwa na mwelekeo wa asili wa kusema uongo au kuiba, au kuwa mwenye vurugu, mvivu, au asiye kuwa na subira. Watu hawapaswi kuwajibika kwa wao kuzaliwa katika hali hiyo ya ukasoro, lakini watu wanakuwa ni wenye hatia wakati wanapoingia kwenye matamano ya asili na kutenda dhambi.

Wakati mwingine unyanyasaji wa utotoni au hali zingine za kimazingira husababisha mtu apambane na misukumo ya ushoga au tamaa zingine mbaya za ngono. Hata hivyo, tamaa mbaya za ngono hazipaswi zionekane ni tofauti na matamano mengine yanayosababisha mtu kutenda dhambi. Mtu anahitaji neema inayofanana kwa ajili ya ukombozi na utakaso kutoka kwa Mungu, kwa sababu zozote zile ambazo zilikusika.

Ukweli kwamba matamano mabaya kwa watu wengine hujisikia ni jambo la kawaida hapaswi kuwa ni jambo la kushangaza. Dhambi kwa ujumla huonekana ni ya kawaida na ya asili kwa yule mtu ambaye ana uzoefu wa tamaa kwa ajili ya kutenda dhambi.

Sisi kwa asili ni watoto wa tabia ya hasira (Waefeso 2:3). Hii inamaanisha kwamba kwa asili sisi ni watu wa mwelekeo wa kutenda dhambi, na tunajileta wenyewe kwenye hukumu kwa kutenda dhambi ambazo ni za asili kwetu. Ukweli kwamba mtu amezaliwa akiwa na mwelekeo fulani wa dhambi haimaanishi kwamba inapaswa ifuatwe, hata kama itaonekana kwamba ni jambo la kawaida kwake.

► Kwa nini hatupaswi kutii tamaa zetu zote za asili?

Biblia inatupa maelezo kwamba sisi tumeitwa ili tufananishwe na mfano wa Kristo (Warumi 8:29). Tunapaswa tumvae Bwana wetu Yesu Kristo. Matamano yetu ya kimwili hayapaswi yawe ndiyo msingi wa maisha, badala yake tunapaswa tuipeleke misukumo isiyokuwa sahihi kwenye mamlaka ya Mungu (Warumi 13:14).

► Je, inaonekanaje kupeleka misukumo yetu isiyokuwa sahihi kwenye mamlaka ya Mungu?

Matamano yako ya ngono yanapaswa yapelekwe kwenye kusudio lako kuu, yaani, kumtukuza Mungu kwa kuonyesha sura ya Mungu. Maisha ya kumfuata Kristo ni maisha ambayo yanaendana na sura ya Mungu uliyo nayo.

## **Utambulisho wa Mwanadamu**

### **Uelewa ulio sahihi wa Utambulisho wa Mwanadamu**

Watu wengine huamini kimakosa kwamba asili yao ya kibinadamu inaweza ikaaminika katika kuwapeleka kwenye njia sahihi. Inaonekana kwao kuwa ni jambo lenye mantiki kwamba matamano ambayo yanatoka kwenye asili yao wenyewe yanapaswa yawaongoze kwenye utoshelevu. Hawatambui kwamba asili yao haiwezi ikaaminika kwa sababu imeharibiwa na dhambi. Matamano ya mtu binafsi hayatamwongoza kwenye utoshelevu kwa sababu matamano yake hayo yamevurugwa. Wala matamano ya asili ya mtu, mbali na Mungu, hayawezi kumwongoza kufanya mambo ambayo kimaadili ni sahihi.

Watu wanaamini kwamba wanapaswa kufuata matamano na mihemuko yao wenyewe katika kutengeneza kusudi lao wenyewe kwa ajili ya maisha. Wanaamini ni muhimu kabisa kuwa na utambulisho binafsi ambao haujafafanuliwa au kuwekewa mipaka na mamlaka yeyote ile au matakwa ya kimaadili. Wanafikiri kwamba watu binafsi wanapaswa kuamua ni mambo gani yanayowafaa na yenye thamani kwa ajili yao wenyewe. Huwa hawataki taasisi au masharti ambayo yanaweka ukomo wa tabia zao. Asili potofu ya mwanadamu inafanyika kuwa ndiyo kipimo cha maadili badala ya Neno la Mungu.

Kwa kuwa kujamiiana ndiyo sehemu yenye nguvu sana ya asili ya mwanadamu, watu wengi huchukulia matamano ya ngono kuwa ndiyo kiini cha utambulisho wao. Wanafikiri kwamba ni lazima wafuate matamano yao ya ngono ili wajione kwamba wao ndiyo wenyewe. Watu hufikiri kwamba kujamiiana siyo kile tu wanachotaka au kufanya, bali kwamba wao ni nani. Wanafanya hivyo kuwa ndiyo utambulisho wao.

Tofauti na jinsi ulimwengu unavyofikiri, **Biblia inatueleza kwamba sisi tumeumbwa katika sura ya Mungu, na tumeundwa kwa kusudi la kuwa na uhusiano na Mungu. Huu ndiyo utambulisho wetu wa kweli kama wanadamu.**

Hakuna kitu chochote katika uwepo wetu duniani ambacho kinaweza kutupa ukomo wa utambulisho wetu wa kweli. Sifa za kuwepo kwetu duniani kwa kawaida ndizo hali tulizo nazo hapa duniani kwa sasa. Hazitufanyi tuwe sisi ni nani. Ukabila wetu, hadhi ya kijamii, au hadhi ya kiuchumi siyo **utambulisho** wetu, bali ndiyo **hali** yetu. Mtu anaweza akawa daktari, nyota wa kuonyesha burudani, au kiongozi wa kitaifa, lakini mtu huyo anasimama mbele za Mungu kama kiumbe wa Mungu aliyeumbwa katika sura ya Mungu, na kwamba utambulisho huo ndio ulio muhimu na wa maana zaidi.

Ujinsia wetu ni sehemu yenye nguvu sana ya hali yetu. Tunayo mielekeo ya ngono, matamano, na mambo ya kukatisha tamaa. Lakini mambo hayo yote siyo utambulisho wetu; ni sehemu tu ya hali zetu.

Tumezaliwa na asili ya dhambi kwa sababu dhambi ya Adamu ilimtenganisha mwanadamu na Mungu (Warumi 5:18). Lakini hata utendaji wetu wa dhambi siyo utambulisho wetu; ni hali yetu, na inaweza ikabadilishwa kwa neema na nguvu za Mungu (Warumi 5:19).

► Kuna tofauti gani kati ya *utambulisho* wa mtu na *hali* ya mtu?

### **Utambulisho wa Binadamu na Maadili Binafsi**

Utambulisho ni muhimu kwa sababu mtu huweka maadili yake juu ya utambulisho wake. Maadili ni kanuni ambayo inatambulisha tabia kama ni njema au na mbaya. Kama mtu atakuwa anafikiri kwamba ujinsia wake ndiyo utambulisho wake, basi ataamini kuwa ni sawa kufuata mielekeo yake ya kijinsia.

Wakati mwingine mtu husema, "Nilizaliwa hivi; ni jambo la kawaida kwa mimi kufanya hivi, siyo vibaya kwangu." Lakini Biblia inafundisha kwamba wote kabisa tulizaliwa katika hali ya dhambi (Warumi 5:12, Waefeso 2:3). Siyo jambo sahihi kwetu sisi kufuata asili yetu ya dhambi kwa sababu tu inaonekana kwamba ni asili yetu.

Asili yetu ya dhambi si utambulisho wetu. Asili yetu ya dhambi si sisi ni nani. Asili yetu ya dhambi ni hali yetu. Ujinsia wetu siyo utambulisho wetu. Badala yake, watu walioumbwa katika sura ya Mungu ndiyo utambulisho wetu. Kama tutaukiri ukweli huu, tutatambua kwamba Mungu huamua ni jambo gani lililo jema na lililo mbaya, na kwamba sisi tunawajibika kwake. Utambulisho wetu unatusaidia sisi kuelewa kiwango kilicho sahihi cha tabia takatifu.

► Je, ni kwa jinsi gani uelewa wa mtu kuhusiana na utambulisho wake unavyogusa maadili yake?

### **Uelewa Sahihi wa Jinsi**

Sisi tunafahamu ukweli kwamba wanadamu na wanyama wengi wametenganishwa kwenye dume na jike. Tunaweza tukahisia kwamba Mungu ni mwanamume au mwanamke, lakini hilo litakuwa ni makosa. Mungu ni kiumbe ambaye yuko kwenye asili iliyo kubwa kuliko jinsi, ambaye alikuwa yupo kabla ya jinsi kuwepo. Jinsi zote mbili za wanadamu zilitokana na sura ya Mungu (Mwanzo 1:27). Jinsi zote mbili za wanadamu ni udhihirisho wa sura ya Mungu.

Sura ya Mungu siyo tu kitu ambacho kimejumuishwa kama sehemu ya asili ya mwanadamu. Sura ya Mungu siyo tu silika fulani tulizopewa sisi kama vile uwezo wa kupenda, kuthamini uzuri, na uelewa wa mema na mabaya. Asili yote ya mwanadamu ni kielelezo cha sura ya Mungu.

Hakuna kitu chochote isipokuwa sura ya Mungu ambacho kinaweza kuchukuliwa maanani kwamba ndicho kiini cha uwepo wetu. Kimsingi sisi ni viumbe tulio katika sura ya Mungu. Hakuna maelezo ya kina kuhusiana na hali yetu ya kibinadamu yanayoweza kukubalika yawe ndiyo utambulisho wetu wa msingi au msingi thabiti wa maadili yetu.

Chaguo la Mungu la jinsi kwa ajili ya kila mtu ni sehemu ya mpango wake wa jinsi ambavyo mtu huyo atakavyoweza kuonyesha sura ya Mungu. Baadhi ya watu wanakataa kukubaliana na jinsi ambayo Mungu aliwapa. Wanaweza hata kujaribu kuishi kama mtu wa jinsi iliyo tofauti na jinsi yake. Baadhi ya watu hujaribu hata kubadilisha miili yao kwa njia ya upasuaji. Huu ni uharibifu mkubwa na kusikitisha wa uumbaji wa Mungu, kwa sababu kusema kweli mtu hawezi akabadilisha jinsi kwa kuubadilisha mwili wa asili. Kila mtu ni mwanamume au mwanamke kwenye maeneo yote ya asili ya mtu – na siyo tu kimwili. Mungu anatutaka sisi tumtukuze yeye na tuakisi sura yake tukiwa kwenye jinsi aliyotupa kila mmoja wetu.

### **Kiwango cha Mungu kuhusu Maadili**

► Mwanafunzi anapaswa asome Waebrania 13:4 kwa ajili ya kikundi.

Aya hii inatueleza kwamba ndoa inapaswa iheshimike katika kiwango cha hali ya juu sana. Dhambi ya kufanya ngono ni kuivunja heshima ndoa. Mungu atahukumu uasherati.

► Mwanafunzi anapaswa asome 1 Wakorintho 6:18 kwa ajili ya kikundi.

Dhambi za kingono zinajumuisha mawazo ya tamaa, uasherati, uzinzi, kujamiana na wanandugu, ubakaji, unyanyasaji wa kingono kwa watoto, shughuli za ushoga, na matumizi ya picha au video za ngono.

- **Mawazo yenye tamaa:** Kupenda kuwazia mawazo ya tamaa na mtu yeyote ambaye siyo mwenzi wako.
- **Uasherati:** Kufanya ngono kunakohusisha watu ambao hawajaolewa.
- **Uzinzi:** Kufanya ngono kunakohusisha mtu ambaye tayari yuko kwenye ndoa na mtu mwingine.
- **Kujamiiana na wanandugu:** Kufanya ngono na mtu wa karibu wa familia ambaye siyo mwenzi wako.
- **Vitendo vya ubakaji:** Unyanyasaji wa kijinsia, kulazimishwa mtu kufanya ngono kwa nguvu bila ya hiari yake.
- **Unyanyasaji wa kingono kwa watoto:** Kufanya ngono kunakohusisha mtu ambaye bado hajafikia umri wa mtu mzima wa kuweza kuamua kufanya kwa hiari tendo la ndoa na/au ambaye bado hajaweza kuwa na matamano ya kufanya ngono.
- **Shughuli za ushoga:** Kufanya ngono kunakohusisha watu wenye jinsi moja.
- **Matumizi ya picha za au video vya ngono:** Kuandika, matumizi ya picha na video zenye maudhui ya kuamsha hisia za kufanya ngono kwa kuonyesha watu wakiwa uchi au wakifanya tendo la ngono.

Yote haya kwa pamoja ni ukiukwaji wa uhusiano wa ndoa.

Kumbuka—kila njaa inayotuvutia katika mwili ni unyonyaji wa hitaji ambalo linaweza kutimizwa vyema na Mungu. Mukadha pekee wa kimungu katika kujamiiana ni kujamiiana kwa watu walioko kwenye ndoa. Ngono haramu ni... tamu mara moja, lakini ni kitu kitakachotia sumu katika hamu yetu ya kiroho hadi tutamani kile ambacho mwisho wake kitatungamiza sisi. Ngono haramu haitatufanyia jambo lolote zaidi ya kutubomolea usikivu wetu dhidi ya utakatifu, haki, na uwepo wa Mungu kwenye maisha yetu.<sup>17</sup>

Katika vifungu vingi, kitabu cha Mithali kinaonya kwamba uasherati hugaribu maisha ya mtu na husababisha kifo (Kwa mfano: Mithali 2:16-19 na Mithali 6:24-29, 32-33).

Robertson McQuilkin anaandika kwamba:

[Makusudi ya Mungu kwa ajili ya kujamiiana kwa mwanadamu] kiakili yanakiukwa kwa kiasi kikubwa sana kuliko hata ambavyo lingetendeka tendo lenyewe. Mungu hakumuumba tu mwanamume na mwanamke; aliwaumba kwa ajili ya kila mmoja kuwa mwandani wa mwingine, kuwa katika dhamana ya maisha ya ndoa, na umoja unaofanania asili yake yeye mwenyewe. Ili kusudi hili la juu liweze kukamilishwa, hali ya kuwa mwandani ni lazima iwe ya kipekee na kujitoa kwa kudumu au vinginevyo haitakuwa umoja. Uaminifu ni wa muhimu zaidi katika akili. Mwandani ulio wa kipekee, kujitoa kwa kudumu, na uaminifu wa mmoja kwa mwingine unakiukwa kwanza kutokea kwenye akili.<sup>18</sup>

► Wanafunzi wanapaswa wasome 1 Wakorintho 6:9-11, 15-20 and Mathayo 5:27-30 kwa ajili ya kikundi.

Kila jamii ina mitazamo ya kitamaduni ya uhusiano kati ya wanaume na wanawake. Mitazamo hii ya kitamaduni ni ya viwango vya chini sana kuliko viwango vya maadili ya kibiblia. Tamaduni nyingi zina desturi nyingi tu kwa ajili ya kudumisha jamii yenye utaratibu. Wanavumilia dhambi ya kujamiiana kama inasimamiwa kwa uangalifu mkubwa ili kuzuia matokeo mabaya au kashfa. Kiwango cha kibiblia kuhusu maadili ni tofauti.

Kwa masikitiko, baadhi ya makanisa hufuata maadili ya tamaduni za jamii zao badala ya maadili yaliyoko kwenye Biblia. Wanawaadhibu watu ambao dhambi zao zimekuwa za dhahiri na za uzembe, lakini wanawavumilia watu ambao wanafanya dhambi zinazofanana na hizo na walio waangalifu zaidi katika kuficha dhambi yao au wanaodhibiti matokeo yake.

Aya hizi zinatueleza kwamba watu ambao wanatenda dhambi hizi siyo waumini na hawataingia mbinguni. Baadhi ya waumini wa Korintho walikuwa wametenda dhambi hizi katika siku za nyuma lakini walikuwa wamekombolewa dhidi ya hizo dhambi.

---

<sup>17</sup> Gary Thomas, *Sacred Marriage* (Grand Rapids, MI: Zondervan, 2000), 210.

<sup>18</sup> Robertson McQuilkin, *An Introduction to Biblical Ethics*, 2nd ed. (Wheaton, IL: Tyndale House Publishers, Inc., 1995), 216.



Fundisho lolote la kiimani linalofumbia macho dhambi hizi kwa mtu ambaye alishakiri kwamba ameokoka ni fundisho potofu. Kama mtu atajinadi kwamba ni mfuasi wa Kristo na bado anaendelea kufanya dhambi ya uzinzi, kwa mujibu wa maandiko, kanisa linatakiwa limwondoe mtu huyo katika kanisa na wasimchukulie kama mtu aliyeamini (1 Wakorintho 5:11-13).

Viongozi wa makanisa wanapaswa waweke mfano mzuri wa tabia. Wakati kanisa linaporuhusu viongozi wa kuongoza ibada wavae mavazi yasiyo na staha au wanaporuhusu aina za ngoma za hisia za mahaba kanisani, wanamaanisha kwamba tamaa mbaya za kingono ni za kawaida. Wanamaanisha kwamba dhambi ya kingono si jambo kubwa.

Mifumo ya uvaaji kwenye jamii inadokeza kwamba mtu anakuwa hajavaa vizuri kama atakuwa hajaonyesha maumbile yake ya kimwili ili kuleta mvuto wa kufanya ngono. Washirika wa kanisa wakati mwingine huangukia katika kosa hili, hasa kwenye matukio maalumu. Wanafikiri hawajavaa vizuri isipokuwa kama wanafuata mitindo ya jamii yao. Kanisa ni lazima lifundishwe kwamba kufanya hivyo ni makosa. Mtu aliyeokoka hapaswi kabisa kusababisha matamano mabaya kwa watu wengine. Katika 1 Timotheo 2:9-10 tunaelezwa kwamba watu waliokoka wanapaswa kuvaa na kutenda kwa namna ambayo mtu yeyote atakayekuwa anawaangalia atajua kwamba wanaishi maisha ya uangalifu, yenye usafi na wasiokuwa tayari kutenda dhambi au kuwashawishi watu wengine kutenda dhambi.

## **Ponografia**

Maana yake ni kuandika, kutumia matumizi ya picha na video zenye maudhui ya kuamsha hisia za kufanya ngono kwa kuonyesha watu wakiwa uchi au wakifanya tendo la ngono.

Mtandao unaifanya hivi kupatikana kwa urahisi duniani kote. Wachungaji na viongozi wa zamani hawakukutana na majaribu haya kwa sababu mitandao ilikuwa bado haijakuwepo wakati wa ujana wao. Wanaweza hata wasielewe yale ambayo kizazi kipya kinapitia. Lakini watu ni lazima wafundishwe kutumia kanuni za Kibiblia kwenye kuchagua mambo ya burudani.

**Ponografia ni mbaya** kwa sababu imekusudiwa kumfanya mtu awaze matendo ya uasherati, uzinzi, na aina nyingi upotovu wa kingono. Ni kivutio kwa mtu ambaye ana matamano ya kutenda dhambi. Ponografia hualika na kumwezesha mtu kushiriki matendo yasiyokuwa ya kimaadili ambayo Mungu anayashutumu. Yesu alisema kwamba kuchagua kufikiria mambo haya ni dhambi (Mathayo 5:28).

**Ponografia pia ni mbaya** kwa sababu inashusha thamani ya watu na mahusiano. Inapunguza tendo la kujamiiana kuwa shughuli ya ubinafsi. Inawatendea watu kama vitu vya kutumia kwa ajili kujifurahisha binafsi badala ya kuwathamini watu kama walioumbwa kwa sura ya Mungu, na walioundwa kwa mahusiano yenye afya.

**Ponografia inaleta uraibu.** Ponografia, kwa ujumla kama dhambi, ni utumwa (Yohana 8:24, 2 Petro 2:19). Mtu anayetumia ponografia anajisikia sana kuwa na hitaji kubwa kwa

ajili yake. Hawezi kufikiria kuishi bila hiyo. Inaonekana kwake kwamba maisha yatakuwa matupu na yasiyokuwa na hamu bila ya kupata mambo ya kufikirika anayoyapata kutoka kwenye Ponografia. Kama uraibu mwingine wowote ulivyo, tamaa inakuwa ya kuteketeza, na mtumiaji huanza kudhabihu vitu vingine vizuri katika maisha yake.

**Ponografia inakua hatua kwa hatua.** Mtumiaji anaanza kuhitaji vifaa ambavyo ni vya wazi zaidi na vimepotoshwa. Ataanza kufurahishwa na mawazo ambayo hapo mwanzoni yangemchukiza na kumletea hofu.

**Ponografia ina madhara.** Mtumiaji anakuwa na uwezo mdogo wa kufurahia tendo la uhusiano wa kawaida. Tamaa zake zinakuwa siyo za asili kiasi kwamba haziwezi kutoshelezwa tena. Anakuwa wa kupuuzia mateso ya wengine na yuko tayari wengine wateseke kwa ajili ya starehe yake.

### **Baadhi ya Madhara ya Ponografia**

Kufikiria vitendo vinavyoonyeshwa kwenye ponografia huathiri akili na miili ya watumiaji kana kwamba kimwili walikuwa wanafanya vitendo hivyo wao wenyewe.

"Shetani anataka 'kuiba, kuua na kuharibu' (Yohana 10:10) furaha yako ya kingono, na ponografia ni silaha yake kuu. Ponografia inaahidi kukuridhisha kingono, lakini kwa kweli inakupokonya uwezo wa kufurahia jambo halisi."

- The Freedom Fight

Ponografia huwakilisha hali zisizo za kweli zinazosababisha ubongo kuwa na majibu ya furaha yenye nguvu zaidi kuliko ambavyo ingeweza ikawa kwenye tendo halisi la asili la kujamiiana.<sup>19</sup> Ubongo hujitengeneza ili kuendana na kiwango hiki cha juu kisicho cha kawaida cha kemikali za kufurahisha. Kwa sababu hiyo ubongo huendelea kudai kiasi kikubwa zaidi cha ponografia na ponografia iliyopotoka zaidi ili mtazamaji aendelee kupata raha. Mabadiliko ya kemikali kwenye ubongo yanaweza hatimaye kumfanya mtu kushindwa kabisa kuwa na au kufurahia uzoefu wa kawaida wa kingono katika maisha halisi. Sehemu ya ubongo inayotuwezesha kufanya maamuzi pia huharibika kutokana na uwepo wa kiwango kikubwa cha kemikali ya raha.

Mungu alikusudia uzoefu wa kingono kuwa wa kuunganisha katika mahusiano. Homoni inayotolewa kwenye ubongo wakati wa tendo la ndoa huunganisha kihisia washiriki, na kuimarisha uhusiano wao. Hili ni zawadi nzuri ndani ya ndoa. Hata hivyo, kutazama ponografia humunganisha kihisia mtazamaji na ponografia yenyewe.

Hatia na aibu ya kutumia ponografia huwatenga watu, kuwazuia wasiweze kuunganishwa tena na watu wengine kwenye mahusiano yenye nguvu. Pia huharibu uaminifu ulioko kwenye uhusiano wa ndoa.

---

<sup>19</sup> Taarifa yote iliyoko kwenye kifungu hiki na vifungu vinne vinavyofuata vimenukuliwa kutoka mtandaoni <https://thefreedomfight.org>, chanzo cha Biblia kilichopendekezwa kwa ajili ya wale wanaotaka kuwekwa huru na kutolewa kwenye kifungu cha matumizi ya ponografia..

Kwa kuwa husababisha uwiano usiokuwa sawa kwenye ubongo, utumiaji wa ponografia unaweza kusababisha mfadhaiko wa akili kwa mtazamaji.

Mambo yanayoonyeshwa kwenye ponografia wakati mwingine husababisha vurugu na unyanyasaji katika maisha halisi ya mahusiano ya ndoa.

Wachungaji na wazazi wanapaswa kuwaonya vijana wao juu ya hatari ya kushiriki ponografia. Wazazi hawapaswi kuwapa watoto ufikiaji usiozuilika kwenye mtandao wakati wanapokuwa hawajakomaa kuweza kuzuia majaribu. Mtu yeyote anayepambana na jaribu la kuzuia matumizi ya ponografia anapaswa mara kwa mara atoe taarifa ya ushindi au kushindwa, kwa mtu wa kimungu na anayeaminika. Uchunguzi wa mara kwa mara utakaofanywa na muumini aliyekomaa unaweza ukasaidia sana kudumisha kujitolea kwa usafi na kupata uthabiti wa ushindi.

► Je, ni mazoea gani unayopaswa kupendekeza kwa watu wengine ili kuwasaidia katika kuwazuia kutokana na hali hii yenye kuzoesha tabia mbaya kutokana na ponografia? Je, kanisa linawezaje kusaidia?

### **Udhalilishaji wa Watoto / Ubakaji**

Udhalilishaji wa watoto/ubakaji ni kufanya tendo la kujamiiana kwa makusudi. Ni upotofu wa ngono unaofanywa kinyume na matakwa ya mtu. Ni tendo la uovu kwa sababu nyingi, ikiwa ni pamoja na:

- Linapingana na makusudi ya mungu yaliyo mema kwa ajili ya kujamiiana ndani ya ndoa ya ahadi (Waebrania 13:4).
- Linaiba hali ya mtoto ya kutokuwa na hatia – kwa kuwa sasa mtoto anajikuta amekuwa na uzoefu wa mambo ambayo bado hakutakiwa kuyajua.
- Linamnyang'anya mtoto ubikira wake (1 Wathesalonike 4:3-7).
- Linampa mtoto hisia ya uwongo ya kuwa ana hatia; mtoto anajikuta yuko kwenye tendo baya, lakini hana uwezo au haruhusiwi kufanya chaguo halisi.
- Linasababisha mtoto kufanya maamuzi yanayohusu kujamiiana ambayo bado hana ukomavu nayo wa kuyafanya.
- Hufanya watoto kuwa kwenye uwezekano mkubwa wa kuchagua tabia zisizokuwa na maadili kwa siku za baadaye kwa sababu wanajihisi wachafu na wasio na thamani (Mathayo 18:6).
- Linaongeza jaribu kwa mtoto la kujihusisha katika tabia na au shughuli zilizo chafu kwa siku za baadaye.
- Linawadhulumu wale ambao wako kwenye mazingira hatarishi na ambao hawawezi kujitetea wenyewe.

- Linamjeruhi mtu aliyefanywa kwa sura ya Mungu, ambaye ana thamani isiyokuwa na kikomo (Mwanzo 1:27).

Udhalilishahi au ubakaji wa mtoto wakati mwingine hufanyika ndani ya familia na miongoni mwa marafiki. Inawezekana kusiwepo na kushukiwa kuwepo kwa hali hiyo kwa sababu wanafamilia na marafiki wanaofanya hayo wanaaminika, na mtoto anakuwa anaogopa kumwambia mtu yeyote kuhusu kile ambacho kimetendeka kwake.

Ubakaji ni kulazimishwa mtu kimwili (aidha mtoto au mtu mzima) kufanya tendo la ngono pasipokuwepo na ridhaa yake. Ubakaji ni uovu kwa sababu nyingi zinazofanana kwamba udhalilishaji wa mtoto ni uovu (Kumbukumbu la Torati 22:25-27).

Aina nyingine ya unyanyasaji wa kijinsia ni usafirishaji wa watu kwa ajili ya biashara ya ngono. Duniani kote, watoto na vijana wanatekwa nyara na watu wasiojulikana, au kuuzwa na wanafamilia na wanaenda kutumika kwa ajili ya kufanya ukahaba au kwa ajili ya kutengeneza ponografia. Familia zilizo katika hali ya umaskini wakati mwingine zinashindwa kuwalinda watoto wao kutokana na biashara hii chafu kwa kuwa wanajihisi kutamani sana kupata fedha. Mtu fulani anapata faida, lakini watoto siyo tu kwamba wanaumizwa kimwili lakini pia wanadhurika vibaya sana kiakili na kihisia. Huu ni ugandamizaji wa dhambi kwa watu maskini na walioko hatarini na kwamba Mungu lazima atahukumu (Mithali 14:31).

Dhambi hizi zilizo kinyume cha watoto zinavunja moyo wa Mungu (Mathayo 18:10-14, Zaburi 146:7-9). Wale wote wanaotenda dhambi hizi hawataponyoka pasipo kupata adhabu ya Mungu (1 Wathesalonike 4:6, Ezekieli 7:8-9). Watu waliookoka wanapaswa kushiriki upendo na huruma ya moyo wa Mungu na kufanya kazi ya kutetea, kuokoa, na kuwaponya wale wote ambao wameingizwa kwenye utumwa (Mithali 24:11-12, Ayubu 29:12-16, Zaburi 72:12-14).

### **Ngono - Binafsi**

Kupiga punyeto ni kitendo kinachohamasisha viungo vya uzazi vya mtu kwa ajili ya kuamsha hisia na furaha ya ngono au kuondoa fadhaa ya ngono.

Biblia haina hukumu mahususi ya hatia kuhusu kupiga punyeto kama ni ukosefu wa maadili. Walakini, ngono binafsi inaweza kuwa chanzo cha kusababisha mawazo ya kutamani, matumizi ya ponografia, na uasherati, ambayo yote ni matendo ya dhambi (Mathayo 5:27-28, Mathayo 15:19-20).

Kupiga punyeto pia siyo tendo la busara kwa sababu ni lenye kuzoesha tabia mbaya inayomtawala mtu: jinsi unavyoendelea kufanya ndivyo unavyojihisi kwamba unapaswa kuendelea kufanya.

Kupiga punyeto kwa kulazimishwa wakati mwingine huelekeza kwenye suala la ndani zaidi, kama vile matatizo ya hisia au uhusiano, au unyanyasaji wa kijinsia.

► Wanafunzi wanapaswa wasome 1 Wakorintho 6:12-13, 18-20 na 1 Wathesalonike 4:1-8 kwa ajili ya kikundi.

Mungu alipanga umoja wa kimwili katika ndoa kwa ajili ya kusaidia kumuunganisha mwanamume na mwanamke kihisia na kiroho (1 Wakorintho 6:16-20, Malaki 2:15).

Watu wengi...wanadhania kwamba kupiga punyeto kunaweza kukasaidia kushughulikia hali ya kuwa kapera hadi pale watakapokuwa wameanza kuoa. Wanashindwa kuelewa hata hivyo, kwamba hilo zoezi linapofanyika kuwa ni la mazoea, linaweza likatishia uzuri na ufanyaji wa ngono ya ndoa katika siku zijazo.

Ngono ya kibinafsi huleta uzoefu wa kufanya ngono ambao unakuwa umekosa kusudi muhimu la ngono: kuunganishwa kwa watu wawili kuwa mwili mmoja, kimwili na kihisia... Kupiga punyeto hakupaswi kutumike kama ni mbadala kwa ajili ya shughuli za ngono zenye afya, na za kawaida ndani ya ndoa.<sup>20</sup>

Je, mtu ambaye hajaoa anapaswa kufanya nini kama kitendo cha kupiga punyeto ni tatizo katika maisha yake?

Hata kama mtu anapiga punyeto kwa madhumuni ya kupunguza tu msukumo wa kufanya ngono, bado ni vyema kuachana na jambo hilo, kwa sababu ya majaribu yaliyopo kwa sasa, na kwa sababu ngono ya kibinafsi haikamilishi makusudi ya Mungu kwa ajili ya kujamiiana.

Kama kuna aina nyingine yeyote ya uasherati katika maisha yao, lazima waungame na kuziacha dhambi hizo. Wanapaswa mara kwa mara na kila mara watoe hesabu ya kushinda na kushindwa kwao kwa mshauri mzee mcha Mungu ambaye atawaombea na kuwapa ushauri.

Ikiwa kupiga punyeto ni matokeo ya hisia au matatizo ya kimahusiano au unyanyasi wa kijinsia wa ngono uliopita, kupata ushauri kutoka kwa mshauri wa Kikristo mtaalamu mwenye taaluma hiyo ni jambo la kufaa sana.

### **Biblia inasemaje kuhusu Matendo ya Ushoga**

Mungu alipanga ndoa iwe ni uhusiano wa kudumu, na wa kujitolea kati ya mwanamume na mwanamke. Mungu aliona kwamba Adamu alikuwa anahitaji kuwa na msaidizi (Mwanzo 2:18). Neno msaidizi linamaanisha mtu anayefanana na mwingine, kuwa msaidizi kwa kuwa tofauti katika njia za kusaidia. Mungu alimuumba mwanamke na siyo mwanamume mwingine awe msaidizi wa Adamu (Mwanzo 2:22). Hitimisho la simulizi ya uumbaji inatoa kanuni ya ujumla ya ndoa kwa wanadamu wote katika ndoa, mwanamume na mwanamke watakuwa kitu kimoja kwa namna ya pekee ya kufanana (Mwanzo 2:24).

Yesu alizungumza kuhusu mpango wa Mungu wa ndoa (Mathayo 19:4-6). Alirejea kifungu kutoka katika kitabu cha Mwanzo na kusema kwamba mwanamume na mwanamke hukutana na kuwa kitu kimoja katika uhusiano wa kipekee na wa kudumu.

---

<sup>20</sup> Dr. Tim Clinton and Dr. Diane Langberg, *The Quick-Reference Guide to Counseling Women*, (Grand Rapids, MI: Baker Books, 2011), 185.

Mtume Paulo alitoa kauli nyingi kuhusu ndoa. Alisema kuwa ndoa ni kielelezo kinachotufundisha sisi kuhusu uhusiano kati ya Kristo na Kanisa (Waefeso 5:22-33). Kwenye kifungu chote cha Waefeso, alitoa kauli kuhusu uhusiano kati ya wanaume na wake zao. Alinukuu kauli kutoka vitabu vya Mwanzo na Mathayo kuhusu uhusiano maalumu kuhusu mwanamume na mke wake (Waefeso 5:31). Ni jambo lililo wazi kutokana na kifungu kwamba ndoa ni uhusiano kati ya mwanamume na mwanamke.

Kitabu cha Mambo ya Walawi kinatoa matumizi ya kina sana kuhusu sheria ya Mungu kwa Waisraeli. Inasema kwamba kwa mwanamume kulala na mwanamume mwingine kama ilivyo kwa mwanamke ni machukizo (Mambo ya Walawi 18:22). Adhabu ya kitendo cha ushoga kwa washiriki wote wawili kilikuwa ni kifo, kwa sababu wote kwa pamoja walifanya machukizo (Mambo ya Walawi 20:13).

Wakati mwingine watu husema kwamba Mambo ya Walawi hayawahusu watu wa kizazi cha sasa. Ni ukweli kwamba baadhi ya maagizo katika Mambo ya Walawi yalikuwa na umuhimu wa sherehe za kiyahudi. Hata hivyo, maamrishi yaliyoko kwenye Mambo ya Walawi 18-20 yanakataza upotofu mwingine wa kijinsia kama vile kufanya ngono na jamaa wa karibu, kufanya ngono na wanyama, na kufanya umalaya na mtoto wa kike wa kumzaa. Maagizo mengine katika sura hizi yanakataza kuwatoa watoto kama dhabihu, kuiba, kuabudu sanamu, kuwatendea vibaya walemavu viziwi na vipofu, kuwakandamiza watu maskini, kutowatendea mema wageni, na kuwa na mizania za uongo. Ni dhahiri kwamba maagizo haya ni matumizi ya viwango vya Mungu vya maadili na haki ambavyo vinatumika kwa watu wote, mahali popote, na kwa wakati wowote.

► Mwanafunzi anapaswa asome Warumi 1:18-32 kwa ajili ya kikundi.

Kifungu hiki kinaanza na taarifa kwamba hukumu ya Mungu inakuja juu ya watu wote ambao kwa kujua wanamwasi Mungu kwa makusudi. Kifungu kinasema kwamba baada ya watu kukataa ujuzi wa Mungu mmoja wa kweli, aliye Muumbaji, walianza kuwa waabudu sanamu, wakiabudu vitu vilivyoundwa na yeye. Kukataa kwao ukweli kulisababisha dhambi ya ngono, hata kusababisha kufikia katika kiwango cha kufanya ushoga. Kifungu kinaelezea kwamba ngono kati ya watu wawili wa asilia moja ni kinyume cha asili. Baadhi ya watu wamesema kwamba kifungu kinarejea ubakaji wa ulawiti, lakini kifungu kinasema kwamba watu *kwa pamoja* walifanya makosa na kupokea hukumu kwa ajili yake, kwa hiyo kinarejea utendaji wa hiari wa pamoja. Kifungu kinaenda mbali zaidi kuorodhesha aina nyingi za dhambi na kuelezea mtazamo wa uasi dhidi ya Mungu.

Mtume Paulo aliorodhesha shughuli za ushoga pamoja na dhambi nyingine ambazo Mungu anazihesabia kuwa ni hatia (1 Wakorintho 6:9-10, 1 Timotheo 1:9-10).

## **Majukumu ya Kanisa**

Baadhi ya makanisa yamejitahidi sana kutafuta njia ya kuonyesha upendo kwa watu ambao wako kwenye dhambi ya zinaa. Baadhi ya makanisa yamehalalisha aina mbalimbali za dhambi za kingono kama za kawaida, za asili, na zisizoepukika.

► Je, majukumu ya kanisa ni yapi kuhusiana na masuala ya maadili ya ngono?

### **Kufundisha na Kupenda Haki**

Wakati mwingine kanisa linaonekana kutohusika na aina mbalimbali za uasherati wakifikiri kwamba hazina madhara na upotofu wake ni mdogo. Kwa mfano, wanaweza kudhania kwamba vijana wengi ambao hawajafunga ndoa watafanya ngono badala ya kuwafundisha jinsi ya kushinda dhidi ya jaribu. Watu waliookoka ni lazima washikilie kiwango cha Mungu cha maisha ya utakatifu na waiache ngono iwe ni akiba ya baadaye kwa ajili ya ndoa.

Ujumbe wa kanisa unapaswa kuwa sawa na maelezo ya Biblia. Mungu atawahukumu wale wote walio na shughuli za kujamiiana nje ya ndoa (Waebrania 13:4). Waumini hawapaswi kuvutiwa na mtu aliye kwenye matendo machafu ya ngono. Wafuasi wa Kristo hawapaswi kufanya mambo ya mizaha kwenye suala la uasherati. Dunia inafundisha kwamba dhambi ya zinaa inapaswa kusimamiwa kwa uangalifu ili kuepuka mimba na magonjwa, lakini ujumbe wa kanisa ndiyo ulio wa umuhimu zaidi. Kanisa linapaswa lifundishe kwamba dhambi ya zinaa hupelekea kwenye majuto, familia kuporomoka, majaribu kuzidi, kutotosheka, na kuwa mwenye hatia.

### **Kushirikisha Injili**

Kanisa linapaswa liwapende watu wote wenye dhambi na kutoa neema na msamaha wa Kristo.

Siyo dhambi kupata majaribu; hata Kristo mwenyewe alijaribiwa, lakini hakutenda dhambi (Waebrania 4:15). Kanisa halipaswi kumfanya mtu ajihisi kwamba amehukumiwa na kuonekana asiyefaa kwa sababu ya majaribu, hata yale majaribu potofu ya ngono. Matamano mabaya hayafanani kati ya mtu na mtu, lakini kila mtu amezaliwa na asili yake ya dhambi pamoja na kasoro za kiroho zinazosababisha matamano mabaya.

Mchungaji anaweza kujihisi kwamba hajafundishwa mahususi kwa ajili ya kumsaidia mtu mwenye matamano mabaya, lakini anaweza kutoa ushauri na kumsaidia huyo mtu mwenye tatizo kama hili kama mtu mwingine yeyote mwenye dhambi. (Sehemu mbili zinazofuata za somo hili zinatoa ushauri mahususi zaidi za ushauri kwa ajili ya kusaidia waumini kuwa washindi dhidi ya majaribu ya uasherati.)

► Je ni kwa jinsi gani kanisa linatakiwa lihusike wakati mshirika wa kanisa anapokuwa ametenda dhambi ya uasherati?

### **Kumrejesha Mwenye Dhambi**

Wagalatia 6:1 inasema kwamba kanisa ni lazima lijaribu kumrejesha mshirika ambaye ametenda dhambi. Hiyo haina maana kwamba mtu huyo ataendelea na nafasi yake ya huduma au kurudishwa haraka katika nafsi yeyote ya utumishi baada ya kuwa amefanya dhambi na kuthibitishwa. Urejesho inamaanisha kwamba ni mtu kurejeshwa tena kwenye ushirika na utunzaji wa kanisa. Kama mshirika ametubu kweli, anasemehewa na Mungu na kanisa. Kanisa linapaswa kutoa uwajibikaji wa kiroho kumsaidia mtu huyo aweze kuimarisha

ushindi na kuwa tena mwenye nguvu za kiroho. Kama muumini aliyerejeshwa tena akiendelea kuishi katika kuwajibika, anaweza hatua kwa hatua akajenga tena kwa upya uaminifu na imani kwa familia yake.

Ikiwa msichana ambaye hajaolewa akipata mimba, kanisa halipaswi kumtenga kutoka kwenye ushirika na uangalizi wa kanisa bila ya kujaribu kumfanyia urejeshwaji wa kiroho. Kama atatubu na kurejea kwenye uwajibikaji wa kiroho, huyo msichana amesameheka. Dhambi yake siyo mbaya kuliko dhambi ya yule mwanamume aliyehusika kumpa mimba. Wakati mwingine anatendewa kwa ukali kwa sababu tu matokeo ya dhambi yake yanaonekana sana hadharani.

Katika maeneo mengine, kanisa linamtendea mtoto tofauti kabisa kwa kuwa alizaliwa nje ya ndoa, lakini hili ni kosa kwa sababu siyo kosa la mtoto. Kanisa kumpenda na kumkubali mtoto haimaanishi kuwa linahalalisha dhambi.

### **Kulinda watu walio katika Mazingira Hatarishi.**

Katika jamii kadhaa, wazazi ambao huona aibu kwa ajili ya mimba ya mtoto wao ambaye mimba yake haijatokana na ndoa wanashawishika kumuua mtoto ambaye bado yuko tumboni ili kutunza hadhi ya familia yao. Lakini kamwe hakuna sababu ya maana kwa ajili ya kufanya mauaji (Kutoka 20:13). Kila mtoto ambaye hajazaliwa ameumbwa katika sura ya Mungu (Mwanzo 9:6, Zaburi 139:13-14). Mtoto wa Msichana huyo ni lazima alindwe, apendwe na atunzwe.

### **Kutoa Njia Mbadala kwa Umaskini**

Kanisa ni familia ya watu wa imani. Haitoshi kwa kanisa kuhukumu dhambi. Kanisa ni lazima lichukue hatua ya kuwatunza washirika wake. Kwa mfano, mtu anayesaidiwa kifedha kutokana na shughuli za dhambi anaweza akahitaji msaada ili aweze kutengeneza usaidizi mwingine mbadala utakaomsaidia kifedha.

Kwa mfano, wasichana kadhaa walikuwa wanahudhuria kwenye kanisa kubwa na walikuwa wakiimba kwenye kwaya ya kanisa. Familia zao zilikuwa maskini. Wasichana hawa walikuwa kwenye mahusiano machafu na wanaume kwa ajili ya kupata fedha za kujikimu katika familia zao. Je, kanisa lifanye nini katika mazingira kama hayo?

► Je, kanisa lako linapaswa kufanya nini ili kuwasaidia watu kuachana na mifumo ya maisha ya dhambi.

### **Msaada kwa wale Wanaostahimili Majaribu**

Tumeshajadili mada nyingi zilizo ngumu kwenye somo hili. Kuna uwezekano kwamba watu wengi wanaosoma somo hili watakuwa wametatizika na baadhi ya masuala haya. Baadhi ya wasomaji ni viongozi wa makanisa ambao wanahitajika kujua jinsi ya kutoa ushauri kwa washirika wao wanaokabiliwa na majaribu.



Haijalishi ni aina gani ya majaribu yaliyoko, kuna baadhi ya tabia na mifumo ya mawazo ambayo inaweza kumsaidia mwamini kuwa mshindi.

Mfuasi wa Kristo anaweza kusaidiwa na mambo yafuatayo:

- 1. Kujikabidhi kabisa kuwa kwenye uhusiano wako na Kristo (Mathayo 16:24-27).** Majaribu ya dhambi ya uasherati, kama yalivyo majaribu mengine yote, ni mashambulizi ya Shetani dhidi ya nafsi yako (1 Petro 2:11). Lengo lake ni ili aibe na kuchinja na kuharibu (Yohana 10:10). Unapaswa ukimbie kwa ajili ya kuokoa maisha yako (2 Timotheo 2:22).
- 2. Kuwa na uhakika kwamba Yesu anakujali (Zaburi 139:1-3, 1 Petro 5:6-10).** Anajali kuhusu imani yako, mahitaji yako ya kimwili, na usafi wako. Katika hali yake ya ubinadamu, alistahimili kwa ushindi majaribu yote ya kimwili na kiakili tunayokabiliana nayo sisi, na anayo neema tunayoihitaji kwa ajili ya kutuwezesha kuwa washindi (Waebrania 4:14-16).
- 3. Kutokuuamini uongo wa Shetani (Yohana 8:44).** Shetani anaweza kukuambia, "Yesu hajali, vinginevyo angeondoa hamu ya ngono ambayo inakukatisha sana tamaa." Katika 1 Petro 5:7-8 tunaambiwa kwamba Yesu anajali na shetani ndiye anayetaka kutuharibu sisi. Shetani anaweza kwa makosa akakushutumu wewe kuwa ni mwenye dhambi kwa sababu ya kuwa mtu mwenye matamania ya ngono (Ufunuo 12:10).
- 4. Kumwagalia Yesu peke yake na kumtukuza kwa jinsi alivyo (Zaburi 105:3-4).** Shetani atakuwa anapendelea kuiharibu imani yako na uhusiano wako na Mungu kupitia jaribu hili (Yohana 10:10). Lakini kusudi la Yesu katika jaribu hili ni kwamba imani yako iweze kuimarishwa, na kwamba utakuwa mtu bora zaidi wa kumtukuza yeye (1 Petro 1:5-9). Unapoelekeza mwelekeo wako kwa kumwabudu Yesu, atakuwa pale ulipo wakati huo kwa ajili ya kukusaidia wewe (Zaburi 46:1).
- 5. Kulitafakari Neno la Mungu (Zaburi 119:9).** Kusoma, kusikiliza, na kulitafakari Neno la Mungu kutakusaidia wewe kusimama kwa ushindi katika wakati wa majaribu. Yesu alipojaribiwa, alitumia maandiko katika kushinda (Mathayo 4). Ni lazima tufanye vivyo hivyo.
- 6. Kumshukuru Mungu hata katika matamania yako ya ngono, wakati unapokuwa unaomba nguvu za kulishinda jaribu (2 Wakorintho 12:7-9).** Unaweza kumshukuru Mungu kwa ajili ya matamania yako ya asili uliyo nayo, kwa sababu ni sehemu ya mpango wa Mungu wa ubinadamu wako na yanakulazimisha kumtegemea Yesu na kutafuta nguvu zake. Udhaifu wako unakupa fursa ya kukomaa katika kutembea kwako pamoja na yeye.
- 7. Kuweka wazi wa maisha yako mbele ya mtu mmoja mwenye busara na mcha Mungu (Wagalatia 6:2).** Kuwa muwazi na mwaminifu kwa mtu mwingine (wa jinsia yako) ambaye amekutangulia mbali kwenye safari ya imani kutakuwa ni

msaada sana kwako. Watakuwa na uwezo wa kuomba kwa ajili yako na kukushauri. Kuzungumza nao kuhusu mapambano yako kutakusaidia wewe kudumisha usafi na kuendelea kutiwa moyo katika imani yako.

**8. Kutumikia watu wengine na kuweka mwelekeo wako kwa ajili ya mahitaji yao (Wafilipi 2:3-5).** Pambana na kuhusika kwako kwa wingi kuhusu mahitaji na matamania yako mwenyewe kwa kuwatumikia watu wengine.

**9. Kuoa au kuolewa na mtu sahihi katika wakati wa Mungu (Mithali 5:15, 18-19).** (Masomo yajayo yanajadili jinsi ya kufanya chaguo lililo zuri kwa ajili ya ndoa).

► Je, katika haya ni mawazo gani yaliyo mapya kwako? Je, ni mawazo gani ambayo umeona ni ya msaada sana katika maisha yako?

► Je, ni tabia gani nyingine au mifumo ya mawazo ambayo imekuwa ni ya msaada kwako?

### **Usafi wa Maadili kabla ya Ndoa**

Vijana hukabiliana na majaribu mazito kabla ya kuoa. Ni muhimu kwao kukumbuka kwamba wanahitaji kuwa na msaidizi wa maisha atakayeweza kuwa mwaminifu.<sup>21</sup> Hawapaswi kufikiria kuwa na uhusiano na mtu ambaye anataka kujiridhisha kwa muda tu bila ya ndoa. Hawapaswi kuwa na uhusiano na mtu ambaye siyo mtu aliyeokoka/mwamini aliyejitoe kabisa (1 Wakorintho 7:39). Wanapaswa tu kufikiria mtu ambaye atakuwa mwenzi mwaminifu na mzazi mzuri kwenye ndoa.

Kijana ambaye anataka awe na ndoa nzuri anapaswa awe mtu mwaminifu, aliyejitoe kuwa mfuasi wa Kristo ili kwamba aina ya mtu aliye sahihi kwake aweze kuvutiwa naye (Mithali 3:4-8). Mtu hudhihirisha tabia yake njema kwa tabia iliyo sahihi na uvaaji wenye heshima (1 Timotheo 2:9-10). Watu wanaofanya mambo ya uzembe na watu wa jinsia tofauti wanamaanisha kwamba wako tayari kuwa na mahusiano yenye msingi wake kwenye matamania ya uovu (1 Wathesalonike 4:1-7). Mtu anayevaa katika njia inayosababisha matamania ya uovu hutaka amshawishi mtu mwingine apate furaha naye ambayo haina ahadi (Mithali 7).

Mungu amewapa dhamana wazazi, wachungaji, na viongozi wengine wa Kikristo kutoa mwongozo katika tabia, mavazi, na chaguzi zinazohusiana na mahusiano. Vijana wanapojikabidhi kwa viongozi hawa katika kumtii Mungu, watakuwa na baraka tele za Mungu na watalindwa dhidi ya madhara mengi na majaribu.

► Wanafunzi wanapaswa wasome 1 Petro 5:5 na Waebrania 13:17 kwa ajili ya kikundi.

Ni jukumu la watoto na vijana kujikabidhi kwa ajili ya hekima na uongozi wa wazazi wao na mamlaka za kiroho. Ni wajibu wa hawa viongozi kuwasaidia vijana kuishi maisha ya ushindi dhidi ya majaribu.

---

<sup>21</sup> Ona Mithali 31:11-12, 1 Timotheo 3:11-12, Malaki 2:14-16, na Mithali 2:16-17.

► Wanafunzi wanapaswa wasome Warumi 13:14 na 1 Wakorintho 10:13 kwa ajili ya kikundi.

Mungu hapendi kuona na au haruhusu watu waliookoka wawe kwenye mazingira ya majaribu juu ya kiwango cha kiwango cha kushindwa kujizuia au kuepuka **endapo** wako tayari kufanya hivyo. Vijana wana wajibu wa kuyakimbia majaribu (2 Timotheo 2:22). Hata hivyo, wazazi wanapaswa wawazuie vijana wao katika kujihusisha na majaribu yasiyokuwa ya lazima kwa kadri itakavyowezekana. Kuna njia tatu ambazo wazazi hufanya haya:

- 1. Kwa kutoa maelekezo mahususi.** Hii ni kuhusiana na yale ambayo watoto wanapaswa aidha wafanye au wasifanye, ni nani wawe naye, na waende wapi (Waefeso 6:1-4). Wazazi hawatakiwi kuwaruhusu watoto wao kuwa kwenye maeneo au hali ambazo ukomavu wao hautoshi kuwazuia dhidi ya majaribu. Kwa mfano, kijana na msichana watakuwa pamoja kwenye maeneo yaliyojificha au ya siri, kuna uwezekano mkubwa wakavutiwa kuingia kwenye tabia ya uovu.
- 2. Kwa kuwafanya watoto wao wawajibike wanapokuwa kwenye mazingira yenye majaribu.** Wazazi wanapaswa waombe wakiwa kwa pamoja na vijana wao na wawaulize maswali kuhusiana na maisha yao. Matokeo mazuri ya uwajibikaji itategemea uimara wa uhusiano uliopo kati ya mzazi na mtoto. Kama mtoto hawezi kumwamini mzazi wake kwamba ni mwenye upendo, anayemkubali, na wa msaada kwake, mtoto hatataka kukiri kushindwa kwa jambo lolote.
- 3. Kwa kuwapa vijana ushauri wa kibiblia.** Wazazi wanapaswa wawasaidie vijana wao wajifunze jinsi ya kutafakari mazingira kwa kutumia kanuni za kibiblia kwenye akili zao (Mithali 4:1-9, Mithali 7:1, 4-5). Wanapaswa wazungumze na vijana wao kuhusu hatari wanazokuwa wanazona dhidi yao. Wanapaswa wawasaidie vijana wao katika kufanya maamuzi mbalimbali ambayo watataka kuyafanya. Wanaweza kuwasaidia vijana wao kutafakari mbele ya muda kuhusu ni jinsi gani wataweza kuepukana na majaribu na ni nini kifanyike wakati watakapokuwa katika majaribu.

Kanisa ni lazima lijitofautishe na utamaduni wao wakati linapokuwa linatetea maadili ya kibiblia. Tamaduni nyingi hazizingatii dhambi ya ngono kuwa ni jambo zito. Wanawategemea vijana ambao bado hawajaoa wawe katika mahusiano ya ngono kabla ya ndoa.

Kanisa kamwe halipaswi liwe na dhana kwamba dhambi ya ngono ni jambo la kawaida kwa vijana. Mungu anasema kwamba mwasherati hatakuwa na urithi katika ufalme wa Kristo (Waefeso 5:5).

► Je, ni kwa jinsi gani kanisa linaweza kusaidia vijana ambao wanapambana na majaribu ya dunia?

► Wanafunzi wanapaswa wasome Waefeso 5:3-7 na Waebrania 13:4 kwa ajili ya kikundi.

Kipindi cha muda ambao uhusiano unakuwa upo kabla ya ndoa (yaani uchumba) siyo kipindi ambacho mahusiano ya ngono yanapaswa kuanza. Badala yake, ni kipindi cha muda ambacho mwanamume na mwanamke wanahakikisha kwamba wanashirikishana vipaumbele vya kiroho na kibiblia. Ni muda ambao wanakuza ufahamu wa kila mmoja kumjua mwenzake kunakowasaidia kukuza kuaminiana kwa kila mmoja kiasi cha kuwawezesha kuingia kwenye ahadi ya kudumu kwa kila mmoja. Kama hawatakuwa na uwezo wa kufikia kila mmoja kuwa mwaminifu kwa tabia ya mwingine, watapaswa wasitishe huo uhusiano na siyo kuendelea kuoana.

Watu kwenye jamii nyingine huchelewesha ndoa kwa sababu katika tamaduni zao wanategemea ndoa iwe na uwigo mpana wa maandalizi na sherehe ya gharama. Mara nyingi, wenzi huishi kwa miaka mingi na wakawa na watoto huku wakiwa bado wanachelewesha kufanyika kwa ndoa. Kwa baadhi ya wenzi, gharama za harusi zinawaathiri kifedha kwa muda mrefu baadaye kwa sababu walitumia kila kitu walichokuwa nacho kwa ajili ya tukio la harusi na inawezekana hata wakaingia kwenye kukopa fedha. Kanisa linapaswa liwe ni jamii ya watu wenye imani ambao wanafanya aina nyingine ya harusi iliyo tofauti na hizo. Ndoa ya Kikristo ni kwa ajili ya mwanamume na mwanamke ambao kila mmoja amejikabidhi kwa mwenzake na kwa Mungu na hawapaswi kutegemea kutumia gharama kubwa ambazo zitachelewesha kufanyika kwa harusi au ambazo zitaumiza wanandoa hapo baadaye.

► Je, kuna njia gani ambazo ndoa ya Kikristo inapaswa iwe tofauti na ndoa za kitamaduni kwenye jamii?

### **Kuwafundisha Watoto Kusudi na Maagizo ya Mungu kuhusiana na Ngono**

Watoto huwa wanaona na kusikia marejeo mengi kuhusu ngono. Wanasikia maoni mbalimbali kutoka kwa watu kuhusu ni lipi jema au baya. Watoto mwishowe huwa wanakuwa na hisia za ngono, matamania, na majaribu, kwa hiyo ni muhimu sana kwa wazazi wa Kikristo kuwaeleza Mungu anasema nini kuhusu ngono. Watoto hawapaswi wajue undani kuhusiana na tendo la ngono, kwa sababu hawajakomaa ya kutosha kuweza kuolewa, na kwamba ujuzi wake utawafanya wapatwe na majaribu yasiyokuwa ya lazima.

Watoto wanahitajika wajue mpango wa Mungu na wajibu wao wa kumtii yeye. Wanahitajika wajue kwamba watajakutana na majaribu huko baadaye. Wanahitajika waandaliwe kumtii Mungu na kutawala matamania yao wenyewe ya kufanya ngono hadi hapo watakapokuwa wameoa au kuolewa.

Fundisho linalofuata ni muhimu kwa ajili ya kufundishia watoto kuhusu mtazamo wa ngono bila ya kuzungumzia kwa undani na kwa kina kuhusu tendo la ndoa. Limeandikwa katika njia rahisi ya kueleweka, jinsi utakavyoweza kuzungumza na watoto.

### **Kuzungumza na mtoto**

► Soma Mwanzo 2:7, 18-24 ukiwa na mtoto.

Kifungu hiki kinatueleza kwamba Mungu aliumba mwanamume wa kwanza na mwanamke wa kwanza na akaweka ndani yao uhusiano mahususi/wa kipekee.

Mungu aliitengeneza ndoa kama uhusiano maalumu kati ya mwanamume na mwanamke. Watu wawili waliooana wanakuwa na upendo maalumu kwa ajili ya kila mmoja. Sehemu ya uhusiano wao ni furaha maalumu wanayokuwa nayo wakati wanapokutanisha miili yao pamoja kwa siri katika tendo linaloitwa kujamiiana. Mungu aliitengeneza kujamiiana ili kumpa mume na mke furaha na wakati mwingi kumfanya mwanamke apate mtoto.

Kwa kuwa tendo la ndoa linaleta furaha maalumu, mwanamume na mwanamke wanakuwa na matamano ya asili ya kuona na kuushika mwili wa mwingine na kila mmoja hufurahia usikivu wa mwenzake.

Ndani ya Biblia, Mungu anatuambia kwamba ngono ni nzuri na sahihi kwa ajili ya mume na mke. Lakini Mungu pia anatueleza kwamba ngono ni mbaya sana kwa watu ambao hawajawahi kuoa au kuolewa. Mungu ametupa maamrishi kuhusiana na tendo la ngono yumkini kwa sababu kuu nne:

(1) Furaha ya tendo la ndoa imetengenezwa kwa ajili ya ndoa.

Mungu ameifanya ngono kuwa sehemu maalumu ya uhusiano wa ndoa. Ingawaje inawezekana kwa kila mwanamume au mwanamke yeyote kuwa na furaha ya pamoja kwa njia hii, furaha hiyo ni ya kipekee zaidi katika ndoa, kwa sababu kila mtu amepewa mtu wake peke yake. Kwa watu ambao bado hawajawa katika ndoa, ngono haina maana hiyo, na hawawezi kuwa na uhusiano kamili ambao Mungu aliukusudia. Kwa hiyo, mtu ambaye bado ni mdogo sana kuweza kuolewa hapaswi kufanya tendo la kujamiiana. Watu hawapaswi kujamiiana hadi wawe wameweka ahadi ya ndoa na kufanya sherehe ya ndoa ya hadharani. Mtu anapaswa kufanya ngono na mwenzi wake tu.

(2) Tamaa za ngono zina nguvu sana.

Siyo kosa kuwa na matamano ya kujamiiana, kwa sababu Mungu ndiye aliyeyaweka matamano hayo. Lakini ni makosa kuongeza kwa makusudi matamano ya kufanya jambo ambalo Mungu hapendi. Kwa sababu hiyo:

- Isipokuwa tu katika ndoa, mtu hatakiwi kufanya mambo ambayo yatasababisha matamano ya kujamiiana kuwa na nguvu zaidi, kama vile kwa makusudi kutazama au kufikiria mwili wa mtu mwingine kwa makusudi.
- Isipokuwa tu katika ndoa, mtu hatakiwi kumgusa mtu mwingine kwa namna yeyote ile ambayo itaongeza hamu yake ya kutaka kufanya ngono.
- Mtu hatakiwi kuchagua kuwa na fikra za kufanya mambo mabaya.
- Mtu hatakiwi kuangalia picha au video ili kufurahia kuona watu wakifanya mambo mabaya.

- Mtu hatakiwi kuvaa kwa njia ambayo itaweza kuwafanya watu wengine kutaka kufanya mambo mabaya au kujenga fikira za kufanya mambo mabaya.
- Mtu hatakiwi kufanya au kuongea mambo ambayo yanaonekana kana kwamba anataka kufanya mambo mabaya.

(3) Matamano yetu hayawezi kutuongoza sisi.

Wanyama wanadhibitiwa na hisia na matamano yao. Sisi siyo wanyama; ni watu tuliombwa kwa sura ya Mungu. Kwa sababu hiyo, ni lazima tufikirie kile tunachotakiwa kufanya, na hatimaye tufanye maamuzi sahihi. Hatupaswi tutawaliwe na hisia au na matamano yetu. Wakati mwingine ni sawa kufanya kile tunachokitaka, wakati mwingine haipaswi iwe hivyo. Matamano yetu hayawezi kutuambia ni lini ngono ni sahihi. Badala ya kuzitii hisia zetu, tunapaswa tufuate maelekezo ya Mungu kutoka katika Biblia kwa msaada wa Roho Mtakatifu.

(4) Kujamiiana wakati mwingine husababisha kuwa na watoto.

Mungu amepanga kwamba watoto wapatikane kutoka katika mahusiano ya upendo. Amepanga kwamba watoto watahitaji miaka mingi ili wakulie katika familia ambayo inawapenda na kuwatunza. Mtoto mdogo ambaye mama na baba hawajaoana kwa kawaida huwa hana baba na mama kwa pamoja ili kumtunza hadi pale atakapokuwa mtu mzima.

Kwa kutambua hizi kweli nne zilizo rodheshwa hapa juu, watu ambao wanataka wampendeze Mungu na wawe na maisha bora watafuata maelekezo ya Mungu. Maelekezo hayo yatatengeneza tabia za uangalifu za kuwasaidia kupinga jaribio la kutokumtii Mungu.

### **Maombi kwa ajili ya Mtoto**

Mpendwa Mungu,

Asante kwa kunifanya mimi niwe (mvulana au msichana). Asante kwa ajili ya mpango wako maalumu na mzuri kwa ajili ya ndoa. Naomba unisaidie kukupenda na kukutii wewe katika maisha yangu yote. Unaona kila kitu ninachokifanya, na unajua kila kitu ninachofikiria. Nakuomba unisaidie mimi ili siku zote niweze kutii maelekezo yako kwa maisha yangu yote. Ninachotaka mimi ni mawazo na matendo yangu yaweze kukupendeza wewe. Nisaidie ili na mimi niweze kuwasaidia marafiki zangu waweze kukutii wewe kwa kuwa kielelezo kizuri kwao. Kwa wakati unaofaa, ninapokuwa mtu mzima. Nisaidie kuwa (mume au mke) unayetaka mimi niwe. Nakupenda, Mungu!

Ameni

## **Maombi**

Baba wa Mbinguni,

Asante kwa kutufanya sisi tuwe katika sura yako, ukiyapa maisha yetu kusudi na maana.

Asante kwa ajili ya kuunda jinsia ili kutusaidia sisi kuakisi sura yako.

Asante kwa ajili ya muundo wako mzuri na makusudi kwa ajili ya kujamiiana kwa wanadamu katika ndoa.

Tunatubu njia zetu ambazo kwazo tumeliasi Neno lako. Naomba utuoshe, utusamehe, na ututakase katika Jina la Yesu (1 Wakorintho 6:11). Utuweke huru kutoka katika utumwa wa dhambi (Warumi 6:6-7). Kwa sasa tunaikabidhi miili yetu kwako, tukijiachilia kabisa kufanya yale yaliyo mema na sahihi machoni pako (Warumi 6:13-14).

Tuwezesha sisi jinsi ya kujifunza tabia za kufikiri na mwenendo wa haki (1 Timotheo 4:7, Zaburi 23:3). Tunakusihi mawazo na matendo yetu yawe ya kukupendeza wewe machoni pako (Zaburi 19:14). Asante kwa ajili ya ahadi yako ya ushindi kwetu katika kila wakati wa majaribu (1 Wakorintho 10:13).

Ameni

## Kazi za kufanya

(1) Soma Wagalatia 5:16-6:9 wakati ukiwa unatafakari mada zilizojadiliwa kwenye somo hili. Jibu maswali yafuatayo kwa kuandika:

- Je, kuna tofauti gani kati ya matamano ya mwili (5:16) na matendo ya mwili (5:19)?
- Je, ni mambo gani mawili yaliyoahidiwa kwa wale wanaotenda matendo ya mwili (5:19-21, 6:7-8)?
- Je, ni kwa jinsi gani mtu aliyeokoka/mwamini atakavyoweza kuwa na nguvu za kutotii matamano ya mwili (5:16, 22-23, 25)?
- Je, ni kweli zipi baadhi ambazo waumini wanapaswa kukumbuka wakati wa majaribu ambazo zitaweza kuwasaidia kushinda? (Taja angalao nne kutoka katika kifungu hiki).
- Je, ni mambo gani ambayo watu waliookoka/waumini wameagizwa kufanya katika kifungu hiki? (Taja angalao nne kutoka katika kifungu hiki).
- Je, ni nini wajibu wa watu waliookoka/waumini mmoja kwa mwingine (6:1-2, 6)?

(2) Soma Warumi 6:1-23. Jibu maswali yafuatayo:

- Je, ni mambo gani ambayo kifungu hiki kinasema kwamba ni ya ukweli kuhusu kila mtu aliyeokoka/mwamini? (Orodhesha mambo 6-8)
- Je, ni maamuzi gani ambayo watu waliookoka/waumini ni lazima wayafanye kwa ajili ya ukweli kwa sababu ya ukweli juu yao? (Orodhesha mambo 6-8)
- Je, kwa nini mtu aliyeokoka/mwamini anatarajia kuwa mshindi kwenye majaribu ya kutenda dhambi? (Andika kifungu kimoja.)

(3) Soma Warumi 8:1-14. Andika maombi kulingana na kweli zilizoko katika kifungu hiki.

(4) Tafakari kwa kichwa Warumi 6:11-14 na Wakolosai 3:5-7. Mwanzoni mwa kuanza kwa kipindi cha darasa kinachofuata, andika au rudia kusema yale uliyokariri kutoka kichwani.



# Somo la 5

## Useja

### Malengo ya Somo

Hadi kufikia mwishoni mwa somo hili, mwanafunzi atapaswa:

- (1) Kuuelewa useja kutokana na mtazamo wa kibiblia.
- (2) Kutambua vipaumbele vya kibiblia kwa ajili ya uchaguzi kuhusu ndoa na useja.
- (3) Kujikabidhi kabisa kwenye usafi wa kimaadili, tabia ya kimungu, na huduma yenye matunda katika kipindi hiki cha maisha.
- (4) Kujisalimisha kwa Yesu kama Bwana na kuwa wake uliyekamilika ndani yake.

### Kumwabudu Yesu, katika Useja au Ndoa

Stefano na Sara walikuwa wakijaribu kutambua kama ndoa yao ilikuwa ni mapenzi ya Mungu kwa ajili yao. Sara alitambua kwamba kama ataolewa na Stefano – ambaye alikuwa mmishenari – maisha yake yangebadilika kwa namna na njia nyingi. Angehamia nchi nyingine, angejifunza lugha mpya, na angejizoeza kuwa kwenye utamaduni mpya. Alijua kwamba angepaswa kuachana na kile alichokuwa amekizoea na kuridhika nacho. Itabidi kuwepo na mambo ya kufadhaisha na ya kujitoa dhabihu. Ndoa ingekuwa tu siyo ahadi ya upendo kwa mume wake, bali tendo la imani na upendo kwa ajili ya Yesu.

Baada ya kitambo kidogo, Stefano na Sara walitambua kwamba hawakuwa wakiendana sawia, na kwamba hawakupaswa kuoana. Sara alijihisi kukata tamaa.

Aliomba kuhusu kukatishwa kwake na tamaa. Aliomba kwamba Mungu amsaidie ili azae matunda kwa ajili yake kwenye kipindi hiki cha maisha yake. Alipokuwa akiomba, alijitambua kwamba kujisalimisha huku kwenye mapenzi ya Mungu kulikuwa tu kitendo cha imani na upendo kwa Yesu kama ambavyo ndoa ingepaswa iwe.

### Useja

Katika kozi hii tunatafiti mpango wa Mungu kwa ajili ya ndoa. Kutoka katika maandiko tunajifunza kuhusu makusudi ya Mungu kwa ajili ya ndoa. Tunajadili maelekezo ya Mungu kwa ajili ya ndoa na njia za vitendo za kuimarisha ndoa zetu. Tunauona uzuri wa mpango wa Mungu kwa ajili ya ndoa.

Kwa watu walio wengi, ndoa ni mapenzi ya Mungu. Lakini watu wengi huishi kwa miaka kadhaa kama waseja kabla ya ndoa. Wakati mwingine huu muda wa kuishi kiseja unakuwa ni mrefu sana. Baadhi ya watu hupitia tena kwenye kipindi kingine cha useja baada ya kifo

cha mwenzi wao au baada ya kupeana talaka. Watu wengine huamua kukaa bila ndoa kabisa.

Mtu anaweza akawa hana ndoa kwa sababu moja au zaidi ya hizi zifuatazo:

- Wanapendelea manufaa ya kuwa waseja badala ya kuwa kwenye ndoa.
- Wana wasiwasi kuhusu ndoa kwa sababu hawajawahi tena kuona mahusiano mazuri ya ndoa.
- Kwa sasa wanajielekeza katika malengo ya elimu au taaluma nyingine.
- Hawajihisi hitaji la kimwili kwa ajili ya ndoa.
- Hawajawahi kupata fursa kwa ajili ya ndoa nzuri.

Kwa kuwa chaguzi za mseja zinaathiri sana uhusiano wa Mungu na watu wengine, somo hili litajielekeza kwenye maisha ya mtu aliyeokoka/mwamini ambaye hana kabisa ndoa.

### **Walichokisema Yesu na Paulo kuhusu Useja**

Mafarisayo walimwuliza Yesu swali lililohusiana na talaka. Baada ya kuwa wamelisikia jibu la Yesu, wanafunzi wake wakaishia kusema haifai kuoa (Mathayo 19:10). Yesu ambaye hakuwahi kuoa na alikuwa mseja katika maisha yake yote hapa duniani, akajibu kwamba, watu wengi wanahitaji kuoa na wachache tu ndio waliojaliwa uwezo wa kukubali kuishi katika useja wa muda mrefu (Mathayo 19:11-12).

Mtume Paulo – ambaye aidha alikuwa hajaoa kabisa au pengine alikuwa mgane – alikuwa na ushauri unaofanana kwa watu waliookoka ambao walikuwa hawana ndoa katika mji wa Korintho. Kwa sababu ya jaribu la zinaa, watu wengi wanapaswa kuoa (1 Wakorintho 7:2, 8-9). Paulo alijua kwamba Mungu alikuwa ameumba uhusiano wa ngono katika ndoa ili iwe zawadi nzuri (1 Wakorintho 7:7, 1 Timotheo 4:1-5, Waebrania 13:4). Alisema kwamba tendo la kujamiiana halipaswi lifanyike nje ya ndoa (1 Wathesalonike 4:3-4).

Paulo alielezea faida ya maisha ya kutokuwa na ndoa. watu waliookoka/waumini wanaweza wakaelekeza muda wao, nguvu zao, na jitihada zao katika kumpendeza Bwana na kuhudumu katika huduma (1 Wakorintho 7:32-35).

Paulo alibakia bila kuoa (1 Wakorintho 9:5). Alichagua kubakia hivyo ili kwamba aweze kuelekeza muda wake kwenye kazi ya umishenari ambayo Mungu alikuwa ameiweka kwa ajili yake. Yeye aliuchukulia useja kama zawadi (1 Wakorintho 7:7-8). Alivumilia mateso mengi katika huduma yake (2 Wakorintho 11:23-28). Mateso yake haya yalikuwa ni rahisi kukabiliana nayo kwa sababu hakuwa na wajibu wa mke au watoto (1 Timotheo 5:8).

Ingawaje Paulo alichukulia kwamba useja ulikuwa ni faida kwa ajili ya huduma yake, kuna pia njia nyingine ambazo ndoa inakuwa ni faida zaidi kwa ajili ya huduma.

► Je, umeuonaje useja kama faida kwa ajili ya huduma? Je, umeshaona kwamba ndoa ni faida kwa ajili ya huduma?

Paulo alisema kwamba watu wanapaswa kuzingatia mambo kadhaa wanapokuwa wanaamua aidha waingie kwenye ndoa au la:

- Uwezo wao binafsi wa kuweza kuishi au kutoweza kuishi kwenye useja (1 Wakorintho 7:9, 36-37)
- Mazingira magumu ya sasa, kama vile mateso (1 Wakorintho 7:26)
- Majukumu ya ndoa (1 Wakorintho 7:27-28, 32-35)

### **Vipaumbele Sahihi**

Si useja wala ndoa ambapo kimoja ni bora au cha kiroho zaidi kuliko kingine. **Kuna majaribu ya kipekee, matatizo, baraka, na nafasi kwenye kila kimoja.** Kila kimoja kinafaa kwa nyakati tofauti na kwa watu tofauti.

Hatimaye, utimilifu na ukamilifu wa binafsi ni lazima utokane na uhusiano wa mtu na Mungu, aidha kama mtu ana ndoa au laa (Zaburi 73:25, Zaburi 107:8-9). Zaidi ya hayo watu wote waliookoka/waumini – wenye ndoa na wasiokuwa na ndoa – ni lazima waweke mwelekeo wao kwenye umilele kwa sababu maisha ni mafupi, na umilele ni hakika (1 Wakorintho 7:31).

► Mwanafunzi anapaswa asome Mathayo 6:26-33 kwa ajili ya kikundi.

Kwenye kifungu hiki, Yesu anaelezea kwamba maadili na vipaumbele vya dunia ni tofauti sana na vile vya watu waliookoka. Lengo kuu la watu waliookoka ni kuwa washiriki kwenye ufalme wa Mungu. Kipaumbele kikuu cha kwanza kwa watu waliookoka ni kuishi maisha ya haki kwa neema ya Mungu. Mungu anaahidi kutoa mahitaji kwa ajili ya mwili na haja nyinginezo za watoto wake wakati wanapokuwa wanayatii maneno ya Yesu katika Mathayo 6:33.

Je, ni wakati gani mwanamume Mkristo anapaswa kuoa? Ni wakati ndoa itakapokuwa inamsaidia zaidi kutumikia ufalme wa Mungu. Ni wakati ndoa itakapomsaidia kuishi maisha ya uadilifu, yenye matunda yenye ushindi.

Je, ni wakati gani mwanamume Mkristo anapaswa kubakia katika useja? Ni wakati harakati za kufunga ndoa au ndoa yenyewe inapomkengeusha atoke kwenye nafasi yake katika ufalme wa Mungu. Ni wakati atakapoweza kuzaa matunda zaidi kiroho akiwa kama mseja. Ni wakati anapoweza kuwa mshindi wa kiroho na kudumisha usafi wa kimaadili bila ya kuwa na urafiki wa kujamiiana unaotolewa katika ndoa.

► Kama wewe bado huna ndoa, tulia kwa ajili ya muda wa kutafakari kwa uaminifu:

- Je, unaishi kwa utii kulingana na Neno la Mungu?
- Je, Mungu amekupa nini cha kufanya kwenye ufalme wake kwa sasa hivi?

- Je, unadhani Mungu amekuitia ufanye nini na maisha yako ya muda mrefu?
- Je, unadhani ndoa itaweza kukufanya ufanye vizuri au vibaya kwenye uhusiano wako na Mungu na kazi yako kwa ajili ya Mungu hapa duniani?

Kukubalina na vipaumbele vya Mungu kunawasaidia waumini ambao bado hawajaingia kwenye ndoa kuamua aidha waendeleo au wasiendeleo na mipango ya ndoa. Pia huimarisha ufahamu wetu wa kile tunachotakiwa kukiangalia katika kutafuta mwenzi muhimu. Kila mtu aliyeokoka aliye na matamano ya kuwa kwenye ndoa, anapaswa amtafute mwenzi ambaye anamtanguliza Mungu kwanza, anayeishi kwa kutii Neno la Mungu, na anayetafuta kuundeleza ufalme wa Mungu.

► Wanafunzi wanapaswa wasome Waefeso 4:17-24 na 1 Yohana 2:15-17 kwa ajili ya kikundi.

Watu wa dunia huishi kwa ajili ya ubinafsi. Wanachagua kufanya yale mambo ambayo miili yao na akili zinataka (Waefeso 2:3), na wako tayari kutokutii Neno la Mungu. Watenda dhambi mara nyingi huwa wanafanya kile ambacho wanakiona kwao kwamba ni kizuri, kinawafaa, au kitawafanya watu wengine wawe makini kuwaangalia. Kipaumbele chao muhimu ni kujifurahisha wenyewe. Wanaweza wakajenga mahusiano ya kimapenzi na mtu mwingine kwa sababu tu kimwili wanamvutia huyo mtu. Wanaweza wakawa kwenye mahusiano na mtu mwingine kwa sababu tu wana hisia zinazowaka wakati ule wanapokuwa wako na yule mtu.

Watu wenye ubinafsi hawatapenda kujitoa kabisa katika uhusiano wa kujiachilia kwa mwingine wa ndoa. Wanaweza wakawa tayari kuwa na mahusiano ya kufanya ngono bila ya ndoa ingawaje Mungu anasema kwamba mahusiano kama hayo ni uovu (1 Wakorintho 6:9-11).

Watu wenye ubinafsi wanaofunga ndoa wanaweza kukata tamaa kwa mwenzi wake wa ndoa wakati ndoa inapokuwa ngumu. Wanaweza kuachana na mwenzi wa ndoa na kuendelea katika mahusiano na mtu mwingine. Mungu analo jambo lililo bora zaidi kwa ajili ya wale watakatii maelekezo ya Neno lake (Zaburi 19:8, 11, Kumbukumbu la Torati 6:24).

Yesu anatuita ili tumpendeze Mungu katika kila jambo (Mathayo 16:24, 2 Wakorintho 5:9, Wakolosai 1:10). Kwa kuwa sisi ni wafuasi wa Kristo, kipaumbele cha maisha yetu ya binafsi ni lazima kiwe ufalme wa Mungu na haki. Zaidi ya hayo kipaumbele katika harakati zetu za kufunga ndoa ni lazima ziwe ufalme wa Mungu na haki yake. Ni lazima tumsikilize Yesu kuhusiana na maadili yake na kutii yale ambayo anasema ni sahihi na mazuri. Kisha ni lazima tumheshimu Mungu kwa kutii matazamio aliyo nayo kwetu kama waume na wake.

### **Kwa Kila Jambo Kuna Wakati Wake**

Utu uzima wa mapema ndiyo muda muafaka zaidi kwa ajili ya watu wengi kutafuta ndoa (Mithali 5:18, Malaki 2:15, Tito 2:4). Kwa kijana aliyekomaa kama mtu mzima, anapaswa awe tayari ameshafundishwa na kuwa tayari kwa ajili ya maisha yake. Mwanamume au mwanamke ni lazima awe aliyekomaa, aliye tayari kubeba jukumu, na mwenye uwezo wa

kufanya maamuzi ya hekima na au busara (1 Timotheo 4:12). Kimsingi, vijana waliokomaa kama watu wazima wako tayari kwa ajili ya kubeba majukumu ya ndoa na kulea watoto. Miili yao pia iko tayari kwa ajili ya kuzaa, na mara nyingi, wana tamaa kali ya kujamiiana na uhitaji wa urafiki wa ndoa.

Kwenye tamaduni nyingi kwa sasa, inakuwa ni jambo la kawaida kwa vijana waliokomaa kuchelewesha ndoa hadi pale watakapokuwa wamekamilisha elimu yao ya juu/vyuo, au watakapokuwa wamejiimarisha kabisa katika nafasi zao za kazi. Vijana wengine waliokomaa hawako na nia ya kuwa na ndoa kwa sababu wanataka kuishi bila kuwajibika.

Vijana wengi waliokomaa kama watu wazima huishi katika maisha ya uasherati kabla ya ndoa zao. Wana matamanio makali ya kufanya ngono. Katika hali ya Kihisia, wanataka ushirika wa karibu. Pamoja na hayo, bado hawataki kujiingiza kwenye ndoa na kuendeleza familia kwa sababu ya aidha malengo yao ya maisha au kutotaka kuchukua wajibu.

Vijana wa Kikristo ambao wanajichelewesha kuingia katika ndoa wanapaswa kufikiria kwa uangalifu vipaumbele vyao. Wanapaswa wahakikishe kwamba wanaishi maisha ya utauwa, yaliyo safi, na yenye kufuata mapenzi ya Mungu. Baadhi yao watahitajika kutafakari umuhimu ambao Mungu ameuweka katika ndoa na katika kukuza/kulea watoto wenye kumcha Mungu.

### ***Wenzi wanaoishi pamoja ingawaje bado hawajaoana***

Wakati mwingine, mwanamume na mwanamke huishi pamoja kwenye mahusiano ya ndoa, lakini wakichelewesha kufunga ndoa. Wanaweza wakawa wamejikabidhi mmoja kwa mwingine, lakini bado wanakuwa hawajafanya agano loa ndoa. Watu wanaofanya hivi wana sababu tofauti za kuwa hivyo:

1. Wakati mwingine matarajio ya kitamaduni yenye mambo mengi ya kuchanganua na gharama za harusi huzuia wenzi ambao siyo wenye uwezo mkubwa kuweza kuwa na harusi inayokubalika.
2. Wakati mwingine wenzi hawajiingizi kwenye ndoa kwa sababu ya hofu kwamba ndoa yao haitadumu. Wanaweza wakafikiria kwamba kutengana kutakuwa na madhara kidogo endapo watakuwa bado hawajafunga ndoa. Wanaweza kutarajia uhusiano wao kuwa na nguvu wakati wakiwa wanaishi pamoja.

Mungu amehifadhi uhusiano wa kimapenzi kwa ajili ya ndoa (Waebrania 13:4). Wenzi wanaoishi pamoja lakini bado hawajafunga ndoa wana hatia ya kutotii Neno la Mungu. Ukaribu wao hauwezi kamwe kuwa vile unavyopaswa kuwa, kwa sababu ya ukosefu wa ahadi ya kudumu na ya kipekee kwa wao kwa wao, pamoja na ukosefu wa uaminifu wa pande zote.

Watu waliookoka hawapaswi kabisa kufuata mfano wa watu ambao hawajaokoka badala yake wanapaswa walitii Neno la Mungu. Kanisa ni lazima lishikilie matarajio ya Mungu kwa ajili ya maadili na kutoa usaidizi wa vitendo ili kuwasaidia wanandoa kufuata mpango wa

kimaandiko kuhusiana na ndoa. Kwa mfano, wanandoa wanapokuwa hawawezi kufanya harusi ya gharama kubwa, familia ya kanisa inapaswa iwape msaada ili kuwawezesha kuwa na harusi ya gharama ndogo. Hili litawasaidia wanandoa kutii kiwango cha Mungu kwa ajili ya maadili kwa kufunga ndoa. Pia ingesaidia wanandoa wasianze ndoa yao kwa kuwa na deni la kifedha. Wakristo ni lazima wakumbuke kwamba ndoa ni muhimu zaidi kuliko sherehe ya harusi yenyewe, hata hivyo, ahadi ya ndoa ya uhakika na ya kudumu ni lazima ifanywe.

► Wanafunzi wanapaswa wasome Warumi 12:2 na Wafilipi 2:15-16 kwa ajili ya kikundi. Jadili jinsi ambavyo kujitolea kwa waumini katika maadili kunavyoweza kubadili utamaduni unaowazunguka.

## Useja wenye Afya

### Suala la Kujisalimisha

Kila mtu aliye mtoto wa Mungu ni lazima akabidhi matamano yake kwa Yesu. Yesu ni Bwana. Katika maisha yote, kila muumini atapimwa katika uaminifu wake kwa Yesu kama Bwana wake. Kitu kigumu kitatokea... au kitu kizuri tunachokitamani *hakitatokea*...na Yesu atatuuliza sisi, wafuasi wake, "Je, mimi ni Bwana wenu? Je, mtaamini wema wangu? Je, mtaamini kwamba ninao mpango mzuri? Je, mtanitii? Je, mtajisalimisha kwangu? Je, mtanyenyekea katika kile ninachokifanya? Je, mtanitukuza mimi katika hili?

"Kutosheka ni kuridhika kunakotokana na kujua kwamba Mungu ndiye aliye mkuu na juu ya vyote katika hali zangu zote, na hunipa mimi kile ambacho ni bora sana kwa ajili yangu."

- Phil Brown

Baadhi ya waseja wanafurahia kuendelea kuwa waseja. Lakini wale wanaotamani kufunga ndoa na hawajapata fursa nzuri ya kuoa au kuolewa wanapaswa kukubali kwa unyenyekevu uchaguzi wa Mungu wa kuizuia ndoa.

Wakristo wanaume na wanawake... wanatambua kwamba ikiwa Mungu atawataka wafunge ndoa, ataliweka jambo hilo liwe wazi kwa ajili ya wakati na njia yake kamili. Lakini ni lazima siku zote aje kwanza, na siku zote ataendelea kuwepo [aaminiwe kabisa].<sup>22</sup>

Mungu ni mwaminifu na ni mwema. Kuna kazi ambayo anataka kuifanya kwenye moyo na maisha ya mwamini ambaye hajaingia kwenye ndoa. Siku zote Mungu ataruhusu kile ambacho ni bora zaidi kwa watoto wake, na muhimu zaidi sana, kile ambacho kitamletea Yesu utukufu mzuri zaidi. Katika mambo yote, Mungu anafanya kazi ya kutufanya tumfanananie Yesu katika mwenendo wetu (Warumi 8:28-29), na kutuwezesha sisi kumwabudu Yesu jinsi tunavyopaswa kumwabudu hata milele (1 Petro 1:6-7).

---

<sup>22</sup> Nukuu kutoka kwa Leslie Ludy, *Sacred Singleness* (Eugene, OR: Harvest House Publishers, 2009), 24.

Mungu anao uwezo kamili wa kumpa kila mmoja wa watoto wake mke mcha Mungu. Anaweza kumsaidia mwanamume Mkristo kumpata mke mwenye kumcha Mungu, huku mwanamume naye akiwa anatafuta mwanamke mwema ambaye atamheshimu Mungu katika maisha yake (Mithali 18:22, Mithali 19:14, Mithali 31:10).

Mwanamke ambaye hajaolewa lakini anaishi kwa ajili ya Kristo anaweza kumwamini Mungu katika kushughulikia mahitaji yake kwa njia iliyo bora kabisa, iwe au isiwe kama Mungu atamwongoza mwanamume kwake kwa ajili ya kutaka kumwoa. Anaweza akaishi maisha makamilifu na yenye matunda ya kiroho kwa sababu ya utoaji na uaminifu wa Mungu.

Ikitokea kuwa useja ni chaguo la Mungu kwake, atamwona Mungu kuwa mpenzi sahihi, mpaji, mlinzi, na kiongozi. Yesu anaweza kuwa mume wa moyo wake (Isaya 54:5), na anaweza kumpenda, kumheshimu, kujitoa kwake, na kumtii yeye, kama mbadala wa mume wa kidunia.

Ikitokea kuwa ndoa itakuwa ndiyo chaguo la Mungu kwake, muda wake alioutumia katika useja utakuwa umeshamfundisha jinsi ya kumtii Mungu (ambaye *peke yake* ndiye mpenzi mkamilifu, mpaji, mlinzi, na kiongozi), hata atakapokuwa anaendelea kujifunza kumpenda, kumheshimu, na kujitoa kwa mume wa kibinadamu, asiye mkamilifu.

### **Ukamilifu katika Kristo**

Waumini wote ni lazima wapate utimilifu wao ndani ya Kristo, na siyo kutoka kwa rafiki wa kibinadamu. Hata kama mtu angependelea kuwa katika ndoa, useja wa muda mrefu unatoa fursa ya kuhakikisha kwamba kwa uhakika amekamilishwa ndani ya Yesu. Useja unatoa fursa ya kuthibitisha kwamba Yesu anatosha (Wafilipi 4:11-13).

Ukweli kwamba Mungu aliumba ndoa, na kwamba tunapaswa kuiheshimu kama taasisi takatifu, ni dhahiri katika maandiko yote...Haikuwa ni jambo jema kwa Adamu kuwa peke yake, lakini hiyo haikuwa ni kwa sababu Mungu mwenyewe hakutosha kutimiza mahitaji ya Adamu? Hakika hapana! Kama Biblia inavyofafanua kwamba, Mungu alimwumba Hawa kwa sababu Adamu alihitaji awe na *msaidizi*, rafiki wa kufanya kazi hapa duniani ambayo Mungu alikuwa amemuita kuifanya. Ndiyo, kulikuwa na baraka na faida nyingi ambazo zilikuja kwa pamoja kwa Adamu na Hawa kupitia urafiki wao, lakini ndoa kamwe haikuchukua nafasi ya Mungu. Yeye bado alikuwa ni Mungu, na bado alikuwa amemaanisha kuwa ndiye kusudio lao la kwanza na la msingi la upendo na kuabudu. <sup>23</sup>

#### **Maombi**

"Mimi ni wako, Bwana.  
Huo ndiyo utambulisho  
wangu,  
wito wangu,  
usalama wangu,  
mfariji wangu,  
kusudi langu,  
furaha yangu, na  
zawadi yangu.  
  
Ninakuhitaji.  
Wewe unatosha.  
Unanijaza.  
Wewe ndiyo asili yangu.  
Unayenikamilisha mimi."

---

<sup>23</sup> Leslie Ludy, *Sacred Singleness*, (Eugene, OR: Harvest House Publishers, 2009), 66-67.

Mtu anaweza kujifunza kujionea upendo zaidi wa Mungu wakati akiwa hana mwenzi au familia kwa ajili ya kutoa huba na mhemuko wa kimwili. Maandiko kama Zaburi 73:25-26 ni faraja wakati wa kupitishwa katika mhemuko na majaribu ya kimwili:

Ni nani niliye naye mbinguni, Wala duniani sina cha kupendeza ila Wewe. Mwili wangu na moyo wangu hupunguka, Bali Mungu ni mwamba wa moyo wangu Na sehemu yangu milele.

Kama Leslie Ludy anavyoandika,

Daudi mwimba Zaburi alikuwa wenzi/marafiki wengi wa kike katika maisha yake. Lakini ni uhusiano wa urafiki wa karibu na Mungu ambao ulimletea utoshelevu uliokuwa kamili kama Aya hizi zinavyofafanua.<sup>24</sup>

Muumini aliye mseja atagundua kwamba Yesu anatosha; na uhusiano na Mungu unaridhisha.

### **Fursa kwa ajili ya Huduma**

Wakati waumini ambao hawana ndoa wanapopata utoshelevu wao ndani ya Kristo, yeye huufanya useja wao uwe ni fursa ya kuwatumikia watu wengine. Badala ya kuweka mwelekeo wao kwenye mahitaji yao binafsi na kujisikia kutoridhika, wanaweza kujifunza kutambua na kukidhi mahitaji ya watu wengine. Kuwasaidia watu wengine ni mojawapo ya njia bora za kuleta kuishi maisha yenye matunda na utoshelevu. Tabia iliyokuzwa kupitia katika kipindi hiki cha maisha itawasaidia kuendelea kuzaa matunda mazuri katika maisha yao yote.

“Ikiwa kama wewe ni mseja, kumbuka haujaitwa kupoteza muda na uhuru wako kwa ajili ya kufuatilia shughuli zenye mrengo wa kibinafsi tu, bali kuhudumu kwa ajili ya kanisa na ulimwengu.”  
- Nukuu kutoka kwa Paul Lamicela

► Wanafunzi wanapaswa wasome Wafilipi 2:3-4 na Tito 3:8, 14 kwa ajili ya kikundi.

Kama ambavyo imeelezwa hapo awali, hali tofauti za maisha hutoa fursa za kipekee. Katika kila hatua ya maisha, kuna mambo ambayo mtu anaweza akayafanya, na kuna mambo mengine ambayo hawezi kuyafanya. Dada mmoja mseja aliitengeneza orodha hii ya mambo ambayo anaweza kuyafanya hasa *kwa sababu* yeye ni mseja. Wanaume na wanawake waseja watakuwa na vitu vingine vya kuweka kwenye orodha zao.

Kwa kuwa mimi bado ni msichana mdogo niliye mseja, ni rahisi kwangu mimi kufanya yafuatayo:

- Kuwatembelea wazee na kutumia muda wangu pamoja nao.

---

<sup>24</sup> Leslie Ludy, *Sacred Singleness*, (Eugene, OR: Harvest House Publishers, 2009), 67. Leslie Ludy alikuwa anarejea kwenye Zaburi 16:11, Zaburi 73:25, na Zaburi 107:9.



- Kutengeneza na kuwapa chakula watu ambao hawana makazi.
- Kujifunza Biblia kwa ukamilifu kisha kuandaa masomo ya Biblia\kwa ajili ya watoto.
- Kuwahudumia wanawake na wasichana wa eneo la nyumbani kwangu
- Kutumia muda wangu usiokuwa na usumbufu kwa ajili ya maombi na maombezi.
- Kujifunza ujuzi mwingine mpya.
- Kuandika barua na kadi za kuwatia watu moyo.
- Kujitolea kuwasaidia watu wengine kwa miradi.
- Kwa haraka hubadilisha ratiba yangu wakati kunapotokea kuwepo na hitaji au tukio la haraka lililojitokeza.

Kila mtu ana fursa au wajibu maalumu kwa sababu ya hali zao za maisha. Orodha ambayo mama mwenye watoto wadogo angeiorodhesha ingeweza kujumuisha mifano ya mambo ambayo anawafundisha watoto wake au njia ambazo anazitumia kuwafundisha. Kwa kuwa yeye ndiye mama yao, Mungu amempa fursa na jukumu la kuhudumu kupitia njia hizi. (Mwishoni mwa somo hili utaandaa orodha yako mwenyewe.)

## **Urafiki**

Ni muhimu sana kwa wale ambao hawajafunga ndoa kujenga uhusiano mzuri wenye nguvu na watu wengine. Kama ambavyo imezungumzwa kwenye masomo yaliyotangulia, Mungu aliumba watu kwa ajili ya kuwa na mahusiano na yeye na pia mahusiano na watu wengine.

- Watu wanaoishi katika useja wanahitaji mahusiano na watu ambao wanaweza kuwatumikia – labda watoto, vijana au wazee.
- Watu wanaoishi katika useja wanahitaji washauri waliokomaa kwa ajili ya ushauri na uwajibikaji.
- Watu wanaoishi katika useja wanahitaji marafiki walio katika hadhi na nafasi moja katika maisha, ili kwamba waweze kutiana moyo kila mmoja na mwingine katika Bwana na kuwa na ushirika wa pamoja.
- Watu wanaoishi katika useja wanahitaji kuwa marafiki na wenzi walioko kwenye ndoa pamoja na familia. Kuna baraka nyingi za kushirikishana kwa faida ya wote kwenye urafiki kama huo.

Kuwa na mahusiano ya aina mbalimbali na watu wengine humpa mtu aliye katika useja fursa nyingi za kuhudumia. Kuwa katika urafiki huweza kupata baadhi ya msaada wa kihisia na kiroho anaohitaji mtu aliyeko kwenye useja. Urafiki husaidia kutosheleza uhitaji wao wa familia hasa pale ambapo hawaishi karibu na familia zao wenyewe.

Tahadhari mbili ni lazima ziongezwe:

1. Mtu Mtu ambaye hajaoa au hajaolewa lazima awe mwangalifu ili kuepuka kuunda mahusiano yasiyo ya busara au yasiyo ya maadili kwa sababu ya mahitaji ya kihisia na kimwili.
2. Mseja ni lazima aweke kipaumbele chake na Mungu kiwe juu ya uhusiano wowote wa kibinadamu.

## **Wazo la Maisha**

Waumini wote ni lazima wafanye kazi kwa ajili ya kuweka mawazo ya maisha yawe masafi kwa neema ya Mungu yenye kuwezesha (Mithali 4:23). Zaburi 19:14 ni maombi, ya kumwomba Mungu atusaidie sis tuishi kwa uangalifu kwa ajili yake katika maneno na mawazo yetu. Maombi haya yanatukumbusha kwamba tunawajibika kwa Mungu kwa makusudio ya mawazo na maneno yetu tunayosema.

Tuna chaguzi mbalimbali kuhusu yale tunayoyaweka kwenye akili zetu (Wafilipi 4:8): yale tunayoyaona, tunayosikiliza, na kusoma. Kama tunataka tumheshimu Mungu, ni lazima tuchague chakula cha kiroho ambacho ni kisafi, na kitakachotuvuta karibu na yeye na kitakachotusaidia kumtii yeye (Warumi 12:2, Warumi 13:14).

Wafuasi wa Kristo hawapaswi kujiliwaza na dhambi za watu wengine (Zaburi 101:3, 1 Wakorintho 15:33). Kufurahia kutazama mambo na tabia chafu ni kushiriki katika dhambi ya mtu (Warumi 1:32). Kutazama na kusikiliza kunamfanya mwamini apate hisia ya kutenda dhambi na kumfanya kupoteza mwelekeo katika kumpendeza Mungu (Mithali 13:20). Neno la Mungu linasisitiza haja yetu ya kumcha Bwana kila wakati (Mithali 23:17) na kuchukia uovu kama yeye mwenyewe anavyochukia (Mithali 8:13). Tunapokuwa na hofu ya Mungu na kujiepusha na maovu, tunabarikiwa (Zaburi 111:10).

Wakati tunapokuwa tumeshindwa kutii maagizo ya Mungu kuhusu yale tunayopaswa kuyaweka katika akili zetu na yale ambayo ni ya kutafakari, ni lazima tukiri makosa yetu na kuacha kabisa kuendelea kufanya mambo hayo. Hata katika hali hizo wakati kwa bahati mbaya tunaweza kusikika au kuona jambo baya, ni lazima kwa makusudi tubadilishe mawazo yanayohusiana na mambo hayo kwa mawazo mazuri na ya kimungu.

► Wanafunzi wanapaswa wasome Zaburi 19:14, Zaburi 1:1-2, Wafilipi 4:6-8, na Waefeso 5:25-27 kwa ajili ya kikundi.

Aya kutoka kwa Wafilipi inatuambia kwamba Mungu anataka kulinda mioyo na akili zetu, lakini ni lazima tushirikiane naye kwa kutafakari kwa makusudi mambo yaliyo sahihi. Kutafakari juu ya maandiko ni muhimu sana kwa ajili ya mawazo ya maisha yenye afya na yaliyo safi. Tunaelezwa katika Waefeso kwamba Neno la Mungu linatutakasa na kutufanya tuwe wasafi. Kwa hakika jambo hili linahusisha akili zetu na mawazo yetu.

► Je, ni shughuli gani zinazokusaidia wewe kuwa na mawazo ya maisha ya kumtukuza Mungu? Je ni Aya gani nyingine ambazo zimeshawahi kukusaidia wewe katika mawazo yako ya maisha?

### **Useja na masuala ya ngono**

*Ikiwa unajifunza somo hili wewe mwenyewe kwa wakati wako, tafadhali pia soma na somo la 4 mahali ambapo usafi wa kijinsia na masuala ya maadili yamejadiliwa.*

### **Hitimisho**

Useja huwapa waumini fursa za kipekee za kukua katika mahusiano yao na Kristo na kujifunza jinsi ya kuhudumia watu wengine. Watu ambao bado hawana ndoa wanapaswa watafute utimilifu wao katika Kristo huku wakiwa wanajenga uhusiano wao mzuri na watu wengine. Wanapaswa watumie fursa zilizopo za useja wao kwa ajili ya utukufu wa Mungu na uzuri wa ufalme wake. Vipaumbele vya Mungu husaidia waumini katika kufanya maamuzi mazuri ya kuzingatia uwezekano wa kuwepo ndoa.

### **Kwa ajili ya Majadiliano ya Kikundi**

- Taja na jadili vipaumbele kadhaa ambavyo vinaweza kuongoza maamuzi kuhusu miaka ya useja, chaguo la kuwa na ndoa, na kufuatilia ndoa.
- Je, ni kwa jinsi gani kanisa lako linaweza kuhudumu kwa ufanisi zaidi kwa washirika ambao bado ni waseja?
- Je, ni kwa jinsi gani familia yako inaweza kufanya urafiki na mtu ambaye bado ni mseja?
- Kama bado wewe ni mseja, ni kwa jinsi gani unaweza kuwa ni mchango kwa familia ya kanisa lako? Je, ni kwa jinsi gani unaweza kuwa ni baraka kwa watu wengine wa vipindi vya marika mbalimbali ya maisha?
- Je, ni mawazo gani mapya uliyoyapata katika somo hili?
- Je, ni jambo gani lingine ambalo ungependelea liweze kujadiliwa katika somo hili?
- Jadili jinsi ambavyo maudhui yaliyoko katika somo hili yanavyofanya kazi kwenye vipindi vingine vya maisha.

## **Maombi**

Baba wa Mbinguni,

Asante kwa kuwa mwaminifu kwetu katika kila kipindi cha maisha yetu. Asante kwa ajili ya mifano ya wale ambao wanaishi kwenye uwepo wako na kwa ajili ya utukufu wako katika miaka yao mingi ya useja.

Tusaidie tujikamilishe kwako kwa uaminifu wetu wote kupitia katika maisha yote. Tusaidie kutafuta na kupata utimilifu wako kwenye mahusiano yetu pamoja na wewe. Tusaidie katika kutumia fursa ulizotupa sisi kwenye wakati wetu wa sasa wa maisha yetu.

Tuwezeshe sisi tukuheshimu wewe siku zote katika chaguzi zetu, mawazo yetu, mahusiano yetu na watu wengine, na huduma zetu. Tufanye tuwe watu wa kuzaa matunda kwa ajili ya utukufu wako.

Ameni

## Kazi za Kufanya

(1) Jaribu kufikiria hali ambayo Yesu amekutaka ujisalimishe kwenye mpango wake. Kwa takribani vifungu viwili, elezea mazingira na mwitikio wako kwa ajili ya jambo hilo. (Hali hii inaweza ikawa ni kwenye hali ya sasa tuliyopo au kitu chochote kinachotokana na wewe cha hapo nyuma.) Je, ni kwa jinsi gani imani yako ilikuwa inajaribiwa? Ni kwa jinsi gani Bwana anavyokuongoza? Je ulijisalimisha kwenye mpango wake? Ulimwambia nini? Utii ulionekanaje kwako katika hali hii?

(2) Je, ni fursa gani ulizo nazo **kwa sababu ya** hali yako ya ndoa, jinsia, au hali ya maisha? Kwa sasa usifikirie juu ya kile kitu ambacho huwezi kukifanya. Badala yake, chukua dakika chache za kuorodhesha mambo ambayo una uwezo wa kuyafanya kwa sababu ya mahali ambapo Mungu amekuweka kwa sasa. Andika, Kwa sababu mimi ni\_\_\_\_\_ninayo fursa ya kufanya\_\_\_\_\_."

(3) Soma na utafakari juu ya kila moja ya maandiko yaliyonukuliwa hapa chini, ambayo kwa pamoja yalikuwa yamerejewa kwenye sehemu ya mwisho ya somo. Mwombe Mungu akuonyeshe chochote unachohitaji kubadilisha, ili kwamba mawazo yako ya maisha yawe safi na yenye kumpendeza Mungu. Andika maombi ya kukiri na kujikabidhi kwa utii.

- Zaburi 1:1-2
- Zaburi 19:14
- Zaburi 101:3
- Zaburi 111:10
- Mithali 4:23
- Mithali 8:13
- Mithali 13:20
- Mithali 23:17
- Warumi 1:32
- Warumi 12:2
- Warumi 13:14
- 1 Wakorintho 15:33
- Wafilipi 4:6-8

(4) Chagua Aya tatu kutoka katika sehemu ya 3 ya Kazi za Kufanya kwa ajili ya kuzikariri kwa kichwa. Mwanzoni mwa kuanza kwa kipindi cha darasa kinachofuata, andika au rudia kusema yale uliyokariri kutoka kichwani.



# Somo la 6

## Maandalizi kwa ajili ya Ndoa

### Malengo ya Somo

Hadi kufikia mwishoni mwa somo hili, mwanafunzi atapaswa:

- (1) Tambua umuhimu wa kuchagua mwenzi wa ndoa kwa hekima.
- (2) Elezea aina ya mtu anayestahili kuwa mwenzi wa mtu aliyeokoka kwa kuzingatia juu ya vipaumbele na kanuni za kibiblia.
- (3) Tekeleza kanuni za kibiblia katika mchango wa wazazi kwenye mahusiano kabla ya ndoa.
- (4) Fanya maamuzi ya hekima kwenye urafiki kabla ya ndoa.

### Ruthi na Samweli

Ruthi alilelewa katika familia moja ya Kikristo huko India. Siku moja familia yake ilimwambia kuhusu mhubiri mmoja kijana aliyeitwa Samweli ambaye alikuwa anahitaji kuwa na mke. Pia walizungumza na Samweli kuhusiana na Ruthi. Ruthi alisema kwamba hakuwa tayari kukutana na huyu kijana. Siku moja Ruthi alirejea nyumbani jioni na akamkuta Samweli akiwa amemsubiria pale kwa masaa kadhaa ili kukutana naye. Hakufurahia kumwona, lakini alikaa chini ili aweze kuzungumza naye. Alisema, "Mimi ni mwalimu wa chuo cha Biblia, Silipwi malipo makubwa. Pia ninasafiri kwenda kuhubiri Injili maeneo mbalimbali, na wakati mwingine huwa ninalala nje kwenye udongo. Je, uko tayari kupata mateso pamoja nami?" Ruthi alianza kulia alipokuwa akisema kwa sababu alijihisi kuwa Mungu alikuwa akimwambia kwamba huyu ndiye mwanamume ambaye angepaswa kuolewa naye. Baada ya mazungumzo yao, walikuwa wakionana mara chache sana, na hawakuwa peke yao, hadi ilipofikia wakati wa harusi. Kwa sasa wameshatumika kwa pamoja katika huduma kwa miaka mingi.

### Chaguo la Mume au Mke

#### Chagua kwa Uangalifu!

Yesu alisema kwamba ndoa ni ahadi ya maisha yote, kwa mpango wa Mungu (Mathayo 19:6-8). Siyo tu kwamba ni kumwoa mtu sasa hivi. Unamwoa mtu wa kuwa na wewe kama mwenzi wako kwa maisha yote hadi mmoja wenu atakapofariki dunia (Warumi 7:2). Fanya uchaguzi wa busara!

Hutashiriki tu nyakati nzuri na furaha za maisha. Utashiriki katika matatizo, shida, maumivu ya moyo, migogoro, na misiba ya maisha. Kuna baraka nyingi zinazotokana na kuoa au kuolewa na mwenzi wako ambaye ni mcha Mungu katika nyakati ngumu. Lakini nyakati

ngumu huwa mbaya zaidi wakati unapokuwa una mwenzi ambaye hana nguvu za Bwana. Unaoa au kuolewa na mtu ambaye atakuwa wako kwa maisha yako yote – na katika hali zote. Chagua mume/mke kwa uangalifu mkubwa!

Unaingia kwenye ndoa na mtu ambaye utanzisha naye familia. Unachagua watakaokuwa wazazi wa watoto wako na babu/bibi wa vizazi vyako. Unamchagua mtu ambaye maisha yake ya kiroho kwa kiwango kikubwa yatashawishi sana maisha ya kiroho ya watoto wako. Unamchagua mtu ambaye kwa mwenendo wake, tabia zake, na hulka zake zitakuwa zinaigizwa (Waefeso 5:1). Unamchagua mtu ambaye atawatengeneza na kuwafundisha watoto wako kupitia mifano na jinsi ya kuongea (Mithali 23:26). Chagua mtu ambaye atawalea na kuwatunza watoto wako, mtu ambaye atawaongoza na kuwafundisha nidhamu kwa uangalifu, bidii, na kwa upendo. Unamchagua mtu ambaye atakuwa na athira kwa vizazi – kwa manufaa au kwa madhara. Chagua kwa busara!

“Haukuchagua kuzaliwa katika familia yako; unapata kuchagua mtu wa kuwa naye kwenye ndoa ili kuunda familia yako ijayo.”

- Gary Thomas,  
*The Sacred Search*

► Wanafunzi wanapaswa wasome Mithali 14:1, Mithali 24:3-4, na Mithali 31:10-12, 30 kwa ajili ya kikundi.

Uchaguzi wako wa mwenzi wa ndoa ni uamuzi wa pili muhimu sana ambao utakuwa umeufanya katika maisha yako; uamuzi wa kwanza kuliko wote ni ule wa kumchukua Yesu kama Bwana na Mwokozi wako. Uchaguzi wako utabadilisha mwenendo wa maisha yako, lakini utaathiri watu wengine pia. Uchaguzi wa busara utakuwa ni wa baraka kwako na kwa watu wengine wengi. Uchaguzi wa kipumbavu utakuwa ni wa madhara kwako na kwa watu wengine wengi. Chagua kwa maombi!

Hakuna watu walio wakamilifu duniani. Wewe una matatizo, madhaifu, na kushindwa. Mwenzi wako pia hatakuwa mkamilifu na atendelea kuwa mtu ambaye hajakamilika katika maisha yake yote. Kwa hiyo, usitake kutafuta mwenzi ambaye amekamilika. Badala yake, tafuta mwenzi ambaye ni mcha Mungu bila kubakiza lolote. Angalia mtu ambaye ni mnyenyekevu wa kutosha wa kukubali na kurekebisha makosa na kushindwa. Mwenzi wa jinsi hii atakuwa baraka kwako, na mnaweza kwa pamoja kupeana msaada kwenye maeneo yenye madhaifu.

► Wanafunzi wanapaswa wasome Mithali 11:14, Mithali 12:15, Mithali 13:18, na Mithali 23:22 kwa ajili ya kikundi.

Chagua kwa busara. Chagua kwa ajili ya maisha ya kudumu. Pata ushauri kutoka kwa watu wenye kumcha Mungu na kwa wazazi wako. Sikiliza maonyo yao. Usipende tu kusikiliza hisia zako mwenyewe. Uchaguzi huu ni wa muhimu sana ambao hautakiwi kabisa wewe kuwa mzembe.



## **Usioane na mtu ambaye Hajaokoka**

Jambo moja ambalo ni la maana sana kwa Mungu ni kwamba watu wake wafunge ndoa na waumini wenzake tu. Hii ni kwa sababu uhusiano wa mtu na Mungu ndilo jambo muhimu zaidi katika maisha yote na hata kwenye umilele. Ndoa – uhusiano wa karibu zaidi kati ya wanadamu—huathiri uhusiano wa mtu na Mungu. Ni jambo gumu zaidi kwa mtu aliyeokoka kudumisha na kutembea kwa ukaribu na kwa uangalifu zaidi na Mungu wakati akiwa anaishi na mwenzi ambaye hajaokoka.

Zaidi ya hapo, kutokuamini kwa mzazi kunaathiri sana watoto dhidi ya Kristo. Kwenye familia ambazo mzazi mmoja anakuwa bado hajaokoka, ni nadra sana kwa watoto wote kuweza kumtumikia Bwana. Mungu huwa anatutaka sisi kumtumikia yeye, na Mungu anatuambia kwamba tuwalee watoto wetu ili waweze kumtumikia Yeye (Mwanzo 18:19; Kumbukumbu la Torati 6:2, 7; Malaki 2:15).

Kwenye Agano la Kale, wana wa Israeli hawakuruhusiwa kuoa au kuolewa na mtu yeyote nje ya familia ya imani.<sup>25</sup> Mungu alitambua kwamba ndoa kwa watu ambao hawajaamini itasababisha watu kuabudu miungu mingine, huku wakiharibu uhusiano wao na Mungu mmoja tu wa kweli! Agano la Kale linatuonyesha sisi kwamba hilo ndilo jambo hasa lililotokea kwa Israeli.<sup>26</sup>

Bado hata sasa, watu waliookoka/walioamini wanapaswa kuwa kwenye ndoa na watu waliookoka tu. Usikubali kuingia kwenye maelewano ya kukubaliana kubatilisha chochote kwenye jambo hili. Usitake kusamehe suala la uhusiano wa mapenzi na mtu ambaye hajaokoka.

► Wanafunzi wanapaswa wasome2 Wakorintho 6:14-18 and 1 Wakorintho 7:39 kwa ajili ya kikundi.

## **Wakati mwenzi wako siyo mtu aliyeokoka**

Mungu hataki kabisa mwamini ambaye hajaingia bado kwenye maisha ya ndoa kuoa au kuolewa na mtu ambaye hajaamini. Jambo hilo ni hakika. Lakini wakati mwenzi mmoja kutoka kwenye nyumba ya familia ambayo haijaamini anapokuja kwa Kristo kuupokea wokovu, atapaswa abakie na mwenzi wake ambaye hajaokoka, isipokuwa kama mwenzi wake atakataa kuendelea kuishi naye (1 Wakorintho 7:12-16). Katika baadhi ya matukio, wenzi walioko kwenye ndoa ambao hawajaokoka wamepata kupokea wokovu kwa sababu ya imani ya mume au mke wake aliyekwisha kuokoka (1 Wakorintho 7:14, 16; 1 Petro 3:1-2). Lakini Wakristo ambao bado ni waseja kamwe hawapaswi kufikiria kufunga ndoa na mtu ambaye hajaokoka.

---

<sup>25</sup> Kutoka 34:11-16, Kumbukumbu la Torati 7:1-6, Yoshua 23:11-13, Ezra 9-10

<sup>26</sup> Waamuzi 3:5-7, 1 Wafalme 11:1-6, Ezra 9:10-15

## Sifa za kuwekea maanani kwa Mwanandoa Mtarajiwa

Wakati wa maandalizi kwa ajili ya ndoa, watu binafsi wanapaswa kukuza sifa pambanuzi na au bainishi ambazo zitawasaidia katika kuwapata wenzi wazuri. Wanapokuwa wanatafuta mtu wa kuingia naye kwenye ndoa, wanapaswa kuangalia mtu ambaye pia anaendelea kukua katika sifa hizi zinazofanana.

1. **Ingia kwenye ndoa na mtu ambaye uhusiano wake na Kristo utakutia wewe moyo katika uhusiano wako binafsi na Kristo na kukuwezesha wewe kuendelea kukua kiroho** (2 Petro 1:5-9, 2 Petro 3:18).

Mwanamume na mwanamke hawapaswi kuingia kwenye ndoa na mwingine hadi kila mmoja aseme kwa moyo safi kwamba, "Nitaweza kuwa na uwezo wa kumtumikia Mungu vizuri zaidi nikiwa niko ndani ya ndoa na wewe kuliko mimi kubakia kuwa mseja."

2. **Ingia kwenye ndoa na mtu ambaye ana tabia nzuri.**

Katika Waefeso 5:33 wanawake wanaagizwa kuwaheshimu wanaume wao pasipo kutia maanani tabia zao, lakini hii ni rahisi sana kufanya wakati wanapokuwa wameoana na wanaume wanaostahili kupewa heshima. Tabia nzuri huwa ni pamoja na zile tabia za kusamehe, kuwa na kiasi, kuwa mnyenyekevu, kuwa na bidii pamoja na kuwajibika na kuwa na roho inayofundishika. Mtu unayetaka uingie naye kwenye ndoa hataweza kuwa mkamilifu lakini anapaswa aweze kuwa mtu wa kukua katika tabia hizi.

Mungu ana viwango vya juu kwa ajili ya viongozi wa kanisa pamoja na wake zao (1 Timotheo 3:2-4, 8-9, 11-12; Tito 1:6-8). Ikiwa kiongozi wa kanisa yuko kwenye ndoa na mwenzi ambaye ana tabia mbaya, huduma itakuwa na kipingamizi kikubwa.

3. **Ingia kwenye ndoa na mtu ambaye anajijengea sifa ya usafi na tabia njema** (1 Timotheo 2:9-10, 1 Timotheo 3:7, 2 Timotheo 2:19, Tito 1:15, Tito 2:4-5).
4. **Ingia kwenye ndoa na mtu ambaye anajifunza kibiblia** (Zaburi 119:66). Wakati wa kukabiliana na majaribu, hofu, mtazamo mbaya au nia mbaya, wanajifunza kukumbuka, kuamini, na kutii neno la Mungu (Mithali 4:4-6, Joshua 1:7-8). Wanapokabiliwa na hali ya kuwa wahitaji, hali ya hatari, taabu, au matatizo ya aina yeyote, wanakuwa wanajifunza jinsi ya kuelekeza mwelekeo wao kwa Mungu na kupata msaada wanaohitaji kutoka kwenye Neno Lake (Zaburi 119:50, 92, 114).
5. **Ingia kwenye ndoa na mtu ambaye anaweza kuwa baba au mama mzuri kwa watoto wako:** Mtu ambaye ataweza kuwafundisha njia za Mungu na jinsi ya kuishi maisha ya Kikristo yenye uthabiti mbele yao (Mithali 6:20-23, Waefeso 6:4, 2 Timotheo 1:5, 2 Timotheo 3:14-15).
6. **Ingia kwenye ndoa na mtu ambaye amechagua kushawishiwa na marafiki wacha Mungu na washauri** (Zaburi 119:63, 2 Timotheo 2:22).

## **7. Ingia kwenye ndoa na mtu ambaye ni mnyenyekevu kwa mamlaka.**

Mwanamume ana busara ya kutafuta mwanamke mnyenyekevu ili awe mke wake (Waefeso 5:22). Mwanamke naye pia anapaswa aingie kwenye ndoa na mwanamume ambaye ni mnyenyekevu kwa Mungu na kwa wale wote ambao Mungu amewaweka kwenye mamlaka juu yake katika kanisa, kwenye kazi yake, na serikalini (Warumi 13:1, Waefeso 6:5-8, Waebrania 13:17, 1 Petro 5:5). Kwa kiwango kile cha unyenyekevu wa mume wake kwa Mungu, mwanamke atakuwa amelindwa na kubarikiwa.

► Je, kati ya sifa zilizoordheshwa hapo juu, ni sifa zipi zinazoonekana kuwa za muhimu sana kwako? Je, umeshawahi kuona mifano gani inayoonyesha umuhimu wa tabia hizi?

### **Ndoa zinazoandaliwa na Wazazi**

Kwenye tamaduni nyingi, ni jambo la kawaida kwa wazazi kuandaa shughuli ya ndoa kwa ajili ya watoto wao. Kwa mfano, kwenye nchi moja kubwa, wazazi hutafuta mwenzi wa ndoa kwa ajili ya watoto wao na kufanya mazungumzo na wazazi wa upande wa pili. Kwa kawaida wao hupanga jinsi ya mtoto wa kiume na wa kike watakavyoweza kukutana. Watoto hawa wanaweza wakawa wakikutana labda mara moja, mbili au tatu, kabla ya kufanya maamuzi ya kuingia kwenye ndoa. Watoto wa kike wanaweza kuruhusiwa kuchagua ikiwa kama watakubaliana na chaguo la wazazi, lakini huwa hawapati muda wa kufahamiana vizuri.

Wazazi walio Wakristo kwenye tamaduni hizi wanapaswa wafuate maadili ya kibiblia wanapokuwa wanatafuta wenzi watarajiwa kwa watoto wao. Wanapaswa kuwatafuta wenzi wacha Mungu, wenye hekima, na waliokomaa kwa ajili ya watoto wao. Wanapaswa kutafuta watu binafsi ambao wanakuwa wamemweka Mungu kama kipaumbele kwenye maisha yao. Mambo haya yote yanatakiwa yawe ni kichocheo kikubwa zaidi kwa wazazi katika kuwachagua wenzi watoto wao na siyo zaidi sana kwenye elimu ya mtu, hadhi yake katika jamii, au kiwango chake cha fedha.

### **Ndoa za Kujitegemea**

#### **Hekima kwa wazazi na Watoto wazima Wanaochagua Wenzi wao.**

Kwenye jamii na tamaduni nyingi, zikiwemo za Ulaya na Marekani ya Kaskazini, ni jambo la kawaida kwa vijana kuchagua wenzi wao wa ndoa bila ya kupata mwongozo mwingi kutoka kwa wazazi wao.

Wazazi Wakristo walio katika tamaduni hizi wanaweza wakajihisi kwamba wana ushawishi mdogo sana kwenye maamuzi ya harusi ambayo hufanywa na vijana wao waliokomaa. Wazazi wanaweza wakajihisi kwamba hawapaswi kupinga hata kama hawajamthibitisha mtu ambaye mtoto wao amedhamiria kwa ajili ya kufunga naye ndoa. Huenda wakahofu kwamba ukosoaji unaweza kuleta matatizo ya mahusiano kwa mtoto wao na kwa mkwe wao katika siku za baadaye.

Ingawa wazazi Wakristo hawawezi kupanga ndoa moja kwa moja kwa watoto wao, wanapaswa kuwa na mchango wa kuelekeza au kushawishi uchaguzi wa mwenzi wa maisha. Wazazi wanapaswa wazungumze kuhusu mambo haya na watoto wao wakati wakiwa bado wadogo. Wazazi kwa makusudi wanapaswa watengeneze mawazo ya kufikiri na maadili ya watoto wao. (Kumbukumbu la Torati 6:5-9). Je, wewe kama mzazi unawezaje kufanya hili?

- 1. Kuwa mfano mzuri wa mwenzi na mzazi mcha Mungu.** Isipokuwa uwe ni mfuatiliaji wa kanuni za Mungu katika maisha yako mwenyewe, maagizo yako ya maneno tu kwa watoto wako hayatakuwa na maana yeyote. Kama mfano wako haulingani na kile unachokisema, watoto wako watasikiliza mfano wako tu badala ya maneno yako.
- 2. Fanya msisitizo wa viwango vya kimungu kwa kusudi la maisha, kusudi na maana ya ndoa, na ni nini kitazamiwe kutoka kwa mwenzi wa ndoa (Zaburi 34:11-12).** Wakati tunapokuwa tunatazama, tunasikiliza, na kuangalia kanuni za kidunia, tunakuwa tunawafundisha watoto wetu kwamba dunia ndiyo kielelezo chetu badala ya Neno la Mungu kuwa kielelezo chetu, Badala ya kufanya hivyo, tunapaswa tustawishe matamano ya kimungu ndani ya watoto wetu kwa kuwadhihirishia watu/kuvuta nadhari ya watu ambao wanafuata mipango ya Mungu iliyo mizuri. Tunatakiwa tuonyeshe matokeo mazuri ambayo watu hawa wanayafurahia kwa sababu ya utii wao kwa Mungu.
- 3. Wafundishe watoto wako kwamba tabia ni kitu cha kujali na kuzingatia sana kuliko kitu kingine chochote wakati wa kuchagua mwenzi.** Kuanzia wakati wangali watoto wadogo, wafundishe watoto wako kutazama kwa ajili ya thamani ya tabia njema kutoka kwa watu wengine, zaidi ya miili ya kuvutia au haiba. Wafundishe kutambua kama wenzao walio nao ni wanaowajibika au kama ni wavivu, watiifu au ni waasi, waaminifu au ni wadanganyifu. Wafundishe jinsi ya kujitunza zaidi na tabia zao wenyewe kuliko jinsi ya kutunza mionekano yao.

Ikiwa kama wazazi wanataka watoto wao wawatambue wakati wanapokuwa wanachagua wapenzi wao wakiwa vijana wakubwa, wanapaswa wawafundishe watoto wao wakiwa wadogo kwamba kuwasikiliza baba na mama ni jambo la busara sana! (Mithali 1:8.). Kwenye ujana au utu uzima ni kuchelewa sana kufundisha jambo hili; wazazi ni lazima wafundishe jambo hili wakati watoto wao wangali wakiwa bado wadogo (Mithali 4:3-9). Kuwasikiliza wazazi wenye kumcha Mungu ni njia ya Mungu kwa ajili ya watoto kupata ulinzi na baraka.

Kama ilivyojadiliwa katika Somo la 4, wazazi wana wajibu wa kuwasaidia vijana wao wadogo kuyaendesha mahusiano yao kwa usafi wa maadili mema. Ili kufanya hivi, unapaswa tayari uwe una uhusiano mzuri na wa wazi na mtoto wako, ambao unawafanya wawajibike kwa hiari kwako na kukubaliana na ushauri wako. Aina hii ya uhusiano inajengewa msingi wake kwenye miaka ya mwanzo ya utoto unapowafundisha kwa bidii, kuwafanyia mazoezi, kuwaongoza, na kila siku kuwaweka kwenye hali ya nidhamu.

## **Hekima kwa ajili ya Kijana Anayechagua Mwenzi Mtarajiwa**

Mungu anayo hekima kwa ajili ya vijana waliookoka ambao ni lazima wafanye maamuzi yao wenyewe kuhusiana na ndoa. Hapa kuna ushauri mdogo wa hekima kwa ajili ya kufanya maamuzi mazuri:

### **(1) Kataa uchaguzi wowote usiokuwa wa kibiblia**

Kwa mfano, tunajua kwamba siyo mapenzi ya Mungu kwa watu waliookoka kufunga ndoa na watu wasiookoka, kwa hiyo hatupaswi hata kufikiria kuwa na uhusiano wa kimapenzi na mtu ambaye hajaokoka.

### **(2) Omba kwa ajili ya kupewa hekima (Mithali 2; Yakobo 3:13, 17).**

Wakati tunapokuwa tunatafuta kumwelewa Mungu kwa moyo wetu wote, anafurahishwa kutupatia sisi hekima. Hekima inapatikana kwa kujifunza kwa uangalifu na kutii Neno la Mungu. Mungu pia hutupa sisi hekima kupitia ushauri wa watu wanaomcha Mungu. Kukubaliana na hekima ya Mungu hutulinda sisi dhidi ya dhambi na madhara. Hekima yake hutupa sisi baraka zake, na hutupa fursa ya kupata uzoefu wa mpango bora kwa ajili ya maisha yetu. Jambo la muhimu zaidi ni kwamba tunapofanya maamuzi ya hekima, tunamtukuza Baba yetu wa mbinguni.

### **(3) Fuata uongozi wa Roho Mtakatifu (Zaburi 119:133, Mithali 3:5-7, Yereimia 10:23).**

Kamwe, Roho Mtakatifu hatakaa atuongoze sisi katika kutotii Neno la Mungu. Badala yake, anatukumbusha kwa uaminifu (Yohana 14:26, Yohana 16:13-14). Anawalinda watoto watiifu wa Mungu wa Mungu kutokana na dhambi na kuwazawadia maisha na amani (Warumi 8:5-6, 13-14; Wagalatia 5:16, 22-25). Huenda siku zote usijue kwa undani mapenzi ya Mungu katika kila hali, lakini unapaswa kufuata kile ambacho unakijua kwa uhakika. Unajua kwamba Mungu anakutaka wewe mwenyewe uwe mwaminifu kiroho na kimaadili. Unajua kwamba Mungu anakutaka wewe uepukane na vitu fulani na ufuate vitu fulani. Fanya kile ambacho unajua ni sahihi wakati huo ukiomba kwa ajili ya kupata mwelekeo/mwongozo wa Mungu.

### **(4) Kuwa makini sana na ushauri unaotoka kwa watu wanaomcha Mungu.**

Vijana wenye wazazi wao wanaomcha Mungu wanapaswa watafute hekima yao. Wanapaswa wawe wazi na waaminifu kwa wazazi wao kuhusiana na wanavyofikiria katika masuala yao ya ndoa. Wanapaswa wazingatie kwa umakini wa karibu mahangaiko yoyote ambayo wazazi wao wanakuwa wanayo. Mungu amewapa wazazi wao ili wawalinde dhidi ya madhara yeyote na kuwatendea mema. Vijana wanapaswa wasipoteze fursa za kubarikiwa kupitia njia hizi.

Vijana wengi wa Kikristo hawana mawaidha wanayopokea kutoka kwa familia zenye umri mkubwa katika kumcha Mungu. Kwa hakika wanapaswa wapokee ushauri kutoka kwenye familia zenye tabia za kimungu ambazo zimeonyesha uwezo wa kufanya maamuzi yenye hekima na matokeo yakawa yanakuwa mazuri.

Hata hivyo, vijana hawapaswi kudharau kupokea mawaidha kutoka kwa wazazi wao, hata ikiwa kwamba wazazi wao siyo watu wanaomtumikia Bwana. Inawezekana kukawepo na baadhi ya matukio ambapo kijana anatakiwa kwenda kinyume na matakwa ya wazazi wake ambao hawajaokoka/hawajaamini ili kumtii Mungu, lakini jambo hili kamwe halipaswi lifanyike kwa kuasi (1 Samuel 15:23) au kukosa heshima (Kutoka 20:12). Bila kujali wazazi wamekaaje kwa Mungu, Mungu ana uwezo wote wa kulainisha mioyo yao ili waweze kuwa ni baraka kwenye ndoa ya mtoto wao wa kiume au wa kike. Kuomba pamoja na kumngojea Bwana abadilishe mioyo ya wazazi wao kutapima na kuimarisha imani ya huyu mtoto wa kiume au wa kike.

► Jadili kanuni au mifano kutoka katika maandiko kuhusu ushiriki wa wazazi katika maamuzi ya ndoa. Je, wazazi wanapaswa wafanye nini ili kushawishi mchakato wa kuchagua mwenzi? Je, mtazamo wa kijana mtu mzima aliye Mkristo dhidi ya wazazi wake unapaswa uweje kwenye maamuzi ya ndoa?

### **Urafiki wa Wanandoa watarajiwa kabla ya Ndoa**

Ikiwa uwepo wa kipindi cha uchumba ni jambo linalowezekana, ni bora zaidi kwa mwanamume na mwanamke kuutumia muda wake dhidi ya mwenzake katika mazingira mbalimbali tofauti. Hali hii inawawezesha kila mmoja kujua mwenzake ana tabia gani, anawasilianaje na watu wengine, anavyowajibika katika hali zinazojitokeza zisizotarajiwa, na jinsi anavyoitikia katika hali mbalimbali ambazo hazikutegemewa. Katika wakati huu kwa pamoja, kunaweza kuwasaidia kuelewa kama watakuwa wenzi wa ndoa wanaofaa.

### **Msimamo wa Usafi**

► Wanafunzi wanapaswa wasome 1 Wathesalonike 4:1-8 na 2 Timotheo 2:19-22 kwa ajili ya kikundi.

Kwa upendo Mungu aliwaumba wanaume na wanawake wakiwa na matamano na uwezo kwa ajili ya kuwa na vitendo vya kimwili kimapenzi na mihemuko. Kwa sababu ya haya matamano, marafiki ambao wanatafuta kufunga ndoa wakati ujao lazima wawe waangalifu kwenye mahusiano yao wenyewe. Mungu anakusudia matamano haya yakamilishwe ndani ya agano la kipekee la maisha yote ya ndoa.

Kama mwanamume na mwanamke kwa makusudi hawatajikusisha wenyewe katika uangalifu na usafi, kuna uwezekano kwamba wataacha kumtii Mungu kwa kufuata hisia zao wakati wa kipindi cha majaribu. Kutotii matakwa ya Mungu ya usafi wa kimaadili kunaumiza kwa njia nyingi na huathiri sana watu wengi, siyo tu kwa mwanamume na mwanamke peke yao. Kutotii matakwa ya Mungu kwa ajili ya usafi wa kimaadili kunasababisha majuto, hali ya kufungwa, kujisikia hatia, aibu, woga, kutoaminiana, na kuvunjika kwa mahusiano.

Kuna baraka nyingi kwa wale wanaofuata mpango wa Mungu wa usafi wa kimaadili. Wale ambao wanamheshimu Mungu kupitia utii wanaweza kupata kila lililo jema ambalo

Kumtii Mungu ni kuamini kwamba anajua na anataka kile kilicho chema sana kiwe kwa ajili yako. (Ona Mithali 3)

amekusudia kwa ajili yao. Badala ya madhara ya kutotii kwa kukosa utiifu, watakuwa na furaha na amani. Watakuwa na uwezo wa kila mmoja kumwamini mwenzake. Watakuwa na uwezo wa uhusiano wenye kustawi na Mungu pamoja na wao wenyewe.

Baraka hizi ni motisha wenye nguvu sana kwa ajili ya kuufuata mpango wa Mungu wa kwa ajili ya usafi wa kimaadili. Hata hivyo, motisha mkubwa zaidi kwa mtu aliyeokoka kwa ajili ya uangalifu katika eneo hili inapaswa iwe ni matamanio yao ya kumletea Bwana Yesu heshima kwenye kila eneo la maisha. Wenzi walioko kwenye uchumba wanapaswa wawe wanajiuliza, 'Je, tunawezaje kumheshimu Mungu **vizuri zaidi** kwenye uhusiano wetu? Je, tunawezaje kumletea Yesu utukufu **zaidi**?'

Ili kuepuka matendo yasiyokuwa masafi, wenzi walio wachumba wanapaswa wawe na tahadhari kutokana na ongezeko lolote la uhusiano wa kimwili linalojitokeza kati yao. Wanapaswa waepuke vipindi virefu vya kukaa peke yao kwenye maeneo ambayo wanadhania kwamba hakuna mtu mwingine atakayejua watakachofanya. Wanandoa hushindana na majaribu wakati kugusana kimwili kunapotokea kuwa ni muhimu katika mahusiano yao kuliko mawasiliano. Wanaweza wakashindwa kushughulika ipasavyo na masuala ya kiroho na kimahusiano kwa sababu fahamu zao na mioyo yao inakuwa imeshamiri matamanio ya kimwili. Mwanzoni mwa mahusiano, wote kwa pamoja fanyeni maamuzi kuhusu ni mambo gani mahususi mtayafanya (na yale ambayo hamtayafanya) kwenye mahusiano yenu kabla ya ndoa. Mipango yenu inapaswa iweze kumlinda kila mmoja dhidi ya kutenda dhambi, ikusaidie kuwapenda wenzi wako wa baadaye, na kukuwezesha kumheshimu Mungu. Jikabidhini kabisa ninyi wenyewe kwenye mpango wenu. Wajibika kwa washauri wacha Mungu na sikiliza ushauri wao na maonyo yao. Kwa pamoja tumieni muda wenu katika kushirikiana na marafiki wanaomcha Mungu na wanafamilia.

Kujidhibiti kwako kwa leo ni zawadi kwa mwenzi wako wa baadaye. Mwenzi wako atajihisi kuwa anayelindwa na kuheshimiwa kwa sababu ya uchaguzi wako wa kumtii Mungu. Mwenzi wako atajihisi kuwa anayependwa sana.

## **Shughuli Zinazokuza Ukuaji**

Kwenye uchumba ndiyo wakati wa kufahamiana, lakini unapaswa pia kunatakiwa kuwepo na muda wa kukua. Yafuatayo hapa ni baadhi ya mawazo kuhusu shughuli za kufanya ambazo wachumba wanaweza kufanya kwa pamoja:

- Shughulika na kazi za miradi.
- Jifunzeni ujuzi ambao ni mpya kwenu ninyi wote wawili.
- Soma na jadili vitabu vyenye maana.
- Jifunze au kariri vifungu sawa vya maandiko, kisha vijadili.
- Pageni na kuendesha shughuli za huduma kwa pamoja.
- Kuweni walezi wa watoto kwa pamoja.
- Tumieni sehemu ya muda wenu kwa ajili ya kukaa na familia ya kila upande.

Shughuli hizi zitakuwa na matokeo yafuatayo:

- Zitasaidia katika kufahamiana zaidi kwa mwanamume na mwanamke.
- Zitawasaidia kujua kama wao ni wenzi wanaofaa mmoja kwa mwenzake.
- Kuongeza uwezo wa kila mmoja kuwasiliana na mwenzake.
- Kutawasaidia kukua.

► Je, ni kanuni na mawazo gani ya uchumba ambayo ni mapya kwako? Je, ni kwa jinsi gani watu waliookoka/waumini katika muktadha wako wanavyoweza kutumia kanuni kibiblia kwa ajili ya usafi wa kimaadili na kumheshimu Mungu katika mahusiano kabla ya ndoa?

### **Mada za Kujadili kabla ya Ndoa**

Kwenye tamaduni ambapo wanandoa hufahamiana kama sehemu ya mchakato wa kufanya maamuzi, kuna masuala ambayo yanapaswa yajadiliwe kabla ya harusi kufanyika.

Kwenye tamaduni kadhaa, mipango ya ndoa hairuhusu mazungumzo hayo ya kina kabla ya harusi. Ili kuwepo na ukamilifu wazazi wa pande zote hushirikishana taarifa kuhakikisha kwamba vijana wao wanandoa wanaendana vizuri kwa pamoja.

Katika hali nyingine ambazo mwanandoa mmoja anafunga ndoa akiwa anamfahamu mwenzake kwa sehemu kidogo sana, wanatakiwa wayafanyie kazi masuala haya baada ya kuwa wameoana tayari, lakini masuala haya hayawezi kubatilisha chaguo lao kwa sababu kila mmoja tayari alishaweka ahadi kwa mwenzake pamoja na Bwana.

Kadiri mwanamume na mwanamke wanavyofanana katika imani, asili, utamaduni, malengo ya maisha, na maadili, ndivyo wanavyoweza kuwa sambamba zaidi katika ndoa. Ikiwezekana, wanandoa wanaofikiria kufunga ndoa wanapaswa kutumia muda kujadil:

- Malengo yao ya maisha
- Maadili ambayo ni muhimu kwa kila mmoja
- Utoto wao wenyewe na jinsi walivyolelewa
- Mahusiano yao na wazazi wao na jamaa wengine
- Mafundisho binafsi ya imani na desturi za imani, kama vile nidhamu binafsi za kiroho, kuhudhuria ibada za kanisa, matendo ya kuhudumu na huduma
- Uelewa wao na imani yao kuhusiana na mambo mengi ya kulea watoto, ikiwa ni pamoja na kuwafundisha, kuwaweka watoto katika nidhamu, na kuwafundisha kumjua na kumtii Kristo
- Maoni yao kuhusu fedha, ikiwa ni pamoja na matumizi, na kuishi katika nyakati ngumu za matatizo
- Uwepo wowote wa matatizo yeyote ya kimwili au kiakili au ulemavu wowote walio nao, na matatizo ya kiafya ambayo ni ya kawaida kwenye familia zao



Katika sehemu hii ya uhusiano, utapaswa kuzungumzia juu ya matatizo katika maisha na mada za maisha magumu. Mkishaweka ahadi zenu kwa Mungu na kila mmoja na mwenzake, mnakuwa mmeoana kwa ajili ya mema au mabaya. Katika ndoa, mume na mke hushirikishana yote jinsi walivyo na yote waliyo nayo kila mmoja, kwa hiyo mawasiliano ya uaminifu kuelekea kwenye ndoa ni ya muhimu sana. Mawasiliano yanapaswa kuzidi kuwa ya wazi na ya kina. Ikiwa mtu unayetaka kuwa kwenye ndoa na mwenzake hayuko tayari kuwa wazi kuzungumza kuhusiana na mambo muhimu yanayowahusu, hiyo ni ishara ya hatari sana.

Muda mfupi kabla ya kufanyika kwa harusi yao, wanandoa wanapaswa wajiadili mambo yanayohusiana na imani zao, matarajio yao, na matamania yao kuhusiana na mahusiano au kujamiiana wakiwa ndani ya ndoa. Kujadili mapema mambo ya kujamiiana wakati wa mahusiano kunaweza kusababisha majaribu yasiyo ya lazima, lakini ni muhimu kuyazungumzia muda mfupi kuelekea ndoa kufungwa.

Mambo ya msaada kwa mwanamume na mwanamke wanaoingia kwenye ndoa:

- Kufanana kiakili
- Kuwa na matarajio yanayofanana katika maisha ya ndoa
- Kuwa na mafundisho ya imani na mazoea ya kiroho yanayofanana
- Kuwa na maadili na mazoea yanayofanana kwa ajili ya matumizi ya fedha na muda
- Kuwa na ushirikishwaji na uelewa wa kina wa maisha na ukuzaji wa watoto

### **Ishara za Hatari katika Uchumba**

John Drescher anaorodheha matatizo manane ambayo yanaweza kusababisha mwanamume au mwanamke kufikiria kwa dhati kukatisha kabisa uhusiano wa uchumba:<sup>27</sup>

- 1. Wewe na rafiki yako mmekuwa na hali ya kuzozana mara kwa mara.**
- 2. Unakwepa kujadili wewe na mwenzako mambo yaliyo nyeti** kisa tu kwa sababu una wasiwasi wa kumwumiza mwenzako kimhemuko. Kama utajiambia mwenyewe, “Ni bora zaidi nisizungumze lolote kuhusiana na jambo hili” – hii ni alama ya hatari. Ndoa ni kumaanisha kwamba unawajibika kujadili mambo mengi kwa ujasiri na upendo.
- 3. Uhusiano wako unaongezeka kuwa wa kimwili zaidi.** Kadri mtakavyokuwa mnaendelea kuhusika zaidi kimwili mkiwa ni wenzi ambao bado hamjafunga ndoa, mtajifunza kwa kiwango kidogo sana kuwasiliana kwa maneno, sauti, sura ya uso, na lugha ya mwili. Kugusa mwili zaidi na kuzungumza kidogo kunaweza kuwa ishara halisi ya hatari.

---

<sup>27</sup> Nukuu kutoka kwa John Drescher, *For Better, For Worse: A Premarital Checklist*, (Morgantown, PA: Masthof Press, 1999), 30-31.

4. **Ikiwa unahisi kwamba uko kwenye uhusiano kwa sababu ya hofu ya aina fulani.** Kwa mfano, "Ninataka nisishe uhusiano, lakini nachelea nisije nikamkwaza mtu yeyote."
5. **Kama rafiki yako hayuko tayari kukubaliana na lawama.** Je, rafiki yako anapokosea, huwa anakataa kuomba msamaha? Huo ni uharibifu kwa sasa, na utakuwa ni uharibifu mbaya zaidi baadaye, endapo mtaoana.
6. **Kama wazazi na marafiki wako muhimu watakuwa na upinzani kuhusu uhusiano wako na uwezekano wa kuwepo kwa ndoa.** Hii kwa hakika inaweza kuwa ni ishara ya hatari ambayo itakulazimu wewe ufikirie kusitisha uhusiano. Ni kweli kwamba hauingii kwenye ndoa na mtu tu, bali unaingia kwenye familia ambayo itakuwa na athari kwenye usalama na mafanikio ya ndoa yako.
7. **Rafiki yako ni mtu wa wivu mwingi unaopitiliza au wa kutilia mashaka.** Kwa mfano, kama rafiki atakuwa anahoji sana maneno yako, au kwa maneno mengine ni kwamba hakuamini, hii ni ishara ya hatari. Kwa hiyo, sitisha uhusiano wako wakati unapokuwa ungali unajimudu kama rafiki yako ni mwenye wivu wa kupitiliza na asiyekuamini.
8. **Kama hisia zako hazikufanyi kujisikia kuwa na amani ya moyoni kuhusiana na uhusiano wako.** Hali hii itatokea wakati hasa unapokuwa uko peke yako na rafiki yako. Unajikuta una mawazo au maono kwamba, "Jambo fulani ni baya." Kuwa makini na hali hiyo ya ukosefu wa amani ya moyo!

### Hitimisho

Mithali 24:3-4, "Nyumba hujengwa kwa hekima, Na kwa ufahamu huthibitika, Na kwa maarifa vyumba vyake hujazwa vitu vyote vya thamani na vya kupendeza."

Chaguo la mwenzi ni moja ya chaguzi muhimu sana katika maisha ambazo mtu anaweza akafanya. Mungu anapenda kusaidia watoto wake kufanya chaguzi za busara wanatafakari na kutaka kuzoeana na wenzi watarajiwa.

### Kwa ajili ya Majadiliano ya Kikundi

► Je, ni maudhui gani mapya kwako ambayo umeyapata kutoka katika somo hili? Je, kwa nini yamekuwa ni muhimu kwako? Je, kuyaelewa maudhui haya kutakusaidiaje katika mahusiano yako? Je, kwa kuyaelewa vizuri haya maudhui kutaathiri vipi huduma yako kwa watu wengine?

## **Maombi**

Baba wa Mbinguni,

Asante kwa kutuongoza na kuwa mtoaji kwa ajili yetu sisi. Asante kwa ajili ya kanuni zako ambazo umetupa sisi kupitia katika Neno lako ambalo linatusaidia sisi katika kufanya chaguzi za busara kuhusu maamuzi muhimu katika maisha yetu.

Tunakuomba utusaidie sisi kuwa na vipaumbele vyako tunapokuwa tunachagua wenzi wetu. Tusaidie katika kuwa wanaume na wanawake unaoututaka sisi tuwe. Tusaidie tuwe wanyenyekevu na wenye kusikiliza ushauri wa watu wanaomcha Mungu.

Tunataka tuishi maisha ya utakatifu, yenye kuzaa matunda ambayo yatakuletea wewe heshima.

Ameni

## **Kazi za Kufanya**

(1) Chagua sehemu yeyote kutoka katika somo hili ambalo utafundisha kwa muktadha wa huduma yako. Unaweza ukawa unamfundisha mtu mmoja au kikundi cha vijana. Mjulishe kiongozi wako wa darasa utakapokuwa umemaliza huduma ya kufundisha nje ya darasa.

(2) Kwa maandishi, elezea tabia za uhusiano wa mwanamume na mwanamke wanaomcha Mungu kutoka kwenye utamaduni wenu ambao bado wanatafakari kuhusu kuingia kwenye ndoa au ambao tayari wamepanga kuingia kwenye ndoa.

(3) Aidha uwe uko kwenye ndoa au laa, fanya marejeo ya orodha iliyotolewa kuhusu sifa za kuzingatia wakati wa kumchagua mwenzi muhimu. Soma kila andiko lililoandikwa kwa ajili ya kufanya marejeo. Mwombe Mungu akusaidie kukuonyesha ni kwa jinsi gani unapaswa kukua.

(4) Kama wewe ni mseja na una mpango wa kuingia kwenye ndoa wakati fulani ujao, tengeneza orodha yenye kuelezea ni mambo gani unayotaka uyaone kwa mwenzi wako mtarajiwa. Hautahitajika kumshirikisha jambo hili kiongozi wako wa darasa, lakini mtaarifu tu kwamba umeshamaliza kuifanya kazi iliyotolewa.



# Somo la 7

## Kustawisha Ndoa iliyo Imara

### Malengo ya Somo

Hadi kufikia mwishoni mwa somo hili, mwanafunzi atapaswa:

- (1) Kuelewa uhusiano kuhusu mpango wa Mungu wa mahitaji ya mwanamume na mwanamke na maelekezo ya Mungu kwa ajili ya mahusiano katika ndoa.
- (2) Kudhihirisha jinsi ambavyo waume na wake wanavyotimiza mahitaji ya kila mmoja kwa kutii kanuni za Kimaandiko.

### Kukubali tofauti za Kibinafsi

Siyo jambo la siri kwamba wanaume na wanawake wanatofautina kwa njia nyingi! Wanaume wengi hujitahidi kujieleza kuhusu mihemuko yao, wakati wanawake wengi huona kwamba kuonyesha udhihirisho wa mihemuko ni sehemu ya mawasiliano ya kweli. Wanaume hupenda kujitolea kwenye mambo yenye hatari zaidi, wakati wanawake kwa kawaida wanapenda kuhusika na mambo ya usalama. Wanaume kwa asili yao huvutiwa sana na uzuri wa maumbile ya mwanamke, wakati wanawake wengi kwa asili yao wanavutiwa na urafiki wa mihemuko. Tofauti nyingi zaidi zinaweza kuorodheshwa.

Kando na tofauti hizi zilizopo kati ya jinsia hizi, mke na mume wanazo tofauti nyingi kwenye mambo ya utu. Yawezekana mmoja akawa anafurahia kuwa na watu wengine, lakini wengine wakawa wanafurahia kukaa wapweke. Kuna mambo madogo wanayopendelea, kama vile ni kwa jinsi gani kiasi cha mwanga kiwepo kwenye nyumba au joto la chumbani liwe kiasi gani. Ndoa nyingi zinatatizwa na kutoelewana kuhusu jinsi fedha zitakavyoweza kutumika. Tofauti hizi hazimaanishi ni lazima ziwe tofauti za tabia; zinaweza tu kuwa ni tofauti za nafsi ya mtu binafsi na maoni.

Kwa kuwa ndoa inamwunganisha mwanamume na mwanamke, wakati mwingine watu hufikiri kwamba tofauti zilizopo zinapaswa zifikie mwisho. Mtu anaweza akafikiri kwamba tofauti alizo nazo mwenzi wake ni kasoro zinazopaswa kurekebisha. Kila mwenzi atakuwa anafanya bidii au jitihada za kujaribu kubadilisha maoni, tabia na mambo ambayo mwenzake anayapendelea.

Ni kweli kwamba kila mtu anapaswa aweze kukua na au kujiendeleza kwa sababu ya uhusiano. Hata hivyo, wakati mwingine majaribio yetu ya kutaka kumbadilisha mtu yanatokea kuonekana kuwa ni shambulio la mambo binafsi ya mtu. Katika ndoa zenye nguvu/afya, kila mwenzi husitawisha nidhamu ya kumpenda, kumheshimu, kumthamini, na kumhudumia mwenzake.

► Je, kuna tofauti gani nyingine kati ya mwanamume na mwanamke? Je, kuna tofauti gani nyingine kwenye nafsi ya mtu binafsi ambazo watu wengine wanapaswa wazikubali?

### Kuchagua Kutumikia

Kwenye kitabu chake, *Ndoa takatifu (Sacred Marriage)*, Gary Thomas anasema,

*Ndoa iliyo nzuri siyo kitu unachokitafuta, bali ni kitu ambacho unapaswa ukifanyie kazi. Inahitajika jitihada kubwa. Ni lazima uusulubishe ubinafsi wako. Wakati mwingine ni lazima ukabiliane, na nyakati nyingine utapaswa kukiri. Zoezi la msamaha ni muhimu. Haikataliwi kwamba ni kazi ngumu, lakini hatimaye ni kazi inayolipa. Hatimaye, inatengeneza uhusiano ulio katika uzuri, uaminifu, na kusaidiana kwa faida ya kila mmoja.*<sup>28</sup>

Thomas anamnukuu Otto Piper:

Ikiwa ndoa...ni tukio la kukatisha tamaa kwa watu wengi, sababu inaweza ikapatikana kwenye [kutojali] kwa imani yao. Watu hawapendi kuambiwa ukweli kwamba baraka za Mungu zinaweza tu zikapatikana na zikafurahiwa wakati zinapokuwa zinatafutwa kwa kung'ang'ania (Mathayo 7:7; Luka 11:9). Kwa hiyo, ndoa kwa pamoja ni zawadi na jukumu ambalo linapaswa likamilishwe.<sup>29</sup>

Mara nyingi ndoa hushindwa kustawi kwa sababu tu waume na wake wanafikiria mahitaji yao wenyewe tu badala ya kujaribu kutimiza mahitaji ya kila mmoja wao.

Sisi **hatuwezi** kukidhi kabisa kwa ukamilifu wote mahitaji ya wengine. Baba yetu wa mbinguni peke yake ndiye mwenye uwezo kamili wa kututosheleza katika mambo tunayohitaji na matamano yetu, na ndiyo sababu Yesu alikuja. Kusudi lake ni ili atukomboe sisi, atujaze na Roho wake - Roho Mtakatifu – na atulete kwenye uhusiano wa kina na unaotosheleza pamoja na "Abba, Father" (Warumi 8:14-15; Wagalatia 4:6).

Hata hivyo, mojawapo ya kusudi la Mungu katika ndoa ni kwamba iwe ni mahali pa kujifundishia utumishi; aina ile ya utumishi unaofanana tunaouona ndani ya Yesu (Yohana 13:14). Mungu anataka akuze ndani ya kila mume na mke moyo wa unyenyekevu wa mtumishi ambaye anawajibika kwa ajili ya watu wengine (Wafilipi 2:3-8).

Baadhi ya ndoa zilizo nzuri, na zenye furaha zipo kwa sababu mwenzi mmoja alichagua kusahau kabisa ubinafsi na kumhudumia mwenzake kupitia hali ngumu isivyo kawaida ya magonjwa, kushindwa, misiba, au mambo ya kuhuzunisha. Baadhi ya waume hutoa ushuhuda kwamba maisha yao yangewezekana yakawa yameharibika kabisa kama wake zao wangukuwa hawaombi kwa ajili yao, kuwasamehe, kuwawajibisha kwa wema, na kuwapenda bila masharti yeyote katika vipindi ambavyo vilikuwa hata havifai kupendwa kabisa. Wake wengine hushuhudia kwamba ilikuwa ni kwa ajili ya uvumilivu wa waume zao

---

<sup>28</sup> Gary Thomas, *Sacred Marriage*, Grand Rapids: Zondervan, 2000), 133.

<sup>29</sup> Ibid.

ambao uliwawezesha kushinda mihemuko ya uharibifu iliyokuwa ikisababishwa na baba mnyanyasaji au kiwewe kingine. Kwa kuwa tunaishi katika dunia iliyoanguka na ya watenda dhambi, ambako viumbe vyote vinaugulia (Warumi 8:22), kila mtu aliyeko kwenye ndoa amebeba vidonda na makovu. Lakini neema ya Mungu inaweza ikatuwezesha sisi kuwa watu tunaojali na kuwatunza watu wengine na kuganga vidonda/majeraha yao!

Kila mmoja wetu alizaliwa akiwa katika hali ya ubinafsi. Kwa asili tunajali zaidi mahitaji yetu wenyewe kuliko mahitaji ya wengine, Neema ya Mungu yenye kuokoa na kutakasa inaweza ikatubadilisha sisi kupitia Roho Mtakatifu akaaye ndani yetu hadi tutakapokuwa watu tunaoweza kutanguliza mahitaji ya watu wengine kwanza kuliko mahitaji yetu. Ndoa huwa zinastawi wakati kila mwana ndoa anapokuwa makini kwenye mahitaji na matamano ya mwenzi wake.

► Je, inamaanisha nini kuchagua kutumika?

### **Mahitaji ya Msingi ya Mume na Mke**

Mungu alipanga wanaume na wanawake wawe na mahitaji na matamano tofauti. Hii inamaanisha kwamba mwanamume hapaswi kuhisia kwamba mwanamke atakuwa na furaha kwa mambo yanayofanana na yale yanayompatia yeye kuwa na furaha. Mwanamke hapaswi kuhisia kwamba mwanamume wake anataka atendewe kama vile na yeye anavyotaka atendewe. Ni wazi kwamba, baadhi ya njia za kupenda na kuheshimu zinapaswa ziwe sawa kwa wote, lakini bado wanaume na wanawake kila mmoja anakuwa na mahitaji fulani ya kipekee.

Kama tutaelewa mahitaji maalumu ya wanaume na wanawake, tunaweza pia tukaelewa jinsi ya kutimiza mahitaji ya mwenzi mwingine. Inasikitisha kwamba mabishano na mijadala mingi kati ya waume na wake hayatatui matatizo kwa sababu kila mtu anashindwa kuelewa mahitaji ya mwingine. Kila mmoja anaweza akawa na hasira na mwenye chuki kwa sababu mwenzake haelewi.

Watu wote wanahitaji kupendwa na kuheshimiwa, lakini kuna tofauti kati ya mwanamume na mwanamke. Hitaji la msingi la mwanamke ni upendo, na hitaji la msingi la mwanamume ni heshima.<sup>30</sup>

► Je, umechunguzaje kwa makini tofauti hii iliyopo kati ya mahitaji ya wanaume na wanawake?

### **Jinsi Mume atakavyoonyesha Upendo kwa Mke wake**

Waefeso 5:25, 28 inasema kwamba, "Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda Kanisa, akajitoa kwa ajili yake... Vivyo hivyo imewapasa waume nao kuwapenda wake zao kama miili yao wenyewe...."

---

<sup>30</sup> Kitabu kiitwacho *Love and Respect* cha Dr. Emerson Eggerich kimekuwa ni cha msaada sana katika sehemu hii.

Mume anapaswa kumwambia mke wake mara kwa mara kwamba anampenda, hapaswi kudhania kwamba anajua kwamba anampenda. Anapaswa pia amwonyeshe upendo wake zaidi sana kuliko maneno tu.

Ni lazima aonyeshe upendo kwa njia ambazo ni muhimu kwa wake. Mume hapaswi afikirie kwamba mke wake ana hisia za kwamba anapendwa kwa sababu tu anamwonyesha upendo katika njia anazoziona kwake kwamba ni muhimu. Mahitaji ya mke wake ni tofauti na mahitaji yake.

### **(1) Mume humpenda mke wake kwa kumpa ulinzi.<sup>31</sup>**

Mke huwa anataka kujua kwamba mume wake anamlinda kimwili na kimhemuko. Mume anapaswa kushughulikia migogoro yoyote inayosababishwa na majirani. Mume anapaswa ahakikishe kwamba makazi yao ni sehemu salama ya kuishi. Atapaswa azungumze upande wake wa kumtetea anapokuwa anakosolewa na watu wengine kwa mambo yasiyostahili, hata kama ikiwa ni wanaukoo. Hapaswi kumpiga mkewe au kumdhuru kimwili kwa njia yeyote ile kama njia ya kumfanya akutii wewe. Anapaswa afanye kila linalowezekana kuhakikisha anatoa mahitaji ya familia yake. Kama mwanamume ni mzembe katika mambo ya fedha, mke wake atakuwa na hisia kwamba hajali kuhusu mahitaji ya familia yake.

### ***Dondoo za Kifedha kwa ajili ya Waume***

Matatizo ya kifedha ni mojawapo ya sababu kuu za vianzo vya migogoro ndani ya ndoa. Waume wanapaswa wafanye yafuatayo:

- Kataa kufanya jambo lolote lisilokuwa la uaminifu au la kifisadi kwa ajili ya kujipatia faida; kumbuka kwamba uko chini ya mamlaka ya Mungu.
- Toa fungu lako la kumi kwenye kanisa kwa sababu unamwamini Mungu pia kutoa kwa ajili yako.
- Tafuta chaguo lililo bora zaidi la ajira lakini uwe tayari kufanya kazi ambayo yaweza isiwe ya kupendeza kwa sasa.
- Aidha kama umeajiriwa au laa, tafuta kazi ya kufanya kila siku ili iweze kukusaidia wewe mwenyewe na watu wengine.
- Usipende kutumia fedha iliyo kwa ajili ya kesho kwa kukopa fedha leo.
- Unapotumia fedha kwa ajili ya jambo la furaha, wahusishe mke na watoto wako.
- Weka akiba kwa ajili ya mambo ya kawaida ya kila wakati kama vile kodi kwa ajili ya nyumba uliyopangisha kuishi.

---

<sup>31</sup> Kuna maandiko mengi ambayo yanahusiana na ukweli huu ikiwa ni pamoja na Waefeso 5:28-31, Wakolosai 3:19 (ulinzi wa mihemuko), 1 Timotheo 5:8 (utoaji wa kimwili), Nehemia 4:13-14 (ulinzi wa kimwili), na 1 Timotheo 2:14 (ulinzi wa kiroho).



- Wekeza fedha kwa ajili ya kuendeleza hali yako kuliko kutumia fedha kwa ajili ya mambo ya starehe.

## **(2) Mume humpenda mke wake kwa kujiwekea akiba kwa ajili yake.**

Mume anapaswa kujiweka yeye mwenyewe katika hali ya usafi wa kimaadili na kujipatia furaha kutoka kwa mke wake, "Ni ayala apendaye na paa apendezaye; Maziwa yake yakutoshe siku zote; Na kwa upendo wake ushangilie daima (Mithali 5:19). Kama mwanamume anakuwa na uhusiano usiofaa au wa kimaadili na wanawake wengine, au anatumia burudani chafu, mke hujisikia kwamba hapendwi.

## **(3) Mume humpenda mke wake kwa kujaribu kumwelewa.**

Mume hawezi kufanikiwa kumwelewa mke wake kila wakati, lakini atapaswa achukue muda wa kumsikiliza na kumchunguza. Maandiko yanawaambia waume kwamba, "Kadhalika ninyi waume, kaeni na wake zenu kwa akili...na kama warithi pamoja wa neema ya uzima..." (1 Petro 3:7).

Ikiwa mwanamume atafanyia mzaha hisia na maoni ya mke wake, mke atajisikia kwamba hapendwi. Atamtaka mume wake ajaribu kumwelewa wasiwasi wake hata kama kauli zake hazionekani kuwa na mantiki kwake.

Kwa kuwa Mungu alimfanya mwanamume kuwa kichwa cha nyumba (Waefeso 5:23), mume ana jukumu ka kuiongoza nyumba yake (1 Timotheo 3:4-5). Hata hivyo, mume na mke wanapaswa kuwa na muda wao kwa ajili ya majadiliano hadi pale watakapokuwa wamekubaliana kwenye maamuzi mengi. Mume hapaswi kuwa mwepesi wa kuamua mambo kwa haraka bila ya kupata hisia na maoni ya mke wake.

Kama hawawezi kukubaliana kwenye jambo lolote, mume anaweza akahitajika kufanya maamuzi, lakini anapaswa ajisikie kusikitika kwa sababu wameshindwa kwa pamoja kufikia kwenye kukubaliana. Kwa kawaida kukosekana kwa umoja ni onyo kwa mume. Wanawake mara nyingi wana hekima na utambuzi ambao wanaume wanahitaji katika kufanya maamuzi mazuri.

► Mwanafunzi anapaswa asome Waefeso 4:2-3, 15-16 kwa ajili ya kikundi. Je, ni kwa jinsi Aya hizi zinatumika kwenye uhusiano kati ya mume na mke?

## **(4) Mume humpenda mke wake kwa kumthamini.<sup>32</sup>**

Wake walio wengi huhisi kwamba waume zao hawathamini kazi wanazozifanya. Mume anapaswa aonyeshe kuwa na shukrani kwa mke wake, Anapaswa atambue juhudi ambazo mke wake anazifanya kwa ajili ya familia yake. Kamwe hapaswi kumkosoa hadharani au mbele ya watu wengine.<sup>33</sup> Anapaswa asifie tabia yake, uzuri wake, na uwezo wake. Kwa

<sup>32</sup> Mithali 31:28-31

<sup>33</sup> Katika muktadha wa ndoa, hii ni matumizi ya maagizo ya Mungu kwetu katika Waefeso 4:29-32; 5:25-29 na Mathayo 7:12.

kadri ile atakayojaliwa, mume anapaswa amsaidie aweze kuvaa vizuri. Mke hajasikii kupendwa wakati anapojiona kwamba mume wake hamjali kuhusiana na mwonekano wake.

Mume anapomkosoa mke wake anaweza akasababisha mke wake akafikiri kwamba yeye hafai kama mtu na akamkatisha tamaa. Paulo anawaambia waumini, "Wasimtukane mtu ye yote, wasiwe wagomvi, wawe wema, wakionyesha upole wote kwa watu wote (Tito 3:2).

Ikiwa ukosoaji uwe ni wa lazima, mume ni lazima awe mwangalifu sana kuthibitisha kwamba uthamini wake kwa mke wake ni mkubwa zaidi kuliko ukosoaji wake. Anapaswa kuepuka kutaja mifano ya wanawake ambao anawajua ni bora kuliko mke wake katika sifa nyingi za tabia.

#### **(5) Mume anampenda mke wake kwa kutenga muda wake kwa ajili ya uhusiano.**

Ili kushiriki maisha pamoja kunahitaji kuwepo na muda wa mazungumzo. Mahusiano huimarishwa kwa maneno (Mithali 16:24, Mithali 20:5). Wanandoa wanapaswa wazungumzie juu ya mambo ambayo yamesheheni kwenye siku zao. Wanapaswa wazungumzie kuhusu urafiki wao, hisia zao, matamania yao, na mambo ambayo wanapaswa wahusike/wawajibike nayo. Mke hujisikia kupendwa wakati mume wake anapopata muda wa kuzungumza naye na kumsikiliza. Mume anapokuwa amerejea nyumbani kutoka kazini anaweza akajisikia kuchoka na hajasikii kuongea au kusikia kuhusu matatizo ya nyumbani, lakini mume hapaswi kudharau kusikiliza. Kama mume anataka urafiki wa kimwili lakini hawezi kumfikisha kwenye urafiki wa mhemuko, mke anajisikia kama anayetumiwa tu lakini hapendwi.

#### **(6) Mume anampenda mke wake kwa kumvumilia katika madhaifu yake.**

1 Petro 3:7 inafundisha, "Kadhalika ninyi waume, kaeni na wake zenu kwa akili; na kumpa mke heshima, kama chombo kisicho na nguvu...." Wanawake wengi hawana nguvu za mwili walizo nazo wanaume wengi. Kadhalika, wanawake wengi ni wahanga wa mihemuko ya maumivu na kuhuzunishwa kuliko wanaume. Mwanamume anapaswa kumfariji na kumtia moyo mke wake. Anatakiwa ajifunze jinsi ya kumwondolea msongo wa mawazo. Anapaswa kujiepusha na kudai kujamiiana wakati akiwa amechoka, akiwa kwenye msongo wa mawazo au kwenye hofu.

#### **(7) Mume anampenda mke wake kwa kumpatia mahitaji yake.**

Kama vile ambavyo mwanamume anavyotaka awe na zana bora zaidi za kazi yake na mahali pazuri pa kufanyia kazi yake, anapaswa pia aandae mazingira mazuri kwa ajili ya mke wake. Atapaswa kuhakikisha kwamba nyumbani kumekarabatiwa vyema na kujazwa vitu ambavyo anavihitaji.

#### **Matokeo wakati Waume wanapokuwa Wanawapenda Wake zao.**

Waume wengi huja kuona kwamba wanapokuwa wameonyesha upendo kwa wake zao, wake zao huitikia kwa furaha na ushirikiano. Wanawake hujisikia furaha wakati waume zao wanapowajibika kwa ajili yao na kuwaonyesha upendo kwa jinsi orodha inavyoonekana.

Wanaume hupata mambo mengi kutoka kwenye ndoa zao wanapokuwa wameonyesha upendo kwa wake zao (Waefeso 5:28).

Hata hivyo, wanaume huwa hawana uhakika wa matokeo. Mwanamume hatakiwi kuonyesha upendo kwa kusudi tu la kupata kitu anachokitaka. Anapaswa aonyeshe upendo ili aweze kumpendeza Mungu na atimize mahitaji ya mke wake kuliko kuhangaika na mahitaji yake mwenyewe.

Baadhi ya wanawake wameathirika kimhemuko kama matokeo ya mambo ya nyuma yaliyopita, na wanaweza wasiwe na mwitikio wa haraka wa upendo wa waume zao. Mazoea haya ya kuonyesha upendo siyo mbinu za kujaribu kwa siku chache kama majaribio. Mume anapaswa kuendelea kuonyesha upendo bila kukoma kupitia njia hizi kwa sababu ya upendo alio nao ndani ya moyo wake kwa ajili ya Mungu na kwa ajili ya mke wake. Kristo analipenda Kanisa kwa aina hii ya uaminifu na kwa kujitolea kama dhabihu binafsi.

### **Jinsi Mke Anavyoonyesha Heshima kwa Mume Wake**

Waefeso 5:33 inaagizwa, "Lakini kila mtu **ampende** mke wake kama nafsi yake mwenyewe; wala mke asikose **kumstahi** mumewe."

Mwanamume anahitaji heshima. Wanaume wengi wako radhi kupewa heshima na watu wengine kuliko kupendwa nao. Mungu aliwaumba wanaume ili kulinda, kuwa msaada, na kuongoza familia zao. Nafasi ya baba na mume inahitaji kuheshimiwa hata kabla hajafanya jambo lolote la kuweza kumletea heshima. Mke anapaswa aonyeshe heshima kwa mume wake hata kama matendo yake ni mabaya. Anampasa amtendee kama mtu, aliyeumbwa kwa sura ya Mungu, ambaye ni muhimu sana hata pale ambapo hatumii mamlaka yake kwa usahihi (Waefeso 5:23). Hii haimaanishi kwamba hawezi kumweleza kwamba hakubaliani na matendo au maamuzi yake mabaya, lakini hapaswi kumtendee hivyo kwa kumkosea heshima.

Wakati mke anapomheshimu mume wake kwa kujitiisha kwa uhuru chini ya mamlaka yake, anaonyesha upendo wake kwa ajili ya Yesu (Waefeso 5:22, 31-33). Baadhi ya wake hufikiri kwamba wanawapenda waume zao hata wakati ambapo wanakuwa wakashindwa kuwaheshimu – wakiwalaumu kwa mabaya huko nje kwa watu wengine, wakiendesha mambo ya siri, na wakitumia maneno yenye kuumiza. Wanapaswa waelewe kwamba hakuna kiwango chochote cha upendo kinachoweza kuwa ni fidia kwa ukosefu wa heshima.

Wanawake wengi wana mwelekeo wenye nguvu wa kuwa mama wa mtoto mchanga. Wana uwezo wa asili na matamano ya asili ya kujali mahitaji ya watoto wachanga, Jaribu kufikiria jinsi mwanamke atakavyokuwa anajisikia ikitokea mtu kusema, "Huna uwezo wa kumtunza mtoto mchanga." Vivyo hivyo, wanaume nao wana mwelekeo wenye nguvu wa kulinda, kulisha, na kuongoza. Wakati mke wa mtu anapomweleza kwamba hana uwezo wa kufanya mambo hayo, mume hujihisi kwamba atakuwa ni mwanamume aliyeshindwa.

Mke anapaswa aelewe kwamba kutakuwepo na wanaume wengine ambao wana haiba yenye nguvu, wanaopata fedha nyingi, au wanaoshikilia nyadhifa mbalimbali za juu kuliko mume

wake. Hapaswi amfanye mume wake kama mtu aliyeshindwa kwa kumlinganisha na wengine. Kama tunavyojifunza kutoka katika kitabu cha Waefeso 5:21-33, mke ni mtu mmoja pamoja na mumewe. Inapotokea mke akamshutumu mume wake au akamlinganisha na wengine, kwa pamoja anajisambaratisha yeye na mwenzake kwa pamoja na kuharibu uhusiano wao.

► Mwanafunzi anapaswa asome Mithali 31:11-12, 26 kwa ajili ya kikundi. Je, Aya hizi zinatufundisha nini kuhusu jinsi ambavyo mke mcha Mungu anavyomtendea mume wake kwa tabia na maneno?

### **(1) Mke humheshimu mumewe kwa maneno ya uthibitisho.**

Mke anapaswa awe na uthibitisho wa uwezo wa mumewe. Heshima itaonekana kuwa dhahiri katika maneno ya uthibitisho ambayo mke huzungumza na mumewe. Maneno yana mguso mkubwa kwa wanaume wengi. Aidha yatajenga au yatabomoa (Mithali 14:1). Aidha yana uwezo wa kutia moyo au kudhoofisha. Aidha yataimarisha matumaini yake na kujiamini kwake au yatasambaratisha moyo wake kabisa (Mithali 18:21). Mwanamume hawezi akawa na mafanikio kwenye kila biashara au akawa na uwezo wa kushikilia nyadhifa mbalimbali, lakini mke wake anapaswa athibitishe jitihada zake za kuutengeneza mji wake na utoaji wa ulinzi kwa familia yake. Hapaswi kwa namna yeyote ile kujaribu kumvunja moyo mumewe kwa maneno yake anapokuwa na mawazo ya kutenda jambo fulani au anapokuwa anakabiliana na changamoto mpya.

► Wanafunzi wanapaswa wasome Mithali 15:4 na Mithali 16:24 kwa ajili ya kikundi.

### **(2) Mke humheshimu mume wake kupitia kujisalimisha kwake (1 Petro 3:5).**

Kujisalimisha kwa mke hakumaanishi kwamba yeye ni mtu wa chini sana kuliko mumewe (kwa cheo, uwezo n.k.) Badala yake ni kumaanisha kwamba majukumu yao ni tofauti. Hata katika Utatu Mtakatifu wa Mungu tunaona kwamba Mwana ananyenyekea kwa Baba ingawa Mwana siyo wa chini sana kuliko Baba kwa asili au nguvu au sifa yake yeyote.

Kwa baadhi ya wake kanuni hii siyo rahisi kwao, hasa ikiwa waume zao hawaishi kufuatana na Neno la Mungu, au kama hawana upendo kwao. Baadhi ya wanawake wanajihisi kwamba wana uwezo wa kufanya maamuzi yaliyo bora zaidi kwa ajili yao wenyewe, au kwa familia zao kuliko ambavyo waume zao wangeweza kufanya. Wakati mwingine mwanamke anakuwa yuko sahihi katika jambo hili, na mwanamume katika makosa. Hata hivyo, endapo mke atanyenyekea kwa mumewe pale tu anapokuwa anakubaliana na yeye, anapoka mamlaka ya mumewe na haina maana kwamba anajinyenyekesha au anajisalimisha kwa ukweli. Kujisalimisha maana yake ni kuruhusu mwingine aweze kufanya maamuzi.

Petro anawaambia wanawake walioolewa ifuatavyo:

Kadhalika ninyi wake, watiini waume zenu; kusudi, ikiwa wako wasioliamini Neno, wavutwe kwa mwenendo wa wake zao, pasipo lile Neno; Kujiipamba kwenu, kusiwe kujipamba kwa nje, yaani, kusuka nywele; na kujitia dhahabu, na kuvalia mavazi;

bali kuwe utu wa moyoni usioonekana, katika mapambo yasiyoharibika; yaani, roho ya upole na utulivu, iliyo ya thamani kuu mbele za Mungu. (1 Petro 3:1, 3-4).

Kuna hali mbalimbali zenye matatizo. Wake wengi huuliza maswali. "Je, kama ataniambia nifanye jambo hili\_\_\_\_\_ kuna ulazima wa mimi kulifanya?" Somo hili haliwezi kuzungumzia kwa mapana hali mbalimbali kubwa za matatizo zilizopo. Hata hivyo, tatizo la kutokujisalimisha kwa mke haliko kwa sababu ya mume kutaka mambo fulani ambayo mke hapaswi kuyafanya. Mke anaweza asitake kujisalimisha/kuwa mtiifu kwa mume wake kwa sababu anafikiri kwamba mume wake atakuwa mtu wa kutofikiri endapo atafanya hivyo. Inawezekana mume hana upendo wala fadhila. Mke hatapenda kusalimisha uhuru wake wa kufanya maamuzi yake mwenyewe. Mke anaweza akawa ana tabia ya ukaidi. Mke hutumia mifano ya matendo au makosa yasiyokuwa na fadhila ya mume wake kama kisingizio cha kukataa mamlaka yake kwa ujumla. Hali hii ni ya kutotaka kutii maagizo ya Neno la Mungu.

Biblia inatuambia kwamba mke mcha Mungu na mtiifu anaweza kumvuta mume wake kwa Bwana. Hatuna uhakikisho kwamba mume anaweza kuokoka kwa sababu ya mke mwema, lakini upo uwezekano mdogo sana wa mume kuweza kuokoka endapo mke wake aliye Mkristo ni mkaidi. Mke anaweza kupata wingi wa kukubalika kwa mume wake kwa kuwa mwenye heshima, lakini hiyo siyo sababu ya msingi ya kufanya hivyo. Anapaswa amheshimu mume wake kwa kuwa anawiwa amheshimu na kwa sababu anataka kumpendeza Mungu.

Mithali 12:4 inasema, "Mwanamke mwema ni taji ya mumewe; Bali aaibishaye ni kama kuoza mifupani mwake." Ikiwa mke anamtendea mume wake pasipokuwepo na heshima mbele ya marafiki zake, anaiondoa heshima aliyo nayo mumewe ambayo kamwe hatakaa aweze kuirejesha tena. Wanaume huvutiwa na wanaume wengine ambao wako na wanawake wao waliojisalimisha kwao kwa unyenyekevu na utiifu. Wanaume huwahurumia wanaume wenzao ambao wana wake wasiokuwa na heshima.

**(3) Mke humheshimu mume wake kwa kuwa makini na mahitaji yake** (Mithali 31:15, 21, 25, 27).

Wakati mke anapojifunza kwa undani mambo ya pekee kuhusu jinsi ya kuandaa chakula na kuitunza nyumba yake kwa njia ambayo inamfurahisha mume wake, mume hujisikia kuheshimika. Ikiwa mke atakataa kubadilisha tabia zake kwa ajili yake, mume hujisikia kwamba yeye sio muhimu kwa mke wake.

Ikiwa mke atakuwa anawajibika na shughuli nyingi za kazi au marafiki au kanisa au mambo ya burudani na hana muda wa kutosha kumsikiliza na au kuzungumza na mumewe au kushughulikia mahitaji yake kama inavyostahili, mume hujisikia kwamba yeye sio muhimu kwa mke wake.

Mwanzo 2:18 inafundisha, "Bwana Mungu akasema, Si vema huyo mtu awe peke yake, nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye."

#### **(4) Mke humheshimu mume wake kwa kumridhisha kimapenzi.**

Kuridhika kutokana na tendo la kujamiiana kunaonekana kuwa ni muhimu zaidi kwa wanaume kuliko ilivyo kwa baadhi ya wanawake. Mwanamke anaweza asijisikie kujihusisha na tendo la kujamiiana mara nyingi labda iwe hisia zaka na matamania yake vimeelekezwa kwake, ambayo ni mara chache kuliko ambavyo mwanamume atakuwa amehitaji. Hii inamaanisha kwamba mara nyingi mwanamume anaweza kuwa haridhiki wakati mke wake anapokuwa haelewi au hashughuliki na hitaji lake. Mke anaweza hata kudharau matamania ya mume wake ya kutaka kujamiiana naye kwa sababu tu ya unyanyasi alioupitia au kuuona wakati wa nyuma uliopita. Mume anapaswa ajaribu kuwa mvumilivu na kumwelewa mke wake. Lakini mke anapaswa aelewe kwamba ni vyema kwake wakati wote atimize hitaji la mumewe la kujamiiana hata katika nyakati ambazo yeye mwenyewe hajasikii kuwa na uhitaji huo. Kama mwanamume ni mwaminifu na anayewajibika kikamilifu kwa ajili ya mke wake, na hana mahusiano mengine mabaya na wanawake wengine, anaweza kujisikia kukasirishwa sana wakati mke wake anapokuwa hajali kuhusu hitaji lake. Uaminifu wa mume kwenye ahadi ya ndoa yake kamwe hakuhitajiki kutegemea kuridhika kwake kimwili, lakini umakini wa mke wake kwenye mahitaji yake ya kujamiiana kunaweza kupunguza mapambano yake dhidi ya majaribu.

Wimbo wa Sulemani unasema: “Mpendwa wangu ni wangu, na mimi ni wake... **Njoo, mpendwa wangu**, twende mashambani, Tufanye maskani katika vijiji... **Huko nitakupa pambaja zangu**. (Wimbo wa Sulemani i2:16; Wimbo wa Sulemani 7:11-12, mkazo umeongezwa; ona pia 1 Wakorintho 7:3-5).

#### **Matokeo ya Kutotii kwa mujibu wa Maagizo ya Mungu**

Maelezo yaliyoko kwenye aya hizi hayatumiki kwenye kila mgogoro ulioko kwenye ndoa lakini ni ya kawaida yaliyozoeleka. Maelezo haya yanaonyesha mizunguko ya asili ya tabia – na -athari – ambayo inatokea wakati wanandoa wanapojibu hisia zao pasipo kiroho, badala ya: (1) Kutambua ni nini wanachokihisi, (2) Kukumbuka ukweli wa Mungu na kile anachotaka kwa ajili yao, na (3) Kumtegemea Roho Mtakatifu awasaidie kujibu kwa njia za Kibiblia.

Ikiwa mke hatembe katika Roho na haruhusu upendo wa Mungu ufanye kazi kupitia kwake anaweza kuwa na mwitikio wa asilia tu am bao unaweza kuleta athari kubwa kwenye ndoa yake. Kama mke hatajisikia kwamba anapendwa, hajasikii kuwa salama. Ataanza yeye mwenyewe kujidai na kutaka kuzuia mamlaka ya mumewe kwa sababu hamwamini katika kumjali yeye. Wakati mke anapokuwa akifanya haya, mume anajihisi kama asiypewa heshima. Akijaribu kutetea mamlaka yake kwa dhati na kudai heshima, mke hujisikia na hata zaidi kwamba mume hana upendo kwake.

Ikiwa mwanamume hatembe katika Roho ili kuruhusu upendo wa Mungu ufanye kazi kupitia yake, anaweza akashindwa kuwa na tabia ambayo itaimarisha ndoa yake. Wakati mwanamume anapojihisi na kujiona kwamba anavunjiwa heshima yake, hujisikia kuumizwa na kuwa na hasira. Anaweza akasema mambo ya kuumiza kwa mke wake. Kama atakuwa

anajaribu kudhibiti hisia zake, anaweza akaamua kunyamaza kimya. Hatapenda kuwa karibu na mke wake au kufungua moyo wake kwake, kwa sababu anahisi kwamba yeye siyo wa kushirikiana naye. Anapokuwa akifanya hayo, mke wake anakuwa haelewi ni kwa nini. Labda alimtendea pasipokuwa na heshima kwa kuwa alikuwa anajaribu kumfanya atambue kwamba hakuwa na furaha na kwamba inampasa kubadilika. Anapokuwa na hasira na kujiondoa kwake, mke anafikiri kwamba mume anadhihirisha kwamba hana cha kujali tena katika hisia zake. Anaweza akajisikia hata na zaidi kwamba anavunjiwa heshima.

Mtu huwa katika hatari zaidi ya kuingia kwenye majaribu wakati uhusiano wa ndoa umeporomoka. Mke hushawishika kuwa mpinzani zaidi kwa uongozi wa mume wake. Anadiriki hata kumzungumza kuhusu habari za mumewe kwa watu wengine wasiohusika kwa kumvunja heshima. Anaweza akaingia kwenye jaribu la kuwa kwenye uangalifu wa mwanamume mwingine wa nje anayeonekana kumthamini zaidi. Mwanamume anashawishika kukaa mbali na mke wake kwa sababu ya kukerwa na tabia yake. Anaweza akashawishika kufurahia kuwa kwenye uangalifu wa mwanamke mwingine anayemthamini mbali na mkewe.

Kila mtu anawajibika kwa Mungu kwa ajili ya uchaguzi. Mungu hawezi akasemehe dhambi ya mtu kwa sababu ya kile ambacho kimefanywa na mwenzi wake. Mungu anaahidi kututia nguvu ya kutusaidia kuishi kama inavyotupasa. Kusudi la taarifa hii siyo kwa ajili ya mtu kudai ni kitu gani kinachohitajika kutoka kwa mwenzi wake au kumlaumu mwenzi kwa kosa la mtu mwingine. Kusudi ni ili mtu aweze kutambua kwamba anao wajibu wa kumpendeza Mungu na kumpa mwenzi wake mahitaji yake anayohitaji.

### **Malengo Mabaya**

Wakati mwingine mtu hutafuta njia ya kuyafanya maisha yake yawe marahisi. Mume anataka kurahisisha maisha yake kwa kutaka mke wake abadilike. Vivyo hivyo, mke naye anaweza akafikiri kwamba maisha yake yatakuwa bora zaidi kama mume wake atabadilika. Mtu anamuuliza mshauri, au mchungaji au marafiki jinsi ya kuweza kumbadilisha mtu mwingine. Kumbadilisha mwenzi wa mtu mwingine siyo lengo lililo sahihi. Mtu ambaye anajaribu kuyafanya maisha yake yawe marahisi kwa kutumia mbinu za mahusiano hazichochewi na upendo kwa ajili ya Mungu au mtu mwingine.

Wakati mwingine mtu hujaribu kwa miaka kusahihisha makosa ya mtu mwingine. Hawaachi kukosoa makosa yanayofanana. Ingawaje kila mmoja anakuwa ana makosa ya ukweli, kila mwanandoa hatimaye ni lazima amkubali mwenza wake kwa makosa yake. Makosa yanaweza yakawa kasoro za mwonekano, kasoro za tabia, au kasoro za kiroho (Zikiwemo hata dhambi). Uhusiano haupaswi utegemee nia ya mtu mwingine ili ubadilike. Anaweza akajihisi kwamba hawezi kubadilika. Iwe ni kwa sababu yeyote ile kwamba habadiliki, kila mwenza anapaswa kuonyesha upendo na heshima, kila mmoja akimthamini mwingine hata katika makosa yake.

## Hitimisho

Mungu aliitengeneza asili za wanaume na wanawake, na aliitengeneza ndoa kukidhi mahitaji ya mwanadamu. Hata hivyo, tunaishi katika ulimwengu wa ambamo ndoa na familia zimeharibiwa kwa kiasi kikubwa sana na dhambi. Kila mmoja wetu kwa nafsi yake ameharibiwa na dhambi zetu sisi wenyewe na dhambi za watu wengine ambazo zimetuathiri. Hatuwezi tukazizoea ndoa kama Mungu alivyokuwa amekusudia bila ya neema ambayo inatubadilisha sisi na inatusaidia sisi kuonyesha neema hiyo kwa watu wengine. Tunahitajika tuwe na Roho wa Mungu wa kututakasa ili tuwe na malengo yaliyo masafi, upendo wenye nguvu, na unyenyekevu ambao unahudumia.

## Kwa ajili ya Majadiliano ya Kikundi

► Je, kuna maudhui gani kwenye somo hili ambayo ni mapya kwako? Je, ni kwa jinsi gani umepanga kubadilisha misimamo yako na tabia zako?

► Je, ni jambo gani ambalo kanisa linaweza kufanya ili liweze kuimarisha ndoa?

## Maombi

Baba wa Mbinguni,

Asante kwa kutengeneza uhusiano wa ndoa ili kukidhi mahitaji mengi sana maalumu. Asante kwa kutupa sisi maelekezo yako kwa ajili ya ndoa.

Tusaidie tuwe na upendo na uelewa wa kujali kama inavyopaswa tuwe. Tusaidie tuwe na familia ambazo zinadhihirisha upendo wako kwa dunia.

Asante kwa ajili ya neema yako ambayo sisi inatusaidia sisi kuwa na upendo kama vile na wewe unavyofanya.

Ameni

## Kazi za Kufanya

(1) Fanya kukariri 1 Wakorintho 13:4-8. Mwanzoni mwa kuanza kwa kipindi cha darasa kinachofuata, andika au rudia kusema yale uliyokariri kutoka kichwani.

(2) Andika maneno yasiyopungua kurasa mbili ukielezea mahitaji ya mume na mke. Toa mfano wa tabia ya mwanandoa ambayo inasaidia katika kukidhi mahitaji hayo. Tumia Maandiko katika kusaidia kila moja ya mahitaji unayojadili.



# Somo la 8

## Lugha Tano za Upendo – Sehemu ya 1

### Malengo ya Somo

Hadi kufikia mwishoni mwa somo hili, mwanafunzi atapaswa:

- (1) Kuelezea sifa na tabia za upendo wa kweli.
- (2) Kufafanua inamaanisha nini kumpenda mtu bila masharti.
- (3) Kuelezea umuhimu wa kuthibitisha upendo kwa lugha ya msingi ya upendo ya mtu.
- (4) Kutumia maneno ya kuthibitisha katika kuonyesha upendo na uthamini kwa ajili ya sifa binafsi za mwanafamilia, sifa bainishi za tabia na sifa bainishi za nafsi ya mtu.

### Yusufu na Hana – Ndoa inayokua

Yusufu alichanganyikiwa kwa kuwa mke wake hakuwa na furaha. Hakujuu ni kitu gani alikuwa anahitaji kutoka kwake. Yusufu alifanya kazi kwa bidii sana na kuweza kuwapa mke na watoto wake nyumba na chakula na kila kitu cha muhimu kilichohitajika katika maisha. Alimruhusu mke wake aweze kununua kitu chochote anachokihitaji. Mke wake hakuwa na wasiwasi kuhusiana na jambo lolote. Je, ni nini cha zaidi ambacho mke anaweza akawa anahitaji? Yusufu alijisikia kwamba mke wake alikuwa hathamini kazi yake anayoifanya.

Hana hakuwa na furaha kwa sababu alikuwa anamtaka Yusufu amwonyeshe upendo wake kwake kwa kufikiria juu ya mambo mahususi kwa ajili yake. Zawadi yake aliyoipenda sana kutoka kwa Yusufu ni kinyago cha mti kilichokuwa kimetengenezwa kwa ajili yake na Yusufu na kilikuwa kimeandikwa jina lake na Yusufu kutoka kwenye duka lake. Badala ya Yusufu kumwambia Hana kwamba anunue chochote alichokihitaji, alitamani Yusufu wakati mwingine amnunulie maua.

Yusufu na Hana walikuwa wakiongelea kuhusu hisia zao na wakaanza kila mmoja kuelewa mahitaji ya mwenzake.

### Upendo wa Kweli ni nini?

- Je, inamaanisha nini kumpenda mtu kwa kweli?
- Mwanafunzi anapaswa asome 1 Wakorintho 13:4-8 kwa ajili ya kikundi. Kutokana na kifungu hiki, orodhesha sifa na matendo ya upendo. Orodhesha mambo ambayo upendo hauko hivyo na upendo haufanyi hivyo.

1 Wakorintho 13 Upendo	
Upendo ni nini	Upendo unafanya nini
Upendo Usichofanania	Usichokifanya Upendo

Inaweza ikaonekana kutoka katika kifungu hiki kwamba upendo unajulikana kwa kile ambacho **sicho** zaidi ya kile ambacho **ndicho**. Lakini maelezo ya kile ambacho upendo **haufanani** nacho yanatufundisha sisi kuhusu upendo **unafanania** nini. Kama upendo hauna kiburi, basi ni nini? Ni kinyume chake. Upendo ni unyenyekevu.

► Sasa andika kinyume cha kila kimoja cha mambo ambayo siyo ya kweli kuhusu upendo, kama ilivyoelezwa kwenye 1 Wakorintho 13:4-8 na kuandikwa kwenye Jedwali la hapo juu.

Upendo Unavyofanania	Unachokifanya Upendo

## Upendo wa Kweli:

- Siyo jambo la hisia tu (ingawa hisia mara nyingi huambatana na upendo)
- Unatolewa kwa kufanya uchaguzi, na siyo kwa sababu ya mahitaji
- Ni ahadi.
- Ni dhabihu.
- Siyo wa masharti; hautegemei matendo ya mtu mwingine
- Ni wa kukusudia, siyo wa bahati mbaya
- Unagharimu kitu.
- Hutafuta ni kitu gani kizuri sana kwa ajili ya mtu mwingine
- Hujidhihirisha wenyewe kwa njia ya utoaji

Unaweza ukawa unatoa bila ya upendo, lakini ni jambo lisilowezekana kabisa ukapenda bila ya kutoa. Upendo ni lazima ukugharimu kitu fulani.

"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee..." (Yohana 3:16). Upendo wa kweli hujidhihirisha wenyewe kwa njia ya utoaji. Hii si lazima iwe kutoa zawadi inayoonekana au ya mali. Wakati mwingine zawadi inaweza ikawa ni maneno mazuri ya upendo; Wakati mwingine zawadi ni muda wako unaoutoa: Kuwa pamoja na mtu na kuwa unapatikana kwa ajili yake. Wakati mwingine upendo hutolewa kupitia matendo ya huduma au mguso wa upendo. Mungu Baba alitupenda sana sisi kiasi kwamba alitoa kile kizuri kuliko vyote alivyokuwa navyo, Mwanawe wa pekee, ili kwamba tuweze kufanyika watoto wake. Tanapokuwa tunawapenda watu wengine kwa ukweli kabisa, ni lazima tutatoa.

Upendo wa kweli hauna masharti. Siyo tegemezi kwenye tabia au kustahili kwa mtu anayetakiwa kupendwa. Haisemi kwamba, "Kama utafanya hivi na kunipendzesha mimi katika njia hii, basi nitakupenda; lakini kama utafanya vile na kunichukiza, sitaweza kukupenda."

Upendo wa masharti unasema, "Kama tabia yako itanifurahisha mimi, nitakuzawadia udhihirisho wa upendo utakaokuwa na maana kwako. Lakini kama hutafanya vile ninavyotaka, nitazuia udhihirisho wangu wa upendo."

Upendo halisi hauna masharti. Utajidhihirisha wenyewe bila kujali kwamba mpokeaji atafanya kitu au hatafanya. Upendo utajieleza wenyewe hata wakati ambapo mpokeaji hana uwezo wa kutoa majibu ya huo upendo; wakati akiwa hana chochote cha kutoa kama mrejesho wake.

Ni muhimu kutambua kwamba kumpenda mtu bila masharti haina maana lazima tumpe kile anachotaka. Haimaanishi kwamba tunawaondolea matokeo ya tabia zao mbaya. Inamaanisha kuwa tunajaribu kila wakati kufanya kile kilicho bora kwao. Ni vigumu sana

kumwona mtu unayempenda akiwa anateseka, lakini ikiwa anatenda mabaya, uzoefu wa mateso anayopitia mara nyingi ni kitu pekee kinachoweza kuwafanya kubadilika kutoka katika tabia zao mbaya za uharibifu. Wakati mwingine kile kilicho bora kwa wapendwa wetu ni kuwa waruhusiwe kupambana. Kwa nyakati nyingine, inakuwa ni jambo jema kwetu kuwasaidia kutoka katika mapambano yao. Mara nyingi tunahitaji ushauri wa kimungu na msaada wa Roho Mtakatifu katika kujua tufanye nini katika hali hizi zote.

► Je, ni kitu gani kitakachoweza kutuchochea sisi kuwapenda watu wengine kwa upendo usiokuwa na masharti?

► Mwanafunzi anapaswa asome Warumi 5:8 kwa ajili ya kikundi.

Watu wengi wanahisi kwamba upendo wa Mungu msingi wake ni kwenye utendaji wao. Kwa sababu hiyo, huwa hawaelewi ni kwa nini wawe na upendo usiokuwa na masharti kwa watu wengine. Lakini katika Warumi 5:8 tunaambiwa kwamba Mungu tayari alikuwa ameshatupenda hata wakati ambapo tulikuwa maadui zake. Alitupa Mkombozi wakati tulipokuwa wenye dhambi. Upendo wa Mungu kwa watu wote ni usiokuwa na masharti. Upendo wake hauna misingi yake kwenye tabia yako au utendaji wako. Mungu anakupenda kwa jinsi ulivyo kama mtu, uliyeumbwa kwa sura yake.

Anapenda tuwapende watu wengine kwa njia ile ile ambayo anatupenda nayo sisi (Yohana 15:12, Waefeso 5:2, 1 Yohana 4:11). Sababu ya msingi ambayo inatupasa sisi tuwapende watu wengine bila ya masharti ni kwamba Mungu ametuita sisi tufanye hivyo (Mathayo 5:43-48, 1 Petro 4:8).

### **Watu hujisikia Kupendwa kwa njia Tofauti**

Mungu anapenda mchanganyiko wa aina mbalimbali za watu. Huwapa watu kuwa wa mwonekano wa kipekee. Hakuna katika watu wawili wakatokea kuwa na njia zilizo sawa za kufikiria na kuwasilisha hisia zao. Kwa sababu ya tofauti zilizo kwenye mwonekano wao, watu walioko kwenye familia zetu wana mahitaji yaliyo tofauti na sisi. Tofauti zetu tulizo nazo kila siku zinaathiri mahusiano ya familia.

Mojawapo ya njia ambazo watu binafsi hutofautiana ni jinsi wanavyodhihirisha upendo na katika kile ambacho kinawafanya wajisikie wanapendwa, wanathaminiwa, na salama katika mahusiano yao na watu wengine.

Kuna njia nyingi za kuonyesha upendo, na pia kuna njia nyingi za kuwafanya watu wajihisi kwamba wanapendwa. Gary Chapman anaorodhesha aina tano za jumla kuhusu udhihirisho wa upendo.<sup>34</sup> Anaziita Lugha Tano za Upendo. Kila moja ya njia hizi za kuonyesha upendo ni utaratibu wote wa tabia, na siyo tu matendo ya mtu binafsi.

---

<sup>34</sup> Mawazo mengi kwenye sehemu hii yana msingi wake kutoka katika kazi ya Gary Chapman, *The Five Love Languages: How to Express Heartfelt Commitment to Your Mate*, (Northfield Publishing, Chicago, 1995)

Ingawa kila mtu anahitaji kupendwa katika njia zote tano, inaonekana kuwa watu binafsi hujihisi kwamba wanaopendwa zaidi na aina moja ya udhihirishwaji kuliko wanavyojisikia kwenye aina nyingine za udhihirisho. Udhihirisho nyingine za upendo hazimaanishi jambo lolote kubwa la maana kwao.

### **Lugha Tano za Upendo**

Watu huonyesha upendo kupitia:

1. Maneno ya uthibitisho
2. Muda ulio bora
3. Zawadi
4. Matendo ya Huduma
5. Mguso wa kimwili

Hata hivyo, watu hutambua na kupokea upendo kwenye hizo njia tano.

### **Lugha ya Msingi ya Upendo**

Watu wengi kwa kawaida hutambua na kudhihirisha upendo kimsingi katika njia moja au mbili ya njia hizo tano. Kama wanafamilia hawataonyesha udhihirisho wa upendo wao kwa ajili ya mwanandoa au mtoto katika lugha ya msingi ya upendo ya mtu huyo, mwanandoa au mtoto huyo huenda asijisikie kama anapendwa, ingawaje wanakuwa wanaonyeshwa upendo kwa njia nyingine.

Mwanamke maalumu kimsingi anaweza kudhihirisha upendo wake kwa kutoa muda wake kwa mtu mwingine ambaye anampenda. Atajaribu kuwa pamoja naye kwa mazungumzo na kuwa kwenye mawasiliano na wale anaowapenda. Atatumia muda wake kwa ajili ya kufanya kazi za pamoja. Vivyo hivyo, kwa kuwa hiyo ndiyo njia ya msingi ya yeye kuonyesha upendo, ndiyo njia ambayo yeye hutambua kwa wepesi zaidi upendo wa watu wengine walio nao kwa ajili yake. Anajisikia anayependwa zaidi sana wakati mtu mwingine anapojitolea muda wake kwa ajili yake. Endapo mume wake atamnunulia zawadi au akamfanyia jambo lolote jema, haiwi na maana kubwa sana kwake kulikoni angeutumia muda wake akiwa pamoja na yeye.

Mwanamume fulani kimsingi anaweza kuonyesha upendo kupitia mguso wa kimwili. Atamkumbatia mke na watoto wake na kuwa mwenye furaha wakati wao wanapokuwa wanamkumbatia yeye na kutaka kuwa karibu na yeye. Anaweza akawa anawakumbatia marafiki zake au angalao kuwapiga kidogo kwenye mabega yao au akawasukuma au akavurumishana nao kwa upendo. Anaweza akathamini kazi ngumu ya mke wake aifanyayo kwa ajili ya familia yao, lakini kazi anayofanya sicho kitu kinachomfanya ajisikie kwamba anapendwa na mke wake. Huwa anajisikia anayependwa wakati anapoketi karibu naye na kumpa fursa aweze kuweka mikono yake juu yake kumzunguka, au wakati mke anapomgusa maeneo mbalimbali ya mwili wake kwa njia ya upendo.

Gari linakuwa na tanki la mafuta. \Wakati tanki likiwa liko tupu, gari linakuwa halina uwezo wa kufanya kazi. Wakati mtu anapoupokea upendo katika njia anayoitambua na anahitaji upendo, husababisha mhemuko wa mafuta. Wakati tanki la mhemuko wa mtu linapokuwa limejaa, anakuwa na uhakika kamili na nguvu kwa ajili ya kukabiliana na changamoto mbalimbali. Anakuwa na uwezo zaidi wa kushirikiana na watu wengine. Anakuwa na uwezo mkubwa wa kutatua migogoro. Anajisikia kuhamasika katika kukuza na kufanikisha malengo.

Wakati mtu anapokuwa hajapokea upendo kwa njia ambayo anaitaka mwenyewe, anakosa mhemuko utokanao na mafuta. Ni nadra sana mtu kufanya juhudi kubwa kwa ajili ya kukamilisha au kuendeleza jambo endapo atajisikia kwamba hapendwi.

Ikiwa mara kwa mara hatutawaonyesha wanafamilia wetu upendo katika lugha ya msingi ya upendo, hawataweza kutambua ni kwa jinsi gani sisi tunawapenda. Huu ndiyo ukweli, bila kujali ni kiasi gani tunachojisikia nacho kwamba tunawapenda. Tunapaswa tuwasilishe upendo wetu kwao katika njia ambayo wanaielewa.

Kama tutakuwa tunamuumiza mtu mwingine kwenye lugha yake ya msingi ya upendo, hali hiyo ni mbaya zaidi. Kwa mfano, kama maneno ya uthibitisho ndiyo nia muhimu zaidi ya kuonyesha upendo kwa mtoto wetu, maneno yetu ya kukosoa yatakuwa yanamuumiza mtoto zaidi sana kuliko ikiwa angekuwa na lugha tofauti ya msingi ya upendo.

### **Kukua Kupitia Upendo Wetu wa Mtu mmoja kwa Mwingine**

Kwenye Somo la 1, tulijifunza kuhusu jinsi ambavyo Mungu aliwaumba watu wote kwa ajili ya uhusiano na yeye mwenyewe pamoja na watu wengine. Mdhihirisho wa upendo ni sehemu muhimu sana kwenye kila aina ya uhusiano. Ni muhimu kwetu kuelewa njia ambazo wanandoa wetu, watoto wetu, na wanafamilia walioshikamana nasi wanavyojisikia kupendwa sana. Elimu hii inatuwezesha sisi kudhihirisha upendo wetu kwa ajili yao katika njia ambazo ni za maana zaidi kwao kibinafsi.

Ndoa ni mara chache sana watu wanategemea iwe jinsi itakavyokuwa. Mara nyingi watu huwa wanakatishwa tamaa na tofauti kati yao wao wenyewe na wenzi wao. Inapotokea kuwa ni suala la kudhihirisha upendo, inaweza ikaonekana kwamba hali itakayokuwa nzuri ni ile ya watu wote kuweza kuwa na lugha ya msingi inayofanana ya upendo. Kutokuelewana kwingi na kufadhaika kungeweza kuepukika endapo wangukuwa katika usawa mmoja wa aina hii. Hata hivyo, tofauti kama hizo zinaweza kuimarisha kama wanandoa wenyewe watakuwa wamejikabidhi kabisa kwenye ndoa yao na kuendelea kukua katika upendo wao kwa ajili ya kila mmoja.

Mchakato wa kila mmoja kujaribu kumwelewa mwenzake, kuzoeana na mwenzake, na kuonyesha kujali katika njia zenye maana humkuza kila mtu na hufanyika ni onyesha la ajabu la upendo wa kweli. Tunapokuwa tunawahudumia wanafamilia wetu kwa

“Bwana na awaongeze na  
kuwazidisha katika upendo, ninyi  
kwa ninyi, na kwa watu wote,  
kama vile sisi nasi tulivyo kwenu;  
- 1 Wathesalonike 3:12

kudhihirisha upendo kwao katika njia ambazo wanajisikia kwamba wanapendwa, huwa tunakua katika uelewa wetu na tabia.

Linapokuja suala la kudhihirisha upendo kwa wanandoa wetu na wanafamilia wengine, ni muhimu sana kutambua kwamba hatuwezi tukadhihirisha upendo peke yake kwa njia zetu wenyewe, au tukadhihirisha upendo wakati tu tunapojisikia. Upendo ni uchaguzi na kujitolea kabisa, kwa kuchochewa na thamani ya uhusiano. Katika masuala fulani, tutapaswa tujifunze njia mpya za kuonyesha upendo. Yawezekana hatukukulia kwenye familia iliyokuwa ikidhihirisha upendo kwa njia fulani, lakini mwanafamilia leo anahitaji kupendwa hivyo kwa jinsi ile. Kwenye hali kama hizi, kudhihirisha upendo kwa njia isiyokuwa ya kuzoeleka kunaweza kuonekana ni kujihisi jambo la kushangaza au lisilofaa kwetu tangu mwanzo, lakini tunaweza tukajifunza. Ni muhimu kwamba kamwe tusitende kama ni jukumu lisilokuwa la kupendeza au kwamba ni usumbufu kudhihirisha upendo wetu. Ikiwa itaonekana kwamba tunatenda nje ya uwajibikaji, udhihirisho wetu wa upendo hautawasilisha upendo wa kweli.

► Wanafunzi wanapaswa wasome Warumi 12:9-10, 16 na 1 Petro 3:7-8 kwa ajili ya kikundi. Kutokana na maandiko haya, taja sababu kadhaa ambazo itatupasa tujali kuhusu njia ambazo familia zetu zinajisikia kuwa zimependwa zaidi sana.

### **Ni jambo muhimu kukumbuka kwamba upendo ni tendo la kujidhabihu binafsi katika kutafuta jambo zuri zaidi kutoka kwa mtu mwingine**

Sisi tumezaliwa na asili ya ndani ya ubinafsi. Upendo wa kweli kwa watu wengine hauji kwa njia ya kawaida kwa yeyote kati yetu. Upendo wa kweli hufanyika ni kitu kinachowezezana kutokana na kazi ya Roho Mtakatifu ndani ya mioyo yetu (Warumi 5:5). Kama watu tuliookoka, tunapaswa tujifunze jinsi ya kushikamana na njia ya Yesu ya kufikiri, kama ambavyo Paulo anaelezea katika Wafilipi 2. Tutakapokuwa tunafanya hivyo, tutafanya yafuatayo:

- Hatutachochewa na tamaa za binafsi (Aya ya 3).
- Hatutakuwa na mtazamo uliokithiri wa kujiangalia umuhimu wetu tu (Aya ya 3)
- Tutakuwa tunawafikiria watu wengine kuwa ni wa maana zaidi kuliko sisi wenyewe (Aya ya 3)
- Tutakuwa waangalifu katika kuangalia maslahi ya watu wengine (Aya ya 4)

Ni lazima tuweke ahadi ya kukua katika upendo wetu kwa ajili ya wanafamilia wetu. Tunapaswa tujifunze kugundua mahitaji yao na kuangalia njia ambazo zitaweza kuwatimizia mahitaji yao. Lengo letu liwe ni kuwaonyesha upendo wetu kwa ajili yao katika njia ambazo watajisikia wenye kupendwa zaidi.

Sisi kama wazazi tunapaswa pia tuwafundishe watoto wetu kuwajali ndugu na dada zao, wazazi, mababu na mabibi zao katika njia hizi. Watu wetu wanahitaji kujifunza kupenda na kutumikia familia zao. Wanaweza wakajifunza jinsi ya kudhihirisha upendo kwa ajili ya

familia zao kwa njia zenye maana zaidi. Ni lazima tufundishe kwa mifano. Tunapaswa pia tuchukue muda wa kuelezea dhana hizi kwao na kuwaongoza katika kuzifanyia matumizi katika mahusiano yao.

► Je, kuna njia gani ambazo wazazi wanaweza kuwasaidia nazo watoto wao kujifunza huu upendo wa kujitoa binafsi kwa ajili ya watu wengine, wakianza na familia zao wenyewe?

### **Upendo wa Lugha ya 1: Maneno ya Uthibitisho**

Watu ambao lugha yao ya msingi ni maneno ya kuthibitisha hujisikia wenye kupendwa zaidi wakati watu wengine wanatumia maneno ya kudhihirisha kuwathamini kwa uaminifu kwa ajili yao. Kama lugha ya msingi ya upendo kwa mwanamke ni maneno ya udhihirisho, mume wake anaweza akadhihirisha upendo wake wakati anapokuwa anaongea naye au anapoongea kuhusu yeye. Anaweza akamwandikia taarifa ndogo, akimwambia baadhi ya sababu mahususi za yeye kumthamini. Anaweza kuzungumza na mtu mwingine yeyote kuhusiana na tabia ya mke wake au kazi yake jinsi ilivyo nzuri. Wakati mke wake atakapokuja kusikia kuhusu maneno yake, atajisikia kupendwa na kuthaminika.

Tunaweza tukawauliza marafiki zetu kwa ajili ya ushauri kwa njia ambayo kwamba inathibitisha thamani yao. Kwa mfano:

- “Wewe unaongeza mtazamo mzuri kila wakati, kwa hiyo nataka nipate mawazo yako juu ya jambo hili...”
- “Wewe ni mzoefu katika jambo hili, kwa hiyo ningependa nipate ushauri wako...”
- “Wewe unajua mengi sana kuhusu \_\_\_\_ kisha ninafanya, kwa hiyo kama una ushauri au mapendekezo yako kwa ajili yangu, nitafurahiwa kama nitayasikia.”

Maneno yote ya uthibitisho yanapaswa yazungumzwe kwa uaminifu. Vinginevyo, yatakuwa hayana maana au yenye kujeruhi. Maneno ya uthibitisho ambayo hayana uaminifu yanadhoofisha mahusiano. Yanakuwa hayako kwenye msingi wa ukweli, kwa hiyo msikilizaji wake hawezi akaamini uhamasishaji wa msemaji.

Maneno ya uaminifu ya uthibitisho ni ya kweli kwa ajili ya ukweli. Siyo ya bandia au yaliyotiwa chumvi nyingi. Kwa kuwa uthibitishaji ni udhihirisho wa kutoka ndani ya moyo. Kinachokuwa kimesemwa ni kile ambacho msemaji kwa ukweli anajisikia nacho na anakiamini.

Maneno ya uthibitisho yanaweza yakamhamasisha msikilizaji kuendelea kukua na kuwa na maendeleo ya baadaye, lakini kamwe hapaswi kuwa mtu wa hila. Hatupaswi tujaribu kuwadhibiti watu wengine kwa maneno ya uthibitisho.

► Mwanafunzi anapaswa asome Waefeso 4:29 kwa ajili ya kikundi. Je, ni maelezo gani yametolewa hapa kwa ajili ya mambo ambayo hayapaswi kusemwa? Je, maneno yetu yanapaswa yakamilishe nini? Je, baadhi ya maneno yanaweza kuwa yanafaa kwenye hali moja na yakawa hafai kwenye hali nyingine?



Kile tunachowaambia watu wengine lazima kila wakati kiwe kinachofaa na chenye neema. Mambo ambayo tunayasema yanapaswa yampe Mungu fursa za kufanya kazi ndani ya maisha ya wale ambao tunazungumza nao. Tunachosema kinapaswa kiwe kinachojenga, na siyo kinachobomoa. Kinapaswa kiweze kukuza afya na uponyaji, na kamwe kisiwe kitakachoharibifu.

### **Mada za Uthibitisho**

Kuna aina tofauti za maneno ya uthibitisho. Siyo maneno yote ya uthibitisho yanakuwa na thamani inayolingana au umuhimu. Maneno ya thamani ya juu ya uthibitisho yanahitaji mawazo mapana na yenye nguvu nyingi kutoka kwa mtu anayewapa; inawezekana hata ikawa ni kujisikia vibaya kuyasema wakati mwingine; lakini maneno haya yanaunganisha upendo katika kiwango chenye nguvu, na njia zenye maana zaidi.

### ***Kusifia Mwonekano***

Kusifia mwonekano wa mtu kunaweza kuwa njia mojawapo ya kutoa uthibitisho, hasa kama unaonyesha kuthamini kwa ajili ya juhudi zao au njia ambazo wanazitumia katika kudhihirisha nafsi ya mtu. Hata hivyo, kusifia mwonekano wa mtu ni uthibitisho ulio dhaifu, hasa wakati inapokuwa kwamba haihusiani na asili ya mtu.

Watu wa kipekee wenye mvuto ambao mara nyingi wamekuwa wakisifiwa huwa wanafikia kutokuwa na uhakika kuhusiana na mwonekano wao, kwa sababu wanaanza kujihisi kwamba thamani yao ndipo inapotegemea, na wanafikiri inapaswa iwe kamilifu.

Thamani ya mtu haiamuliwi na mvuto wake wa nje. Aidha, kuna mipaka katika kile ambacho mtu anaweza kufanya ili kuboresha mvuto wao wa kimwili. Kwa sababu ya mambo haya, aina hii ya uthibitisho haipaswi kutumika kupita kiasi.

### ***Kupongeza Mafanikio na Huduma***

Njia nyingine ya kumpongeza mtu kwa maneno ni kupongeza kwa mafanikio na utendaji wake. Mtu anayekuwa anazungumza huchukua muda mwingi wa kudhihirisha shukrani kwa yale ambayo mtu mwingine ameyafanya, badala ya kuchukulia matendo yake kama ya kawaida.

Mifano:

- Mke anampongeza mume wake kwa kutimiza lengo gumu alilokuwa akilifanyia kazi.
- Mume anaona na kumshukuru mke wake kwa kile alichokifanya katika kumsaidia yeye kwenye mradi aliokuwa akiufanyia kazi.
- Wanafamilia wakimpongeza mpishi aliyetengeneza mlo mzuri kwa ajili ya wao kufurahia.

Wakati unapokuwa unapongeza utendaji au mafanikio, jaribu sana kuepuka kumfanya mtu huyo afikiri kwamba upendo wako unategemea utendaji wake mtu huyo. Kwa mfano,

kumwambia mwanao kwamba unajivunia yeye kwa sababu alipata matokeo mazuri kwenye mtihani kunaweza kukamfanya ajisikie kwamba utampenda kwa kiasi kidogo sana ikiwa atapata matokeo hafifu. Njia moja ya kuthibitisha thamani ya mtu ni kusema, "Nina furaha kwamba uliweza kufanya vizuri kwenye mtihani wako. Ninajivunia wewe kwa kuchukua jukumu la kujifunza na ukafanya vizuri kadri ulivyojitahidi." Lakini hata iwe unafanyaje, usiache kupongeza mafanikio ambayo ni muhimu kwao.

### ***Kutambua Tabia na Juhudi***

Ni jambo zuri zaidi kuthibitisha tabia ya mtu na juhudi ambazo zimefanywa na yeye katika kumfanikisha badala ya kuthibitisha utendaji wake mzuri tu.

Kwa mfano: Mwanariadha mtoto anapaswa apongezwe zaidi kwa jitihada zake na tabia yake nzuri kuliko kushinda mchezo. Watu wachache ndiyo wanaoweza kufanikiwa katika utendaji, lakini mtu anaweza kuchagua kuonyesha tabia njema na tabia ndiyo muhimu zaidi.

### ***Kumpongeza mtu kwa jinsi Alivyo***

Uthibitisho ulio bora zaidi ni ule wa kutambua tabia za mtu: sifa za kibinafsi, sifa bainishi za tabia, na sifa bainishi za nafsi binafsi ya mtu. Aina hii ya uthibitisho una nguvu zaidi kuliko uthibitisho wa mafanikio kwa sababu una misingi yake kwenye thamani ya mtu mwenyewe, na siyo katika hali zinazobadilika.

Mifano:

- "Watoto wanakuwa na mvuto wako! Wewe ni mzuri sana katika kuelezea mambo kwao, na una subira sana kwa maswali yao."
- "Ninakuamini, kwa sababu nimekuja kukuona kwamba wewe ni mtu mwaminifu."

Kuhusishana kwa karibu kwenye aina hii ya uthibitisho, ni utambuzi wa jinsi Mungu anavyofanya kazi ndani ya maisha ya mtu, kwa kuwezesha kuwa na njia fulani au kufanya jambo fulani.

Mifano:

- "Ninapenda kuona jinsi Mungu anavyokutumia katika maisha ya vijana unaowaongoza. Mmoja wao aliniambia kwamba anataka aishi ka ajili ya Yesu kwa sababu ya kukuangalia maisha yako!"
- "Ninaamini kwamba Mungu anakwenda kukusaidia wewe katika changamoto ya hili jukumu ulilokabidhiwa. Nitakuwa nikikuombea!"

Mdhihirisho wa furaha na shukrani kwa ajili ya uwepo wa mtu na uhusiano ni baadhi ya maneno yenye nguvu ya uthibitisho, Vinaonyesha thamani ya mtu.

Mifano:

- "Mikusanyiko ya kifamilia huwa ni ya kipekee zaidi wakati ukiwa pale."

- “Ninapenda kuwa na wewe.”
- “Wewe ni wa thamani sana kwangu, na ninakupenda!”

### **Taarifa Muhimu Kuhusiana na Maneno na Uthibitisho.**

1. Kamwe usilaumu au kudhihaki tabia za mtu za kimwili. Watu hubeba pamoja nao tabia za mwilini katika maisha yao yote. Kamwe usitake kumpa mtu jina la utani lenye msingi wake katika tabia zake za mwilini, haswa anapokuwa ana kasoro za kimwili.
2. Uthibitishaji wa uwezo, sifa, na tabia njema humpa motisha msikilizaji kuendelea na kukua ndani yake. Kuonyesha dosari husaidia mara chache sana.
3. Kutoa ushauri kunaweza kuwa na maana kwamba kuna kosa kwa msikilizaji. Kama unataka kutoa ushauri kwa mtu, toa uthibitisho wenye nguvu ukiambatana na huo ushauri.
4. Mapendekezo yanayotolewa kwa njia ya malalamiko hayaleti motisha. Kwa mfano, kusema kwamba kazi hiyo inapaswa kuwa imefanywa tayari, au kuonyesha aibu kutokana na kushindwa kwa mtu kuitekeleza, huwa haisaidii. Kauli hizi humfanya mtu ajisikie kama tayari ameshindwa; kama ataendelea kufanya kazi hiyo baadaye, bado atajisikia kwamba ameshindwa.

### **Maneno ya Kuumiza**

Mtu ambaye anahitaji sana maneno ya uthibitisho huwa anakuwa ameumizwa zaidi na maneno kinzani yanayotolewa. Kukosolewa kimsingi kunaumiza sana na kunamfanya anayekosolewa kuwa na mashaka kuhusu thamani yake kama mtu. Kutokuwa na subira, na maneno ya hasira husababisha madhara ya mhemuko ambako mtu anayefanyia hayo anaweza kamwe asipone tena kabisa. Hii wakati mwingine ni kweli wakati msemaji anapokuwa haelewi maumivu yanayosababishwa na maneno yake na kamwe hataomba msamaha.

Kama na maneno yenye nguvu ya uthibitisho yanavyohusiana na thamani ya mtu, ni vivyo hivyo ilivyo mbaya zaidi, kwamba kauli zenye kuumiza ni shambulio la binafsi. Kwa mfano, “Natamani nisingekutana nawe kamwe.”

Kauli mbaya zaidi zifuatazo ni zile ambazo zinatangaza jambo fulani kuhusiana na tabia muhimu ya mtu: “Wewe ni\_\_\_\_\_.” Kauli zinazoleta madhara kuhusu tabia ni pamoja na “Wewe kila wakati\_\_\_\_\_” au “Wewe kamwe \_\_\_\_\_.” Kauli hizo zinadokeza kuwa mtu huyo hana uwezekano tena wa kuimarika kwa sababu ya dosari muhimu zisizoweza kubadilika.

Ikiwa mtu atakuwa amejeruhiwa – hasa ikiwa ameumizwa katika sehemu yake ya msingi ya lugha ya upendo – kwa kawaida atajaribu kujiondoa kutoka katika kuendelea kupata majeraha zaidi. Watu wanaotumia maneno yaliyo hasi kwa kawaida siyo watu wakarimu kwa maneno chanya, kwa hiyo msikilizaji anakuwa anayo matumaini madogo sana kwamba

anaweza akapata tiba iliyo nzuri zaidi kwa kubadilisha tabia yake. Hatakuwa ametiwa moyo wa kuboresha tabia yake ili aweze kuvuna upendo.

Wakati mwingine watu walio wa hasira husema mambo ya kuumiza kwa sababu lengo lao ni kutaka kuumiza mtu mwingine, Nyakati nyingine, msemaji huwa anakuwa ana nia njema, lakini bado maneno yake yatakuwa ni yenye kuumiza. Watu wengine hutumia maneno hasi kutaka kumlazimisha mtu fulani awe na tabia nzuri, lakini hilo nalo kamwe haliwezi kufanya kazi.

► Mwanafunzi anapaswa asome Wakolosai 3:8 kwa ajili ya kikundi. Watu waliookoka hawapaswi kuendelea kutenda dhambi dhidi ya Mungu na dhidi ya watu wengine katika njia kama hizi.

### **Kwa ajili ya majadiliano ya Kikundi**

► Kwa maneno yako mwenyewe, elezea kuhusu upendo wa kweli. Je, kwa nini ni lazima Roho Mtakatifu atusaidie kuwa na uwezo wa kuwapenda watu wengine kama inavyotupasa?

► Fafanua inamaanisha nini kumpenda mtu bila masharti. Kuna umuhimu gani wa upendo wa Mungu kwako usiokuwa na masharti?

► Je, kwa nini ni muhimu hasa kudhihirisha upendo kwa mwenzi wako au mtoto kwa lugha yao ya msingi ya upendo?

► Je, ni kwa jinsi gani kupokea maneno ya kuthibitisha kumekuwa na manufaa kwako?

► Je, ni kwa jinsi gani umeonyesha upendo wako kwa ajili ya wanafamilia wako kwa maneno ya uthibitisho katika wiki hii.

### **Maombi**

Baba wa Mbinguni,

Asante kwa kunifundisha mimi kuhusu upendo wa kweli usiokuwa na masharti. Asante kwa kuuelezea katika Neno lako na kwa kuudhihirisha kupitia upendo wako kwangu.

Nisaidie nijifunze jinsi ya kupenda na kuitumikia familia yangu kama Kristo naye alivyonienda na kunitumikia mimi. Nipe uwezo wa kuzingatia ustawi wa mwenzi wangu wa ndoa, watoto, ndugu zangu na wazazi.

Asante kwa kunikumbusha umuhimu wa maneno ninayoyasema. Ninasikitika kwa maneno ambayo nilishawahi kuyasema na ambayo yamekuwa ni ya kuumiza watu wengine na kukuvunja wewe heshima. Naomba unisaidie katika kukumbuka kwamba maneno yangu ni lazima yawe yenye kuthibitisha, ya kujenga, na ya kuponya.

Ameni

## Kazi za Kufanya

(1) Zungumza na wanandoa walio katika ndoa yenye nguvu, ukiwauliza maswali ya kujifunza kutokana na maisha yao. Utakapokuwa umemaliza mazungumzo, andika aya mbili kuhusu maarifa waliyoshiriki na chochote ambacho unataka ukitumie wewe kwenye ndoa yako mwenyewe.

Hapa kuna mawazo kuhusiana na maswali utakayouliza:

- Je, kuna tofauti gani kati ya nafsi zenu binafsi ambazo zimeathiri uhusiano wenu?
- Je, ni kwa jinsi gani kila mmoja wenu amekua kutokana na hizi tofauti?
- Je, ni kwa jinsi gani umelazimika kurekebisha matarajio yako, mtazamo wako na tabia yako ili uweze kuheshimu na kutumika kwa kila mmoja?
- Je, ni njia gani za kivitendo unazotumia kuonyesha upendo wenu kwa kila mmoja?
- Je, mwenzi wako hufanya nini au kusema mambo gani ambayo yanakusaidia wewe kujua kwamba unapendwa?
- Je, ni kwa jinsi gani uhusiano wako na mwenzi wako umeathiri uhusiano wako na Mungu?

(2) Katika Mithali 31:10-31 mwandishi amejumuisha maneno mengi ya uthibitisho kwa ajili ya mke wake. Maelezo ya tabia na maneno yake yanatuambia kuhusu tabia yake. Je, yeye anamthibitisha mke wake kwa mambo ya aina gani? Angalia kifungu kwa ajili ya mambo haya:

- Mwonekano wake
- Mafanikio yake na huduma
- Tabia na juhudi yake
- Yeye ni nani kama mwanadamu?
- Yeye ni nani kama mwamini?

Je, tunaweza kujifunza mambo gani kutokana na yale yaliyowekewa msisitizo katika kifungu hiki?



# Somo la 9

## Lugha Tano za Upendo – Sehemu ya 2

### Malengo ya Somo

Hadi kufikia mwishoni mwa somo hili, mwanafunzi atapaswa:

- (1) Kuelewa lugha tano ambazo ndani yake upendo hudhihirishwa.
- (2) Kujadili hatari zinazohusiana na matumizi mabaya au kupuuzia mojawapo ya lugha tano za upendo.
- (3) Kuelezea faida za mhemuko wa tanki la watoto kujaa.
- (4) Kutambua lugha za msingi za upendo za wanafamilia wa karibu.
- (5) Kuorodhesha njia mahususi za kuonyesha upendo kwa wanafamilia katika kila mojawapo ya lugha tano za upendo.
- (6) Kujitolea kuonyesha upendo kwa ajili ya wanafamilia katika lugha zao za msingi za upendo.

### Utangulizi:

Katika somo lililopita, tulijifunza kuhusu upendo wa kujitolea binafsi usiokuwa na masharti. Pia tulijifunza kwamba kuna angalau njia tano tofauti (lugha) ambazo ndani yake upendo unaweza ukadhihirishwa. Kwa kawaida watu wengi hutambua na kudhihirisha upendo kimsingi katika moja au mbili ya hizi njia tano.

Tulijadili kuhusu maneno ya kuthibitisha na tukagundua njia za kivitendo za kuwasilisha upendo wetu kwa wanafamilia. Kwenye somo hili, tutajifunza kuhusu aina nne zilizobakia za lugha za upendo, kisha tutafanya matumizi maalumu kwa ajili ya kudhihirisha upendo wetu kwa watoto wetu.

### Lugha ya Upendo ya 2: Muda ulio Bora.

Watu ambao lugha yao ya msingi ya upendo ni Muda ulio Bora hujisikia kuwa wamependwa zaidi wakati watu wengine kwa kukusudia wanatenga muda wao binafsi ili kuwa pamoja nao. Muda huu unatengwa kwa uangalifu sana kwa ajili ya kuwa pamoja, mwelekeo ukiwa ni kwa kila mmoja. Ni muda wa kufurahia na kufanya ushirika pamoja.

Muda ulio bora hauji kwa bahati mbaya au kama muda wa ziada. Ikiwa umekwama kwenye foleni au unasubiri miadi, unapaswa kutumia muda huo kwa busara sana, lakini muda huo kwa kawaida si sawa na ubora wa wakati wa kawaida wa pamoja. Mwenzi au mtoto wako anaweza akafanya kazi kwenye mradi mmoja na wewe, na hilo ni jambo la thamani, lakini

muda huo wa pamoja hauwezi siku zote ukakidhi hitaji lenu kwa ajili ya muda ulio bora pamoja nawe.

Mazungumzo yasiyoingiliwa na jambo lolote au kitu chochote ndiyo aina bora kabisa ya muda ulio bora. Katika mazungumzo ya aina hiyo, kila mtu anakuwa yuko makini kabisa kumsikiliza mwenzake. Kila mmoja hupuuzia usumbufu wa aina yeyote kama vile meseji zinazolingia kwenye simu au miito ya simu ili aweze kuuweka mwelekeo wake kwa mtu aliye naye na kwenye mazungumzo yao.

Hapa kuna njia nyingine chache ambazo wewe unaweza ukaonyesha na kudhihirisha kwamba unasikiliza kwa umakini mkubwa:

**1. Dumisha mtazamo wa macho.**

**2. Sikiliza kiutendaji.** Toa majibu kwa kile ambacho mtu mwingine anasema. Usifikirie tu kile ambacho utataka ukiseme baadaye. Badala yake, chukua muda wa kukagua uelewa wako kuhusu kile ambacho mtu mwingine anafikiria na kusema. Unaweza kuthibitisha kwamba unayaelewa mazungumzo kwa usahihi kwa kusema kitu kama, "Kama ninakusikia vizuri na kwa usahihi, unahisi kwamba...."

**3. Usiingie katikati ya mazungumzo.** Msikilizaji mara nyingi hujifikiria kwamba tayari ameshaelewa wazo na kwa haraka huingilia mazungumzo akitaka atoe maoni yake. Hali hii humfanya muongeeji kujisikia kana kwamba msikilizaji hakutaka kuchukua muda wa kuelewa kiuhalisia.

**4. Sikiliza kwa kujisikia, na siyo tu kwa yale yaliyotendeka au kufanywa.** Wakati tunapojaribu kutaka kuelewa mitazamo ya watu wengine, tunakuwa tunaonyesha kwamba tunafikiri mazungumzo ni ya thamani. Tunaposikiliza kwa umakini wote wa mioyo yetu, tunawasilisha kwamba maoni na hisia zao ni muhimu sana kwetu; na kwamba wao wenyewe pia ni muhimu kwetu!

Muda ulio bora zaidi ni wakati ambapo hufanyi jukumu lolote lakini unawasiliana na kila mtu, aina nyingine za muda pia ni za thamani. Familia zinaweza zikatumia muda ulio bora kwa pamoja kila siku kwenye muda wa chakula, wakiweka mwelekeo wao juu ya kila mmoja wanapokuwa wanakula kwa pamoja.

Kusoma hadithi kwa watoto wadogo, kucheza pamoja, au kufanya shughuli ya burudani pamoja ni njia nyingine ambazo familia zinaweza kutumia muda ulio bora kwa pamoja. Kufanya mradi au mambo ya ufundi kwa pamoja ambavyo ni kwa ajili ya kufurahisha tu, siyo kwa ajili ya shule, au kazi, au huduma, pia ni muda ulio bora.

Wakati mtu anapokuwa mbali na nyumbani kwake, muda ulio bora unaweza kutumika kwa kutembeleana kwa njia ya simu kwa ajili ya kuwasiliana pamoja.

Muda ulio bora ni uliotengwa, usiovurugwa, usioharakishwa katika kuweka mwelekeo na kufurahia ushirika wa kila mmoja. Ni bora zaidi kutenga muda ulio mzuri na mwenzi wako pamoja na watoto kila siku.



## **Wakati Muda unapokuwa Haujatengwa.**

Wakati mwenzi au mzazi anapokuwa ni kiongozi wa huduma, ni vigumu sana kwake kutenga muda ulio bora pamoja na familia yake. Watoto wa mchungaji mara nyingi watakuwa wanahisi kwamba mtu mwingine anaweza kumwita na kumpata kwenye simu na kupata usikivu wa baba yao, lakini akawa ana shughuli nyingi akashindwa kuchukua muda wake kwa ajili yao. Inaweza ikaonekana kwamba muda kwa ajili ya familia unatolewa kafara kwa ajili ya huduma.

Vipingamizi haviwezi kuepukika kabisa kwa mtu aliyeko kwenye huduma, lakini ni lazima kujaribu kutenga muda kwa ajili ya familia. Kama utafanya hivyo, watakuwa kwenye uwezekano mkubwa wa kuelewa majukumu yako ya kawaida na usumbufu wa ziada unaojitokeza ambao hauwezi kuepukika.

Mtu ambaye lugha yake ya msingi ya upendo ni muda ulio bora hujisikia anayependwa kwa kiasi kidogo sana wakati anapokuwa hana muda wa makusudi na muda wenye mwelekeo na familia yake. Hujisikia kujeruhiwa sana wakati muda ulio bora haupewi kipaumbele, na wakati ambapo mipango iliyopo kwa ajili ya muda ulio bora inapowekwa pembeni wakati Vipingamizi vinapojiinua. Inakuwa ni vigumu sana kwake wakati familia yake inapokuwa na shughuli nyingi za kuwafanya washindwe kuwasiliana na yeye. Hujisikia mwenye kuthaminika kwa kiasi kidogo sana wakati wanafamilia wanapokuwa hawamsikilizi wakiwa na umakini uliogawanyika.

Kama unashindwa kumpa mwenzi au mtoto wako umakini na uangalifu wa binafsi, hawawezi kuhisi upendo ulio nao kwao, ingawaje unafanya mambo mengi kwa ajili yao. Mwanamume anaweza akawa anafanya kazi ngumu kwa ajili ya familia yake, lakini bado mke wake akajisikia kwamba hapendwi kwa kuwa mume wake ana shughuli nyingi sana zinazomfanya akose kuwa na wakati pamoja naye.

Mvulana mdogo alikwenda kwa baba yake kumwelezea hadithi ambayo alikuwa ameisikia katika siku za karibuni. Baba yake alikuwa anasoma kitabu, lakini akatulia ili aweze kumsikiliza kwa dakika moja, kisha akaendelea na kusoma kitabu chake wakati kijana wake akiwa katikati ya masimulizi ya hadithi yake. Katika maisha yake yote yaliyoendelea, kijana alikuwa anakumbuka jinsi alivyokuwa amejisikia katika wakati ule.

► Je, muda ulio bora kwa kawaida unaonekanaje ka familia yako? Je, ni matatizo gani uliyo nayo ya kuyashinda ili uweze kutumia muda wako wenye maana pamoja na familia yako?

## **Lugha ya Upendo ya 3: Zawadi**

Watu ambao lugha yao kuu ya upendo ni kupokea zawadi hujisikia kuwa wanaopendwa zaidi sana wakati watu wengine wanapowapa kitu ambacho kinaonyesha kwamba walikuwa wanawafikiria.

Zawadi zinazoweza kuwafanya watu wajisikie kama wanaopendwa ni zawadi ambazo zinatolewa kwa kufikiria sana. Zinachaguliwa kwa kuangalia hali ya matamano ya mpokeaji.

Siyo lazima ziwe za vitendo au ambazo zinazohitajika. Zawadi za upendo hazitolewi tu kwa sababu mtoaji alikuwa hazihitaji tena. Zawadi zinatakiwa zichaguliwe kwa makusudi fulani au zitengenezwe na mtoaji mwenyewe.

Zawadi inayomfanya mtu ajisikie kwamba anapendwa siyo lazima iwe ya gharama kubwa. Inaweza ikawa ni kitu kisichodumu kwa muda mrefu kama vile, chakula maalumu au peremende; au inaweza ikawa ukumbusho wa kudumu unaoonekana kuwa wenye uhusiano na mtoaji.

Kwa mtu ambaye lugha yake kuu ya upendo ni kupokea zawadi, siku za kuzaliwa, maadhimisho ya kumaliza miaka kadhaa, na siku za mapumziko ni za muhimu sana. Ni muhimu sana kwa ajili ya wanafamilia kukumbuka siku hizi wakiwa pamoja na zawadi maalumu kwa ajili ya mtu husika. Kutokupokea zawadi katika sikukuu hizi maalumu kiuhalisia inakuwa ni kuchungu sana kwa huyu mtu.

Kutoa zawadi hakupaswi kufungamana na siku maalumu tu, ingawaje; inapaswa kiwe ni kitu endelevu katika maisha. Mwanandoa, mzazi, au mtoto wa mtu fulani ambaye lugha yake ya msingi ya upendo ni kupokea zawadi anapaswa ajenge tabia ya kuangalia zawadi ambazo zitawasaidia wapendwa wao kukumbuka kwamba wanafikiriwa na kupendwa.

Mke ambaye lugha yake ya msingi ya upendo ni kupokea zawadi anaweza akajisikia asiyependwa kabisa kama atafikiria kwamba mume wake alijaribu kuokoa gharama kwa kumpatia zawadi ambayo ingeweza ikaonekana kama tu ni muhimu. Labda anahitaji ufagio mpya, na akamletea ufagio mmoja. Ni vyema kwake kuwa na huo ufagio, lakini zawadi hiyo haiwezi kumsaidia ajisikie kwamba anapendwa.

Zawadi ni za muhimu wakati zinapodhihirisha kwamba mtoaji alikuwa anaelewa na kujali kuhusu anayekwenda kuipokea zawadi hiyo. Zinakuwa ni za muhimu wakati ambapo kulikuwa hakuna ulazima huo. Zawadi inakuwa muhimu wakati mtu anapokuwa amejifikiria, akaweka juhudi na gharama katika kuipata.

Watoto ambao lugha yao kuu ya msingi ya upendo ni kupokea zawadi hujisikia kupendwa zaidi wakati baba anapowanunulia aiskrimu kuliko anapowalipia malipo yao ya shule, ingawaje malipo ya shule ni makubwa na muhimu zaidi. Badala ya kudai kwamba wanafamilia wakubaliane na kile ambacho ulikuwa unakitoa kama utaratibu wa mazoea wa kawaida, tafuta njia ya kufanya jambo ambalo litakuwa ni maalumu kwao.

Watu wengine huwafanya watoto au wenzi wao kuwa waombaji wa kila kitu. Mtu anayetumia fedha sana na mara chache hujinunulia vitu kwa ajili yake mwenyewe anaweza asione kuwa ni jambo rahisi kuwa mkarimu na kutoa zawadi zinazoonekana kwake kwamba siyo muhimu. Anakuwa hataki wanafamilia wake waanze kutegemea kupata zawadi kutoka kwake. Lakini kama angekuwa na mwenzi wake au mtoto ambao zawadi ni muhimu kwao, atafanya kazi ya ziada ili kuishinda tabia yake ya kawaida. Atajaribu kuziona zawadi kama zinavyoonekana kwao – zenye umuhimu na thamani. Wakati wa kutoa zawadi, toa kwa uhuru, ukiwa na furaha!

► Mwanafunzi anapaswa asome 2 Wakorintho 9:6-9 kwa ajili ya kikundi. Kwenye kifungu hiki, Paulo anawaasa Wakorintho waliookoka kwamba watoe kwa ukarimu kwa waumini wenzao walio katika uhitaji. Kutokana na Aya hizi, jaribu kutambua aina nne au tano za motisha kwa ajili ya ukarimu. Je, ni kwa njia gani kanuni hizi kutoka katika Aya hizi zinavyotumika kwa ajili ya ukarimu ndani ya wanafamilia wetu?

► Je, utoaji zawadi una nafasi gani katika familia yako? Je, unapata matatizo yoyote katika kudhihirisha upendo kupitia utoaji wa zawadi? Je, matatizo hayo ni yapi na ni kwa jinsi gani unaweza kuyashinda?

#### **Lugha ya Upendo ya 4: Matendo ya Huduma**

Watu ambao lugha yao ya msingi ya upendo ni matendo ya huduma hujisikia kupendwa zaidi wakati watu wengine wanapofanya mambo kadhaa kwa ajili yao.

Matendo ya huduma yanakidhi mahitaji ya vitendo. Yanaweza yakawa au yasiwe kwamba ni mambo ambayo mtu alikuwa anashindwa kufanya kwa ajili yake mwenyewe. Huduma inaweza kuwa ni rahisi sana kama vile mtu anapokuwa anampatia mtu mwingine kinywaji. Inawezekana ikawa ni kumtunza mtu ambaye ni mgonjwa. Inaweza ikawa ni kusaidia mtu katika hali ya uhitaji.

Kwenye familia nyingi, kunatokea kuwepo na vipindi vya muda mrefu ambavyo mwanafamilia mmoja atahitaji apewe uangalizi binafsi wa kila wakati. Kwa sababu ya upendo wa familia na kujitolea kwa ajili ya mtu huyo, wanaendelea kufanya vitendo vingi vya huduma kwa ajili yake. Ingawaje muda mwingi huwa unatengwa kwenye matendo ya huduma, wanafamilia wanapaswa kudhihirisha upendo kwa mtu mwingine, kwa njia yenye maana pia, hasa kama lugha ya msingi ya upendo ya mtu siyo matendo ya huduma.

Baadhi ya vitendo vya huduma hasa vya kufanana ni mpangilio wa kawaida wa kila siku na vinaweza vikadharauliwa au vikachukuliwa kama ni vya kawaida tu. Wanawake wengi wanadhihirisha upendo wao kutokana na vyakula vizuri wanavyopika kila siku na kutunza nyumba. Mwanamume anaweza kufanya kazi kwa ajili ya kutoa matumizi kwa familia yake. Kama tayari unaihudumia familia yako kila siku katika njia kama hii, bado unatakiwa utafute njia nyingine maalumu za kufanya matendo ya huduma kwa ajili ya wanafamilia wako kwa njia hii ya msingi ya lugha ya upendo.

Wakati mwanamke anapoonyesha kutokuwa na shauku na mahitaji madogo ya mumewe, anashindwa kuzungumza lugha hii ya upendo. Labda anafikiri kwamba, "Anaweza akajichukulia maji ya kunywa yeye mwenyewe." Lakini kama atanyanyuka na kumchukulia hayo maji ya kunywa, itadhihirisha kwake upendo wake maalumu.

Vivyo hivyo, mume naye anapaswa kuonyesha kumfikiria mwenzake. Wakati anapompa mke wake mapumziko kutokana na jukumu ambalo kwa kawaida analifanya, kwa kufanya jambo hilo kwa ajili yake, anampa heshima kwa jukumu lake na anatambua kwamba kazi yake ni ngumu na ni ya muhimu.

Mume anaweza kuhisi kwamba tayari anafanya kazi za kutosha, na kwamba jukumu la mke wake ni kushughulikia kazi zote za nyumbani. Anaweza hata kufikiri kwamba anapaswa kuwa na ufanisi zaidi kuliko alivyo. Ikiwa anadhani kwamba kazi za nyumbani ziko chini ya hadhi yake, inaonyesha kwamba anawachukulia wanawake kama wa chini na wanaostahili kazi za chini. Wanawake si wa chini, na kazi za nyumbani si za chini zaidi kuliko kazi za nje ya nyumba.

Mwanamume anaweza kujihisi kwamba ni kama anafanya jukumu la mtumishi wa nyumbani (aliye chini ya mke wake) wakati anapokuwa anasaidia kufanya kazi za nyumbani, lakini hivyo siyo kweli. Kama atajitolea kufanya kwa kutoa utumishi huo, anaonyesha thamani ya kazi hiyo na thamani ya mtu ambaye anamsaidia kufanya kazi hizo. Utumishi wake humheshimu mtu ambaye kwa kawaida ndiye anayefanya majukumu hayo na huonyesha uthamini wake kwao. Mkewe hatamwona mume wake kama ni mtumishi tu bali pia anayeheshimika zaidi.

Iwapo watu wanasaidiana kwa hasira na kwa shingo upande, wanaonyesha kwamba wanaolazimishwa kusaidia. Kitendo chao cha kufanya huduma hakiwasilishi dhana ya upendo. Kama watafanya matendo ya huduma kwa uaminifu na kufanya kwa juhudi zao zote, itaonyesha kwamba wako huru kuchagua kuhudumia, kwa sababu hakuna mtu yeyote atakayeweza kuwalazimisha kufanya huduma kama hiyo. Huduma hii ya furaha hudhihirisha upendo kwa uwazi. Inasaidia pia kupata heshima kutoka kwa wapendwa wao.

► Je, ni wakati gani unaouona ni mgumu kwako kutoa huduma kwa familia yako? Je, ni kwa jinsi gani kufikiri kuhusu huduma kama udhihirisho wa upendo kunavyobadilisha mtazamo wako?

### **Lugha ya Upendo ya 5: Mguso wa Kimwili**

Watu ambao lugha yao kuu ya upendo ni mguso wa kimwili hujisikia kuwa wanapendwa zaidi wakati wanapoguswa kwa upendo na wanafamilia wao.

Kuna njia tofauti za kuonyesha upendo kupitia mguso wa kimwili. Baadhi zinafaa na ni sahihi katika mahusiano kadhaa lakini siyo yote, na katika mazingira fulani lakini zinakuwa hazifai katika mazingira mengine ya mahusiano. Hapa kuna mifano michache:

- Kukumbatiana
- Kuweka mikono kuzunguka mgongoni na juu ya bega la mtu
- Kuwekeza mikono yako juu ya mabega ya mtu
- Kupapasa mgongo au bega la mtu
- Kukaa pamoja
- Kushikana mikono
- Kila mmoja kumbusu mwenzake
- kukanda mgongo
- Kumshikilia mtoto
- kuchana nywele za mtoto

- Kutoa huduma ya taratibu na kwa upole wakati mtu akiwa ni mgonjwa au akiwa ana udhaifu mwingine wa kimwili

Mguso pia unaweza kuwa na maana ya kipekee wakati mtu anapokuwa anapitia katika wakati mgumu wa maisha. Wakati wa huzuni, uchungu, upweke, na mfadhaiko, kukumbatiana na kupeana busu kunaweza kuwa na maana zaidi kwa mtu ambaye lugha yake ya msingi ya upendo ni mguso wa kimwili kuliko maneno au matendo ya huduma mengine yoyote.

Kwa mtu ambaye lugha ya msingi ya upendo ni mguso wa kimwili, ni muhimu kuendelea kudhihirisha upendo wako kimwili hata wakati ambapo wao ni wagonjwa, ikiwa uwezekano huo utakuwepo. Kumbuka kwamba upendo siyo wa masharti na ni wa kujidhabihu binafsi. Yule baba katika Luka 15:20 alimkumbatia na kumbusu mtoto wake aliyekuwa ametubu, ingawaje mtoto huyo alikuwa ananuka harufu mbaya, alikuwa mchafu, na asiyependeka kwa njia yeyote ile.

Lugha ya upendo ya mguso wa kimwili siyo lazima iwe kuhusu kujamiiana. Shughuli ya kujamiiana ni kategoria ya mguso. Matamania ya kugusa na kuguswa inaweza kupelekea kuwa ni kichocheo na udhihirisho wa kusababisha tendo la kujamiiana, lakini tendo la kujamiiana peke yake halitamtosheleza mtu ambaye lugha yake ya msingi ya upendo ni mguso wa kimwili.

Matamania ya kuhisi kwamba unapendwa kupitia mguso wa kimwili yanaweza kumfanya mtu ashawishike kuingia kwenye tendo la uasherati. Ni muhimu sana kwa wazazi kutoa midhihirisho ya kutosha isiyohusiana na mambo ya kujamiiana ya mguso wa kimwili kwa vijana wao wa kike na wa kiume, ili kwamba mahitaji ya watoto wao ya mguso wa kimwili yaweze kufikiwa. Mtoto anayejisikia kupendwa ana ujasiri mzito wa kujizuia na vishawishi au majaribu.

### **Dhambi Zinazotokana na Mguso wa Kimwili**

Wale ambao lugha yao kuu ya upendo ni mguso wa kimwili wanahisi kuumizwa au kuvunjiwa heshima na ukatili wa kimwili. Kumpiga mtu kwa hasira (Wagalatia 5:20), Kumpiga mtu makofi usoni kwa madhumuni ya kumdhalilisha (Mathayo 5:39) au kumpiga mtu kama matumizi mabaya ya mamlaka (Mathayo 24:48-49) ni kufanya uovu. Kutokana na maandiko haya, tunajua kuwa wazazi kamwe hawana haki ya kuwaumiza watoto wao, hata kama wanahisi hasira na kuchanganyikiwa. Mungu pia anasema kwamba ni uovu kwa watoto kuwapiga wazazi wao (Kutoka 21:15).

Nidhamu ya kimwili ifaayo na inayodhibitiwa ya watoto inayotolewa na wazazi kwa roho ya upole (Wakolosai 3:21), kwa ajili ya kuwasahihisha na kuwaongoza kwa ya haki, siyo dhambi. Badala yake, ni takwa la Mungu kwa wazazi la kuwawezesha kuokoa nafsi za watoto wao (Mithali 13:24, Mithali 19:18, Mithali 29:15, Waebrania 12:5-7).

Vitendo vyote vya uasherati na unyanyasi wa kingono, pamoja na kujamiiana watu wa ukoo mmoja ni uovu (Mambo ya Walawi 20:11-12, 14).

## **Kutambua Lugha yako kuu ya Upendo**

Watu si mara zote wanatambua lugha yao kuu ya upendo. Wanaweza hata wasiwe wanafikiria kuhusu njia ambazo watu wengi mara nyingi hudhihirisha upendo wao kwa watu wengine. Wanaweza hata wasiwe na ufahamu kuhusu mambo mengine yanayofanywa na watu wengine ambayo yanawafanya watu wao wajisikie wanapendwa. Chukua muda kidogo wa kutafakari tena kuhusu yale unayoyajua kuhusu lugha tano za upendo.

► Je, ni kwa lugha gani ya upendo ambayo unaitumia zaidi sana katika hali ya kawaida na mara kwa mara katika kudhihirisha upendo wako kwa ajili ya watu wengine?

► Je, lugha yako kuu na ya pili ya upendo ni zipi? Ikiwa unapata ugumu kutambua ni maonyesho yapi ya upendo yanayokupa maana zaidi kwako, hapa kuna maswali kadhaa ya kukusaidia kupata jibu kamili:

- Je, ni mifano gani ya mambo yanayokufanya wewe uwe na furaha?
- Je, mambo yako muhimu ya kukumbuka unayopendelea sana ni yapi?
- Je, huwa unalalamika kuhusu mambo gani (hata katika ukimya tu)?
- Je, ni mambo gani yanayokufanya wewe ujisikie kuumizwa sana?

## **Lugha Tano za Upendo na Watoto**

Watu wote mara kwa mara wanahitaji kupokea udhihirisho wa upendo katika lugha zote tano za upendo, lakini jambo hili ni la kweli hasa kwa watoto. Ili watoto waweze kuwa sawasawa, watoto wenye afya kihisia, wanahitajika kuambiwa mara kwa mara na kila wakati kwamba wanapendwa na wazazi wao bila ya masharti yoyote. Wazazi wanapodhihirisha upendo wao kwa ajili ya watoto wao kwa njia mbalimbali, mara nyingi kila siku, ni kama mvua inayonyesha polepole na kuitunza ardhi ya mioyo ya watoto wao.

Usitake kudhania kwamba watoto wanajua na wanajihisi upendo wako kwa ajili yao. Ni lazima mara kwa mara na kila wakati waone ukidhihirisha upendo wako katika lugha yao ya msingi ya upendo na pia katika lugha nyingine za upendo.

## **Kutambua Lugha ya Msingi ya Upendo ya Mtoto**

Gary Chapman na Ross Campbell wametoa orodha ya mawazo ya jinsi utakavyoweza kugundua lugha ya msingi ya upendo ya mtoto wako:<sup>35</sup>

1. Angalia kwa makini ni kwa jinsi gani mtoto wako anavyodhihirisha upendo wake kwako.
2. Angalia kwa makini ni kwa jinsi gani mtoto wako anavyodhihirisha upendo wake kwa watu wengine.

---

<sup>35</sup> Dr. Gary Chapman and Dr. Ross Campbell, *The Five Love Languages of Children*, (Northfield Publishing, Chicago, 1997), 101-103.

3. Kuwa msikivu na yale mambo ambayo mtoto wako anaomba mara kwa mara.
4. Tambua yale mambo ambayo mtoto wako anayalalamikia mara kwa mara.
5. Mpatie fursa mtoto wako awe na uchaguzi kati ya mambo mawili ya kuchagua.

Huenda isiwezekane kubainisha lugha ya msingi ya upendo ya mtoto kabla ya kufikisha umri wa miaka mitano.

### **Vidokezo maalumu kuhusu Lugha za Upendo kwa ajili ya Watoto.**

Hatutaingia kwa kina kuhusu kila kipengele cha lugha za upendo hapa kwani kila kimoja kilishajadiliwa hapo awali. Badala yake, tutazingatia tu vidokezi maalumu na matumizi yake kwa ajili ya kuonyesha upendo kwa watoto.

#### ***Maneno ya Uthibitisho.***

Inajitokeza kuwa ni vigumu kutoa uthibitisho hasa wakati ambapo mtu kila mara anafanya makosa na hatendi vizuri. Lakini kama unaweza kutafuta au kupata kitu cha ukweli na chenye kuthibitisha kwa kusema, kinaweza kuwahamasisha watoto wako, na kuna uwezekano mkubwa kwamba wao wenyewe watakuwa na uwezo wa kukua.

#### ***Muda ulio bora.***

Ni jambo la manufaa sana kwa familia kula pamoja angalao mlo mmoja kwa siku na kuweka mwelekeo wa kutembeleana wakati huo.

Katika familia mbalimbali zilizo na watoto wengi, ni rahisi kupuuzia suala la muda ulio bora pamoja na mtoto binafsi. Hata hivyo, kutenga muda wa kuweza kufanya jambo la kipekee na kila mtoto binafsi kutawasaidia kujihisi upendo wako kwao. Muda wa kuwa katika faragha nao pia kunawapa nafasi isiyokuwa na usumbufu ya kushirikishana mawazo binafsi ambayo wangekuwa hawako tayari kuyashirikisha wakiwa mbele ya ndugu zao au wanafamilia wengine.

Mara nyingi, watoto wataomba kwa ghafla kuwa na muda ulio bora wa kukaa peke yao na mmoja wa wazazi wao. Wakati mwingine katika kipindi cha kulala mtoto mmoja anaweza kuwa wazi na kuomba kuongea na mzazi juu ya jambo fulani ambalo linawaumiza na au kuwaelemea katika mioyo yao. Ni muhimu sana kwa wazazi kupata muda wa kuwasikiliza watoto wao katika nyakati hizi. Mara nyingi, mtoto anashughulika na jambo la kiroho, na kwa kuja kwa mama na baba yake faraghani, anatafuta kupata msaada wa kiroho. Wazazi wana nafasi maalumu ya kuwaongoza watoto kwa Yesu katika nyakati hizi.

Katika wakati wako bora na watoto wako, jifunze kuwauliza maswali ya wazi ambayo yatakusaidia wewe kuelewa jinsi wanavyofikiri, na ni kwa jinsi gani wanavyojihisi. Maswali ya wazi hayawezi kujibiwa kwa maneno, "Ndiyo" au "Hapana." Maswali ya wazi hayana jibu maalumu. Maswali ya wazi kwa kawaida huanza na "Kwa nini..." "kwa vipi..." au "Nini..." Mazungumzo ya wazi huanza na misemo kama, "Niambie kuhusu..." au "Je, unafikiria nini kuhusu..."

Mtoto wako anapokuwa anajibu swali lako, hakikisha unakuwa makini sana kusikiliza majibu yao na kuchukua hatua ipasavyo. Katika nyakati nyingine utaweza kutaka kuuliza swali la kufuatilia. Wakati mwingine utataka kubainisha kuhusu maswali yao ili kutaka kuhakikisha kwamba unaelewa kile wanachojaribu kuelezea. Wakati mwingine unapaswa kuwathibitisha katika kile ambacho wanakiona na kukihisia. Ni muhimu sana kwamba mtoto asijisikie kana kwamba anahojiwa, lakini mazungumzo yawe ya asili na kawaida. Umakini wako wa kusikiliza utamsaidia mtoto wako kujisikia kwamba anasikilizwa, anathaminiwa, na kupendwa.

Kuchukua muda hasa katika kumsikiliza mtoto akielezea hadithi yake pia kunawasilisha upendo wako kwake katika njia ambayo ni ya muhimu sana kwa ajili yao. Kuchukua muda wako ili kuwasiliana nao hadithi au jambo la historia pamoja na kusoma vitabu ni njia nzuri ya kushiriki muda ulio mzuri kwa pamoja.

Kucheza michezo pamoja au kufanya mradi wa kufurahisha pamoja ni njia nyingine ya kushirikishana muda ulio bora pamoja na watoto wako.

Wazazi wengine hawawapatii watoto wao muda ulio bora. Wanajaribu kufidia hili kwa kuwapa watoto wao zawadi. Zawadi haziwezi kuwa mbadala wa muda ulio bora. Watoto wanahitaji muda ulio bora zaidi na wazazi wao, haijalishi lugha yao ya msingi ya upendo ni ipi. Hakuna kiwango chochote cha zawadi kitakachoweza kuwa mbadala wa kutumia muda ulio bora na watoto wako.

### ***Zawadi***

Ni mara chache sana wazazi kuwanunulia watoto toyi za kuchezea au vitabu vya hadithi au vya kuvutia., kwa sababu vitu hivyo vinaonekana havina ulazima. Vitu hivyo vinaweza kusaidia sana ukuaji wa mtoto, mbali ya kuwa ni udhihirisho wa upendo.

### ***Matendo ya Huduma***

Mawazo bainifu ya kudhihirisha upendo kwa ajili ya mtoto wako kwenye matendo ya huduma:

- Andaa chakula wanachokipenda kwa ajili ya kumbukumbu ya sikukuu zao za kuzaliwa.
- Wapatie utunzaji wa huruma wanapokuwa wagonjwa.
- Msaidie mtoto wako katika kuifanya kazi aliyopewa shuleni.
- Fanya kazi za nyumbani na mtoto wako na uonyeshe shukrani kwake kwa kazi yake aliyoifanya.
- Fanya kitu chenye msaada pamoja na mwanao kwa ajili ya mtu mwingine ambaye siyo wa nyumba yenu.



## ***Mguso wa Kimwili***

Watoto wadogo na pia wale wachanga ni lazima wapate upendo kupitia mguso wa kimwili. Watoto wachanga wana mahitaji yao ya vitendo, kama vile kulishwa chakula na kubadilishiwa nepi zao, lakini pia wanahitaji kushikwa, kubebwa, kubembelezwa, na kubusiwa. Mguso huu wa upole wa kimwili huwasilisha upendo kwa njia wanayohisi ni muhimu kwao kwa ajili ya mhemuko wa kiafya na kiakili.

Kwa baba kuvurumishana na watoto wake inaweza kuwa ni udhihirisho wa upendo kwao. Ushindani huo haupaswi ulete hatari ya kuumiza, kuacha kutawala, kushindwa kudhibiti, au kusababisha hasira.

## **Athari za muda mrefu za Matendo na Maneno ya Mzazi**

Wazazi wanapaswa wafuate mfano wa Mungu katika kushughulika kwao na watoto wao. Mungu siku zote huwarudi watoto wake kwa upendo mkamilifu, wa kujitolea, na usio na masharti. Anaadabisha kwa nidhamu, anasahihisha, na kuwafundisha watoto wake kwa sababu ya upendo wake alio nao kwa ajili yao (Waebrania 12:5-7). Ni katika muktadha huu wa uhusiano wa baba na mtoto ambao unafanya kazi ndani ya maisha ya watu waliookoka ili kuwafanya wamfafananie yeye (Waebrania 12:10-11).

Siyo jambo la kufaa kwa upendo wa wazazi uwe kwenye kushikamanishwa na tabia ya watoto wake. Bila shaka, zawadi chanya au matokeo mabaya kwa ajili ya tabia za watoto wao ni sehemu ya mkakati wa kumfundisha mtoto, lakini udhihirisho wa upendo haupaswi usitishwe kutolewa au uzuiwe kwa ajili ya tabia ya mtu.

Ikiwa mtoto mara kwa mara anakuwa katika upendo wa wazazi wake usiokuwa na masharti kwa wepesi zaidi anaweza kumfahamu na kumwamini Mungu kwa ajili yake mwenyewe. Hata hivyo, ni vigumu zaidi kwa wale ambao walikuwa wamenyanyaswa na kukataliwa kama watoto kuweza kuelewa na kuamini katika upendo wa Baba wa Mbinguni, hata pale wanapokuwa wameshakuwa watu wazima.

Watoto kujielewa wenyewe- hasa thamani yao kama watu binafsi – takribani siku zote unatoka kwa yale mambo wanayoyasikia na kutambua kutoka kwa watu wengine. Matendo na maneno ya wazazi wao ni yenye ushawishi zaidi, lakini wanajamii na marafiki wana mguso mkubwa pia. Aidha iwe watoto wanapata au hawapati udhihirisho wa upendo ambao wanahitaji inakuwa ni aina ya kile kitu ambacho kinaunda muonekano wao wa binafsi. Wakati upendo unapokuwa umeondolewa kwa watoto, au watoto wakakutana na unyanyasaji wa mihemuko au kimwili, inabomoa na kuharibu taswira ya uthamani wao katika njia ambayo inavuruga maisha yao yote.

Maneno ya wazazi huleta ushawishi wa uelewa wa watoto wao wenyewe. Kwa mfano:

- **Maneno ya uthibitisho:** “Ninajivunia wewe kwa kufanya kazi kwa bidii sana! Najua una uwezo wa kufanya hivyo!” hii ni kuwaambia watoto kwamba jitihada zinafaa na kwamba unaamini wanaweza kufaulu.

- **Maneno yenye kuleta uharibifu:** “Wewe ni mvivu sana. Siwezi nikakutegemea wewe kwa lolote!” Katika hali hii unaweza kusababisha mtoto kuamini kwamba hana uwezo wa kubadilika; hakuna sababu ya kujaribu kubadilika au kupata heshima yako, kwa sababu tayari umeshakata tamaa juu yao. Inaweza ikawafanya au ikajenga hisia kwa watoto kujisikia kwamba umeshawakataa.
- **Maneno ya uthibitisho:** “Ni sawa. Sisi sote wakati mwingine hufanya makosa, na kisha tunajifunza jinsi ya kufanya vizuri zaidi wakati mwingine.” Hii ni kuwaambia watoto kwamba ni jambo salama kufanya makosa – upendo wako kwao hautegemei utendaji wao ambao hauna dosari. Pia hii ni kuwaambia watoto kwamba wategemee kuwa na uwezo wa kukua, na kwamba kuna kila sababu ya kuendelea kujaribu.
- **Maneno yenye kuleta uharibifu:** “Wewe ni mpumbavu sana. Kila wakati wewe unavuruga.” Hali hii inaweza kusababisha mtoto akaamini kwamba ni ujinga kutaka kujaribu. Inaweza ikawasilisha ujumbe kwao kwamba thamani yao inategemea utendaji mkamilifu; na kwa kuwa wakati wote wanavuruga, kamwe hawana tena uwezo wa kuwa watu wa thamani. Hawatakuwa na thamani ya kupendwa tena...na wewe mwenyewe au na mtu mwingine yeyote.

Kujielewa kwa mtoto yeye mwenyewe kama mtu kunategemezwa na upendo ambao unawasilishwa au unashikiliwa kutoka kwake. Uwezo wake wa kujihusisha na watu wengine katika njia zenye ubora ni kwamba, aidha kunakuzwa au kunalemazwa na uhusiano wake na mzazi wake. Mtoto anayependwa vizuri ana uwezo wa kujifunza ya kuwapenda watu wengine kwa upendo wa kujitolea kabisa, usiokuwa na masharti. Pia ana hifadhi ya upendo ambayo anaweza kuitumia.

Upendo wa kweli ni mafuta ya mhemuko kwa ajili ya watoto, kama na vile ilivyo kwa watu wazima.

### **Faida za Tanki Lililojaa Hisia.**

Kuna njia nyingi ambazo watoto hupata faida kutokana na kuwa na matanki ya mafuta ya hisia. Wakati watoto wanapojijua kwamba wanapendwa, wanakuwa na nguvu na utulivu wanaohitaji ili kukabiliana na changamoto na kukua ipasavyo.

Watoto wanaojijua kwamba wanapendwa bila ya masharti wanakuwa wako salama kihisia. Kwa sababu hiyo, wanakuwa na utayari zaidi wa kukubali nidhamu, masahihisho, na mwongozo kutoka kwa wazazi wao kuliko wangukuwa vinginevyo. Pia wanakuwa na uwezo wa kukataa vishawishi ambavyo husababishwa na makundi rika, kwa sababu wako salama kwa jinsi tu walivyo, na hawahitaji kujithibitisha wenyewe kwa watu wengine.

Msichana ambaye huchezea hisia za wavulana anaweza kuwa anafanya hivyo kwa sababu anaogopa kuwa, kama hatafanya hivyo, hawatampenda wala kumtilia maanani.

Msichana ambaye anaona aibu kwa wavulana anaweza kuogopa kwamba hawatampenda ikiwa ataonyesha tabia yake halisi. Binti ambao wanapokea uthibitisho na upendo kutoka

kwa baba zao wana uwezo wa kuchangamana vizuri na vijana kwa njia zilizo nzuri na usahihi bila ya kuwachokoza au kuona aibu. Wanakuwa salama kwenye utambulisho wao kwa sababu ya upendo wa baba zao.

Upendo wa kweli wa wazazi usiokuwa na masharti unaodhihirishwa mara kwa mara katika lugha zote tano za upendo huwalinda watoto dhidi ya madhara mengi. Watoto wanaopendwa vizuri hawatafuti upendo na usalama kutoka kwa watu wengine ambao wana dhamira ya kuwadhuru.

Kwa muhtasari, kuna faida nyingi za kuwa na tanki lililojaa mafuta ya hisia kama mtoto:

- Uelewa sahihi wa thamani ya mtu na chanzo chake.
- Uelewa sahihi wa juhudi, makosa, ukuaji, na upendo usiokuwa na masharti.
- Uwezo wa kujifunza jinsi ya kuwapenda watu wengine vizuri.
- Nguvu na uimara wa kukabiliana na changamoto na kujiendeleza ipasavyo.
- Usalama Kihisia.
- Uwezo wa kukubaliana na nidhamu, masahihisho, na mwongozo.
- Uwezo wa kukataa vishawishi vibaya kutoka kwa makundi rika.
- Hawako katika hatari ya kudhalilishwa kwenye mahusiano ya baadaye.

► Je, ni njia gani nyingine umeona ambazo watoto hufaidika kutokana na kupendwa inavyopaswa?

### **Hasara za Tanki Tupu la Kihisia.**

Watoto wanaohisi kwamba hawapendwi wanaweza wakapingana na miongozo inayotolewa kwao kwa sababu wanakosa hamasa ya kuwafurahisha mama au baba. Bila kuwa na tanki lililojaa mafuta ya hisia, watoto wengi hukosa uhusiano wenye nguvu na wa kimaadili wa uaminifu kwa wazazi ambao wanajaribu kuwaongoza.

Watoto ambao matanki yao ya mafuta ya hisia yako matupu wako katika hali ya hatari zaidi kuliko watoto walio katika mahusiano ya upendo wenye nguvu kubwa na wanafamilia wao. Kwa kuwa hawajisikii kwamba wanapendwa, wanaweza kutafuta kupendwa na watu ambao wanapenda kuwatumia na au kuwaletea madhara.

### **Sifa za Familia zilizo Imara**

Katika mafundisho haya tumejifunza kuhusu aina tano za lugha za msingi za upendo. Ijapokuwa watu huwa na lugha moja au mbili za msingi za upendo, kila mtu anahitaji kupendwa mara kwa mara katika aina zote tano. Familia iliyo imara ni ile ambayo kila mtu kwa makusudi au malengo hukuza mahusiano na watu wengine kwa kila siku kuzungumza maneno yenye kudhihirisha upendo, kutumia muda ulio bora kwa pamoja, matendo ya huduma, na kutumia mguso wa upendo wa kimwili. K utoa zawadi kwa mtu mwingine inaweza isiwe tukio la kila siku lakini bado ni sehemu nyeti ya mahusiano yaliyo imara ndani ya familia.

► Je, ni kwa jinsi gani upendo hudhihirishwa mara kwa mara kwenye familia yako? Je, upendo hudhihirishwa katika aina zote tano za lugha za msingi za upendo? Je, udhihirishwaji wa upendo unashirikishwaje mara kwa mara?

Uchunguzi wa miaka 25 usiokuwa wa kidini kutoka katika familia 14,000 unaonyesha kwamba familia nyingi zilizo imara, zilizofanikiwa na zilizo na malezi yaliyokamilika kutoka katika malezi ya tamaduni mbalimbali zinashirikisha sifa kuu sita zinazofanana.<sup>36</sup> Baadhi ya sifa hizo zina uhusiano wa moja kwa moja na lugha mbalimbali za upendo, jambo linaloonekana kwamba kuna msisitizo wa udhihirisho wa aina mbalimbali kuhusiana na upendo. Stinnett na Beam waliorodhesha hizo sifa sita na kuzitolea maelezo kwa kila moja:

1. **Kujitolea.** Wanafamilia katika familia zilizo imara na zenye nguvu wanakuwa wamedhamiria kukuza ustawi na furaha ya kila mmoja. Wanathamini umoja wa familia.
2. **Kuthamini na kupendwa.** Wanafamilia katika familia zilizo imara na zenye nguvu huonyesha kuthaminika kwa kila mtu mara kwa mara. Wanaweza wakajisikia kwamba familia zao ni nzuri.
3. **Mawasiliano chanya.** Wanafamilia katika familia zilizo imara na zenye nguvu wana ustadi mzuri wa kuwasiliana na hutumia muda wao mwingi sana kuzungumza na kila mmoja.
4. **Muda wa kukaa pamoja.** Wanafamilia katika familia zilizo imara na zenye nguvu hutumia muda ulio bora kwenye mambo mengi ya ukarimu – na kila mmoja.
5. **Ustawi wa kiroho.** Aidha wawe wanakwenda kwenye ibada za kidini au hawaendi, wanafamilia katika familia zilizo imara na zenye nguvu wana hisia zilizo kubwa za mambo mazuri au yenye nguvu katika maisha.
6. **Uwezo wa kukabiliana na msongo wa mambo au migogoro.** Wanafamilia katika familia zilizo imara na zenye nguvu wana uwezo wa kuona msongo wa mambo na au migogoro kama fursa za kukua.

## Matumizi Binafsi

Tumezingatia mambo mengi katika mafundisho au masomo haya mawili. Tulianza na majadiliano kuhusu upendo wa kweli, kisha tukazitambua aina tano za lugha ambazo kwa kawaida hutumika kuwasilisha upendo. Tumejifunza kuhusu matanki ya mafuta ya hisia na hitaji la wanafamilia kuwa na uzoefu wa upendo kwa ajili yao katika lugha yao ya msingi ya upendo. Tulizungumzia kuhusu tofauti za tabia ndani ya familia zinavyoweza kutufanya tukue katika upendo.

---

<sup>36</sup> Dr. Nick & Nancy Stinnett and Joe & Alice Beam, *Fantastic Families: 6 Proven Steps to Building a Strong Family*, (Brentwood, TN: Howard Books, 2008)

Baada ya hayo, tulifanya upembuzi yakinifu kwa kila moja ya aina tano za lugha za upendo kwa kina, tukiangalia kila moja kwa mfano, na uharibifu unaosababishwa inapotokea kila moja kupuuzwa au kunyanyasika. Tumejifunza ni kwa jinsi gani watoto wanavyofaidika kwa kuwa na matanki yaliyojaa hisia, na jinsi wanavyoteseka wakati matanki yao yanapokuwa yamepungua sana. Tumezungumzia kwa marefu na mapana kuhusu kudhihirisha upendo wetu kwa watoto wetu. Kisha, tukaona jinsi kufanyia kazi aina tano za lugha za upendo zinavyounganika na sifa kuu sita za kawaida za familia zilizo imara na zenye nguvu.

Tunapofikia tamati ya masomo haya, tutajadili wajibu wako binafsi –ni nini utakachoweza kufanya na unachopaswa kufanya na kile ambacho ulijifunza katika masomo haya.

### **(1) Unawajibika kuipenda familia yako.**

Unapaswa uwe tayari kubadilika kwa namna yeyote ile inayohitajika bila ya kusubiri wanafamilia wako wakupende wewe. Upendo wa kweli kabisa haungojei hadi mtu mwingine aonyeshe upendo kwako. Unajidhihirisha wenyewe hata wakati ambapo mtu mwingine anaonekana hastahili kabisa, kwa sababu upendo hautegemei uthamani wa mtu anayeupokea.

### **(2) Unawajibika kujitahidi kwa hali yako kudhihirisha upendo wako kwa ajili ya familia katika njia ambazo ni muhimu zaidi kwao.**

Kuna uwezekano mkubwa kwamba itakupasa uweke juhudi za ziada katika kudhihirisha upendo katika aina moja au zaidi ya lugha ambazo haziji kwako katika njia ya kawaida au ya asili. Mwanzoni, baadhi ya udhihirisho wa upendo unaweza kuhisi kwamba siyo wa kawaida au asili, ni wenye kufedhehesha au ni wa kipumbavu kwako.

Jifunze kutambua fursa zinazoonyesha upendo kwa wanafamilia wako. Kuwa makini na kile ambacho wanafamilia wanaweza wakahitaji katika wakati maalumu. Hapa kuna mfano wa kila moja ya aina za lugha za upendo:

- **Maneno ya Uthibitisho:** Fikiria, “\_\_\_\_\_ pengine anahisi kutokuwa na uhakika kuhusu kile alichosema hivi punde. Lakini alikuwa sahihi katika kile alichosema. Nahitaji kusema jambo la kuthibitisha.”
- **Muda ulio Bora:** Uliza, “Je, ungependa kuzungumzia juu ya jambo hilo?” Kisha acha kile unachofanya, na wape umakini wako wote, na onyesha kwa njia ya lugha ya mwili kwamba kwa uhakika unawasikiliza.
- **Zawadi:** Wakati unapokuwa unakabidhi zawadi sema kwamba, “Nilikiona hiki na kikanifanya nikukumbuke.”
- **Matendo ya Huduma:** Jaribu kuruka juu na uulize, “Je, ninaweza kukupatia hiyo?” au Je, ninaweza kukusaidia kwa hilo?”
- **Mguso wa Kimwili:** Nenda kwa mtu huyo na umwambie, “unaonekana kama unahitaji kukumbatiwa” – huku ukimzungushia mikono yako kumkumbatia.

### **(3) Unawajibika kwa Hisia zako mwenyewe.**

Mungu alikuumba ili uwe na mahusiano yaliyo imara na yenye afya na watu wengine. Lakini hilo liwe linawezekana au haliwezekani, Mungu mwenyewe ndiye chanzo chako kikuu pamoja na utoshelevu. Familia yako haiwajibiki peke yake kwa ustawi wa mihemuko yako. Mungu anakupenda kikamilifu, ingawaje kamwe hakuna mwingine anayeweza kufanya hivyo. Anaweza akafidia upungufu wowote utakaoweza kuwa nao, unapokuwa umeshikamana naye katika upendo wake (Yohana 15:9-11).

Familia yako inaweza isidhihirisha upendo kwako katika lugha yako ya msingi ya upendo. Inawezekana labda hawana ufahamu na lugha yako ya msingi ya upendo na mahitaji ya mihemuko yako. Huenda wanakosa motisha au ushawishi wa kudhihirisha upendo kwako kwa njia ambayo ni ya muhimu zaidi kwako. Unaweza kuwa na uwezo wa kuwaeleza ni kwa jinsi gani unajihisi kupendwa zaidi. Lakini huwezi kuwafanya wachague kudhihirisha upendo wao kwako kwa njia hiyo.

Huenda familia yako inadhihirisha upendo wao kwako kwa njia nyinginezo. Utakapokuwa una ufahamu wa lugha za upendo, utanza kutambua njia ambazo familia yako tayari inazo kwa ajili ya kuonyesha upendo wao kwako. Kwa kuwa huna uwezo wa kuweza kuwabadilisha, unaweza ukachagua kukubali udhihirisho wao wa upendo na wewe ukaonyesha kuridhika nazo kwa ajili ya upendo huo.

#### **Maombi**

Baba wa Mbinguni,

Asante kwa kunipa mimi familia. Nisaidie katika kumthamini kila mmoja wao kama ninavyokusudia, na kustawisha uhusiano mzuri na kila mmoja na kwa mwenzake.

Asante kwa fursa niliyo nayo ya kufikiria njia ambazo ninaweza kuonyesha upendo wangu kwa familia yangu. Nifundishe jinsi ya kumfanania Yesu: kuutoa muda wangu, nguvu za kimhemuko na za kimwili, na rasilimali za kuwabariki na kuwatia moyo familia yangu. Nisaidie niwe na moyo wa unyenyekevu, ili kwamba niweze kutoa kipaumbele kwa mahitaji ya watu wengine kuliko ya kwangu. Nisaidie niwe na ufahamu wa fursa nilizo nazo za kudhihirisha upendo wangu kwa kila mwanafamilia wangu.

Baba, umenionyesha mimi kwamba upendo wa kweli ni upi. Unanitegemea mimi kufanya kitu kinachofanania huo upendo kwa familia uliyoitengeneza kwa ajili nyangu. Ninachagua kumpenda mwenzi na watoto wangu kwa upendo wa kujitoa kabisa na usiokuwa na masharti. Naomba unijalie neema na rehema kwa ajili ya njia nyingi ambazo nilishashindwa. Niwezeshe kuwapenda wote kwa kadri ninavyopaswa kufanya.

Ameni

## **Kazi za Kufanya**

(1) Fikiria kuhusu lugha za msingi za upendo za mwenzi wako na za kila mtoto wako. Orodhesha majina ya wanafamilia wako wote. Kisha orodhesha lugha moja au mbili za msingi za upendo kwa kila mwanafamilia.

(2) Je, ni udhihirisho gani wa upendo unaohitaji jitihada za ziada kwa sehemu yako? Ziwekee alama zote. Andika mawazo machache kuhusu ni kwa jinsi gani kwa kumaanisha unavyoweza kudhihirisha upendo wako kwa ajili ya familia yako kwa kutumia njia hizi.

(3) Chunguza utamaduni wako, haswa kikundi chako cha kijamii. Orodhesha lugha tano za upendo. Je, Katika utamaduni wako, kila moja ya lugha ya upendo inadhihirishwaje? Je, kuna yoyote kati ya hayo matano ambayo huwa hayazingatiwi? Je, ni baadhi ya njia zipi mahususi ambazo watu katika kikundi chako cha kijamii wanaweza kuonyesha upendo kwa njia bora kuliko ilivyo kawaida katika utamaduni wako? Andika aya kadhaa ukijibu maswali haya.





# Somo la 10

## Suala la Kutokuwa na Mtoto

### Malengo ya Somo

Hadi kufikia mwishoni mwa somo hili, mwanafunzi atapaswa:

- (1) Kuelewa na kujibu utasa kutoka kwa mtazamo wa kibiblia.
- (2) Kumthamini kila mtu kama aliyechuka sura ya Mungu.

### Huzuni ya Busaba

Busaba alikuwa ni msichana aliyezaliwa katika nchi moja ya Asia. Alifurahi alipoolewa na mfanyabiashara kijana, na walitegemea kuwa na maisha ya furaha wakiwa pamoja. Miaka kadhaa ilipita, na Busaba alikuwa bado hajibahatika kupata watoto. Daktari aliwaambia kwamba Busaba hangekuwa na uwezo wa kupata watoto. Mume wake alijawa na masikitiko mengi na hasira kali. Mwisho wa mambo yote aliamua kumpa Busaba talaka na akamwoa mwanamke mwingine. Busaba sasa ni mzee. Anaishi kwenye nyumba ndogo yeye mwenyewe na hana jamii inayoshughulika naye katika maisha yake. Kwa kuwa yeye ni wa dini ya Bhudha, ana mategemeo kwamba siku moja katika maisha ya baadaye atakuwa na watoto na aibu yake itakuwa imekoma na au imefikia mwisho.

► Je, kama wewe ungelikuwa ni mchungaji kwenye jamii ya Busaba, ungelisema nini na yeye? Je, ujumbe wa Kristo kwa Busaba ni nini?

Kwenye somo hili au mafundisho haya tunaenda kuangalia mtazamo wa kibiblia kuhusiana na suala la kukosa mtoto.

### Watoto na Programu ya Mungu ya Baraka.

Mara tu baada ya Mungu kumuumba mwanamume na mwanamke wa kwanza, aliwaambia kwamba wazae watoto, waongezeke, na wakaijaze nchi (Mwanzo 1:28).

Kwenye Agano la Kale, wakati mwingine Mungu alitoa ahadi za baraka siyo tu kwa mtu binafsi bali kwa vizazi vingi vya familia. Kwa mfano, Mungu aliahidi baraka kwa Ibrahimu ambazo hazikuja tu kwa Abrahamu mwenyewe bali pia kwa vizazi vyake vya baadaye. Mungu alikuwa amemuahidi Abrahamu kwamba wazao wake wangukuwa wengi kama mchanga wa bahari. Mimba ya mtoto wa Ibrahimu aitwaye Isaka ilipatikana kimiujiza. Kisha kwa kadri familia ilivyokuwa inaongezeka kwenye kila kizazi, idadi ikaongezeka ikiwa ni udhihirisho kwamba Mungu alikuwa anatimiza ahadi yake.

Katika Kutoka 23:25-27 Mungu aliwaambia Waisraeli kwamba atawabariki watakapokuwa wanaingia katika nchi yao mpya. Mungu aliwaahidi Waisraeli kwamba atabariki vyakula vyao, atawaondolea magonjwa, hataruhusu utasa au kuharibika kwa mimba, na kuwaharibu maadui zao. Ahadi hizi zilitegemea utiifu wa Waisraeli, na Mungu akafafanua mahitaji yake

kwao (kama vile amri iliyoko katika Kutoka 23:32). Ahadi hizo zilikuwa zimetolewa kwa ajili ya taifa zima la Israeli na siyo kwa ajili ya watu binafsi. Watu binafsi wangehusishwa na kutii au kutotii kwa taifa. Kwa mfano, mtu anaweza kuwa mgonjwa, au mwanamke akawa hana watoto, siyo kwa sababu ya dhambi zao wenyewe, bali ni kwa sababu walikuwa kwenye taifa ambalo halikuwa mwaminifu kwa Mungu. Kwa hiyo, mwanamke ambaye hakuwa na mtoto huenda asiwe anateseka kutokana na matokeo ya dhambi zake mwenyewe.

Kumbukumbu la Torati 7:12-15 ni kifungu chenye ahadi kwa taifa la Israeli. Kutakuwepo na mafanikio, hakuna magonjwa, na hakuna utasa kwa wanadamu au wanyama. Aya ya 12 inasema kwamba Waisraeli watapokea baraka hizi kama watamtii Mungu kwa sababu Mungu alifanya maagano na babu zao. Mtu aliyeko Israeli anaweza kuwa maskini, au mwanamke anaweza kukosa mtoto, kama taifa halikuwa na uaminifu kwa Mungu.

Watoto walikuwa muhimu katika mpango wa Mungu kwa ajili ya watu wake. Katika sehemu nyingine za kozi hii, tulizungumza kuhusu jinsi ambavyo watoto wanapaswa kuthaminiwa kwa sababu wameumbwa katika sura ya Mungu. Kila mtoto ni wa thamani na anapaswa kutendewa kwa upendo na kutunzwa. Hata hivyo, wakati mwingine watu huhisia kwamba mtoto ni wa thamani kwa sababu anaweza kuifanya familia ikawa imara katika siku za baadaye. Wakati mwingine baba huwathamini watoto kwa sababu ni sehemu ya mwendelezo wa utambulisho wake yeye mwenyewe. Tunapaswa tukumbuke kwamba Mungu hutupatia watoto kwa ajili ya malengo yake mwenyewe (Malaki 2:15).

► Kikundi kitapaswa kiangalie katika Zaburi 127:3-5 kwa pamoja na mtu akiwa anasoma kwa sauti.

Kifungu hiki katika Biblia kinasema kwamba watoto ni baraka kutoka kwa Mungu. Ni kama urithi ambao Mungu ameubariki. Ni zawadi kutoka kwa Mungu. Ni walinzi na usalama wa familia zijazo.

Baraka za aina mbili ambazo wakati mwingine huzungumziwa kwa pamoja katika Maandiko ni maisha marefu na uzao wa wajukuu. Ayubu alibarikiwa kwa sababu alikuwa na watoto kumi na aliishi maisha marefu ya kutosha kiasi ambacho aliona vizazi vyake vinne (Ayubu 42:13, 16). Baraka zilizoko katika Zaburi 128:6 ni zawadi ya kuishi ili kuweza kuona wajukuu zako.

Mungu alibariki familia ya Yonadabu kwa ahadi kwamba daima kutakuwepo na mtu wa kuongoza kizazi kitakachofuata cha familia (Yeremia 35:19). Mungu alitoa ahadi kwa familia ya Mfalme Daudi kwamba siku zote atakuwa na mtu atakayekaa kwenye kiti cha enzi cha ufalme (2 Samuel 7:16).

Kwa hiyo tunaona kwamba baraka za Mungu kwa ajili ya familia kwa kawaida huhusisha watoto, na ni njia ambayo baraka za Mungu zinaendelezwa hadi kwenye vizazi vya baadaye.

## **Ufahamu wa Kibiblia kuhusu Ugumba/Kukosa Mtoto**

Ugumba/kukosa mtoto katika visa vingine inamaanisha kwamba Mungu ameilaani familia. Biblia inatueleza kuhusu matukio ambayo Mungu alizilaani familia kwa ugumba. Kwa mfano, kwa kuwa mfalme Abimeleki alitenda makosa, Mungu alizuia wanawake wote wa nyumba yake wasipate watoto hadi aliporekebisha makosa yake (Mwanzo 20:18). Wanawake katika jambo hili hawakuwa na hatia, lakini walipata matokeo ya dhambi ya mfalme.

Baada ya Adamu na Hawa kutenda dhambi, Mungu alisema kwamba dunia ingeathiriwa kutokana na dhambi yao. Laana iliyotolewa ilihusisha pamoja na mambo mengine, mahusiano magumu ya kibinadamu, kuzidishiwa uchungu na utungu wa kuzaa watoto, kazi ngumu, upinzani wa ardhi katika kilimo, na mwishowe kifo (Mwanzo 3:14-19). Kila mwanadamu kuanzia wakati wa Adamu amekuwa katika hali ya dhambi kuanzia siku anapozaliwa, hata kabla hajatenda dhambi kwa binafsi yake yeye mwenyewe. Hata Yesu, ambaye hakuwahi kuwa na dhambi kabisa, aliingia katika uumbaji wa dunia akiwa katika mwili wa mwanadamu uliokuwa katika hali ya laana. Kwa hiyo, hatupaswi kusema kwamba mateso ya mtu binafsi ni matokeo ya dhambi yake mwenyewe. Watu wote tunazeeka, tunapatwa na magonjwa, tunakutana na mateso kwa njia mbalimbali, na hatimaye tunakufa. Matatizo haya yote, ikiwa ni pamoja na matatizo ya kutokupata watoto/ugumba, ni matokeo ya dhambi ya kwanza ya Adamu.

Mbali na dhambi ya asili ya Adamu, tunaathiriwa na dhambi za wazee wetu, kwa sababu matendo yao yalitengeneza jamii ambayo ndiko tulimozaliwa. Tumeathiriwa na dhambi za familia zetu, jamii, na taifa. Waumini kila mahali duniani wamekumbana na hali ambazo zimetengenezwa na jamii wasiyoidhibiti. Familia inaweza ikajikuta katika hali ya umaskini kwa sababu wako kwenye sehemu ambayo ina uhuru kidogo na fursa. Mtoto mchanga anaweza akazaliwa akiwa na ulemavu wa mwili ingawaje hajawahi kufanya uchaguzi wowote wa kutenda dhambi (Yohana 9:1-3).

Mungu hafanyi maamuzi kuhusu kutupa watoto kwa ajili ya sababu ambazo tunaweza kuwa na ufahamu nazo. Wakati mwingine watu wanaoishi maisha ya uzembe, ya uasi wa dhambi wanakuwa na watoto wengi na hawana mpango wa kuwalea katika njia ambazo zinampa Mungu utukufu (Zaburi 17:14). Wakati mwingine waumini walio waaminifu kabisa hawajawahi kupata watoto. Kwa hakika, hatupaswi kudhania kwamba dhambi fulani ya mtu ndiyo iliyosababisha ugumba au kutopata mtoto.

Tunajua kwamba Mungu anao uwezo wa kuingilia kati kwa uponyaji na baraka zake wakati wowote anaochagua, lakini kwa ujumla, waumini huvumilia hali zote za ulimwengu. Tunasubiri kwa imani wakati ambapo Mungu atafanya upya tena uumbaji wake (Warumi 8:18-23).

Siyo haki kumlaumu mwanamke kwa kutokuwa na mtoto, kana kwamba dhambi yake mwenyewe ndiyo iliyomsababishia laana. Vivyo hivyo, mtoto mtarajiwa anapokufa kabla hajazaliwa, kifo hicho kwa kawaida siyo kwa sababu ya jambo lolote ambalo mama yake atakuwa amelitenda. Watu binafsi wanapitia mateso kwa njia mbalimbali kutokana na

dhambi ya Adamu, dhambi za watu wengine, na hali ya ujumla ya dunia ilivyo. Kwa kuwa kila mmoja ametenda dhambi, ubinadamu unashirikishana kwa pamoja hatia kwa ajili ya hali ya ulimwengu, lakini watu binafsi wanapitia mateso kwa njia mbalimbali mahususi.

## **Miujiza ya Mungu**

Yesu alidhihirisha upendo wa Mungu wakati alipoponya na kutenda miujiza mingine mingi. Katika historia yote iliyoandikwa katika Biblia, tunaona miujiza mingi ya Mungu iliyofanyika kwa ajili ya watu wake.

Mungu anataka sisi tuishi kwa furaha na bila mateso katika dunia hii ya uzuri (Mwanzo 1:28, 31, 1 Timotheo 6:17). Hata hivyo, kipaumbele cha kwanza kabisa cha Mungu ni kutuokoa katika dhambi ili tuweze kufurahia uhusiano wa milele pamoja naye. Wokovu kwa ajili ya wenye dhambi huchukua muda kwa sababu watu ni lazima wachukue maamuzi ya kutubu na kuamini. Kama Mungu angeamua kumaliza maumivu na mateso yote kwa sasa, ni watu wachache sana watakaotubu, kwa sababu watakuwa hawajui ubaya wa dhambi. Kwa hiyo, kwa sasa hivi, mateso ni lazima yaendeleo wakati Injili ikiwa inahubiriwa kila mahali duniani. Hatuwezi tukategemea miujiza iwe ndiyo utatuzi wa matatizo yetu yote na iondoe maumivu yetu yote, ingawaje mara chache hufanya miujiza kwa ajili yetu.

Mwishowe, mateso yote yataisha kwa wale wote ambao watakuja kwenye uhusiano binafsi na Mungu. Lakini kwa wakati huu, Mungu anahuzunika pamoja nasi katika mateso yetu (Yohana 11:35), na hutufariji kwa njia nyingi (2 Wakorintho 1:3-7).

Mojawapo ya miujiza ya Mungu ni kumfanya mwanamke asiyekuwa na mtoto aweze kuwa mama mwenye watoto (Zaburi 113:9).

Biblia ina kumbukumbu zilizoandikwa sizizopungua sita ambazo Mungu amempa mtoto mwanamke ambaye hakuwahi kuwa na mtoto hapo kabla. Ingawaje Mungu amefanya miujiza hii mara nyingi, hizi za mara sita zilinukuliwa kwa sababu watoto walikuwa ni muhimu kwa ajili ya historia: Isaka alizaliwa na Sara (Mwanzo 21:1-3). Yakobo na Esau walizaliwa na Rebeka (Mwanzo 25:21, 25-26). Yusufu alizaliwa na Raheli (Mwanzo 30:22-24). Samsoni alizaliwa na mke wa Manoa (Waamuzi 13:2-3, 24). Samweli alizaliwa na Hanna (1 Samweli 1:20). Yohana alizaliwa na Elizabethi (Luka 1:13, 57).

Katika kila moja ya matukio haya sita, wanandoa walikuwa wamepitia katika kipindi cha huzuni kwa sababu mke alikuwa hajajaliwa kupata mtoto. Kwenye kumbukumbu za Biblia, Mungu hakuwahi kumlaumu hata mmoja wao kwa ajili ya mwanamke kukosa mtoto. Biblia haionyeshi mahali popote kwamba Mungu hakuwa amependezwa na mmojawapo wa mzazi yeyote kati ya hawa sita. Luka 1:5-7 anasema kwamba Zakaria na Elizabethi walikuwa watu wenye haki mbele za Mungu, wakitii kwa ukamilifu wote amri na maagizo yake, lakini bado walikuwa hawana mtoto hadi kwenye uzee wao. Hakuna kumbukumbu yeyote katika hesabu ya hawa wazazi kwamba waliwahi kutubu au kukiri makosa yao walipokuwa wakiomba miujiza kwa ajili yao. Ujumbe wa Mungu kwa wazazi hawa hautaji sababu yeyote

kwamba hawakuwahi kuwa na watoto tayari. Matukio haya yanaonyesha ukweli kwamba watu hawapaswi kulaumiwa binafsi kwa ajili ya kutopata au kukosa watoto.

Inafaa sana kwa ajili yetu tuombe kwamba Mungu atatupa baraka za watoto, lakini mwishowe, ni lazima tukubaliane na uamuzi wa Mungu. Hatupaswi kudhania kwamba ni mapenzi ya Mungu atoe mtoto kwa kila hali, kama vile pia ambavyo Mungu hafanyi uponyaji kwenye kila hali ya ugonjwa au kuchukua kila aina ya mateso.

Mtume Paulo aliomba mara tatu kuhusu kitu ambacho alisema ni kama mwiba katika nyama za mwili wake (2 Wakorintho 12:8-10). Hatujui ni tatizo gani mahususi alilokuwa nalo, lakini inavyoonekana ilikuwa ni tatizo la kimwili. Ilikuwa ni kitu ambacho alimtegemea Mungu kwamba kingebadilika, kwa hiyo aliomba kwa ajili ya muujiza wake. Mungu alimjibu kwamba badala ya kumwondolea huo mwiba wake, atampa neema ambayo ingekuwa kubwa kuliko udhaifu aliokuwa nao. Paulo alisema kwamba udhaifu huu mahususi ungemletea Mungu utukufu kwa sababu ulimsaidia yeye kuonyesha nguvu ya Mungu. Paulo aliendelea kusema kwamba anapendezwa na madhaifu na mateso kwa sababu vinaleta hali ambayo itamletea Mungu utukufu.

Mtume Paulo alikuwa mtu wa imani kubwa, lakini siyo kila wakati alikuwa anapata miujiza aliyokuwa anahitaji. Alikubaliana na mapenzi ya Mungu. Ingawaje tunataka tupate muujiza wa baraka kutoka kwa Mungu, ni lazima tukubaliane na maamuzi ya Mungu. Wakati mwingine Mungu hujipatia utukufu zaidi katika njia ile anayoitumia kufanyia kazi kupitia madhaifu yetu.

► Toa mfano wa muda ambao Mungu alionyesha kukuhudumia katika maisha yako bila ya kukufanyia muujiza uliokuwa ukiutegemea.

### **Mwitikio wa Kitamaduni kuhusu Ugumba/Kukosa Mtoto.**

Tamaduni zote hazifanani kwa jinsi wanavyowathamini watoto. Katika baadhi ya nchi, familia zinataka ziwe na watoto wengi. Watoto wanaweza wakasaidia katika kazi ambazo zinategemeza familia. Jamii inayounganishwa katika familia – binamu, wajomba, na wengineo huwalinda na kuitunza jamii wakati inapohitajika. Kila mke kwenye jamii inayounganishwa kifamilia hutaka kuiongeza familia kwa kuwa na watoto. Mume mwenye watoto wengi, hasa wa kiume, ni muhimu kwenye jamii inayounganishwa kifamilia. Familia hiyo inategemea kutunza wanafamilia wazee walioko.

Katika nchi nyingine, familia nyingi zinaishi kwenye majiji na miji na zinawezeshwa kimaisha na ajira ya baba na mama. Katika majiji, watoto hawana uwezo wa kuiwezesha familia kimaisha. Kuwawezesha na kuwapa elimu watoto kunaweza kuwa ni kwa gharama sana. Baada ya muda mrefu, jinsi familia zitakavyokuwa zinaendelea kuishi kwenye jiji kwa vizazi kadhaa, wanaweza wakawa wanataka kuwa na idadi ndogo sana ya watoto. Familia nyingi zinazoishi kwenye maeneo ya mijini zinataka mtoto mmoja au wawili tu.

Thamani ya watoto ni nzito sana katika tamaduni nyingi kiasi kwamba kila wanandoa ni lazima wawe na watoto ili wajisikie kwamba wanaheshimika na kuthaminika. Mwanamke

ambaye hajajaliwa kuwa na mtoto hujisikia kwamba ni mwenye kushindwa katika jukumu lake muhimu la kuzaa. Mwanamke ambaye kamwe hajaolewa hujisikia mwenye aibu kwa sababu ya kutokuwa na watoto na kwamba alikuwa hajachaguliwa kuwa mke wa mtu.

Katika tamaduni nyingi familia huwa zinataka kuwa na watoto wengi wa kiume kwa ajili ya kuongoza na kuimarisha familia kwa vizazi vingine vinavyofuata. Wasichana wanathaminiwa kwa kiwango kidogo sana. Watoto wachanga wa kike wanaojulikana kabla ya kuzaliwa aidha huweza mimba kutolewa au wakatupwa wakishazaliwa. Baadhi ya nchi zimepiga marufuku kujua kabla ni jinsia gani ya mtoto ambaye hajazaliwa kabla ya wakati wake, kwa sababu familia nyingi sana huuwa vichanga vya kike ambavyo bado havijazaliwa. Tunajua kutokana na maandiko kwamba wasichana wana heshima na thamani sawa na ile waliyo nayo vijana wa kiume kwa sababu wote wameumbwa katika sura ya Mungu (Mwanzo 1:27). Kwa hiyo familia zinazomfuata Kristo zinapaswa kuwathamini kwa usawa unaolingana vijana wa kike na wa kiume haijalishi kuna jambo gani la kawaida katika tamaduni.

Ikiwa familia ina uhitaji mkubwa wa kujivunia mtoto, wanaweza wakamkataa mtoto mlemavu kimwili au kiakili. Kwenye baadhi ya nchi, watoto wengi walio na ulemavu wako kwenye vituo vya kulelea watoto yatima kwa sababu wazazi wao hawakuwataka. Utendaji huu kwa watoto ni mbaya, kwa sababu wameumbwa kwa mfano wa Mungu na ni wa thamani mbele zake, bila kujali uwezo wao au mipaka yao.

Katika baadhi ya tamaduni, desturi ya ndoa zaidi ya mke mmoja inategemea na thamani ya watoto. Mwanamume atataka kuwa na watoto wengi kwa kuwa na wanawake kadhaa. Biblia inatuambia sisi kwamba mpango wa Mungu ni mwanamume mmoja awe na mke mmoja (Mwanzo 2:22-24, 1 Timotheo 3:2).

Agano la Kale lina kumbukumbu ya nyakati kadhaa ambazo mwanamke anampa mumewe mjakazi wake ili aweze kujipatia watoto naye. Mke alipata hadhi yake kutoka kwa watoto wa mjakazi. Raheli na Leya, wake zake Yakobo, kila mmoja alimtoa mjakazi wake akampa Yakobo ili wajipatie hadhi kupitia kuwa na watoto wengi.

Matumizi ya wajakazi kwa ajili ya kuongeza watoto kulisababisha kuwepo na mahusiano yaliyokuwa na utatanishi mkubwa. Sarai alimkabidhi Hajiri kwa Abrahamu, akitarajia kwamba hadhi yake mwenyewe ingekuwa bora zaidi kama Hajiri angempatia mtoto (Mwanzo 16:2-6). Hajiri akabeba mimba na akajisikia sana kuwa yuko juu ya Sarai. Sarai alimwadhibu vikali Hajiri kwa kujaribu kujiona kwamba yuko juu zaidi yake na kuanza kujitengenezea mamlaka yake mwenyewe.

Lelia alikuwa amezaliwa katika nchi moja ya Afrika Magharibi. Baada ya kuwa ameolewa kwa miaka mitatu akawa hakujaliwa kupata mtoto. Kwa mujibu wa utamaduni wa Lelia, kuasili mtoto hakuondoi aibu ya mwanamke ya kutokuwa na mtoto wake mwenyewe. Lelia alimpata mwanamke fulani kutoka katika familia maskini kijijini ambaye alikuwa mjamzito na akapanga amnunue mtoto wake. Lelia alivaa kitu fulani ndani ya shati lake ili aonekane mjamzito kwa miezi kadhaa. Ilipofikia wakati wa mtoto kuzaliwa, Leila alijifanya kwenda

hospitalini kwa ajili ya kujifungua, kisha akarejea tena nyumbani akiwa na mtoto wake aliyetoka naye kijijini.

Kama familia kimsingi inataka watoto kwa ajili ya faida yao kwa familia, wanaweza kushindwa kumthamini mtoto kama aliyeumbwa katika sura yake Mungu. Wanaweza wakakataa kuwapenda na kuwapokea watoto walemavu. Wanaweza wakamkataa mtoto wa kike kwa sababu walikuwa wanataka mtoto wa kiume. Wanaweza kumfanya mwanamke ambaye hajajaliwa kupata mtoto ajione ni wa aibu na asiyekuwa na thamani. Hawaoni thamani ya kuasili watoto yatima au watoto wasiokuwa na maskani. Tabia zote hizi na matendo haya yote ni ya kibinafsi na ni makosa. Tunamdhalilisha Muumbaji wetu tunapokuwa tunawatendea ubaya watu binafsi kwa sababu yeyote ile iliyoko hapa (Kutoka 4:11, Mithali 14:31).

Henry VIII alikuwa ni mfalme wa Uingereza kuanzia mwaka 1509-1547. Alikuwa ametarajia sana kuwa na mtoto wa kiume. Kwa kuwa mke alikuwa na binti lakini hakuwa na mtoto wa kiume aliye hai, Henry alimtalaki mkewe na kuoia mke mwingine. Mke wake wa pili aliposhindwa pia kumpatia mtoto wa kiume, alimshutumu na kumshitaki kwa makosa ya uhaini, na akaamrisha anyongwe.

Sayansi ya tiba imethibitisha kwamba manii ya kiume ndiyo huamua jinsia ya mtoto. Mwili wa mwanamke haufanyi maamuzi kama aidha atapata mtoto wa kiume au wa kike. Hata hivyo, wanaume wengi wamekuwa na hasira dhidi ya wake zao kwa sababu ya kuwa na watoto wa kike na siyo wa kiume.

Mwanamume mmoja aliyeitwa Yusufu na mke wake walikuwa na watoto wawili wa kike. Wakati mke wake Yusufu alipokwenda hospitali kwa ajili ya kujifungua mtoto wake wa tatu, Yusufu alitarajia kupata mtoto wa kiume. Mtoto wa tatu aliyezaliwa pia naye alikuwa wa kike. Yusufu alipandisha hasira sana kiasi kwamba alikataa hata kwenda hospitalini kumtembelea mke wake na kulipa gharama za matibabu.

Katika Ayubu 24, Ayubu ametoa maelezo marefu kuhusu matendo ya mtu mwovu. Tendo moja lililotajwa ni kwamba mwanamume mbaya humtendea ubaya mwanamke asiyekuwa na mtoto (Ayubu 24:21). Mungu hapendezwi pale mwanamke asiyekuwa na mtoto akitendewa mambo yasiyofaa na yasiyokuwa na upendo.

► Je, ni kwa jinsi gani utamaduni wa kwenu unawathamini watoto? Je, ni sababu zipi zinazofanya watu watake kupata watoto?

► Je, ni mambo gani ya udhalimu ambayo hutokea kwa sababu ya mila au desturi zilizoko kwenye utamaduni wenu?

### **Anachokisema Mungu**

Kwenye masimulizi sita yaliyorekodiwa katika Maandiko wakati Mungu akiwa anatoa mtoto wa kiume kwa mwanamke asiye na mtoto, wazazi hawakulaumiwa kwa njia yoyote kwa kukosa mtoto hapo awali. Kwa kweli, wanandoa hao walichaguliwa hasa na Mungu kuwa

wazazi wa watoto wa kiume pekee. Zakaria na Elizabethi waliitwa wenye haki (Luka 1:5-6). Hatupaswi kamwe kudhani kwamba mwanamke hana mtoto kwa sababu hajampendeza Mungu.

Ayubu 24:21 anasema kwamba kumtendea vibaya mwanamke mgumba ni kitendo cha mtu mwovu. Mungu hamhukumu wala kumtendea vibaya mwanamke mgumba, na sisi pia hatupaswi tufanye hivyo.

Katika Isaya 56:4-5 Mungu anazungumza na mtu asiyeweza kuzaa watoto. Mungu anasema kwamba ikiwa mtu huyu atamtii Mungu na kuishi katika agano lake, atakuwa na nafasi na sifa ambayo ni bora kuliko ambayo angekuwa nayo kutokana na kupata watoto wa kiume na wa kike.

Mtume Paulo alijiita mwenyewe baba yake na Timotheo (1 Timotheo 1:2) na Tito (Tito 1:4) na Onesmo (Philemoni 10). Akajiita tena mwenyewe baba wa waumini wa Korintho (1 Wakorintho 4:15). Hakuwa baba yao wa kibiolojia, lakini alikuwa ni baba wa kiroho. Kuwa baba wa kiroho kulikuwa ndiyo jambo muhimu zaidi.

Mathayo 12:46-50 inatuambia juu ya wakati ambapo mama na ndugu zake Yesu walikuja kumwona akiwa anafundisha. Yesu aliwauliza wasikilizaji wake, "Mama yangu ni nani? Na ndugu zangu ni akina nani? Baadaye akawaambia kwamba, "Ye yote atakayeyafanya mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni, huyu ndiye ndugu yangu, na umbu langu, na mama yangu." Tunatambua kwamba Yesu alijali sana kuhusu familia yake; hata alipokuwa pale msalabani alipanga kuhusu utunzaji wa mama yake (Yohana 19:26-27). Lakini Yesu anasema kwamba familia ya kiroho ni muhimu zaidi kuliko familia ya kibiolojia.

Familia yenye imani haiwezi ikawa mbadala wa familia ya kibiolojia, lakini nafasi ya mtu katika familia ya imani inaweza kumpa mwanamume au mwanamke utambulisho ulio muhimu zaidi. Maneno haya *kaka* na *dada* yanayotumika katika kanisa yanaonyesha umuhimu uliopo wa mahusiano ya familia ya imani (Wakolosai 1:2).

Debora alikuwa nabii wa kike aliyehudumu kama mwamuzi kwa ajili ya Israeli (Waamuzi 4:4). Debora pia aliongoza taifa la Israeli katika vita vya kutafuta uhuru wao kutoka katika taifa lililokuwa la uonevu. Katika Waamuzi 5:7 Debora alijiita mwenyewe mama wa Israeli. Biblia kamwe haijawahi kuwataja watoto wa kibiolojia wa Debora, lakini alikuwa mama kwa ajili ya Israeli kwa sababu aliwajali watu kwa uongozi wake.

Mtume Petro alisema kwamba wanawake wanaofuata mfano wa Sara ni watoto wake. Jaribu kufikiria hadhi kubwa hivyo anayopewa Sara kwa tamko hilo! Hii ni hadhi iliyotokana na mfano wake wa imani na utiifu, na siyo kwa ajili ya jukumu lake kama mama wa Isaka.

Watu wote ambao wameokolewa kwa neema kwa njia ya imani wanaitwa wana wa Abrahamu (Wagalatia 3:7). Abrahamu anapewa heshima ya hali ya juu kabisa kama baba wa mamilioni ya watu wote walioamini/waliookoka. Kutokana na mifano ya Abrahamu na Sara tunaweza kuona kwamba Mungu kwa kiwango cha juu anaheshimu ubaba na umama wa kiroho.



Mtume Paulo alielezea faida za mtu kuwa mseja. Mtu mseja anaweza kuzingatia kumpendeza Mungu bila ya kuwepo na majukumu mengine mengi (1 Wakorintho 7:32-35). Ingawaje mtu mseja hana mtoto, Paulo alisema kwamba useja ni mzuri tu kama mtu anaweza kuishi maisha ambayo ni ya usafi. Kwa sababu ya matamko haya, tunaweza kuwa na uhakika kwamba useja ni mapenzi ya Mungu kwa baadhi ya watu.

Kama ilivyo katika useja, pia kuna faida za kutokuwa na mtoto. Kama vile Mungu alivyo na nafasi mahususi kwa wale ambao ni waseja, kadhalika anazo nafasi mahususi kwa ajili ya wale waliooana lakini hawajajaliwa kupata watoto. Ingawaje hawakuwahi kuchagua wakae bila ya kuwa na watoto, wanapaswa wafanye jitihada zote nzuri za kufanya kazi kwa ajili ya Mungu.

Kwenye useja au ugumba, na hali yeyote ile tuliyo nayo, tunaweza kumwamini Mungu kwamba atafanya kazi kupitia kwetu kwa ajili ya kutuletea sisi faida za kiroho na kwa watu wengine (Warumi 8:28).

Kuna watoto wengi ambao hawana wazazi wa kuwatunza au kuwajali. Kuna uwezekano mkubwa kwamba hakuna mtu wa kuhudumia hitaji hili maishani mwao isipokuwa pawepo na baadhi ya watu binafsi au wanandoa katika familia ya imani wafanye juhudi za ziada za kuonyesha upendo kwao.

Tumeitwa ili tuitoe miili yetu iwe dhabihu iliyo hai kwa Mungu, na tuishi kama moyo wa ibada kwa Mungu (Warumi 12:1).

### **Vidokezo kwa Muhtasari**

1. Watoto ni baraka kutoka kwa Mungu, na ni haki kwa wanandoa kuomba kwa ajili ya Mungu kuwapa watoto.
2. Ni makosa kudhania kwamba wakati wote ni mapenzi ya Mungu kufanya muujiza wa kutoa mtoto. Siyo wakati wote huchagua kutoa mtoto, kama na vile ambavyo siyo wakati wote atafanya muujiza kwa kila hitaji lingine.
3. Ni makosa kumlaumu mwanamke au mwanandoa kwa ajili kukosa watoto. Hali ya mwanadamu imeathiriwa na dhambi ya Adamu, dhambi za mababu zetu, na dhambi zinazofanyika katika jamii yetu.
4. Tunapaswa tuwapende na kuwathamini kwa uwiano ulio sawa watoto wa kiume na wa kike kwa sababu ni watu walioumbwa kwa sura ya Mungu.
5. Mtu anaweza akawa baba au mama wa kiroho ambaye ana ushawishi kwa vizazi vingi hata bila ya kuwa na watoto wa kibiolojia.
6. Mungu hutoa fursa mahususi za huduma kwa waseja na watu ambao ni wagumba.
7. Tunapaswa kujitoa kwa Mungu na kumtukuza katika hali anazotuchagulia.

## **Huduma ya Mchungaji**

Kwa bahati mbaya, makanisa kwenye maeneo mengi yamefuata tamaduni zao zaidi kuliko Neno la Mungu wakati wanashughulikia suala la kutokuwa na watoto.

Mchungaji anapaswa kuwafundisha watu wake waweze kuliona suala la ugumba/kukosa watoto kwa mtazamo wa kibiblia, hasa kama ilivyowekwa kwa muhtasari katika sehemu iliyotangulia.

Ikiwa mchungaji anaombea muujiza kwa wanandoa wasio na watoto, haipaswi kuweka jukumu la imani kwa mke au mume. Yesu alipomponya mtoto mdogo au kufufua wafu, mtu aliyeponywa au kufufuliwa hakuwa na imani kwa muujiza wake mwenyewe. Ikiwa mchungaji ana uhakika kwamba Mungu anataka kufanya muujiza huo, mchungaji anapaswa kuwa na imani na asimlaumu mke au mume kwa ukosefu wa imani.

Katika Warumi 12:15, tunaambiwa tulie pamoja na wale wanaolia. Mchungaji anapaswa kufahamu huzuni ya watu katika kusanyiko lake. Anapaswa kuchukua hatua ya kuwatia moyo na kuwafariji wale wanaoomboleza kwa sababu ya kukosa watoto au kufiwa na mtoto. Mwanandoa pia hupatwa na huzuni wakati kichanga chake kinapokufa kabla ya kuzaliwa na ambaye hakuwahi kuishi. Kumbuka kwamba mume na mke wanateseka kwa pamoja, ingawaje watakuwa wanaonyesha hali zao kwa njia tofauti. Mchungaji asingojee watu walio na huzuni waje kwake ili kupata ushauri. Mchungaji anapaswa kufundisha kusanyiko lake kuhusu kutiana moyo na kusaidiana kila mmoja na mwenzake.

Mchungaji anapaswa aliongoze kundi katika kujenga mahusiano na kuwatunza wanandoa wazee au watu binafsi ambao bado hawajajaliwa kupata watoto. Wanafamilia wa imani wanapaswa wawachukulie kama ni wazazi, au mababu na mabibi kwa kuonyesha upendo wao, kuchukua muda wa kuwa pamoja nao, na kuwasaidia katika mahitaji yao ya msingi.

Mchungaji anapaswa awasaidie waseja na watu ambao bado kupata watoto wapate njia nzuri za kutumika na kulibariki kanisa na jamii. Mchungaji anapaswa kuthibitisha umuhimu wa kila mtu katika familia ya imani.

## **Kwa ajili ya Majadiliano ya Kikundi**

- Je, ni kwa jinsi gani watu katika utamaduni wa kwenu wanawachukulia watoto? Je, ni ka jinsi gani wanawachukulia wagumba na au watu ambao hawajawahi kupata watoto?
- Je, waumini katika utamaduni wako wana mtazamo gani kuhusiana watoto? Je, waumini katika utamaduni wako wana mtazamo gani kuhusu kutokuwa na watoto?
- Je, ni kwa jinsi gani uelewa wako kuhusu utasa/ugumba umebadilika au kupinga kwa kujifunza kanuni za kimaandiko zilizowasilishwa katika somo hili?
- Je, kuna wanandoa wowote ambao inawezekana wanapambana na hali ya utasa ndani ya familia yako ya imani ya kanisa? Kama ndivyo, ni kwa jinsi gani kanisa lako linaweza kuwa kuunga mkono na kuwapa sehemu salama kwa ajili ya kushirikisha mapambano yao?

## Maombi

Baba wa Mbinguni,

Asante kwa ajili ya familia za Kikristo. Asante kwa ajili ya waume na wake ambao wanaishi kwa ajili yako, na kwa mchango wao katika ufalme wako.

Tunaomba kwa ajili ya wale wanandoa ambao wanapambana na utasa. Tunaomba kwamba uwafaraji na uwatie moyo ndani ya mioyo yao. Wasaidie katika kujua kwamba upendo wako kwao ni endelevu na usiokoma hata katika kukosa uwezo wa kupata watoto.

Ikiwa ni mapenzi yako kwao kupata watoto wa kibaiolojia, tunakuamini utafanya iwezekane kwa wakati wako. Aidha Iwe umewapa au hujawapa watoto wao wenyewe, wasaidie waweze kuwa wababa na wamama wa kiroho kwa ajili ya watu wengine.

Wasaidie waumini wote kuona thamani ya kila mtu kama walioumbwa kwa sura yako.

Ameni

## Kazi za Kufanya

(1) Andika karatasi ya kurasa mbili ambamo:

- Utaelezea mitazamo ya jamii yako kuhusiana na watoto na ugumba/utasa.
- Utaelezea kuhusu maandiko yanayofundisha kuhusiana na watoto.
- Utaelezea kuhusu maandiko yanayofundisha kuhusiana na utasa/ugumba.
- Utaelezea kutoka katika kanuni za kimaandiko ni kwa nini wanandoa hawapaswi kulaumiwa kwa lolote kutokana na utasa/ugumba wao?

(2) Watie moyo wale ambao wanakabiliana na tatizo la utasa/ugumba.

Uchaguzi wa 1: Elezea kwa maandishi jinsi utakavyoweza kudhihirisha huruma na utunzaji wako kwa mtu unayemjua kwamba anahangaika katika huzuni ya kutoweza kuzaa. Kuwa mahususi katika kutaja baadhi ya mambo ambayo unaweza kuyafanya au kusema yatakavyoweza kuwa baraka kwa kaka na dada yako aliye ndani ya Kristo.

Uchaguzi wa 2: Andika barua fupi ya kumtia moyo mtu unayemjua ambaye anashughulika na tatizo la utasa/ugumba. Jaribu kuelewa hali wanayoipitia. Waache wajue kwamba unajali kuhusu jinsi wanavyojisikia. Waeleze kwamba unaomba kwa ajili yao. Utakapokuwa unawapa hiyo barua fupi, uwe tayari kuwasikiliza na kudhihirisha kwao kwamba unajali kwa ajili yao kwa njia inayofaa.

## Uzazi wa Mpango

Kabla ya kuendelea na Somo la 11, darasa linapaswa **kujifunza na kujadili Kiambatanisho "B"**. Haya ni majadiliano mafupi kuhusiana na uzazi wa mpango, na ni mada inayohusiana na ndoa na familia.



# Somo la 11

## Maendeleo na Utunzaji wa Mtoto

### Malengo ya Somo

Hadi kufikia mwishoni mwa somo hili, mwanafunzi atapaswa:

- (1) Atambue vyema kazi ya Mungu ya ajabu katika uumbaji wa kila mtu.
- (2) Aamini kwamba maisha ya mwanadamu ni ya heshima sana.
- (3) Kuhamasika katika kuyalinda maisha ya mwanadamu kuanzia tu kwenye kipindi cha kutunga kwa mimba.
- (4) Umuhimu wa malezi ya wazazi kwa ajili ya ukuaji endelevu wa afya kwa watoto.

### Mapacha Wadogo

Marko na Mariamu waliishi katika nchi ya India. Walikuwa wameoana kwa miaka kadhaa bila kupata watoto na ghafla fursa ikawatokea. Mmoja wa ndugu wa ukoo wa Mariamu alikuwa amejifungua mapacha wawili wa kike na alihisi hawezi kuwatunza. Marko na Mariamu kwa pamoja walikubali kupokea zawadi ya watoto hao wawili kwa furaha kubwa, lakini walikabilikabiliwa na changamoto nyingi. Watoto hao walikuwa wamezaliwa njiti wakiwa na uzito wa takriban pauni tatu kila mmoja. Wazazi wapya walipata usaidizi mdogo au ushauri kutoka kwa marafiki walipokuwa wakijaribu kuwalisha na kuwatunza hawa mapacha wa kike. Walikesha mara nyingi bila ya kupata usingizi wa kutosha kwa ajili ya hawa watoto, lakini wasichana hawa waliishi na wakakua kwa jinsi ya ajabu na wenye afya njema.

### Mtoto

#### Kukua kwa mtoto wakati wa Mimba

► Mwanafunzi anapaswa asome Zaburi 139:13-18 kwa ajili ya kikundi.

Kifungu hiki kinatupa taarifa kwamba Mungu alitujua mwanzoni tangu tulipotungwa mimba kwenye matumbo ya mama zetu, hata kabla miili yetu haijaumbwa (Aya ya 16). Mungu alikujua wewe na alikuwa na mpango kwa ajili yako kabla hata hajazaliwa.

Wakati manii kutoka kwa mwanamume zinapogusana na yai la mwanamke lililoko ndani yake, mtoto anatumwa – maisha mapya ya binadamu – kiumbe kipya – vinaanza kuwepo. Taarifa zote za kinasaba kwa ajili ya mtu huyo zinakuwepo ndani ya hiyo seli moja. Masaa 24 tu baada ya mimba kutungwa, seli hiyo hugawanyika na kuwa seli mbili. Kila mojawapo ya hizo seli mbili hugawanyika tena katika seli nyingine mbili. Katika kipindi cha wiki moja, mtoto sasa anakuwa kwenye seli nyingi ambazo hushikiliwa kwenye tumbo la uzazi la mama

ambako hukua na kuongezeka. Kila seli inakuwa na “mfumo wa siri wa kanuni na taratibu” kwa ajili ya kumfanya mtu huyo (DNA). Seli hizo hufuata maelekezo ya “mfumo wa siri wa kanuni na taratibu” (DNA) na hufanya kazi mahususi ya kutengeneza kila sehemu ya mwili.

Kwenye wiki ya 3 ya umri wa mimba, uti wa mgongo wa mtoto na ubongo huanza kujitengeneza. Kwenye wiki ya 4 ya umri wa mimba, macho ya mtoto huanza kutengenezwa, moyo huanza kazi na mikono ya mtoto huanza kutengenezwa. Kwenye wiki ya 12 ya umri wa mimba, mwili wa mtoto una kila kiungo muhimu kinachohitajika.

Kufikia wiki ya 14 baada ya mimba kutungwa, alama za kipekee za vidole vya mikono ya mtoto huwa zimekamili kabisa. Kufikia wiki ya 16-24 za ujauzito, mama anaweza kuhisi mtoto wake akicheza tumboni mwake. Kwenye wiki ya 26-28 mapafu ya mtoto huwa yamekua kiasi cha kutosha kuanza kupumua, na mtoto atakuwa na uzito wa paundi mbili. Kwa kawaida watoto huzaliwa kati ya wiki ya 38-40 tangu siku ya kupata ujauzito. Kila mtoto mchanga ni kiumbe cha ajabu, cha pekee kilichofanywa na Mungu Muumbaji wetu.

► Mwanafunzi anapaswa asome Mhubiri 11:5 kwa ajili ya kikundi.

Ni ukweli kabisa kwamba ni muujiza jinsi Mungu anavyoumba, anavyotengeneza na anavyokuza mtoto kwenye tumbo la uzazi la mama yake. Watu kamwe hawawezi kufahamu mchakato wote au mambo yote yanavyofanyika. Lakini bado, kupitia mabara yote ya dunia, jamii na tamaduni zote, maendeleo ya wanadamu hufuata mlolongo na mpangilio ulio sawa usiobadilika. Ubunifu wa Muumbaji ni wa uhakika ulio mkamilifu!

► Mwanafunzi anapaswa asome Ayubu 10:8-12 kwa ajili ya kikundi.

Katika hizi aya za Ayubu anatumia mlinganisho unaorejea mimba na ukuaji wa mtoto akiwa tumboni mwa mama yake. Ayubu anatuambia kwamba Mungu Muumbaji ndiye anayetoa au mpaji wa uhai.

### **Thamani ya Kuumbwa katika Sura ya Mungu**

Mwanzo 1:26-27 na Mwanzo 9:6 tunaambiwa kwamba tumeumbwa kwa sura ya Mungu. Maisha yote ya mwanadamu ni ya heshima sana. Kwa sababu hiyo, ni dhambi kumwua mwanadamu yeyote (Mwanzo 9:5, Kutoka 20:13).

Katika Ezekieli 16:20-21, 36, 38 Mungu anazungumzia vikali dhidi ya wale wote watakaomwondolea mtoto uhai wake. Anawaonya wana wa Israeli kuhusu utoaji wa dhabihu za watoto wadogo kwa madhabahu za kishetani na anatangaza kwamba adhabu yao ni kubwa sana.

Katika Isaya 46:3-4, Mungu anazungumzia kuhusu uangalizi wake kwa ubinadamu katika hatua zote kukua kwa mwanadamu anapotoa kauli hii nzito:

Nisikilizeni, enyi wa nyumba ya Yakobo, ninyi mlio mabaki ya nyumba ya Israeli, mlio chukuliwa nami tangu tumboni, mlio inuliwa tangu mimbani; na hata uzee wenu

mimi ndiye, na hata wakati wenu wa mvi nitawachukueni; nimefanya, nami nitachukua; naam, nitachukua na kuokoa.

Hii ni ahadi bora sana!

Watu wote ni wa thamani, ikiwa ni pamoja na watoto ambao bado hawajazaliwa, walemavu, wenye mahitaji maalumu, na wazee. Thamani ya mtu haitegemei kile kitu anachoweza kukifanya, au ikiwa kama angeweza kuishi ikiwa angekuwa pake yake. Kila mtu ana thamani kwa sababu watu wote wameumbwa kwa sura ya Mungu.

Biblia inatuambia kwamba kila mtoto ni wa thamani mbele za Mungu tangu wakati ule wa kutungwa kwa mimba yake (Zaburi 139:13-18). Kwa sababu hiyo, tunajua kwamba sisi ni wanadamu tangu siku ile ya kutungwa mimba. Kutoa mimba kwa kukusudia ni kumuua mwanadamu.

Kuna angalao njia nne tu ambazo wafuasi wa Kristo wanapaswa kufanyia kazi ili kulinda maisha ya watoto ambao hawajazaliwa pamoja na kuwahudumia akina mama:

1. Wanapaswa kushawishi serikali zao na taratibu za mahakama za mataifa yao kutengeneza sheria na kupitisha hukumu kali ka ajili ya kuwalinda watoto ambao hawajazaliwa kutokana na kuuawa.
2. Wanapaswa kutoa msaada wa vitendo kwa wanawake ambao wanajisikia kwamba uchaguzi wao wa mwisho ni kutoa mimba, ili waweze kujisikia kwamba wana uwezo wa kuyalinda maisha ya watoto wao.
3. Wanapaswa wawatunze watoto wanaotupwa au kuachwa.
4. Wanapaswa kutoa neema na usaidizi wa kiroho kwa wanawake ambao wametoka katika hatia ya kutupa mimba zilizopita.

### **Utunzaji wa Mtoto ambaye Hajazaliwa**

Ni jambo muhimu kutambua kwamba mtoto anayekuwa amebebwa na mama katika tumbo lake la uzazi ana hatima yake ya milele. Mtu huyo atakuwepo milele. Kwa sababu hiyo, wazazi wanapaswa kuwajali na kuwatunza watoto wao katika vipengele vyote vya maisha yao: kimwili, kiakili, kijamii/kimhemuko, na kiroho!

► Mwanafunzi anapaswa asome Mathayo 18:2, 10 kwa ajili ya kikundi.

Tabia ya mwanaume inaweza kuathiri afya ya mtoto wake ambaye bado hajazaliwa na pia inaweza kumzuia ashindwe kuwa baba tangu mwanzoni. Ulevi wa pombe, madawa ya kulevya, au uvutaji wa sigara vyote vina uwezo wa kuharibu manii ya kiume na hivyo kuwepo na uwezekano mkubwa wa utasa (kushindikana kupatikana kwa mimba) au mimba kutoka (mtoto kufa wakati wa mimba).

Mama mwenye mimba kutumia vitu ambavyo vina madhara, kama vile madawa (yaliyopigwa marufuku), ulevi wa pombe, au uvutaji wa sigara vina uwezo wa kuharibu

kabisa na kusababisha madhara kwa mtoto. Vitu hivyo vinazuia kukua kwa mtoto na kusababisha azaliwe akiwa na matatizo ya kimwili au kiakili.<sup>37</sup>

Mojawapo ya nyakati ngumu wakati wa ukuaji wa mtoto kabla ya kuzaliwa ni wakati ambapo viungo vyake na tishu zake ndiyo kwanza vinaanza kukua, hasa kati ya wiki ya 3-4 ya umri wa mimba. Katika wakati huu, wanawake wengi huwa hawajijui kama wameshabeba mimba!

► Mwanafunzi anapaswa asome 1 Wakorintho 10:31 kwa ajili ya kikundi.

Ingawa mama hawezi kudhibiti afya ya mtoto wake ambaye hajazaliwa, anaweza akamsaidia mtoto kwa kadri inavyowezekana, kwa kuhakikisha kwamba anapata lishe bora na kuepukana na vitu vyenye madhara. Mungu anasema watoto ni wa thamani kubwa, na tunamtukuza Mungu wakati tunapowatendea kwa jinsi hiyo waliyo nayo.

Ni jambo liletalo huzuni sana wakati mtoto aliye tumboni haishi hadi kufikia wakati wake wa kuzaliwa. Kwa kawaida kifo cha kitoto kichanga tumboni ambacho hakijazaliwa siyo matokeo ya jambo lolote ambalo mama amelifanya. Kunakuwepo na hisia kubwa sana kwa wazazi ya kupoteza mtoto, kwahiyo, waumini wengine wanapaswa wajaribu kuwafariji katika kipindi hicho.

## **Kuzaliwa**

Wakati kukiwa na tofauti nyingi za kitamaduni zinazozingatia uzoefu wa kuzaa, mambo mengi yanafanana takribani kila mahali ulimwenguni kote. Katika Mwanzo 3:16, Mungu alisema, "Hakika nitakuzidishia uchungu wako, na kuzaa kwako; kwa utungu utazaa watoto...."

Karne nyingi zimepita, na maneno ya Mungu bado yameendelea kubakia kuwa ya kweli ulimwenguni kote. Matokeo ya dhambi ya kwanza ya Adamu na Hawa bado yameendelea kugusa mchakato mzima wa uzazi hadi sasa. Hata Mariamu, mama yake na Yesu, hakuachwa katika mchakato huu, kwani alipitia pia katika maumivu ya kuzaa (Luka 2:6-7).

## **Hali ya Mwanzo ya Utotoni**

### **Kukua Kimwili**

Mtoto hukuza uwezo wa kimwili katika hatua zinazotabirika. Mtoto kwanza atainua kichwa chake, kisha kukaa, kisha kutambaa, kisha kutembea. Wakati mojawapo ya haya hayafanyiki ndani ya muda uliotarajiwa, wazazi huanza kuwa na wasiwasi. Jinsi watoto wanavyoendelea kukua, tunawategemea wawe na uwezo wa kurukaruka, kupanda na kukimbia wanapokuwa kwenye umri wa miaka 4-5 tangu kuzaliwa. Wanaendelea kutoka kwenye kunywa maziwa pekee hadi kula vyakula vigumu. Wanafamilia hufurahia, na

---

<sup>37</sup> Greg Cook & Joan Cook, *The World of Children*, 3rd ed. (Pearson Education, 2013), 85.



hushanglia kwa kuendelea kutia moyo katika hatua hizi za maendeleo ya kawaida ya kimwili ya mtoto wao.

### **Kukua Kiakili**

Walezi husikilizia kilio cha kwanza cha mtoto mchanga na kutarajia mtoto kutoa sauti za furaha akiwa kwenye takribani miezi miwili ya umri wake tangu kuzaliwa. Baadaye, mtoto huanza kunguruma na kurudiarudia sauti mbalimbali. Wazazi hufurahishwa sana wanaposikia mtoto akisema “Mama” au “Baba” anapokaribia kuwa na umri wa miezi sita (6) ya kuzaliwa kwake. Kwa kawaida watoto huanza kutamka maneno wakati wakiwa na umri wa mwaka mmoja (1), na huanza kutengeneza sentensi zilizokamilika na kueleweka wakiwa katika umri wa miaka miwili (2).

Watoto wadogo hutushangaza kwa mambo wanayokumbuka. Wanauliza maswali mengi sana. Siku zote watakumbuka kama ulishawaahidi kufanya jambo la kipekee au maalumu pamoja nao. Ukuaji wao wa kiakili hutokea kwa sababu ya mpango wa Mungu aliouweka, lakini malezi ya wazazi na walezi wengine huleta tofauti kubwa katika kuwasaidia kukua hadi kufikia kwenye uwezo wao kamili.

### **Kukua Kijamii na Kimhemuko**

Watoto wanahitaji wazazi wao kuwasaidia kuwa na afya njema ili waweze kukua kimwili. Hata hivyo, wanahitaji kutiwa moyo kwa ajili ya maendeleo yao ya kijamii na kihisia hata zaidi. Wazazi, walimu, na walezi wengine wanapaswa kumsaidia kimakusudi kila mtoto kukua kijamii na kihisia.

Jinsi wazazi watakavyokuwa wanafanya mambo yaliyoko kwenye orodha, kadhalika watoto wao wanasaidiwa kustawi na kukomaa kijamii na kimhemuko.

► Soma hadi mwisho orodha hii. Kisha ipitie tena orodha hii kwa mara ya pili. Kando ya kila kitu ambacho wewe kama mzazi unajaribu kukifanya vizuri, andika mfano wa njia mahususi unayotumia kufanya hivyo. Weka alama pembeni mwa orodha ambayo kwa makusudi hujamudu kufanyia kazi. Kama wewe siyo mzazi, unaweza ukachagua vipengele kwenye hiyo orodha ambavyo unaweza kufanyia kazi kwa ajili ya watoto ambao ni wa jamii zako au ambao ni wa karibu na familia yako.

### ***Njia ambazo unaweza kuwasaidia watoto wako Wakomae*<sup>38</sup>**

(1) Kwa kujijali mwenyewe:

- Dhibiti mifadhaiko yako ya binafsi.
- Dhibiti rasilimali za familia yako.
- Toa msaada kwa wazazi wenzako.

---

<sup>38</sup> Imenukuliwa kutoka kwa Charles A. Smith, et al., *National Extension Parent Education Model*. (Manhattan, Kansas: Kansas Cooperative Extension Service, 1994). Imepakuliwa kutoka <https://www.k-state.edu/wwparent/nepem/nepem.pdf> Julai 31, 2023.

- Omba na ukubali usaidizi kutoka kwa watu wengine inapohitajika.
- Tambua uwezo wako wa binafsi na uwezo wako wa malezi.
- Kuwa na makusudi yaliyo wazi katika kupanga malengo ya kulea watoto.

(2) Kwa kuwa mtu mwelewa:

- Angalia na uwaelewe watoto wako na maendeleo yao.
- Tambua jinsi watoto wanavyoathiri na wanavyoitikia kile kinachowatokea.

(3) Kwa kuweka mwongozo:

- Fanyika mfano sahihi unaofaa, na tabia inayohitajika.
- Weka na udumishe mipaka inayofaa.
- Wape watoto fursa wajifunze jinsi ya kuwajibika. (Fursa zinatakiwa ziende sambamba na hatua ya maendeleo yao).
- Fundisha ujuzi wa kutatua matatizo.
- Weka umakini wako kwenye shughuli za watoto.
- Kusimamia jinsi watoto wanavyowasiliana na uzoefu wao na watoto wengine pamoja na watu wazima.

(4) Kwa Kulea:

- Onyesha mapenzi na huruma.
- Kuza kujiheshimu na matumaini ya watoto.
- Sikiliza na uhudumie hisia na mahitaji ya watoto
- Fundisha kuhusu wema.
- Toa mahitaji ya lishe, malazi, mavazi, afya na usalama kwa ajili ya watoto.
- Furahia maisha pamoja na watoto.
- Wasaidie watoto wajisikie kwamba wameunganishwa katika historia ya familia na urithi wa asili.

(5) Kwa Kuhamasisha:

- Wafundishe watoto kuhusiana na wao wenyewe, watu wengine, na dunia inayowazunguka.
- Chochea hamu ya kudadisi, mawazo, na utafutaji wa ujuzi.
- Weka mazingira ya kujifunza yaliyo na manufaa.
- Wasaidie watoto katika kuchakata na kudhibiti taarifa.

#### (6) Kwa Kutetea:

- Tafuta, tumia, na anzisha rasilimali za jamii kwa ajili ya kuwafaidia watoto wako mwenyewe na jamii ya watoto.
- Changamsha mabadiliko ya kijamii ili kutengeneza mazingira yatakayokuwa ni msaada kwa ajili ya watoto na familia.
- Jenga mahusiano na familia, majirani na vikundi mbalimbali vilivyoko katika jamii.

#### **Maendeleo ya Kiroho**

Kwa sababu Mungu alituumba na maisha ya kiroho (Mwanzo 2:7), tunapaswa kuwafundisha watoto wetu kuhusu imani na kuwaongoza kuishi katika uhusiano na Mungu.

► Wanafunzi wanapaswa wasome Zaburi 78:5-8 na Kumbukumbu la Torati 6:4-9 kwa ajili ya kikundi.

Je, unatumia njia gani katika kutii maagizo ya Mungu ya kufundisha watoto wako kwa bidii? Je, kuna maeneo gani ambayo unahitaji kuyaendeleza?

Ni lazima tuzingatie kwa kumaanisha maagizo ya Mungu kuhusu kufundisha familia zetu. Vinginevyo, tunashindwa kuishi katika kumtii Mungu, na watoto wetu pia watakuwa ni wa kukataa mamlaka ya Mungu.

Kuna aina mbalimbali za ufundishaji wa watoto, ikiwa ni pamoja na: Kusoma Biblia, Kuimba nyimbo zinazohusiana na Yesu, Kukariri maandiko, Maombi, Kufundisha kwa kutumia maswali na majibu, Kuwa na majadiliano ya kila siku. Kushiriki katika kanisa pia ni muhimu kwa ajili ya familia nzima.

Wakati mwingine mzazi anaweza kuwashikila watoto kwa muda wanapotaka kwenda kulala waimbe nyimbo zinazohusiana na imani na upendo wa Yesu kwa ajili yetu. Watoto hukuza imani iliyo na nguvu sana wanaposikia kuhusu upendo wa Mungu na uaminifu wake wakati wakiwa katika uangalizi wa upendo wa wazazi wao.

#### **Hitimisho**

Unapokuwa mzazi, siku zako ni nyingi. Ni siku za kazi nyingi; ni siku zinazochosha; siyo siku zako mwenyewe. Hata hivyo, katikati ya kilio, maziwa yaliyomwagika, nepi chafu, na ratiba zisizokuwa na mwisho, chukua muda wa kusitisha kwa muda ili upate mtazamo mwingine. Kumbuka kwamba unamtunza mmoja wa watoto wa Mungu, ambaye yeye, katika mpango wake wa milele, alikuamini wewe na kukukabithi. Hajakutaka wewe uwe na nyumba nzuri, bajeti nzuri inayovutia, milo ya kifahari, au mavazi ya gharama kubwa kwa ajili ya watoto wake. Anachokitaka Mungu kutoka kwako ni hiki hapa:

Nawe mpende Bwana, Mungu wako, kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote. Na maneno haya ninayokuamuru leo, yatakuwa katika moyo wako; nawe uwafundishe watoto wako kwa bidii, na kuyanena uketipo katika

nyumba yako, na utembeapo njiani, na ulalapo, na uondokapo. (Kumbukumbu la Torati 6:5-7).

### **Kwa ajili ya Majadiliano ya Kikundi**

- ▶ Je, ni vipengele gani vya malezi ya watoto mara nyingi hupuuza katika jamii yako?
- ▶ Je, familia zinakabiliwa na matatizo gani? Je, kwa nini siyo jambo rahisi wao kutoa uangelizi wa mtoto kama inavyoelezwa katika somo hili?
- ▶ Je, ni kwa jinsi gani waumini wanaweza kuwasaidia wamama waja wazito waweze kujitunza wenyewe pamoja na watoto wao ambao bado hawajazaliwa?
- ▶ Je, ni njia zipi ambazo familia za Kikristo zingeweza kufanya kazi pamoja kubariki maisha ya watoto wadogo na mama zao?
- ▶ Je ni kwa jinsi gani kanisa linaweza kuandaa huduma ambayo itakuwa inajali mahitaji ya watoto wadogo?

### **Maombi**

Baba wa Mbinguni,

Tunakuabudu wewe, uliye Muumbaji wetu wa kustaajabisha. Ulitumba sisi ndani ya matumbo ya uzazi ya mama zetu na umekuwa ukitujali katika maisha yetu yote. Unajua kila kitu kuhusiana na sisi hata kabla hatujazaliwa.

Tusaidie kufanya yale tuyawezayo kulinda watu walio katika mazingira magumu, kutia ndani wale ambao bado wako matumboni mwa mama zao. Wabariki wale wanaohudumia akina mama wawazito.

Asante kwa kutuamini sisi kwa kibali na wajibu wa kuweza kuwakuza watoto wetu. Unapokuwa unawaumba na kuwaendeleza watoto wetu, tusaidie tuweze kuwa waangalifu na makini kwenye utunzaji wetu kwa ajili yao na mafunzo yetu kwa ajili yao pia.

Tunataka kuwa watiifu kwako kwa jinsi tunavyowalea watoto wetu. Tusaidie kukuwakilisha vyema kwa watoto wetu. Utuwezeshe kuwafundisha watoto wetu kukupenda na kukutii.

Ameni

## Kazi za Kufanya

(1) Soma 2 Timotheo 1:3-5; 1 Wakorintho 4:17; Wafilipi 2:19-23. Andika ibara moja yenye kujibu maswali haya:

- Je, wanawake wawili waliotajwa ni kina nani na walikuwa na majukumu gani katika familia zao?
- Je, inavyoonekana walikuwa na ushawishi gani juu ya Timotheo?
- Je, kulikuwa na matokeo gani ya ushawishi wao kwa ajili ya maisha ya kanisa la mwanzo?

(2) Fanya marejeo ya vifungu vya maandiko ambavyo umekariri wakati wa kozi hii: Kumbukumbu la Torati 6:4-9, Warumi 6:11-14, Wakolosai 3:5-7, na mistari uliyochagua ili kukariri katika Somo la 5, Zoezi la 4. Je, aya hii inakuathiri vipi unapofanyia kazi?

(3) Kariri Zaburi 78:4-8. Mwanzoni mwa kipindi cha darasa linalofuata, andika au nukuu kifungu kutoka kwa kumbukumbu..

(4) Omba kipekee kabisa kwa ajili ya kila mtu katika familia yako kwa mahitaji yao ya binafsi. Jiombee pia na wewe mwenyewe. Je, Mungu anakuita wewe uwe katika familia ya aina gani?



# Somo la 12

## Kuwalea Watoto Kwa Makusudi

### Malengo ya Somo

Hadi kufikia mwishoni mwa somo hili, mwanafunzi atapaswa:

- (1) Elezea wajibu ambao Mungu amewapa wazazi.
- (2) Elewa umuhimu wa ukuzaji wa tabia mapema.
- (3) Kuwezesha kwa makusudi ya kupanga kwa ajili ya maendeleo ya watoto katika maeneo tisa ya maisha.
- (4) Kuelezea mwingiliano uliopo kati ya hiari huru ya mtoto na vishawishi kutoka nje dhidi a mtoto.
- (5) Kujikabidhi kabisa kwa ajili ya uanafunzi wa uaminifu kwa watoto.

### Yonathani Edward, Baba wa Urithi wa Familia.

Yonathani Edward alikuwa ni mchungaji aliyeheshimiwa na mwanateolojia aliyeishi katika miaka ya 1700. Yeye na mke wake Sara walikuwa ni wazazi wa watoto kumi na moja (11). Sara alikuwa mke na mama mzuri sana, akiwa na ushawishi mkubwa katika malezi na uundaji wa tabia za watoto wake. Mwenyewe Yonathani alikuwa ni baba aliyejitolea sana. Tunaambiwa kwamba "kila usiku wakati Bwana Edward akiwa nyumbani, atautumia muda wake wa saa moja na familia yake na kisha akiomba baraka ziwe juu ya kila mmoja."<sup>39</sup>

A. E. Winship, mwelimishaji mkubwa wa mwishoni mwa miaka ya 1800 alifanya utafiti kuhusu urithi wa Yonathani na Sara Edward, akifuatilia maisha ya vizazi vyao hadi miaka 150 baada ya kifo cha Yonathani. Aligundua kwamba urithi wa Yonathani ulijumuisha yafuatayo:

- Makamu wa Raisi wa Marekani - 1
- Mkuu wa shule ya sheria - 1
- Mkuu wa shule ya udaktari - 1
- Maseneta wa Marekani - 3
- Magavana - 3
- Mameya -3
- Maraisi wa wanafunzi Vyuo Vikuu - 13

---

<sup>39</sup> Nukuu na taarifa hii kwa ajili ya sehemu hii ilipatikana kutoka kwa Larry Ballard, "Multigenerational Legacies – the Story of Jonathan Edwards," YWAM Family Ministries, Julai 1, 2017. Imepakuliwa kutoka <https://www.ywam-fmi.org/news/multigenerational-legacies-the-story-of-jonathan-edwards/> Januari 11, 2021.

- Waamuzi - 30
- Madaktari - 60
- Maprofesa - 65
- Maofisa wa Kijeshi - 75
- Watu walioajiriwa ofisi za serikali - 80
- Wanasheria - 100
- Wachungaji na viongozi wengine wa makanisa -100
- Wahitimu wa Vyuo Vikuu – 285

Je, urithi wenye matunda kiasi hicho unawezekanaje? Je, ni kitu gani kiliwekezwa kwenye maisha ya watoto kumi na moja wa Edward ambacho kilizalisha vizazi vilivyojulikana kwa uadilifu wao, uwajibikaji, uongozi, na huduma nyingine kwa jamii? Kwa hakika, Yonathani alikuwa baba mcha Mungu na mwenye bidii ambaye alikuwa mfano wa uaminifu kwa ajili ya watoto wake waliokuja kufuata.

Biblia Inatuonyesha kwamba uchaguzi wa wazazi huathiri uhusiano wa watoto wao na Mungu kwa vizazi vingi vinavyofuata.

► Wanafunzi wanapaswa wasome Kumbukumbu la Torati 5:9-10 na Kumbukumbu la Torati 7:9 kwa ajili ya kikundi.

Haijalishi ni uamuzi gani ambao wazazi wamefanya, kila mtu anayo nafasi ya kumtumikia Bwana na kuwa mzazi mcha Mungu kwa ajili ya watoto wake mwenyewe. Wewe na uzao wako mnaweza mkamtumikia Bwana kwa uaminifu na kupata baraka na neema zake. Je, uko tayari kujitoa kuwa mzazi ambaye unamtumikia Mungu kwa uaminifu na kuwaongoza watoto wako waweze pia kumjua yeye?

### **Utangulizi wa Mtoto kwa Mungu**

Wakati Mungu alipozungumza kwanza na Yakobo, hakusema, “Mimi ni Mungu wa ulimwengu huu,” au “Mimi ni Mungu ambaye niliumba dunia,” ingawa matamko hayo bado yanguweza kuwa ni ya kweli. Badala yake alisema, “Mimi ni Bwana, Mungu wa Ibrahimu baba yako, na Mungu wa Isaka” (Mwanzo 28:13). Yakobo hakuanza uhusiano wake na Mungu bila ya ufahamu wa awali wa kumjua Mungu. Alijua kuhusu Mungu kwa sababu ya mafundisho ya baba na babu yake. Abrahamu alianza desturi ya kumwabudu Mungu. Watu wengine waliofuata walimwamini Mungu kwa sababu ya Abrahamu, hata kabla hawajakutana binafsi na Mungu. Wakati mtumishi wa Abrahamu Eliezeri alipoomba, alisema na Bwana, Mungu wa bwana wake Abrahamu (Mwanzo 24:12).

Baadaye Mungu alijulikana mara nyingi kama “Mungu wa Abrahamu, Mungu wa Isaka, Mungu wa Yakobo” (kwa mfano, Kutoka 3:15). Yusufu, katika kizazi kingine kilichofuata, alirejea ahadi za Mungu ambazo alikuwa amefanya na Abrahamu, Isaka na Yakobo (Mwanzo 50:24). Yusufu alitegemea familia yake iwe na uaminifu kwa Mungu sababu ya ahadi za Mungu zilizokuwa zimetolewa kwa vizazi vilivyokuwa vimetangulia.



► Kutokana na jinsi ambavyo Mungu alikuwa amejitambulisha mwenyewe, je, tunajifunza nini kuhusu njia ambazo watu walikuja kumjua Mungu?

Kwa kawaida watu hawaji kwenye uhusiano na Mungu tu kutokana na kusikia mafundisho ya imani kuhusiana na Mungu. Kwa kawaida, watu hujifunza kuhusu Mungu kwa kuangalia maisha ya watu wengine ambao wako kwenye uhusiano mzuri na Mungu. **Ushawishi mkubwa zaidi hutoka kwa wazazi ambao wamejitoa kabisa kwa Mungu.**

Hapa kuna baadhi ya maswali muhimu sana ya binafsi kwa ajili ya kutafakari: Je, Watoto wako wanajifunza nini kuhusu Mungu wanapotazama maisha yako? Je, watoto wako wanataka kuwa waaminifu kwa Mungu kwa sababu wanaona uhusiano wako na Mungu?

### **Wajibu wa Wazazi**

Mungu amewapa wazazi jukumu kubwa la kufanya. “Mlee mtoto katika njia impasayo, Naye hataiacha, hata atakapokuwa mzee” (Mithali 22:6).

Wazazi wanapaswa wawe na kusudi katika kuwafundisha watoto wao kumfuata Mungu. Wazazi wanapaswa kuelewa wajibu wao wa kuongoza na kuwafundisha watoto wao.

Jukumu la kuwafundisha watoto kwanza ni la wazazi, na siyo jamii, shule au kanisa. Mzazi anapaswa ahakikishe kwamba watoto wake wako kanisani, lakini hapaswi kudhania kwamba kanisa litamfundisha mtoto wake kwa ajili yake.

► Mwanafunzi anapaswa asome Waefeso 6:1-4 kwa ajili ya kikundi.

Je, wababa wanapaswa kufanya nini?

Jukumu la kufundisha watoto siyo tu la mama peke yake. Baba pia analo jukumu la mwisho kwa ajili ya ulinzi wa kiroho wa familia yake.

Wazazi wana jukumu nyeti la kufundisha watoto wao kwa ajili ya maisha. Kufundishwa kwa ajili ya maisha haimaanishi ni kufundishwa kwa ajili ya kupata kazi; bali inamaanisha ni kufundishwa jinsi ya kuishi kwa haki, maisha ambayo Mungu atayabariki. Wazazi hawapaswi kuwaachia watoto wao kufuata dhambi, wakitumaini kwamba wanaweza wakabadilika baadaye.

Maandiko yanatuonya kwamba tusijifunze falsafa potofu za duniani.

► Mwanafunzi anapaswa asome Wakolosai 2:8 kwa ajili ya kikundi.

Andiko hili linatuonya sisi kwamba tunaweza tukaibiwa kwa kuamini falsafa potofu kukubaliana na mfumo wa maisha mabaya. Dunia inaweza kuwalaghai watoto wetu kwa kuwafundisha kufuata njia za ulimwengu badala ya kumfuata Kristo.

Ni jambo bora zaidi ikiwa elimu ambayo watoto wetu wanaipata ni kutoka kwa waalimu wa Kikristo na wazazi. Kwenye maeneo ambayo shule za Kikristo hazipo, wazazi wanapaswa kuhakikisha kwamba mtoto bado anaweza kujifunza mtazamo sahihi wa maisha.

Elimu ya dunia inaweza kumfundisha mtoto imani kwamba hakuna Mungu, mabadiliko, na ubinadamu. Watoto wako hatarini zaidi kudhurika na mafundisho potofu na au ya uongo (Waefeso 4:14), na wazazi pia ni lazima wawalinde watoto wao. Wachungaji wanapaswa wajifunze jinsi ya kufundisha mafundisho ya imani yenye uwezo wa kuwazuia watu kutenda dhidi ya falsafa za uongo. Wachungaji na waalimu wanapaswa kuwapa familia taarifa ambazo zinaweza kuwasaidia kuwaweka watoto wao kwenye ukweli.

## **Mafunzo ya Awali**

► Mtu fulani aliandika kitabu kiitwacho *Watoto ni Sementi yenye unyevu*. Je, unadhani jina hili linamaanisha nini?

Wazazi wanapaswa kutambua kwamba watoto hujifunza kuhusu maisha na kuamua ni jambo lipi muhimu wangali wakiwa bado wadogo. Tabia huundwa wakati mtoto akiwa bado mdogo.

Ufuasi mwingi utatokea kabla ya watoto kufikia miaka yao ya ujana. Malengo mengi ya kifasihi ya kibiblia, malengo ya tabia, na tabia za kibinafsi, kijamii, na kiroho zinapaswa kukuzwa kabla ya miaka ya ujana.

Hata kabla ya kufikia umri wa miaka mitano (5) mtoto anakuwa ameshajifunza mambo ya misingi ya jinsi watu wanavyohusiana wenyewe mmoja kwa mwingine na ni tabia gani itakayompatia matokeo anayoyataka. Anajua kama anapaswa kutarajia haki au la, na kama adhabu na zawadi zinakuja kwa mfululizo. Anajua kama anapendwa. Anajua ikiwa hisia zake zitawafanya watu wengine wajali. Anajua kwamba anaweza kusamehewa anapokuwa amekosa. Aidha anajua kusema ukweli au kuficha makosa yake na dhambi zake. Anaweza kuamua kwamba aidha iwe au isiwe watu walioko kwenye mamlaka wanaweza kuaminika katika kumtunza na kutimiza ahadi zao.

Watoto hujifunza kutoka katika maneno na mifano ya wazazi wao, hata wakati ambapo wazazi hawajaribu kutaka kuwafundisha wao (Waefeso 5:1). Mifano ya watu wazima huwapa watoto dhana yao ya maisha. Watoto hujifunza ni jambo gani muhimu kwa kuona kile ambacho ni muhimu kwa watu wazima. Watoto hujifunza mambo ya kuwatendea watu wengine, jinsi ya kutendea kazi hali fulani zinazojitokeza, na jinsi ya kuwajibika kwa kuwatazama watu wazima. Hali hii huanzia pale mtoto anapozaliwa.

Wakati mwingine wazazi wanafikiri kwamba wanakuwa wanawafundisha pale tu wanapokuwa wamemweleza mtoto ni kitu gani afanye. Hata hivyo, mzazi anakuwa anafundisha wakati wote mtoto anapokuwa anatazama kile anachokifanya.

Mtoto hutazama watu wazima na kujifunza mambo yafuatayo: anajifunza jinsi ya kukabiliana na msongo wa mambo mengi, anajifunza jinsi ya kuwatendea watu wageni, anajifunza jinsi ya kuchukuliana na watu wa hadhi ya chini, anajifunza jinsi ya kujibu shutuma, anajifunza jinsi ya kushughulika na mahitaji ya watu wengine. Wazazi wanafundisha watoto wakati wote hata wakati ambapo hawajui kwamba wanafanya hivyo.

Endapo mtoto atakuwa anakosolewa mara kwa mara, anajifunza jinsi ya kuficha makosa yake, hutoa visingizio, na kuwalaumu wenzake. Akifikia kuwa mtu mzima atakuwa mtu wa kulaani, mnafiki na msiri sana. Ikiwa kuna migogoro ya mara kwa mara nyumbani, atakuwa na hofu na fujo. Ikiwa wanafamilia wanamdhihaki, anaweza akajiondoa kwenye kuchangamana na watu, au akawa mnyanyasaji wa watu wengine. Kama wazazi wake wanamfanya aaibike kila wakati, anajifunza kuishi na hatia, bila ya kujisikia kwamba anakubalika na Mungu. Kama atakuwa hawezi kufikia kiwango cha tabia ambacho kinahitajika na wazazi wake, hatimaye ataasi na huenda akajiunga na kikundi cha waasi wengine ambacho anakiona kama kinakuwa ni mbadala wa familia yake.

Kama watu wakiwa na subira na mtoto, anajifunza jinsi ya kuwa na subira kwa watu wengine. Kama watu watamtia moyo, anakuwa na kujiamini kwamba anaweza kujaribu. Ikiwa atapongezwa, anajisikia kuwa wa thamani sana na atakuwa tayari kutoa sifa kwa watu wengine. Ikiwa ataona haki ikitendeka, atataka naye kutenda haki.

Endapo mzazi atakuwa mtu wa kuvunja sheria na huku akimtaka mtoto wake kutii, mtoto atajifikiria kwamba siku moja na yeye atakapokuwa na umri wa mtu mzima atavunja sheria vilevile. Kama mzazi hana fadhili kwa watu wengine, mtoto anaweza kutegemea kuwa na nguvu sana za kutoweza kuwafadhili watu wengine. Kama mzazi atafikiria kwamba matatizo na mahitaji ya mtoto wake siyo muhimu, mtoto atafikiri kwamba atakapokuja kuwa mtu mzima ataweza kujihudumia yeye peke yake na kutothamini mahitaji ya watu wengine.

Kila mara wazazi wanapaswa kuonyesha utiifu wao kwa Mungu. Watoto watapaswa wajue kwamba wazazi wao wanalitii Neno la Mungu. Kama mzazi ataonyesha kwamba mapenzi yake mwenyewe ndiyo yaliyo muhimu kuliko mapenzi na au mamlaka ya Mungu, watoto wake watategemea waje kuishi hivyo. Mzazi atapaswa mara kwa mara aelezee kwa mtoto sababu za kufanya uamuzi na vigezo vilivyozingatiwa. Hali hii inamfundisha mtoto jinsi ya kufanya maamuzi.

Watoto hujifunza wakati wazazi wao wanapokuwa wanacheza nao. Wanatakiwa wajifunze kuhusu haki, wema, na kuwa na majibu kwa watu wengine. Michezo hukuza ujuzi wa mtoto. Madhumuni ya michezo ya familia ni pamoja na kujifunza, maendeleo binafsi, na kufurahia mahusiano na wanafamilia wengine. Mashindano kwenye michezo ya familia ni mazuri lakini hayapaswi yawe ni kwa sababu kuwatawala wengine ili mshindi aweze kufurahia kuwa bora zaidi kuliko mwingine. Swali la kutafakari wakati wa mchezo ni hili, "Je, kila mtu anafurahia mchezo?" Iwapo mshindi pekee ndiye atakayekuwa anafurahia mchezo, makusudi yasiyo sahihi yanatekelezwa. Kama watu wanapatwa na hasira wakati wa mchezo, mchezo huo haupo kwa ajili ya kukidhi makusudi yaliyo sahihi.

Wazazi hudhihirisha thamani ya mtoto wao wanapotumia muda wao pamoja na shughuli za mtoto. Wazazi wanapaswa wamsaidie mtoto wao katika miradi ya shule, kutengeneza au kufanyia ukarabati vifaa vyake vya kuchezea, na kumpa nafasi ya kibinafsi nyumbani, kusikiliza hadithi zake na vichekesho vyake, na kumfariji anapokuwa amefadhaika.

Wazazi wanapaswa wawajue waalimu wa mtoto wao. Wanapaswa wahudhurie kwenye kila mkutano ulioratibiwa kwa ajili ya kukutana na waalimu ili kujua hali ya mtoto inavyoendelea shuleni. Kama kuna uwezekano, wazazi wote wawili wanapaswa wahudhurie kwenye mkutano huo. Kama baba hataweza kushiriki katika kikao hicho, inakuwa na maana kwamba mambo mengine anayoshughulikia ni ya maana zaidi kuliko mtoto wake. Wazazi wanapaswa wawaulize na au wawahoji waalimu kuhusu ufaulu wa mtoto na mambo mengine yanayoendelea hapo shuleni. Waalimu wanategemewa wafanye mambo mazuri kwa mtoto kadri ya uwezo wao na kumlinda mtoto dhidi ya kutendewa mambo mabaya ya unyanyasaji ikiwa wanajua kwamba wazazi wa mtoto wanapendezwa na hatua hiyo.

Watu wanaoishi pamoja kama familia wanajuana vizuri sana. Wanajifunza mahitaji na makosa ya kila upande. Wanaweza wakapendana na kudhihirisha kwamba upendo huo ni zaidi ya wanavyoweza kumpenda mtu mwingine yeyote katika dunia. Kama hawawezi kupendana, wanaweza wakaumizana kwa njia nyingi kuliko mtu mwingine yeyote. Watu wengine huwatendea familia zao vibaya kabisa kulikoni hata wanavyowatendea watu wengine wasiowajua. Kwenye nyumba ya Kikristo inapaswa pawe ni mahali pa kuonyesha ustahimilivu, msamaha, utunzaji, na wema.

### **Ajira kwa Watoto**

Mtoto mdogo anahitaji muda wa kucheza na burudani kila siku. Mtoto anahitaji muda wa kupumzika, kutumia mawazo yake, kusoma vitabu, kucheza, kutengeneza vitu vyake au kujenga kitu, na kufurahia mazingira ya asili. Katika hali ambayo familia hufanya kazi pamoja kila siku katika kuzalisha chakula au kufanya majukumu mengine, inaweza kuwa ni jambo zuri kwa watoto kushirikishwa katika kazi za familia, lakini wazazi wanapaswa kukumbuka maadili mengine pia.

masaa mengi kazini ni ngumu kwa mtoto sio tu kwa sababu ya mahitaji ya mwili, lakini kwa sababu kazi anayopewa mtoto kwa kawaida ni ya kurudia-rudiwa na ya kuchosha. Anatamani kupata muda kwa shughuli zinazotumia mawazo yake. Inasikitisha ikiwa mtoto lazima afanye kazi nyingi sana kiasi kwamba wakati wake pekee wa burudani ni anautumia kwa ajili ya kula na kulala ili aweze kufanya kazi tena.

“Wakati mtu anapokuwa hana tena huruma kwa vijana, manufaa yake duniani yanakaribia kumalizika.”

- George MacDonald

Baadhi ya familia zinapitia katika hali ngumu kiuchumi na kuwa na fikra kwamba zinahitaji msaada wa kipato kutokana na kazi za watoto wao. Hata hivyo, ikiwa wanashindwa kuwasomesha watoto wao, huenda hali ya familia yao isibadilike kamwe. Kama mtoto atakuwa anafanya kazi badala ya kwenda shule, labda atatumia maisha yake yote kwenye kazi zenye ujira mdogo tu au kazi za vibarua. Kazi nyingi na fursa za kibiashara hazitaweza kupatikana kwa ajili yake.

Baadhi ya watu hutoa elimu kwa watoto wao wenyewe lakini wako tayari kuwatumia vibaya watoto wa familia maskini kwa kuwaajiri kwa masaa mengi kwenye mashamba au kazi za nyumbani, au katika biashara ya kuuza mtaani, huku wakijua kwamba hawakuwahi

kupatiwa elimu. Wakristo wanapaswa kushirikiana kwa pamoja ili kutafuta suluhisho lililo bora kwa ajili ya familia zilizoko katika jamii zao.

Watoto wanaweza kufurahia kazi ikiwa wanapewa majukumu yanayowapa hisia ya mafanikio. Pia Wanaweza kufurahia kufanya kazi na wazazi wao ikiwa wazazi watawatia moyo. Wazazi wanapaswa matarajio ya kimaendeleo juu ya kile ambacho mtoto anaweza kufanya na watoe mrejesho wa kujenga kwa njia chanya ili mtoto ahamasike kuendelea kujifunza na kukua.

Ni jambo zuri kwa watoto kuwa na majukumu ya kufanya kila siku ya kuwafundisha kuwa watu wa kutegemewa na wa wazi. Wazazi wanapaswa wawathibitishie kwa maneno ya kutamkwa wazi kuhusu sifa za tabia wanazoziona kwa mtoto anapokuwa anafanya kazi, kama vile, uwezo wa kuanzishia mambo au kuvumbua njia, kufanya kwa bidii, uangalifu, na ustahimilivu. Wazazi wanapaswa wawafundishe watoto wao kanuni za kazi zinazofundishwa katika Neno la Mungu.

Ni jambo zuri kwa watoto kuwa na fursa za kujipatia fedha ambazo wanaweza wakajichagulia namna ya kuzitumia. Wanajifunza thamani ya kazi yao na wanajifunza jinsi ya kutumia fedha zao kwa njia ya faida nzuri na bora zaidi. Mtoto anayefanya kazi ili kupata fedha anaweza akajitambua kwamba hapaswi kuzitumia zote kwa ajili ya kununulia pipi; atataka anunue kitu ambacho anaweza akakihifadhi mwenyewe. Wazazi wanapaswa kuwafundisha watoto wao kufikiri kuhusu fedha na namna ya kuzitumia kwa njia za kimungu.

Ni jambo zuri kwa watoto na vijana kutambulishwa kwenye aina mbalimbali za kazi ambazo zinaweza kuendeleza uwezo wao. Ni jambo zuri ikiwa kijana mdogo atakuwa na fursa ya kufanya kazi na watu wa aina mbalimbali wenye vipaji vinavyotofautiana ili aweze kujifunza.

► Je, ajira za watoto zilizopo katika jamii yenu ni za hali gani? Je, wazazi wawe wakifanya nini? Je, kanisa liwe likifanya nini?

### **Makusudio ya Maendeleo ya Mtoto**

Wazazi wanalo jukumu la kukuza tabia ya mtoto wao. Wanandoa fulani wa Kikristo, Matt na Mariamu Friedeman, waliorodhesha sifa ambazo walitaka ziwasaidie watoto wao kustawi. Baada ya kutengeneza orodha hiyo, waliikagua na kutengeneza mipango kwa ajili ya hatua ambazo zingesaidia watoto wao kukua kupitia kwenye kila kipengele cha sifa hizi. Mchakato wenyewe haupaswi uwe wa haraka. Sifa hizi hazijitokezi kwa ghafla. Wazazi wanapaswa kuwa na makusudio na mwelekeo thabiti katika miaka yote ya kuwalea watoto wao. Orodha iliyoko hapa chini ni baadhi ya sifa zilizoorodheshwa na Friedemans.<sup>40</sup> Sifa nyingine zimeongezwa kwenye orodha hiyo.

---

<sup>40</sup> Matt Friedeman, *Discipleship in the Home*, (Wilmore: Francis Asbury Society, 2010), 31-33.

Aina	Sifa za kuwa nazo ifikapo umri wa miaka 18
Kiroho	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Kufahamu kwamba wao ni wabebaji wa sura ya Mungu pamoja na thamani ya umilele.</li> <li>• Kufahamu kwamba wao ni wenye dhambi wanaomhitaji Mwokozi.</li> <li>• Kuamua kujitoa kabisa kwa Kristo</li> <li>• Kuwa na maisha ya ibada kila siku</li> <li>• Kufanyia kazi karama za Kiroho</li> <li>• Kuwa tayari kwa ajili ya huduma ya Kikristo</li> <li>• Kubakia wasafi bila kujamiiana hadi wafikie ndoa</li> </ul>
Elimu ya Biblia	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Kuelewa mafundisho ya msingi ya imani za Kikristo</li> <li>• Kuweza kukariri maandiko muhimu (Aya 300)</li> <li>• Kujua hadithi za Biblia</li> <li>• Kujua vitabu vyote vilivyoko katika Biblia</li> <li>• Kujua Amri zote Kumi za Mungu na Hotuba ya Mlimani ya Yesu</li> <li>• Kutambua mada za Injili zinazohusiana na dhambi na wokovu katika Biblia nzima</li> </ul>
Mtazamo wa dunia wa Biblia	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Kufahamu jinsi ya kutetea imani yao</li> <li>• Kuwa na uwezo wa kujibu hoja kubwa za maisha kutoka katika mtazamo wa Kibiblia</li> <li>• Kufahamu ni nini kinachofanya Ukristo uwe wa kipekee miongoni mwa dini zote na madhehebu yote ya dunia</li> </ul>
Uwezo wa Kufikiri (Elimu)	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Kupata elimu ya Kikristo kama uwezekano utakuwepo</li> <li>• Kuanzishiwa nidhamu ya kusoma au kusikiliza podikasti au video za kufundishia</li> <li>• Kuhudhuria chuo cha Biblia au vituo vya mafunzo ya taaluma, kulingana na vipaji vyao na wito wao</li> </ul>

Tabia	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Kufanya mazoezi ya Kujidhibiti mwenyewe</li> <li>• Kuwa mnyenyekevu-na uwezo wa kuomba msamaha</li> <li>• Kuonyesha heshima kwa mamlaka zilizopo</li> <li>• Kuongea kwa wema</li> <li>• Kujifunza jinsi ya kuenenda na kutumia muda kwa busara—wao wenyewe kujiweka katika nidhamu ya matumizi ya vyombo vya habari vya kijamii, burudani na mengineyo</li> </ul>
Fedha na Huduma	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Kufahamu kuhusika kwa Mungu kwa ajili ya watu maskini</li> <li>• Kuwa wakarimu na kuwahudumia maskini</li> <li>• Kuwa watoaji wa mafungu ya kumi na kuweka akiba</li> <li>• Wajifunze jinsi ya kutumia bajeti ya fedha</li> </ul>
Mahusiano	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Kuonyesha upendo na kuambatana na ndugu</li> <li>• Kudhihirisha adabu ya kawaida katika mpangilio mzima wa kijamii</li> <li>• Kujifunza jinsi ya kuwa rafiki mwaminifu</li> <li>• Kuwa na uwezo wa kuzungumza na watu wazima kwa heshima na kujiamini</li> </ul>
Afya	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Kufanyia mazoezi tabia nzuri ya usafi</li> <li>• Kufanya mazoezi ya mwili ya mara kwa mara</li> <li>• Kula chakula chochote kinachopatikana kwa ajili yao</li> <li>• Kuchagua chakula kilicho bora kila inapowezekana</li> </ul>
Ujuzi	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Kuendeleza ujuzi na vipaji ambavyo Mungu amewapa</li> <li>• Kuendeleza ujuzi na vipaji vyao kupitia nidhamu ya mazoezi endelevu ya mara kwa mara</li> </ul>

Matt Friedeman alielezea kile walichokifanya yeye na mke wake baada ya kuwa wameorodhesha sifa hizi:

Mara tu baada ya kuwa na sifa hizo hapo juu kwenye karatasi yetu, tulichora mstari katikati ya karatasi na tukajiuliza wenyewe, "Sasa tunatakiwa tufanye nini [tufanye

sehemu yetu ya kuendeleza sifa hizi kwa watoto wetu]?” Kwenye upande wa kushoto wa karatasi, tuliandika hapo majukumu [yetu] ya wazazi.<sup>41</sup>

Ikiwa hili litaonekana kama ni jukumu kubwa, kumbuka tu kwamba Mungu ametupa sisi miaka ya 16-18 ya kufanya uanafunzi kwa ajili ya watoto wetu.

Ni muhimu:

1. Kutekeleza mapango wa mwanafunzi.
2. Kuanzisha ratiba za mazoea za kifamilia, kama vile kupata chakula au mlo wa kila siku na dakika chache za mafundisho/mafunzo yaliyopangwa.
3. Kufanya uanafunzi kama sehemu ya maisha ya kila siku, kwa kutumia fursa nyingi za mafundisho na mafunzo.
4. Kuendelea kuombea watoto wako kwa kutumia Neno la Mungu.
5. Usikate tamaa hata pale unapona umeshindwa.

► Chagua vipengele vichache kutoka kwenye jedwali lililopo hapo juu na uelezee ni nini ambacho wazazi wanaweza kufanya kwa makusudio ya kufikia malengo hayo.

### **Kipengele cha Mapenzi ya Mwanadamu.**

► Wakati mwingine mtu husema, “Matukio niliyokutana nayo yamenifanya kuwa aina ya mtu nilivyo sasa.” Kauli nyingine inayofanana na hiyo ni, “Mtu alivyo ni matokeo ya mazingira yake mwenyewe.” Je, hizi kauli zina ukweli?

Wanadamu wameumbwa kwa sura ya Mungu. Watu hufanya maamuzi ya uhakika na siyo ya kudhibitiwa na silika au mazingira. Katika maandiko yote Mungu amewaita watu kuchagua aidha kufanya mambo yaliyo mema na kukataa maovu.<sup>42</sup> Mungu huwahukumu watu kutokana na maamuzi yao.

Mazingira na uzoefu wetu wa mambo mbalimbali hutushawishi sisi, lakini havina uwezo wa kutudhibiti kwa sababu kama wanadamu tulio katika sura ya Mungu tunafanya maamuzi ya uhakika. Hiyo inamaanisha kwamba hatimaye mtoto anaweza kufanya maamuzi yake mwenyewe yanayotofautiana na ya nyumba na mazingira aliyolelewa. Mtoto aliyetoka katika nyumba ya upagani ambako maisha ya dhambi yalikuwa ni jambo la kawaida kwao anaweza akatubu na akaishi kwa ajili ya Mungu. Mtoto aliyetoka katika nyumba ya Kikristo anaweza akachagua kuishi kwa kutokumfuata Mungu.

Ingawa watu hufanya maamuzi ya uhakika, siyo kwamba wako huru kabisa. Biblia inatuambia kwamba tunazaliwa na asili ambayo ina mwelekeo wa kutenda dhambi (Zaburi 51:5, Zaburi 58:3). Wanadamu wana mwelekeo wa asili wa kupingana na mamlaka,

---

<sup>41</sup> Matt Friedeman, *Discipleship in the Home*, (Wilmore: Francis Asbury Society, 2010), 33.

<sup>42</sup> Yoshua 24:14-15, Ezekiel 33:10-11, Ufunuo 22:17



kuchagua mwelekeo wao wenyewe, kujiingiza kwenye majaribu, kudanganya watu wengine, na kuwa wabinafsi (Waefeso 2:1-3).

Watoto hutafuta kwa haraka njia za kutekeleza matamania yao binafsi hata kama itakuwa ni lazima wadanganye na kutotii ili kupata kile wanachokihitaji. Zaidi ya hapo, tunajua kwamba Shetani hujaribu kuwadanganya na kuwajaribu (Waefeso 2:2, Ufunuo 12:9).

Wazazi ni lazima watambue kwamba maelekezo pekee hayatoshi kumfanya mtoto afanye atende haki. Kuna mapambano ya kiroho (Wagalatia 5:17). Wazazi wanapaswa waombe ili Roho wa Mungu aweze kumshawishi na kumwongoza mtoto. Wazazi wanapaswa kumtegemea Mungu kwa ajili ya hekima na kwa ajili ya kupata nguvu ya kuwa mifano mizuri ya kiroho. Wazazi wanapaswa kuomba bila kukoma na au kwa bidii ili kwamba watoto wao waweze kutubu na kuweza kuzaliwa upya kiroho katika umri mdogo.

Hata kama mtoto ameokoka, mzazi hapaswi kutarajia kuwa mtoto wake atakuwa anafanana na Mkristo aliyekomaa. Tabia zake na hisia zake hazitakuwa sawa. Wakati mwingine anaweza akajiingiza kwenye majaribu. maadamu mtoto anaonyesha nia ya kutenda mambo mema, mzazi hapaswi kumkatisha tamaa kwa kumwambia kwamba anashindwa kuishi kama Mkristo. Badala yake, mzazi anapaswa kumpongeza mtoto kwa mambo yake mema anayofanya kama Mkristo na kumtia moyo wa kuomba kwa ajili ya kumsaidia katika mapambano yake.

Ingawa kila mwanadamu amezaliwa akiwa na mwelekeo wa kutenda dhambi, kila mwanadamu pia anamhitaji Mungu. Roho Mtakatifu huzungumza na kila mtu na kutoa matamania ya kuwa kwenye uhusiano na Mungu. Tunajua kwamba tunasaidiwa na Mungu tunapokuwa tunawafundisha watoto wetu Neno la Mungu. Roho wa Mungu ni kama wakili aliye ndani ya mtoto, akithibitisha kuhusu ukweli na kumpa matamania ya kuwa kwenye uhusiano na Mungu.

### **Muda wa Ibada wa Familia**

Familia zinapaswa kukutana kila siku kwa dakika chache kwa ajili ya usomaji wa Biblia, majadiliano, na maombi. Wazazi wote pamoja na watoto wote walioko kwenye nyumba wanatakiwa wahudhurie. Baba anapaswa kuongoza, lakini anaweza kuwataka wanafamilia kusoma maandiko na kushiriki kwa njia nyingine mbalimbali.

Muda wa ibada siyo lazima ufuata mtindo au utaratibu wa kila siku unaofanana. Muda huu unaweza kuwa na miundo mbalimbali ya ibada, na unaweza ukajumuisha kusoma hadithi za Biblia, hadithi za historia ya Kikristo na umisheni, kujadili maswali yaliyoulizwa, matumizi ya maswali ya kukariri, na majibu ya kufundisha kweli za mafundisho ya imani, kusoma Maandiko mbalimbali yanayohusiana na Ukristo nyimbo, kukariri Biblia, maigizo, na njia mbalimbali za kufanya maombi.

Mfano wa wakati wa shughuli ya ibada: Chagua hadithi ya Biblia na waambie wanafamilia waigize.

Wachungaji wanapaswa watumie sehemu ya muda wao kufundisha kanisa kuhusu muda wa ibada wa familia. Wazazi wanapaswa wakumbuke kwamba Mungu amewapa jukumu la kuwafundisha watoto wao Neno la Mungu (Kumbukumbu la Torati 6:5-7).

### **Kwa ajili ya Majadiliano ya Kikundi**

- Je, kuna dhana gani kutoka katika somo hili ambazo ni mpya kwako? Je, umejipangaje kuutumia ukweli uliujifunza?
- Je, kanisa linaweza kufanya nini ili kuimarisha familia na kuwasaidia wazazi katika kulea mtoto?
- Je, watu wa kanisa wanawezaje kufanya kazi kwa pamoja ili kusaidia katika changamoto ya kufundisha watoto ili wamfuate Kristo?
- Je, kuna baadhi gani ya mifano ya mazoea ya kila siku ambayo familia zinapaswa kufuata?

### **Maombi**

Baba wa Mbinguni,

Asante kwa kuunda familia na kuwapa watu upendeleo mkubwa wa kuwa wazazi.

Tusaidie kuwapenda watoto wetu kama wewe unavyofanya. Tusaidie kukumbuka daima kwamba wameumbwa kukujua na kukutumikia wewe.

Tupe upendo, subira na ufahamu tunaohitajiili kwamba tuwafundishe na kuwashawishi watoto wakufuate wewe.

Wawezeshe waumini ndani ya makanisa yetu kuweza kuwatayarisha familia, vijana, na watoto kuwa na nguvu katika imani na utii.

Ameni

## Kazi za Kufanya

(1) Soma kila moja ya kipengele cha Aya zinazofuata. Tumia aya hizi kuandika kurasa tatu kuhusu kile ambacho andiko linafundisha kuhusu wajibu wa wazazi:

- Mwanzo 18:17-19
- Kumbukumbu la Torati 6:4-9
- Zaburi 78:1-8
- Wakolosai 3:21
- Waefeso 6:4
- 1 Timotheo 3:4-5, 12
- 2 Timotheo 3:14-17
- Mathayo 18:5-6

(2) Aidha wewe ni mzazi au siyo, chagua sifa tano kutoka katika mojawapo ya malengo yaliyoorodheshwa katika jedwali lililotolewa katika somo hili. Andika njia tatu za vitendo zinazofaa za kuwasaidia watoto wako kufikia kila moja ya malengo matano ya sifa zilizochaguliwa.

(3) Kama wewe ni mzazi, andika mpango na ahadi yako ya kuwa na ibada za kila siku pamoja na watoto wako. Jiwajibishe mwenyewe kwa mtu mwingine kwa ajili ya mpango na ahadi ambayo umeifanya.



# Somo la 13

## Mambo Yanayohusu Kulea Mtoto

### Malengo ya Somo

Hadi kufikia mwishoni mwa somo hili, mwanafunzi atapaswa:

- (1) Apate mtazamo wa Mungu kuhusu nidhamu na usahihishaji wa watoto.
- (2) Ajitolee kutengeneza mazingira mazuri ya nyumbani kwa ajili ya kufanya uanafunzi kwa watoto.
- (3) Kuelewa wajibu wa mtoto kwa Mungu.
- (4) Ajazwe na mawazo ya vitendo kwa ajili ya hali za kila siku za malezi.

### Susanna Wesley, Mama Mwenye Kusudi

Susanna Wesley alizaa jumla ya watoto 19, lakini kutoka na hali za nyakati zile, watoto tisa (9) hawakuweza kuishi kwa muda refu wakifariki dunia. Watoto kumi (10) aliowalea ni pamoja na Yohana na Charles Wesley. Mtoto wake Yohana, baada ya kuwa mtu mzima, alimsihi mama yake amwandikie maelezo kuhusiana na mbinu zake za kulea watoto, na mama akamtumia barua yenye maelezo haya.<sup>43</sup>

Watoto walikuwa wamefundishwa kuhusu Sala ya Bwana mara tu walipoanza kuongea, na walikuwa wakiirudia kila siku asubuhi na jioni. Watoto walikuwa wakisoma sura moja ya maandiko kwa pamoja kila siku. Nyakati hizo wanawake wengi walikuwa na elimu duni, lakini Susanna alisisitiza kwamba watoto wake wote wanapaswa wafundishwe kusoma. Alipa kipaumbele ufahamu wa kusoma na kuandika kuliko kujifunza kazi.

Susanna alisema, "Ubinafsi ndio shina la dhambi na taabu zote." Aliwafundisha watoto wake jinsi ya kudhibiti misukumo yao na kujikabidhi kwa mamlaka halali. Alisema kwamba kila kitendo cha utii kinapaswa kupongezwa hata kama hakikufanyika vizuri au kwa ukamilifu. Makosa yanaweza kuvumiliwa, lakini kila uasi wa kukusudia unapaswa kuadhibiwa.

Siku zote familia walikula chakula wakiwa pamoja, na watoto walijifunza kula chochote ambacho kilitolewa bila ya kuwepo na manukuniko.

### Masahihisho na Nidhamu

Biblia inatuambia kwamba, "Ujinga umefungwa ndani ya moyo wa mtoto..." (Mithali 22:15). Mtunga Zaburi anasema kwamba watoto huzaliwa wakiwa wanasema uongo, "...Tangu

---

<sup>43</sup> Eliza Clark, *Susanna Wesley*, (London: W. H. Allen & Co, 1886), 30-36. Kinapatikana: <https://archive.org/details/susannawesley00clariala/page/30/>.

tumboni wamepotea, wakisema uongo.” (Zaburi 58:3). Kwa kuwa jambo hili ni la kweli wazazi wana wajibu wa kusahihisha watoto wao.

Ikiwa ungempa mtoto wa miaka mitatu chaguo kati ya kuwa na bakuli la aiskrimu hivi sasa au kumiliki kiwanda cha aiskrimu mwaka mmoja ujao, angechagua kuwa na aiskrimu sasa. Hata kama mzazi ataelezea uchaguzi mwingine, mtoto angechagua aiskrimu sasa ikiwa angefanya uamuzi wake mwenyewe. Mfano huo unatuonyesha kwamba maelezo peke yake hayatoshi kumrekebisha mtoto.

Maelezo kuhusu mema na mabaya hayatoshi kumsahihisha/kumrekebisha mtoto, kwa sababu:

1. Mtoto hawezi kuelewa mawazo ya mtu mzima (1 Wakorintho 13:11).
2. Mtoto hawezi kuona matokeo kamili na ya muda mrefu kuhusiana na matendo yake.
3. Mtoto hajakomaa vya kutosha kuweza kudhibiti misukumo na matamania yake kwa kufikiri.

Labda itaonekana ni ukatili kuleta maumivu ya kimwili kwa mtoto, lakini baba anayewapenda watoto wake atafanya hivyo ili kuzuia madhara mabaya zaidi: “Yeye asiyetumia fimbo yake humchukia mwanawe; Bali yeye ampendaye humrudi mapema.” (Mithali 13:24). Kwa mfano, mtoto mdogo anayecheza karibu na moto anaweza akaanguka ndani yake na kusababisha kupata majeraha makubwa kwa sababu haelewi madhara ya moto. Lakini ikiwa mama yake atamrudi kwa kumchapa fimbo anaposogea kutaka kuwa karibu sana moto, yale maumivu madogo ya kuchapwa fimbo yatazuia kutokea kwa maumivu makubwa yatakayotokana na moto.

Baadhi ya watu wengine wamenyanyaswa kimwili na watu wengine ambao wasiowapenda. Uzoefu wao unawafanya wachukie wazo la mtu yeyote kumwadhibu mtoto kimwili. Hata hivyo, mzazi anayepuuza kumsahihisha mtoto ipasavyo husababisha matatizo mengi kwa mtoto wake baadaye.

► Wanafunzi wanapaswa wasome Mithali 19:18 na Mithali 29:17 kwa ajili ya kikundi.

Masahihisho kwa mtoto yanapaswa yaanze wakati ana umri wa kutosha kuweza kuelewa kwamba anapingana na wazazi wake. Hata yule mtoto sana huwa anajua anachokifanya wakati anapokataa kuonyesha ushirikiano na mzazi.

Masahihisho mengi kwa mtoto ni lazima yafanyike wakati mtoto akiwa ni mdogo na mwepesi wa kuweza kuumia (Mithali 22:15). Kama vile udongo unavyozidi kuwa mgumu kadri muda unavyopita na kuwa vigumu kuweza kuufinyanga katika umbo unalolitaka, ndivyo tabia ya mtoto inavyokuwa ngumu zaidi kuitengeneza kadri muda unavyozidi kupita. Kama mtoto anaendelea kutotii wazazi wake baada ya umri wa miaka kumi (10), wazazi wanakuwa hawajafanikiwa kwenye masahihisho ya mtoto wao, na fursa zao za kufaulu kumsaidia kwa ukamilifu zinazidi kufifia. Masahihisho ya kimwili nayo huwa hafifu na yasiyotosha kadri mtoto anavyoendelea kukua. Ni makosa kwa mzazi kufikiria kwamba masahihisho kwa

mtoto yatakuwa marahisi zaidi wakati atakapokuwa amekua katika umri mkubwa, itakuwa ni vigumu zaidi na hatimaye itakuwa haiwezekani tena kabisa.

Kadri mtoto anavyosogelea utu uzima, inakuwa haiwezekani tena kumsahihisha kimwili kama wakati alivyokuwa mtoto. Kijana wa kiume au wa kike anahitaji heshima hata kama tabia zao hazijakomaa. Mzazi anaweza akatumia njia nyingine za kufanya masahihisho kama vile kupunguza muda wa burudani kwa mtoto, au muda wa matumizi ya simu au shughuli za kijamii, lakini mawasiliano ya upendo na yaliyo makini yatakuwa ni ya muhimu zaidi. Ni lazima mzazi atambue kwamba kijana anafanya maamuzi ya kweli, na ingawa mzazi ana ushawishi wake, hawezi kumzuia kijana asitumie mapenzi yake binafsi na kupata matokeo ya maamuzi.

Baadhi ya wazazi hawana uhakika wa jinsi ambavyo wanapaswa kuwa wakali wakati wa kutoa adhabu ya kimwili kwa mtoto. Kama mtoto atakuwa bado ni mwenye hasira na mwenye kuendelea kuasi baada ya masahihisho, adhabu itakuwa haikuwa nzito ya kutosha kumwadhibu (kanuni hii haiwezi kutumika kwa mtoto ambaye ni mkubwa sana kiasi kwamba hawezi kurekebisha kwa njia ya adhabu ya kimwili kwa ufanisi). Masahihisho yanapaswa yawe makali sana ili kumfanya mtoto ajutie kutotii kwake na achague kutii mamlaka. Masahihisho hayapaswi yasababisha madhara ya kimwili. Masahihisho ambayo husababisha michubuko au kuweka alama zinazobakia kwa muda mrefu kwenye ngozi ya mwili inaweza ikawa ilikuwa ni kali sana kupita kiasi.

Biblia inatumia mfano wa adhabu ya kimwili kuelezea njia ambayo Mungu hushughulika na watoto wake.

► Wanafunzi wanapaswa wasome Mithali 3:11-12 na Waebrania 12:5-8 kwa ajili ya kikundi.

Vifungu hivi vya maandiko vinatuambia kwamba Mungu huwaadibisha watoto wake kwa sababu anawapenda. Vivyo hivyo, Baba humuadhibu mtoto wake kwa sababu anampenda. Kuadhibiwa kiukamilifu ni ishara ya upendo. Kukosekana kwa nidhamu ni ukosefu wa upendo.

Marekebisho ya kimwili humfundisha mtoto kujidhibiti yeye mwenyewe kwa sababu hujifunza jinsi ya kujizuia na vishawishi, kwa sababu anajua kwamba atakutana na adhabu kama akitenda makosa. Anapokuwa anapinga vishawishi vya kutenda maovu, anajenga tabia yenye nguvu. Anapokuwa mtu mzima atakuwa na uwezo wa kujizuia na majaribu kwa sababu ana uelewa wa madhara na au matokeo yake na siyo kwa sababu ya adhabu ya kimwili. Hata hivyo, mtoto ambaye hapatiwi masahihisho ya mara kwa mara anakuja kuwa mtu mzima ambaye ni mdhaifu sana kuweza kuzuia majaribu hata wakati anapotambua kwamba ni mabaya kwake.

Jaribu kufikiria mzazi anayempa mtoto wake peremende tu za kula kwa sababu mtoto anataka. Hataki kumfanya mtoto asiwe na furaha, lakini anafanya jambo litakalotea madhara kwa mtoto. Vivyo hivyo, mzazi anayekubaliana na au anayetetea tabia mbaya ya mtoto wake kila wakati anafanya uharibifu mkubwa kwenye tabia ya huyo mtoto na kwenye

hali yake ya baadaye. Hata hivyo Biblia inasema kwamba mzazi asiyetumia fimbo yake kumsahihisha mtoto wake anamchukia (Mithali 13:24).

Mtoto anayeishi katika nyumba isiyo na mipaka hana furaha. Mipaka huleta usalama Ikiwa mtoto anajifunza kwamba huwa anapata kitu anachokitaka kwa kugombana na kupandishiana hasira, atakuwa anafanya hivyo kila wakati, lakini hatafurahi. Watoto wanakuwa na furaha wanapojiona wako kwenye usalama na wanaongozwa chini ya misingi yenye mipaka, bila kuhisi kwamba ni lazima wapigane na kukataa udhibiti ili kuwa na chochote. Mtoto asiye na nidhamu huwa na furaha mara chache.

Wakati mtoto mdogo anapofikia kuwa mtu mzima, dunia haitaweza kumpatia chochote atakachokihitaji. Hataheshimiwa na kukuzwa ikiwa hana adabu, ni mtu mbinafsi, na asiyewajibika. Mzazi anapaswa kumlea mtoto wake katika njia ambayo itamtayarisha kwa ajili ya maisha. Wazazi ni lazima wakumbuke kwamba hawalei watoto wadogo; bali wanalea watu wazima.

Mzazi anapaswa kueleza na kuonyesha kwamba kumsahihisha mtoto wake ni kwa kusudi la kumsaidia mtoto asitawi na kuwa mtu wa tabia nzuri anayeweza kutegemewa na kuheshimiwa.

► Wanafunzi wanapaswa wasome Mithali 22:15, Mithali 23:13-14, na Mithali 29:15 kwa ajili ya kikundi.

Kumbuka kwamba kusudi la kufanya masahihisho ni kumkuza mtoto. Mtoto anapokuwa ameelewa kosa alilolifanya na tayari akaonyesha kujuta, masahihisho ya kimwili hayawi ya lazima tena. Kusudi kubwa ni masahihisho, na siyo kumhukumu; mzazi hana hitaji tena la kuhakikisha kwamba mtoto wake anapata adhabu inayostahili.

► Je, marekebisho ya mzazi yana tofauti gani na matendo ya mtu anayedhulumu na kusababisha madhara ya kimwili ili kuwafanya watu wafanye anachotaka?

Mtu mjeuri yuko tayari kuwadhuru watu wengine ili kupata kile anachotaka. Mzazi anampenda mtoto wake. Masahihisho ya kimwili ni kwa manufaa ya mtoto. Mzazi mwenye upendo hatataka amduru mtoto wake. Mtu hawezi kuhisi kwamba mnyanyasaji au mkandamizaji anampenda, lakini mtoto anaweza kujua kwamba anapendwa hata anaporekebishwa. Anaweza akatambua kwamba anapendwa hata katika wakati ambao amefanyiwa masahihisho. Anaweza akatambua kwamba maisha kwake ni mazuri zaidi kutokana na mamlaka ya wazazi wake.

Baadhi ya wazazi huadhibu kwa ukali sana na kwa mambo yasiyokuwa sawa kwa sababu ya hasira au ukatili. Wanamduru mtoto wao kimwili na kimhemuko. Wanawaadhibu watoto wao kama njia ya kuwaondolea mfadhaiko au kuchanganyikiwa na maisha. Hili ni tatizo kubwa ambalo halipaswi kuendelea kuvumiliwa na watu wengine wanaoliona. Marafiki, majirani, na jamaa wa ukoo wanapaswa kukabiliana na mtu anayemdulumu mtoto. Mwenzi wa mzazi anayemnyanyasa mtoto anatakiwa atafute msaada kutoka kwa jamaa wa ukoo, marafiki au mchungaji. Ni jambo la muhimu sana kumlinda mtoto.



► Baadhi ya wazazi huwadhalilisha watoto wao hadharani wanapokuwa wamefanya makosa. Je, hii ni njia nzuri ya kufanya masahihisho?

► Mwanafunzi anapaswa asome Waefeso 6:4 kwa ajili ya kikundi.

Mtoto anahitaji kuwa na uhakika kwamba wazazi wake wanampenda na kwamba masahihisho yeyote yanayofanywa ni kwa ajili ya manufaa yake. Wakati mtoto anapokuwa amenyanyaswa na wazazi wake, hujisikia kutopendwa. Anaweza kuwa na uchungu na kujihisi kwamba mamlaka ya wazazi wake ni jambo baya sana analohitaji aliepuke. Wazazi wanapaswa kuwarekebisha watoto wao faraghani na kuepuka kuwaadibisha watoto wao mbele ya kadamnasi ya watu. Wazazi wanapaswa wawaelekeze na kuwasahihisha watoto wao kwa upole na uvumilivu.<sup>44</sup> Kwenye Mithali 16:21b tunaambiwa kwamba "...Utamu wa maneno huongeza elimu."

► Jaribu kufikiria kwamba ulimwambia mtoto wako akusaidie kulisha wanyama wako. Uliporudi nyumbani jioni ukakuta kwamba bado wanyama hawakulishwa. Umechoka kwa kufanya kazi siku nzima, lakini sasa ni lazima ulishe wanyama kabla hujaanza kupumzika kwa sababu mtoto wako hakutaka kukutii wewe. Je, utashikwa na hasira? Je, ni kosa kwa mzazi kuwa na hasira dhidi ya mtoto wake?

Mzazi anapaswa akumbuke kwamba kusahihisha kunapaswa kumnufaisha mtoto. Mzazi anapokasirika kwa sababu anajisikia kutoheshimika au kwa sababu ya mtoto kutomtii kunamsababishia usumbufu na au maudhi, anakuwa na hasira isiyoweza kufanya jambo lolote jema (Yakobo 1:20). Hasira yake ni ya ubinafsi.

Mzazi anaweza kudhihirisha hasira yake ifaayo kwa mtoto kwa njia hii: "Mwanangu, hukuwalisha wanyama wangu kama nilivyokuwa nimekuagiza. Wanyama walikuwa na njaa, na wangeendelea kuwa na njaa hata usiku kama siyo mimi kuchukua hatua ya kuwalisha. Ilibidi niamue kuwalisha ingawaje nilikuwa nimechoka sana kwa kazi za siku nzima. Nina hasira kwa sababu sitaki uwe mtu unayepuuzia mahitaji ya watu wengine kwa ajili ya wewe kutotimiza wajibu wako. Katika Mithali 12:10 tunafundishwa kwamba, 'Mwenye haki huufikiri uhai wa mnyama wake; Bali huruma za mtu mwovu ni ukatili.'"

Rebeka aliwaambia watoto wake wasichukue chakula au kinywaji kwenye chumba ambacho kilikuwa na zulia jipya sakafuni. Siku iliyofuata aliona mmoja wa watoto akila chakula kwenye lile zulia, akamkemea. Baadaye tena mmoja wa watoto wake alitembea kwenye zulia akiwa amebeba bilauri ya juisi na akamkemea. Katika siku chache nyingine zilizofuata wakati mwingine watoto walikuwa wanachukua vinywaji ndani ya kile chumba, lakini Rebeka akawa katika shughuli zake nyingi na akashindwa kuwasahihisha wale watoto. Siku moja kijana wake alimwaga Coca-Cola kwenye lile zulia. Rebeka alikasirika na kumpiga.

---

<sup>44</sup> Ingawaje katika 2 Timotheo 2:24-25 na Wagalatia 6:1 ziliandikwa kwa ajili ya kushughulika na dhambi ndani ya kanisa, maelekezo kuhusu kudhihirisha uvumilivu na upole wakati wa kufanya masahihisho kwa wale ambao wamekosa zinahusika pia kwenye muktadha wa malezi ya wazazi kwa watoto.

► Je, kuna shida gani kwenye njia ambayo Rebeka alikuwa anaitumia katika kuwasahihisha watoto wake?

Sheria ya Rebeka ilikuwa ni kwamba watoto walipaswa wasipeleke vyakula au vinywaji kwenye chumba kilichokuwa na zulia, lakini baadaye akawavumilia wakati wakiwa wanavunja sheria yake hadi wakati ilipotokea ajali. Aliadhibu ajali badala ya uvunjaji wa sheria. Hali hii ni fundisho kwa watoto kwamba walikuwa na uwezo wa kuvunja sheria ali mradi wajizuie na kusababisha ajali au matukio mabaya. Wazo hili linakuza tabia mbaya kwa sababu ndio msingi mkuu wa uvunjaji wote wa sheria. Mtu anavunja sheria kwa sababu anafikiri kwamba anaweza kupata matokeo anayoyataka yeye wakati huo akijizua na matokeo mabaya. Wazazi wanapaswa wasahihisha ukosefu wa utii kuliko kutoa adhabu kwa watoto kwa ajili ya kufanya ajali.

Michaeli aliwaambia watoto wake kufungia baiskeli zao ndani kila ifikapo jioni. Kila siku katika wiki, wakati Michaeli alipokuwa akirejea nyumbani, baiskeli zilikuwa bado ziko nje hazijafungiwa ndani. Kisha siku moja Michaeli akiwa kazini alipoteza chombo kimojawapo cha kufanyia kazi zake, na kwa bahati mbaya alikuwa amejumiza kidole chake, na akawa na pancha ya tairi katika gari lake wakati akiwa anarejea nyumbani. Wakati alipofika nyumbani alikuta bado baiskeli hazijafungiwa ndani, na akachukua hatua ya kuwaadhibu vijana wake.

► Je, kuna shida gani kwenye njia ambayo Michaeli alikuwa anaitumia katika kuwasahihisha vijana wake?

Wazazi wengi wana tabia ya kuvumilia uvunjifu wa utiifu wakati wanapokuwa katika hali nzuri na kuadhibu uvunjifu wa utiifu wanapokuwa kwenye mazingira magumu ya kimaisha. Watoto hawajifunzi kutii isipokuwa pale wazazi watakapokuwa wakiwasahihisha mara kwa mara.

► Angalia vipengele vifuatavyo na elezea ni kwa nini kila kimoja ni muhimu. Je ni nini kinachotokea endapo mzazi hataweza kufuata maelekezo haya?

- Mahitaji yanapaswa yaendanae na uwezo na ukomavu wa mtoto.
- Adhibu tu jambo lililofanyika kwa kutotii, lakini siyo kwa jambo lililofanyika kwa bahati mbaya.
- Sheria na mahitaji yanapaswa yawe wazi na yenye kueleweka.
- Wakati mtoto anapokosa kuwa mtiifu, mzazi anapaswa kueleza ni nini ambacho mtoto alipaswa kufanya.
- Kamwe usimwadhibu mtoto kwa kitu ambacho hakikuwa chini ya udhibiti wake.

### **Maelekezo ya Vitendo Kutoka kwa Watoto**

Miaka kadhaa iliyopita, mwanasaikolojia wa Uingereza, Dr. R.F. Hertz, alifanya mradi wa utafiti. Aliwauliza watoto 100,000 waliokuwa na umri kati ya miaka 8 na 14 kutoka katika

nchi 24 ili kupata orodha ya sheria kwa ajili ya wazazi. Utafiti huu hauna mamlaka ya Neno la Mungu, lakini angalao unatuonyesha sisi baadhi ya mahitaji ambayo watoto wanahitaji.

Hapa kuna baadhi ya majibu ambayo ni ya kawaida sana:

- Usigombane mbele ya watoto wako.
- Usiseme uongo kwa mtoto.
- Siku zote jibu maswali kutoka kwa watoto wako.
- Watendee watoto wako kwa uwiano unaolingana.
- Ni lazima kuwepo na [urafiki] kati ya wazazi na watoto.
- Watendee marafiki wa watoto wako kama wageni waalikwa.
- Usipende kuwalaumu na kuwagombeza na au kuwaadhibu watoto wako mbele ya marafiki zao.
- Jikite katika vipengele vizuri kutoka kwa watoto wako na usitake kuweka mkazo sana kwenye mambo aliyoshindwa.
- Kuwa thabiti na imara katika hali yako ya upendo na hisia zako.

Mzazi mmoja anapomchambua mwenzake kila mara mbele ya watoto, watoto wanaweza kujidhanja kwamba hata wao wanapaswa kutokukubaliana na kuona makosa ya mzazi asiyeheshimiwa.<sup>45</sup> Wazazi wanapaswa kujadili kutokukubaliana kwao kwa baadhi ya mambo wakiwa peke yao faraghani na kutengeneza sera ambazo wataweza kuzifuata kwa ushirikiano.

Wazazi hawapaswi kusema uongo kwa mtoto wao (Wakolosai 3:9), hata kumpa sababu za kushirikiana au kumwondolea wasiwasi. Mtoto anapotambua kwamba mzazi wake anamdanganya, hajisikii salama tena. Baadhi ya wazazi hawana uwezo wa kuwafariji au kuwaelekeza watoto wao wanapokuwa na mashaka kwa sababu unakuta watoto hawaamini yale yanayosemwa na wazazi wao.

► Chagua mojawapo ya vipengele vilivyoorodheshwa hapo juu kisha elezea matatizo yanayojitokeza endapo mzazi hatafuata mwelekeo huo.

### **Nyumbani kwa Mkristo**

► Anapokuja mgeni nyumbani kwako, je, anaona kwa mara moja kwamba ni nyumba ambayo Wakristo wanaishi? Kwa namna gani?

► Mwanafunzi anapaswa asome Kumbukumbu la Torati 6:6-9 kwa ajili ya kikundi.

---

<sup>45</sup> Maelekezo na kanuni kutoka katika Waefeso 4:29-32, Waefeso 5:33; 1 Petro 3:7-12 zote zinatumika hapa.

Waisraeli walipaswa kuzingatia kuchagiza maisha yajayo kwa kuunda tabia ya watoto. Wangefanyeje? Walipaswa kuwa na mazingira yaliyolindwa kwa ajili ya mafunzo ya watoto wao kwa mujibu wa kanuni za kibiblia. Walikuwa wabandike Maandiko kila mahali (wayaandike juu ya miimo ya milango ya nyumba zao na juu ya malango yao.) Siyo tu kwamba Maandiko yanapaswa yabandikwe kuhalisi nyumbani, lakini muhimu zaidi, kila kitu nyumbani kilipaswa kuendana na Maandiko.

Familia hizi hazikupaswa kuweka Amri Kumi za Mungu kwenye ukuta mmoja na picha nyingine ya mtenda dhambi kwenye ukuta mwingine. Hali hiyo ingekuwa inachanganya sana ufahamu wa watoto kuhusiana na maadili.

Watoto huathiriwa sana na mambo wanayoyaona na kuyasikia kila siku. Kama kituo cha radio kinaweza kusikika kikipiga muziki nyumbani kwao kila siku, wao watachukua baadhi ya falsafa ambazo msingi wake ni ule muziki.

Haiwezekani kwa wazazi kuwakingia watoto na kila falsafa mbovu au ushawishi wa kidunia, lakini wazazi wa Kikristo ni lazima wawafundishe watoto wao kufanya tathmini ya kila kitu wanachosikia na kuona ambacho kinakuja kwao kupitia Neno la Mungu. Yesu aliomba kwamba, "Mimi siombi kwamba uwatoe katika ulimwengu; bali uwalinde na yule mwovu... Uwatakase kwa ile kweli; neno lako ndiyo kweli (Yohana 17:15, 17).

Watoto hugundua ni nani wazazi wao wanamvutia kama shujaa wao. Wanajua ni nani wazazi wao wanamheshimu. Ni jambo lisilokubalika kwa mzazi kuwafundisha watoto wake kuhusu ukweli wakati yeye mwenyewe anashikamana na kupendezwa na watu wa kidunia wasiokuwa na maadili. Mzazi anayefanya hivyo ni kama kumjulisha mtoto wake kwamba angefurahi zaidi awe mwanamuziki wa kidunia mwenye mafanikio kuliko kuwa Mkristo mwaminifu.

Baadhi ya wazazi hufikiri ni jambo lililo sawa kuruhusu mtoto wao ajiingize kwenye mambo ya dhambi kama watakuwa wamemweleza huyo mtoto kwamba ni kwa nini hayo mambo ni mabaya. Hebu fikiria kuhusu hili: Kama ulikuwa unajaribu kumfanya mtoto wako ale chakula kilicho kizuri, hutapenda kuweka lundo la peremende na keki mbele yake, na kisha ujaribu kumweleza ni kwa nini anapaswa ale mboga za majani. Maelezo yote kuhusiana na vitamini hayataweza kushinda matamania yake ya asili ambayo yanachochea ale peremende zilizoko mbele ya macho yake.

Baadhi ya wazazi huruhusu televisheni zao kuwa wazi muda wote bila hata ya kuonyesha kuwa wasiwasi na kuhusika na kile ambacho watoto wao wanaangalia. Wakristo wanapaswa wakumbuke kwamba jamii inafundisha kwamba dhambi ni jambo la kawaida lisilokuwa na shida mradi tu matokeo yake yadhibitiwe. Televisheni huonyesha watu wanaoishi kwa dhambi na hawajapatwa na matukio yeyote, lakini hayo siyo maelezo ya kweli ya maisha halisi. Televisheni humfanya mtoto aone kwamba wazazi wake wanamzuia yeye kutofurahia maisha, na atangojea muda ambao anaweza kufanya vile anavyotaka yeye mwenyewe.

Wakristo wengi wanaishi kwenye nyumba zao pamoja na ndugu ambao siyo Wakristo. Kwenye hali kama hizo, nyumba siyo mazingira ambayo yamelindwa dhidi ya kuvutia mambo mabaya. Ni muhimu kwa mzazi Mkristo kuweka mfano wa upendo, uaminifu, usafi, na furaha, huku akiomba kwamba Roho Mtakatifu amsaidie mtoto katika kuweza kuchagua mwelekeo sahihi wa maisha.

### **Familia zisizo kamilifu**

Kwa kuwa familia hazijakamilika, mahusiano mara nyingi huwa yanakuwa na historia ya makosa mengi yaliyopita na migogoro ambayo haijatatulika.

Hata wazazi wa Kikristo hawajakamilika. Huenda zisiwe thabiti kila wakati katika kutengeneza na kutekeleza sheria zake. Hawaelewi kila wakati kuhusu hali ya kijana wao – mambo yamebadilika kwenye kizazi kipya. Kila wakati hawawezi kuwa na huruma ya kutosha kwa ajili ya maswala halisi yanayohusiana na mtoto wao. Siyo mara zote huwa na msimamo ulio bora na wanaweza wakasema maneno yenye kuumiza.

Mungu aliumba watu wa kwanza na kuunda familia. Alimfanya mwanamume, akamfanyia na mke, na akawapa watoto wa kuwalea. Mungu anajua kila kitu. Mungu alijua kwamba wazazi watangefanya makosa lakini bado aliunda uzazi. Aliona kuwa hiyo ndiyo ilikuwa njia bora zaidi, pamoja na kasoro zote ambazo wanadamu wanazo. Hii inamaanisha kwamba ni lazima kuwepo na njia ambayo itaifanya familia ifanikiwe. Kuna faida nyingi za mfumo wa familia hata wakati ambapo inaonekana siyo kamilifu.

Ukweli kwamba Mungu alianzisha kuwepo na uzazi ni muhimu kwa ajili ya watoto. Hali hii inamaanisha kwamba wakati watoto wanapoasi wanakuwa wameamua kutokukubaliana na mfumo ambao Mungu ameuweka. Mungu alisema, "Enyi watoto, watiini wazazi wenu ..." (Waefeso 6:1). Wazazi huwa waasi dhidi ya mfumo wa Mungu aliouweka wakati wanapopuuzia kutimiza majukumu ambayo Mungu ameyaweka juu yao. Kuukata mpango wa Mungu ni kuasi dhidi ya Mungu.

### **Jukumu katika Kumlea Mtoto**

Katika hali hii ya kuwa mzazi, kuna maeneo matatu (3) ya kuwajibika: Mtoto analo eneo lake la kuwajibika. Mzazi analo eneo lake la kuwajibika. Mungu analo eneo lake la kuwajibika.

Tayari tumeshaangalia kwa kina eneo la uwajibikaji la mzazi katika haya masomo mawili yaliyotangulia. Kwa sasa tutazingatia uhusika wa Mungu kwenye maisha ya watoto na majukumu ya watoto.

### **Kazi ya Mungu kwenye Maisha ya Watoto**

1. Mungu anataka watoto wawe na uhusiano wa kibinafsi na yeye kupitia imani iliyo katika Yesu Kristo. (Soma Mathayo 18:1-6 na Mathayo 19:13-15.)

2. Mungu ni mwaminifu kuwavuta watoto wetu kwenye uhusiano huu pamoja naye. (Soma Yohana 6:44.)
3. Mungu huzungumza na watoto wetu kupitia Neno lake. (Soma 2 Timotheo 3:14-15.)

### **Watoto katika Mahusiano na Mungu**

1. Watoto wanaweza wakasamehewa dhambi zao. (1 Yohana 2:12).
2. Watoto wanaweza wakamjua Mungu (1 Yohana 2:13).
3. Watoto wanaweza wakakua kwenye mahusiano na Mungu (1 Samweli 2:26).
4. Watoto wanaweza kumwabudu Mungu (Mathayo 21:15-16).
5. Watoto na Vijana wanaweza wakatumiwa na Mungu (Yoeli 2:28).

Katika Maandiko kuna mifano mingi ya watoto na vijana wanaotumiwa na Mungu katika kufanikisha makusudi yake: Samweli, Mtumishi wa kike wa mke wa Naamani, kijana aliyetumiwa na Yesu kulisha makutano, Daniel, Yusufu, Daudi, na Mariamu, kwa kutaja tu wachache.

### **Jukumu la Mtoto**

Jukumu la mtoto, kwa mujibu wa Neno la Mungu, ni kuwatii wazazi wake (Waefeso 6:1-3). Je, itakuwaje kama wakati mwingine mzazi anafanya makosa? Mtoto ni lazima atimize jukumu lake na siyo kuliweka jukumu lake katika masharti ya jinsi mzazi anavyofanya. Hilo siyo jukumu la mtoto. Jukumu lake ni kutii.

Kama mtoto ataamua tu kutii wakati anapofikiri kwamba mzazi yuko sahihi, mzazi hataweza kuwa na mamlaka. Hilo haliwezi likawa lile ambalo Mungu alikusudia, kwa sababu hilo litaharibu kabisa mfumo mzima wa malezi.

Siyo jukumu la mtoto kuwajibika na jinsi ambavyo mzazi anatumia mamlaka yake. Eneo lake la uwajibikaji ni kwenye kutii. Je, itakuwaje kama mzazi atamwambia mtoto kwamba afanye jambo lisilofaa, kama vile akamletee kinywaji cha bia kwenye jokofu? Mtoto hapaswi kuwa na jukumu la kuamua kama mzazi yuko sahihi au laa. Anaweza kutoa maoni yake kuhusiana na jambo hili kwa hekima na au heshima lakini ni lazima akubali kutii.

Mambo kinzani kwenye jukumu la kutii ambayo yanaweza kuleta madhara kwenye unyanyasaji wa kimwili au matendo ya uovu yanapaswa kutolewa taarifa kwa mamlaka ambazo zina majukumu ya kuwalinda watoto. Matatizo ambayo watoto huwa nayo kwa wazazi wao kwa kawaida siyo kwa sababu wanauliza kama maagizo hayo yanaenda sawasawa na kanuni za Kikristo. Mtoto aliye muasi kwa kawaida hukinzana na wazazi wake katika mambo ya kawaida, kama vile kufanya usafi wa chumba chake, kufanya kazi za nyumbani, kuwepo nyumbani kwa nyakati fulani, na vizuizi kwenye mambo mengine ya burudani zake.

Mtoto anayeasi hupingana na dhana ya mamlaka ya mzazi kwa kudai haki ya kuamua wakati akitaka kuona kwamba amri za mzazi wake ni mbaya. Upinzani wake unatokana na matamano ya msingi ya kupewa uhuru. kujitawala, kuwa na mamlaka binafsi, na uwezo

wa kujiamulia atakavyo. Je, ni katika umri gani mtu anapatiwa mambo hayo? Kamwe hapana, na sivyo.

Dhana ya uhuru wa aina hii ni kama njozi. Daima utakuwa na majukumu yanayotokana na kuwafikiria watu wengine, Wakati wote kutakuwepo na kazi ambazo unajua binafsi kwamba unapaswa uzifanye, hata kama mama yako hayuko pale kukuambia uzifanye. Mtu anayesisitiza kuishi bila ya kuwajibika kwa watu wengine huwa anaacha mabaki ya maumivu na uharibifu, akiumiza mtu yeyote anayemwamini na anayemtegemea yeye.

Wakati mwingine watoto huchukizwa na mahangaiko ya wazazi wao, wakihihi kwamba wazazi wanapaswa wawaamini wao zaidi. Ikiwa mtoto anaweza kujaribu kuelewa na kuheshimu mahangaiko ya wazazi, mzazi anaweza kumwamini mtoto huyo zaidi na kuwa kurekebisha viziwi vyake. Wakati mtoto anapokataa kuona mahangaiko ya mzazi wake, wazazi hujihihi kwamba kuna hitaji la kumwekea viziwi zaidi.

### **Kukiri Makosa**

Watu wengi wanaogopa kukiri kosa wawapo kwenye uhusiano kwa sababu Wanahofia kwamba ukiri huo unaweza kuwadhoofisha kwenye migogoro mingine ya baadaye. Kiuhalisia, nafasi ya kuwa mwaminifu na utayari wa kufanya jambo ambalo ni la haki ni nafasi kubwa ya kutaka mtu awepo. Njia pekee ya kuwepo kwenye nafasi hiyo na kukaa ndani yake ni kukiri makosa yako uliyoyafanya na kuanza kutenda yaliyo mema, na pia kuwa tayari kusahihishwa wakati wowote unapokuwa na makosa.

Wakati mwingine mtu aliyeko kwenye mamlaka huwataka watu walioko chini yake kukiri makosa yao lakini yeye hayuko tayari kukiri makosa yake mwenyewe kwa sababu anafikiri kufanya hivyo kutamshushia hadhi ya mamlaka yake. Hilo ni kosa. Kama mtu aliyeko kwenye mamlaka hawezi kukiri makosa yake, walioko chini yake hawawezi wakamwamini yeye. Kanuni hii inatumika kwenye nafasi ya aina yeyote ya mamlaka, ikiwa ni pamoja na wazazi.

Wazazi, kama mko kwenye mgogoro na mtoto wenu, huenda ikawa labda umefanya makosa ambayo inabidi yatambuliwe. Mtoto ataweza kuwa anajihalalishia makosa yake kwa kutumia makosa yako. Omba msamaha kwa maneno yako makali, majibu ya haraka haraka, na kushindwa kuitambua hali. Pengine kunaweza kusiwepo na maendeleo ya kumaliza mgogoro, hadi pale utakapokuwa umeweza kuomba msamaha, "Mungu huwapinga wajikuzao, bali huwapa neema wanyenyekevu" (Yakobo 4:6b).

Aidha wewe ni mzazi au ni mtoto, unahitaji kukiri makosa yako. Kutubu, kuomba msamaha, na kujitiisha mara kwa mara kwa mamlaka iliyotoka kwa Mungu kwa kawaida itakupa ushirikiano ulio bora kutoka kwa watu wengine, lakini hiyo siyo sababu inayokupasa ufanye hivyo. Unapaswa ufanye hivyo ili kumpendeza Mungu.

Wakati unapokuwa umekiri makosa yako uliyotenda, huhitajiki tena kutaka kuhakikisha kwamba mtu mwingine anayehusika na yeye analaumika kwa makosa yake. Usiyatumie makosa ya mtu mwingine ili kupata radhi kwa matendo yako mabaya uliyoyafanya.

Uhusiano unaweza ukaimarika mara moja, au unaweza ukachukua muda. Wakati mwingine watu watalazimika waone mabadiliko yako kama ni halisi kabla na wao hawajaanza pia kubadilika. Lakini sababu ya kukutaka wewe kutenda lililo la haki siyo kwa ajili ya kumfanya mtu mwingine abadilike. Unapaswa tu ufanye kile ambacho Mungu anakutaka ukifanye. Inawezekana huyo mtu mwingine asibadilike, lakini utakuwa na dhamira iliyo safi na baraka za Mungu kwa sababu umetimiza jukumu lako. Mwamini Mungu katika kutimiza jukumu lake.

### **Umuhimu wa Kila Eneo la Maisha kuwekwa chini ya Mamlaka ya Mungu.**

Jaribu kufikiria kisiwa kimoja kinachoitwa Zhivia. Kisiwa kingine kilicho karibu kiitwacho Grekia kinataka kukishinda Zhivia. Mtawala wa Grekia anaahidi serikali ya kisiwa cha Zhivia kwamba nchi zao mbili zinaweza kuwa na amani kama atakuwa tayari kumpatia ekari kumi (10) tu katikati ya kisiwa chao. Je, hilo litakuwa ni suluhisho zuri la kuleta amani? Ikiwa Zhivia atampa adui eneo katikati ya nchi yake, adui anaweza akajipanua katika eneo hilo kwa ajili ya kutaka kutawala eneo lingine zaidi.

Jaribu kufikiria kwamba maisha yako ni kama nchi yenye mikoa/majimbo mbalimbali. Mkoa/Jimbo moja linaweza likawa ni ajira au shule. Mkoa/Jimbo lingine linaweza kuwa ni burudani. Eneo lingine ni uhusiano wako na wanafamilia. Kuna maeneo mengine mengi.

Nchi yote, ikiwa na mikoa/majimbo yote inapaswa iwe chini ya mamlaka ya Mungu. Unadhani ni nini kitatokea kama mkoa/jimbo moja la uhusiano wako na familia, likawa haliko chini ya mamlaka ya Mungu? Umemruhusu Shetani aingie na kukaa kwenye mkoa/jimbo hilo. Kutoka kwenye mkoa/jimbo hilo ataanza kuvamia mikoa/majimbo mengine ya maisha yako ili yawe chini ya mamlaka yake. Vivyo hivyo, kama mtu siyo msafi katika mambo yake ya burudani, maeneo mengine ya mikoa /majimbo ya maisha yake yataweza kuvamiwa na Shetani. Mkristo anapaswa aweke kila mkoa/jimbo la maisha yake chini ya mamlaka ya Mungu.

### **Vipengele kadhaa kwa Wazazi**

► Wanafunzi wanapaswa wasome Waefeso 6:4, Wakolosai 3:21, 1 Wakorintho 13:11, na Wakolosai 3:8 kwa ajili ya kikundi.

Kama mtoto wako anaonyesha hisia kali, ya kuonyesha hasira au kuchanganyikiwa, anaweza kuhisi kwamba humwelewi. Huenda pia anahisi kwamba humjali vya kutosha katika kumsikiliza na kujaribu kumwelewa.

Jaribu kumsikiliza na kumwelewa. ikiwa mara kwa mara unapuuzia matatizo yake kama yasiyokuwa na maana au ni ya kijinga, hujamwelewa anakabiliana na nini hasa. Ikiwa inaonekana kama ni tatizo kubwa kwake, basi ni changamoto kwa imani na tabia yake. ikiwa huwezi kuelewa ni kwa nini anaonyesha hisia nzito kiasi hicho, basi huwezi kuelewa umuhimu uliojizingira katika hali yake iliyopo.



Kamwe usimkatie tamaa mtoto wako, na usitoe matamko yanayoonyesha kana kwamba sasa umefikia mwisho au huwezi tena.

Usifikiri kwamba watoto wako wote wanafanana.

► Mwanafunzi anapaswa asome Waefeso 4:30-32 kwa ajili ya kikundi.

Matatizo yanapojitokeza, usifanye marejeo ya historia ya mambo yaliyokuwa yameshindikana. Mtoto anataka kufikiria kushindwa kwake kwa zamani kama mambo yasiyo na umuhimu kwa hali ya sasa. Anafikiria kwamba kwa sasa amebadilika na itakuwa siyo kumtendea haki wewe kuendelea kumkumbusha kuhusu kushindwa kwake huko nyuma. Hata hivyo, usimtarajie kwamba atakuwa mkarimu sana kwako.

### **Kwa ajili ya majadiliano ya Kikundi**

► Je, kuna maudhui gani kutoka katika somo hili ambayo ni mapya kwako? Je, ungependa kushirikisha baadhi ya mambo ambayo umepanga kuyabadilisha katika utendaji wako?

► Jadili njia nyingine za zaidi ambazo familia za kanisa zinaweza kufanya kazi kwa pamoja ili kuendeleza maisha sehemu za nyumbani na kusaidia watoto wa kanisani.

### **Maombi**

Baba wa Mbinguni,

Tunataka nyumba zetu ziwe maeneo a upendo, usalama, na baraka. Tusaidie kuwa watakatifu na wenye upendo katika yale yote tunayoyatenda kwenye nyumba zetu.

Tusaidie tuweze kuwa na utaratibu unaowiana kwenye mafundisho na tabia ya Kikristo. Wape watoto wetu shauku ya kukufuata wewe.

Asante Bwana kwa kuwa mwaminifu kwa kila mmoja wa watoto wetu. Tunajua kwamba Roho Mtakatifu wako anafanya kazi ndani ya mioyo yetu.

Ameni.

## Kazi za Kufanya

(1) Kusanya orodha ya maelekezo saba ya kibiblia kwa ajili ya familia. Kisha orodhesha matumizi maalumu kwa ajili ya hali halisi ya maisha. Andika maelezo yanayoelezea kila kipengele cha matumizi (jumla ibara saba).

(2) Chagua mojawapo ya mada zilizoorodheshwa hapa chini. Pitia kitabu cha Mithali na orodhesha Mithali zinazoelezea kuhusu mada hizo. Andika aya mbili zenye kuonyesha muhtasari wa kile ambacho Mithali anasema kuhusiana na mada. Kisha andika aya tatu kuhusu jinsi ambavyo mzazi anaweza kumfundisha mtoto au kijana wake kanuni zilizoainishwa. Mada ni kama zifuatazo:

- Kusema ukweli
- Mambo ya fedha
- Tofauti iliyopo kati ya thamani ya hekima na thamani ya fedha
- Uaminifu
- Usafi wa kujamiiana
- Unyenyekevu
- Kupokea maelekezo na masahihisho
- Kuwa na bidii/kuchukua hatua kwa kutumia akili yako mwenyewe
- Mungu anasema nini kuhusu furaha
- Uwezo/Kipaji cha kusema
- Mahusiano na watu wengine
- Ukarimu

# Somo la 14

## Malezi wakati wa Ujana

### Malengo ya Somo

Hadi kufikia mwishoni mwa somo hili, mwanafunzi atapaswa:

- (1) Aelee vipaumbele vya Mungu kwa ajili ya vijana.
- (2) Kuchukua jukumu la kushawishi na kufundisha vijana kwenye maandalizi ya kuingia kwenye utu uzima.
- (3) Kuwa na motisha wa kutengeneza mahusiano yenye afya/nguvu na yenye kuzaa matunda kwa vijana.
- (4) Kuwa tayari kujazwa na kuwezesha kufuata kanuni za kimaandiko wakati wa kukabiliana na changamoto za ujana.

### Martha – Mkufunzi wa Nyumbani

Kila siku jioni, Martha alikuwa na muda wa kufanya maombi na kusoma Maandiko akiwa na watoto wake wawili. Atasoma baadhi ya Aya za Maandiko, atapumzika mwishoni mwa kila Aya na kuanza kuzungumzia kuhusu matumizi yake katika maisha. Watoto wake walipokuwa vijana, Martha aliwapa zamu za kusoma na kufafanua vifungu vya Maandiko. Walifafanua vifungu vya Maandiko vizuri sana kwa sababu walikuwa wamejifunza kwenye mfano wa mama yao. Walikuwa na uwezo wa kutumia maneno yao wenyewe kuelezea kanuni za maisha ambazo walikuwa wamejifunza kutoka kwa mama yao.

### Kipindi cha Ujana

Kila jamii ina jina la kipindi kati ya utoto na utu uzima. Hiki ni kipindi ambacho kijana mdogo huanza kuwa na hamu ya kuwa mtu mzima, kama vile kujamiiana, lakini akiwa bado hawezi kuchukuliana na majukumu ya utu uzima. Kwenye baadhi ya nchi, mtu anahesabika kisheria kwamba ni mtu mzima anapokuwa na umri wa miaka 18. Kwenye nchi hizo, mtu aliye chini ya miaka 18 hawezi kuoa au kuolewa, kutumika jeshini, au kufanya mikataba ya kisheria bila ya kibali cha mzazi.

Umri wa kuhesabika kuwa kijana kamili haufanani kabisa kila mahali. Kwenye jamii nyingine, mtu anaweza kuhesabika kuwa ni mtu mzima mapema akiwa chini ya umri wa miaka 18, akiwa ameshajifunza mambo ambayo watu wazima anafanya. Kwenye jamii nyingine, mtu anaweza kuendelea kuwategemea wazazi wake kwa miaka kadhaa akiwa ameshapitiliza umri wa miaka 18, wakati akiwa bado anamalizia elimu yake.

► Je, ni neno gani katika jamii yenu linaloelezea kundi la vijana kwenye hatua ya utoto hadi utu uzima?

► Je ni nini maana ya *mtu mzima*?

Ufafanuzi mmojawapo wa *mtu mzima* unaotumika kwa pamoja kwa ajili ya watu na wanyama ni huu: Ni kiumbe ambacho kimekua hadi kufikia ukomavu wa kimwili. Hata hivyo, utu uzima wa binadamu unamaanisha zaidi ya ukomavu wa kimwili. Kijana mdogo anaweza akawa na umbo na nguvu kama za mtu mzima lakini unakuta bado hajaweza kuchukua majukumu ya mtu *mzima*.

► Je, ni tabia gani walizo nazo watu wazima mbali na ukomavu wa kimwili?

Kwa ujumla, mtu mzima ni yule mtu ambaye anaweza kujiongoza na kuwajibika kwa ajili ya maamuzi. Ufafanuzi huu siyo tafsiri kamili sana kwa sababu viwango vya majukumu binafsi vinatofautiana sana. Kila mtu ambaye hajatengwa kabisa anashawishiwa na watu wengine, na hata watu wazima hawana uhuru wote kamili katika kila uamuzi. Hata hivyo, utu uzima kwa ujumla una sifa ya kufanya na kuwajibika kwa maamuzi ya mtu mwenyewe. Mwishoni mwa kipindi cha ujana, mtu anapaswa kufanya maamuzi kwa ajili yake mwenyewe. Lengo la wazazi ni kuwaandaa vijana kwa ajili ya jukumu hilo.

Yesu alielezea hadithi moja ya mtoto ambaye alikwenda kudai urithi wake kutoka kwa baba yake, ambaye alikuwa bado hai (Luka 15:11-32). Mtoto alichukua fungu lake la fedha na akazipoteza kwa matumizi ya uzembe mkubwa sana. Huu ni mfano mzuri wa mtu ambaye amemaliza hatua ya ujana na kuwa kwenye hatua ya mtu mzima lakini hakuwa tayari kufanya maamuzi yenye hekima. Kuna vijana wengi ambao wanapatwa na madhila ya maamuzi mabaya waliyofanya kwa sababu hakukua vizuri kabla ya kupokea uhuru na majukumu ya mtu mzima.

Neno la Mungu lina hekima kubwa sana kwa ajili ya ujana, kipindi muhimu cha wakati wa kuendelea kukua kwa mwanadamu.

### **Maendeleo ya Kimwili na Kiakili**

► Mwanafunzi anapaswa asome Luka 2:40, 52 kwa ajili ya kikundi.

Yesu aliingia kwenye ujana akiwa anakua kiakili na kimwili. Katikati ya hizi Aya mbili, kuna simulizi la Yesu kutembelea hekalu ili kuongea na waalimu wa dini. Siyo tu kwamba alikuwa anaongezeka kukua kimwili, lakini pia alijisikia mwenyewe kama angeweza kuwa huru zaidi. Alikuwa pia tayari kushirikishana mawazo na watu wengine zaidi ya familia yake marafiki zake.

Mariam na Yusufu walishangazwa na mazungumzo ya Yesu na waalimu wa dini, lakini Mariamu alimwambia Yesu kwamba yeye pamoja na Yusufu walikuwa na wasiwasi kwa siku tatu (Luka 2:46-48). Yesu akawaambia kwamba hawapaswi kuwa na wasiwasi kwa sababu alikuwa anaanza kutekeleza kazi ya Baba yake (Luka 2:49). Akiwa kijana alikuwa na matamanio ya kawaida ya kuanza kufuata shauku ya maisha yake. Hata hivyo, alirejea nyumbani na kutii mamlaka ya wazazi wake kwa miaka yake yote ya ujana yaliyokuwa yamebakia (Luka 2:51).

Wakati wa ujana wa mapema, mwili wa mtoto hubadilika kuwa kama mtu mzima. Mtoto anaweza kukua haraka kwa kuongezeka urefu. Nywele huanza kukua katika maeneo kadhaa kwenye mwili. Sauti inaweza ikabadilika na kuwa nzito. Baba au mama anapaswa kuhakikisha mtoto wake anaelewa kuwa mabadiliko hayo ni ya kawaida. Mungu alipanga ukuaji wa kawaida wa kimwili na kiakili kwa mwanadamu.

Kuwa na uhusiano mzuri na watoto wako kutawasaidia kujisikia kwamba wana uwezo wa kuanzisha mazungumzo ya wazi na wewe katika kipengele hiki cha maisha. Mtoto ambaye hajasikii kuwa na amani kuzungumza na mzazi wake kuhusu mambo haya anaweza kuwa na hofu ya siri na anaweza akatafuta kupata taarifa kutoka kwa marafiki na kwenye mitandao.

### **Maendeleo ya Kihisia**

Ujana siyo tu mwendelezo wa maisha ya mtoto kama ilivyokuwa hapo awali. Wazazi wanakosea kufikiri wanaweza kuendelea kutoa maelekezo na kufundisha kijana kama vile wangemfundisha mtoto mdogo. Ufahamu wa kijana na mambo anayoyapendelea hubadilika. Anahisi kuwa na shauku ya kuwa kijana aliye huru, mwenye mafanikio, na heshima. Vijana huchanganyikiwa wakitendewa na au kuchukuliwa kama mtoto mdogo.

Katika Maandiko yote kuna mifano ya vijana wadogo wenye kufanya maamuzi ya hekima, kama Yesu, au maamuzi ya ovyo, kama tunavyosoma katika hadithi iliyosimuliwa na Yesu (Luka 15:11-32). Wazazi wanapaswa kuelewa jinsi ambavyo kijana au binti yao anakua kihisia. Lengo la mzazi ni kumsaidia kijana aweze kusitawisha udhibiti wake binafsi wa maeneo yake yote, ikiwa ni pamoja na hisia, ili kwamba udhibiti wa baba au mama hautakuwa unahitajika tena.

► Soma Waefeso 6:1-4. Je, ni maelekezo gani maalumu tunapata kutoka katika kifungu hiki?

Watoto wanapaswa kuwatii wazazi wote, ikimaanisha kwamba baba na mama wanapaswa kushirikiana. Kifungu hicho kinaunganisha kwa uzito mkubwa utii kwa wazazi na wajibu wa kumtii Mungu. Wazazi ambao hawawafundishi watoto wao kutii wanakuwa hawawapi maandalizi ya kumtii Mungu. Kuruhusu watoto kufanya uasi dhidi yako kama mzazi kunawaandaa pia kumwasi Mungu.

Maandiko haya yanatoa mwongozo mahususi kwa akina baba. Akina baba wanapaswa kuleta nidhamu katika njia ambayo kwamba haiwachanganyi au kuwakatisha tamaa watoto kufanya yale mambo ambayo ni sahihi. Adhabu na masahihisho ni mambo muhimu, na hayamfanyi mtoto kuwa na furaha mara moja, lakini baba anapaswa awe asiyebadilika mara kwa mara na mwenye upendo. Hii inamaanisha kwamba baba anapaswa aelewe kitu kuhusu maendeleo ya kihisia ya mtoto.

Baba hapaswi kutoa marekebisho tu, lakini pia malezi ya kiroho na mafundisho kutoka kwa Bwana. Hatuwaendelezi watoto wetu kwa kushambulia tu makosa yao. Ni lazima tujaribu

kuwaelewa na kuwatia moyo watoto wetu. Tunatumia ukweli wa Mungu na siyo tu matakwa yetu wenyewe. Tunadhihirisha kwamba sisi pia tunaishi kwa kumtii Mungu.

Wakati mtoto anapokuwa amejifunza kuheshimu na kutii katika miaka yake ya utotoni, mafunzo yake kwenye ujana yanakuwa rahisi zaidi! Uhusiano ambao wazazi walianzisha kwa watoto wao wakati wakiwa wadogo utasaidia sana wakati wa mabadiliko ya kimwili, kihisia, na kiroho ambayo vijana wanapitia. Hakuna maelekezo kwa ajili ya kufanya malezi yawe marahisi, lakini kukuza mahusiano mazuri ya mapema kunafanya mawasiliano yawezekane katika ujana wote.

Wazazi wanatamani watoto wao wawe wasikivu, lakini mara nyingi baba au mama lazima wasikie kwanza. Tafadhali kwa ajili yako na wao – weka chini simu yako, kitabu chako, kazi, au kitu chochote unachokifanya na uwape umakini wako wa kuwasikiliza wanapotaka kuzungumza. Wasikilize kwa makini kana kwamba hakuna kitu kingine tena cha kufanya. Sikiliza bila kurekebisha makosa yao hadi pale utakapokuwa umeelewa kwa uhakika kwamba wanataka kusema nini. Wanataka wajisikie kwamba unawathamini kwa ukweli pamoja na mitazamo yao, na kwamba unawaheshimu kama watu. Hata kama hawapendi ushauri wako, watauheshimu zaidi baada ya kujua kwamba kwa uhakika umewasililiza.

Huenda ikawa ni vigumu kusikiliza wakati kijana anapoonyesha kuchanganyikiwa, hasira, au kutaka kujiondoa. Kumbuka kwamba kijana haelewi kabisa hisia zake mwenyewe. Wakati mwingi kijana husema yale anayoyasema kwa sababu hisia zake zimeathiriwa na mazingira, mahusiano, na miili yao. Mambo haya yote yanaweza yakaathiri hisia ya kijana: msongo wa mambo kutokea shuleni, shinikizo la kukubaliwa na marafiki, wasiwasi kuhusiana na mabadiliko ya mwili, chuki kwa ajili ya kuhisi kutothaminiwa au kutoheshimiwa, kile ambacho kinafanywa na homoni zao, na uchovu unaotokana na tabia ya kutolala kwa nyakati zinazofanana.

## **Maendeleo ya Kiroho**

► Soma Mhubiri 11:9-12:1, 13. Je, ni kwa jinsi gani unaweza kuelezea amri zilizopo kwenye Aya hizi kwa kijana?

Dunia inaweza kutoa udhuru kwa tabia ya uzembe na uasherati kwa vijana, lakini Aya hizi zinawataka vijana wakumbuke kwamba watahitajika kuwajibika kwa Mungu kwa matendo yao. Yeye peke yake ndiye jaji au mwamuzi wao.

Kufundisha Neno la Mungu katika nyanja mbalimbali za maisha bado ni muhimu sana kwenye hatua hii ya maisha (Kumbukumbu la Torati 6:6-7). Hata hivyo, ni vigumu zaidi, kwa sababu kijana anakuwa na shughuli nyingi za kufanya nje ya kikundi cha familia. Wanakuwa na mambo wanayoyataka wao wenyewe, shughuli za elimu, shughuli za michezo, na kushiriki katika vikundi vya marafiki. Wazazi wao hawawezi kuwa pamoja nao kwa muda wote, lakini Mungu anaweza, na wazazi wanapaswa wawe waaminifu kuomba kwa ajili yao. Wababa na Wamama anapaswa watafute hekima kutoka kwa Mungu kwa ajili ya kupata muda wa kuwa na mazungumzo mahususi pamoja nao. Ni muhimu sana kwa

wazazi waendeleo kuhusika na kuwa makini na vipengele mbalimbali vya maisha ya vijana wao.

► Soma 1 Wathesalonike 2:11-12 kwa pamoja. Je, ni jukumu gani ambalo Mungu amewapa wababa kwenye mahusiano yao na watoto wanaokua?

Wazazi, msidhanie kwamba kila kitu kiko shwari kwa sababu tu matatizo hayaonekani wazi. Ni jambo unalopaswa kutegemea kwamba kijana au binti yako atakabiliana na majaribu na kupitishwa kwenye madhaifu, kwa sababu ndivyo itakavyokuwa. Wasaidie ujuzi wa jinsi ya kuwajibika kwa ajili ya fedha zao, jinsi ya kutumia muda wao, chaguzi za mambo ya maisha wanayofanya, na usafi wao wa kijinsia. Omba hekima na ushauri kutoka kwa watu wengine. Sikiliza kutoka kwa waalimu na watu wengine ambao wanadhihirisha nia ya kuhusika. Hata kama hukubaliani na maoni ya mtu mwingine kuhusiana na mtoto wako, unapaswa usikilize na ujaribu kuyaelewa mahitaji ya mtoto wako.

Waombe vijana wako na uwaambie kwamba unawaomba. Ni vyema wasikie ukiomba kwa ajili yao. Shiriki nao maombi maalumu unayoomba. Kwa mfano, unaweza ukasema, "Naomba kwamba muwe wenye njaa na kiu ya haki (Mathayo 5:6); na kama ayala aioneavyo shauku mito ya maji (Zaburi 42:1). Ninamwomba Mungu mjazwe na Roho Mtakatifu (Waefeso 5:18) ili umpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote na jirani yako (au ndugu yako) kama nafsi yako (Mathayo 22:37-39)."

► Je, kuna vifungu gani vingine vya Maandiko ambavyo unaweza kuvitumia kwa ajili ya kuwaomba vijana wako?

Mwisho, kwenye hii safari ya kiroho pamoja na vijana wako, tumia Neno la Mungu pamoja nao:

- Kuwa mfano kwao: Mara kwa mara tumia muda wako binafsi kwa kujifunza Biblia. Zungumza na kijana wako wa kiume au wa kike kuhusu kile ambacho Mungu anakufundisha wewe na ni kwa jinsi gani unalitumia hilo Neno la Mungu kwenye maisha yako. Hata kama hawatakuwa na jibu la shauku yao au hawataendelea na mazungumzo, wanasikiliza na watakuwa wanaguswa na Neno!
- Kariri vifungu vya Maandiko kwa pamoja kama familia na rudia kutoka moyoni kwenye kila muda wa chakula au mwisho wa siku.
- Soma na zungumza kupitia kitabu cha Mithali aya moja kwa wakati mmoja. Mithali ni kitabu cha ajabu sana na kizuri kutumika wakati wa nyakati fupi za ibada, kikiwa na hekima za vitendo kwa ajili ya maisha ya kila siku. Kitabu hiki kinatoa fursa nyingi kwa ajili ya majadiliano na kinaleta mguso mkubwa usiokuwa wa kawaida.
- Maelekezo, kanuni, na mifano katika Maandiko yote yanatumika katika majira yote ya maisha, kwa hiyo jifunze Neno lote la Mungu ukiwa na vijana wako wa kiume na wa kike.

## Maendeleo ya Kijamii

Andiko la Luka 2:52, linalofafanua maendeleo ya Yesu alipokuwa kijana, linasema kwamba alisitawisha uhusiano wake pamoja na wengine. Mungu anapendezwa sana na mahusiano yetu. Alituumba tuwe na mwingiliano wa kibinadamu na ushirika wa pamoja.

Kando na wanafamilia, tunashawishiwa na wanafunzi, majirani, vikundi vya kanisa, waajiri, waalimu, na viongozi wengine na vyombo vya habari. Kwa kawaida watu walio katika marika yanayofanana ndiyo wenye ushawishi mkubwa zaidi kwa mambo mema au mabaya. Wazazi wa Kikristo wanapaswa kufuatilia mwingiliano wa kijamii wa watoto wao na vijana.

Jinsi kijana wako anavyoendelea kuwa mtu mzima, fikiria kwa uangalifu na kwa maombi ni jinsi gani atakavyoweza kushughulika na hali hiyo. Kwenye kompyuta na vifaa vingine vya kiselula vya familia yako, tumia manenosiri ya kufunga na kufungua baadhi ya programu mahususi kwa ajili ya kuilinda familia yako katika kuingia na kuangalia mambo ya uovu. Weka muda maalumu wa kufungua na kutumia vifaa hivyo. Fuatilia tovuti, filamu, vipindi vya televisheni na majukwaa ya mitandao ya kijamii. Kwa jinsi ile ile ambayo huwezi ukaruhusu vijana wako kutumia muda wao na baadhi ya watu fulani kwenye ujirani wako, pia usiwaruhusu wafuatilie au kuunganika na watu wabaya kwenye vifaa vyao vya kielektroniki.

► Haitoshi tu kuwalinda vijana wako. Katika ujana, pia unamwandaa kijana wako wa kiume au wa kike kuchukua majukumu kwa ajili ya kufanya maamuzi yao wenyewe yenye hekima na ambayo yanampa Mungu utukufu na kulinda roho zao. Je, ni kwa njia zipi unazoweza kuwafundisha vijana wako majukumu na uwajibikaji kwenye matumizi ya teknolojia katika jamii yao ya dunia?

Vijana hupenda kuunda vikundi vya marafiki ambavyo hutumia muda wao mwingi kwa pamoja. Wanajifunza kushirikishana mambo wanayoyapendelea, kama vile kufurahia aina za burudani zinazofanana. Wanaanza kushirikishana tabia zao zinazofanana dhidi ya kanisa, wazazi wao, shule, na taasisi nyingine. Mara nyingi wazazi hushangaa wanapoona mabadiliko yao katika hatua hii ya ujana. Vijana wakati mwingine wana maoni na shutuma zisizotegemewa au kutarajiwa na wanatumia misamiati ambayo huwa wamejifunza kutoka kwa marafiki zao. Kundi la marafiki hujitokeza kuwa ni familia mbadala inayowapa wanachama wake hadhi ya kukubalika. Kijana anavutiwa kwa nguvu sana kuwa kwenye familia mbadala kama familia yake mwenyewe haimpi hisia ya thamani, utambulisho na kukubalika.

Mzazi huona ni vigumu sana kumtoa kijana wake katika kundi la marafiki alilojiunga nalo au kupunguza ushawishi wa hilo kundi. Wakati mzazi atakapokosoa hilo kundi au watu binafsi, kijana hutaka kuwalinda kwa kuwatetea na anahisi kwamba mzazi wake haelewi. Baba au mama wanaweza kumsaidia kijana kwa kuonyesha kumjali, kutambua anayoyataka, na kumpenda. Wakati mzazi anapotoa mahitaji ya mihemuko ya kijana, huwa hawana haja tena ya kutegemea kundi la marafiki kwa ajili ya kuwa familia mbadala.



► Je, ni kwa jinsi gani wazazi wa familia kadhaa wanaweza kufanya kazi kwa pamoja ya kuwasaidia vijana wao?

► Je, ni kwa jinsi gani kanisa lako linaweza kuwasaidia wazazi wa vijana wanapokuwa wanawasaidia vijana wao waweze kuwa na maisha bora yenye nguvu na jamii inayomheshimu Mungu?

### **Matatizo ya kipindi cha mpito kuelekea Utu Uzima.**

Mtoto hawezi akawa mtu mzima kwa wakati mmoja au mara moja. Mtoto huwa anapitia kwenye kipindi cha mpito ambacho kinafikia mwisho baada ya miaka kadhaa.

Kati ya Maandiko yote, kitabu cha Mithali kiliandikwa mahususi kwa ajili ya vijana. Katika Mithali, Mfalme Sulemani anazungumza na kijana wake aliyekuwa anajifunza kuhusu maisha na kukuza mtazamo wake wa kidunia. Sulemani alizungumza na mwana wake kuhusu kila sehemu ya maisha, kuhusu thawabu zinazoweza kupatikana kwa kuchagua kwenda katika njia za Mungu na kuhusu hatari na au madhara ya kukataa hizo njia za Mungu.

Imani zilizoundwa wakati wa utoto na kwenye miaka ya ujana, na chaguzi zilizofanywa katika kipindi hicho ni muhimu sana kwenye maisha ya mtu. Tunapochunguza changamoto kadhaa za kipindi cha mpito cha kuingia kuwa mtu mzima, tutazame ni kwa jinsi gani Neno la Mungu linavyoweza kutusaidia tusafiri kwenye miaka ya ujana na vijana wetu.

**Changamoto ya 1:** Kijana hutathmini yale yote ambayo amefundishwa na kuamua ni kipi anachoweza kukiamini.

Kijana huwa anataka kile anachokiamini kiwe wazi kwenye akili yake, kwa hiyo hutathmini na kujiuliza maswali kwamba ni kitu gani amefundishwa. Kuna uwezekano mkubwa kwamba hatakubaliana na kila kitu ambacho wazazi wake walimfundisha. Wazazi huhofia hatari hiyo. Ikiwa wanajihisi kwamba hawawezi kumsaidia kuelewa masuala anayofikiria, wanaweza wakaanza kumchukulia kama ni mtoto tena, wakidai kwamba akubali yale wanayoyaamini bila kuuliza. Hali hii humfanya kijana ajisikie kwamba hawampi nafasi ya kufikiria na kujiamulia mambo yake mwenyewe.

Mzazi anapaswa kwa ustahimilivu aelezee sababu za kuamini yale wanayoamini na kumpa kijana nafasi ya kuweza kuzungumza na watu wengine ambao wanaweza wakasaidia kutoa ufafanuzi.

► Soma Mithali 23:22-23 kwa pamoja.

Katika mistari hiyo, Mungu anasema kwamba kijana anapaswa kuchagua kusikiliza hekima ya wazazi wake. Baba au mama hawawezi kufanya chaguo hili kwa kijana wao, lakini wanaweza kusitawisha uhusiano mzuri. Kama wazazi wataendelea kuwasiliana kwa uwazi na kwa heshima pamoja kijana wao wa kiume au wa kike, itawatia moyo vijana wao kufanya uchaguzi huu.

**Changamoto ya 2:** Kijana anaanza kuchukua jukumu kwa ajili ya kufanya maamuzi.

Kijana anaanza kuelewa jinsi maamuzi yanavyofanywa, na anajisikia mwenye uwezo wa kufanya maamuzi peke yake, lakini wazazi wake na watu wengine hudhibiti chaguzi zake. Atashawishika kufanya uasi dhidi ya mamlaka yao kwa sababu anafikiri hawatambui uwezo wake. Kwa kawaida, kama atafanya uasi, wazazi watajibu kwa kumwekea ukomo zaidi.

Wazazi wanapaswa kuweka msingi mzuri kwenye hatua hii ya maisha ya watoto wao wakati wakiwa wadogo zaidi. Wanaweza wakawaonyesha watoto wao kwamba kile wanachohitaji kwao ni kwa ajili ya manufaa yao wenyewe kama vile nidhamu ya Mungu ni kwa ajili ya manufaa yetu (Waebrania 12:9-10). Wazazi wanaweza wakadhihirisha kwamba hawatengenezi tu sheria ambazo zitawasaidia wao tu wenyewe kama wazazi.

Pili, wazazi wanaweza kuwapa watoto wao hatua kwa hatua jukumu la kufanya maamuzi makubwa na muhimu zaidi katika miaka yao yote ya utoto na ujana. Hilo huwawezesha vijana kujizoeza kuwajibika, kuthibitisha uaminifu wao, na kujitayarisha kwa ajili ya utu uzima.

Wazazi bado wanawajibika kwa Mungu katika kuwawekea vijana wao mipaka (1 Timotheo 3:4), lakini miaka ya ujana ni ya kujitayarisha kwa ajili ya utu uzima, wakati kijana atakapowajibika kikamilifu kwa Mungu kwa ajili ya maamuzi yake. Wazazi wanapaswa kuwaandaa vijana wao kwa ajili ya huu msimu unaofuata. Kitabu cha Mithali kimeandikwa na baba akimsihi mtoto wake afanye maamuzi ya busara. Sulemani alijua kwamba akiwa kama mzazi hangeweza kumfanyia mtoto wake maamuzi, lakini angeweza kufanya maamuzi yaliyo sahihi ambayo yangeonekana kuwa yenye mvuto zaidi.

**Changamoto ya 3:** Kijana hana ukomavu alio nao mtu mzima.

Huenda vijana wasielewe hatari na uthubutu ambao unawahusu wazazi wao. Vijana kwa kawaida huhisi kwamba wanaweza kukamilisha malengo yao na kuziepuka hatari mbalimbali zilizopo. Mara nyingi wanahisi kuchanganyikiwa kwamba wazazi wao hawana imani katika uwezo na utambuzi wao.

Mithali inatuonyesha kwamba ni muhimu kwa wazazi sio tu kuwaambia vijana wao yaliyo mazuri na mabaya au kuwawekea tu mipaka, bali kuzungumza na vijana wao kuhusu matokeo ya kila chaguo. Kusikiliza maagizo haya kutamsaidia kijana kujifunza kufikiri kwa njia ya ukomavu.

► Soma 1 Petro 5:5 kwa pamoja.

Jambo la busara zaidi ambalo kijana anaweza kulifanya ni kujikabidhi kabisa kwa mamlaka ya wazazi wacha Mungu na kusikiliza ushauri wao wa busara. Kama Petro anavyotunyeshwa katika 1 Petro 5:5, kwamba kijana anayefanya haya ana upendeleo maalumu wa Mungu.

**Changamoto ya 4:** Kijana ana matamano ya mtu mzima lakini hawezi kuwa na marupurupu ya mtu mzima.

Watu wazima wana fursa za marupurupu mengi ikiwa ni pamoja na ndoa, umiliki wa mali, nafasi za uongozi, na uhuru wa kufanya maamuzi. Kwa kuwa vijana bado hawawezi kuwa na marupurupu haya, ingawa wana matamania ya asili ya mambo haya, wanajisikia kuchanganyikiwa. Matamania yao husababisha vishawishi na au majaribu makali. 2 Timotheo 2:22 husaidia vijana kujua ni kitu gani wafanye kuhusu tatizo hilo.

► Soma 2 Timotheo 2:22 kwa pamoja.

Mungu ameachilia neema kwa vijana ambao wako tayari kumtii yeye. Atawasaidia katika kujitoa kabisa kwa mamlaka zao na kukataa kukamilishwa kwa matamania yao ambayo yako nje ya wakati au mapenzi yake. Atawasaidia vijana wa Kikristo kuyageuza matamania hayo kuwa motisha wa kujiandaa kuingia utu uzima kwa kukua katika ufahamu, tabia, na stadi za maisha.

**Changamoto ya 5:** Kijana huona kwamba kuna utofauti kati ya kinachosemwa na wanavyoishi wengine na anachukizwa kwa hilo.

Mara nyingi, vijana wamekatishwa tamaa na watu wengi ambao walipaswa kuwa mifano bora na viongozi bora wa kiroho. Hilo linapotokea, vijana hushawishika kutomwamini kila mtu. Kwa sababu hii, ni muhimu kwako kama kiongozi wa kanisa na kama wazazi kuishi maisha thabiti, ya kumcha Mungu. Mambo kinzani katika maisha yako yanaweza kusababisha vijana kutumia umilele kuzimu. Ingawaje Yesu alikuwa anazungumza kuhusu watoto, na siyo vijana, Mathayo 18:6 kwa hakika hapa inahusiana.

► Soma Mathayo 18:6 kwa pamoja.

Kijana Mkristo anaweza kuwa kielelezo cha mcha Mungu, hata kama hajawi kuona ukiwa kwa watu wengine. Katika Agano la Kale, Samweli ni mfano wa jambo hili. Samweli alilelewa kwenye familia ya kikuhani ambayo haikumcha Mungu na iliyokuwa fisadi kwa njia nyingi, hata hivyo aliamua tangu akiwa na umri mdogo kuishi kwa ajili ya Mungu (1 Samweli 1:20; 1 Samweli 2:11-18, 22-26). Hata akiwa bado mtoto na baadaye kijana, aliendelea kuyaishi maisha matakatifu (1 Samweli 3:19, 21).

► Soma 1 Timotheo 4:12 kwa pamoja.

**Changamoto ya 6:**

Kijana anakabiliwa na msisimko wa maamuzi mengi na fursa nyingi.

Vijana wanaiona dunia iliyojaa wingi wa fursa. Wanaweza wakajitahidi kutafuta mwelekeo kwa ajili ya maisha yao wenyewe. Wanapokea ushauri unaokinza kutoka kwa watu mbalimbali.

Wanafikiri kwamba mtu anapaswa kuwapa kile wanachohitaji ili kufuatilia fursa zilizopo. Ni muhimu kwa vijana kujizoeza kuwa waaminifu katika mambo madogo na kumwamini Mungu katika kufungua fursa nyingi zaidi kwa ajili yao katika muda wake mkamilifu.

► Soma Luka 16:10 kwa pamoja.

Ni jambo la muhimu pia kwa vijana kuchagua kusikiliza ushauri wa kimungu.

► Soma Mithali 11:14 kwa pamoja.

Vijana watagundua kwamba kuna baraka na uhuru katika kufuata njia za hekima ya Mungu.

### **Kwa ajili ya Majadiliano ya Kikundi**

► Je, ni mawazo gani katika somo hili ambayo umeyaona ni ya msaada sana kwako? Je, ni kwa jinsi gani yatakugusa wewe na familia yako, jamii, na au kanisa lako?

► Ikiwa umewahi kuwa mzazi wa kijana wa kiume au wa kike, ni ushauri gani unaoweza kushirikisha kuhusu kustawisha uhusiano ulio wazi na wenye kuheshimika na mtoto katika hatua hii ya maisha? Kuwa mkweli kuhusu makosa yako.

► Je, ni mambo gani ya vitendo ambayo unaweza kuyafanya ili kusaidia vijana kujifunza jinsi ya kufikiri kwa hekima na kufanya maamuzi mazuri?

► Je, wewe kama mzazi unajua wakati wa kupanua mapendeleo na majukumu ya mtoto wako?

► Fanya majumuisho ya majukumu muhimu ya mzazi na majukumu muhimu ya mtoto akiwa amefikia kuwa kijana.

► Je, ni sehemu gani za maisha ambazo baba anapaswa atoe motisha, maonyo na kuwaongoza watoto wake wanapoendelea kukua kwenda ukubwani?

### **Maombi**

Baba wa Mbinguni,

Asante kwa kutuamini katika majukumu uliyotupa ya kuwatunza watoto wetu hadi kufikia watu wazima waliokomaa. Jukumu hili ni ngumu kwa njia nyingi, na ni lazima tuwe na ufahamu kutoka kwako.

Katika Neno lako, tumeona jukumu letu la kuwafundisha watoto wetu hekima, kujidhibiti, na kukutii wewe. Tunaomba msamaha kwa nyakati zote ambazo tumeshindwa kuwa na mwelekeo juu ya vipaumbele hivi kwenye mahusiano yetu na vijana wetu.

Tumekuwa tunasoma na kulitii Neno lako, tupe hekima mahususi kwa ajili ya mahitaji ya watoto wetu. Ni matamanio yetu makubwa sana kwamba watakufuata wewe kwa uaminifu katika siku za maisha yao yote.

Ameni

## Kazi za Kufanya

(1) Tafuta angalao maandiko matatu, aya au vifungu ambavyo unaweza ukavitumia kwa ajili ya kuombea vijana kwenye familia yako au chini ya ushawishi wako. Tafuta vifungu vya maandiko vinavyohusiana na:

- Mahitaji yao ya kiroho
- Ukuzaji wa tabia zao
- Mambo na watu ambao wanawashawishi
- Njia ambazo watazihitaji kwa ajili ya kukua na kustawi

Andika vifungu hivyo mahali ambapo unaweza kuziona mara kwa mara. Anza kutumia Maandiko haya kwa ajili ya kuwaombea vijana wako kila siku.

(2) Chagua maswali mawili ya majadiliano ya kikundi kutoka katika mwisho wa somo hili. Andika angalao ibara moja inayohusiana na kila kipengele.

(3) Chagua kifungu cha maandiko kwa ajili ya kusoma:

- Mithali 4-5
- Mithali 6
- Mithali 23
- Mithali 24

Unapokuwa unasoma, tafakari maswali yafuatayo kutoka kwenye kifungu...

- Je, ni vipaumbele gani mzazi wa kijana anapaswa kuwa navyo?
- Je, ni vipaumbele gani kijana anapaswa kuwa navyo?
- Je, mzazi wa kijana anapaswa awe na fikra/mitazamo gani?
- Je kijana anatakiwa awe na fikra/mitazamo gani?
- Je, mzazi wa kijana anapaswa afanye nini?
- Je, kijana anapaswa afanye nini?
- Je, ni maeneo gani katika maisha ambayo mzazi na kijana wanapaswa wawe wanaongelea?

Andika orodha ya taarifa kwa muhtasari za ujumbe wa kila kifungu kwenda kwa mzazi wa kijana. Andika orodha ya pili ya taarifa kwa muhtasari za ujumbe wa kila kifungu kwenda kwa kijana.



# Somo la 15

## Kijana Aliyekomaa

### Malengo ya Somo

Hadi kufikia mwishoni mwa somo hili, mwanafunzi atapaswa:

- (1) Kuelewa taswira ya Mungu kuhusu majukumu na masuala muhimu ya miaka ya kijana mtu mzima.
- (2) Awe amewezeshwa kuweza kuwachochea na au kuwashawishi vijana wafanye maamuzi ya hekima na kutii maagizo ya Mungu.

### Marcus, Kijana Aliyehamasishwa

Marcus alipokuwa mtoto, wazazi wake walimfundisha jinsi ya kufanya kazi vizuri. Alikuwa na furaha kila wakati alipopata nafasi ya kufanya kazi na kujipatia pesa. Siku zote alikuwa tayari kufanya kazi yoyote ambayo mtu angemuajiri. Kama kijana alifanya kazi ya kutunza mazingira ya uani, kusambaza magazeti, na kutengeneza baiskeli. Marcus alikuwa na matamano ya kuwa mfanyabiashara lakini pia alijua kwamba Mungu alikuwa anamwita kwenye huduma. Marcua alijifunza katika chuo cha Biblia. Ili aweze kulipa gharama za chuoni, alifanya kazi za usafi wa maofisi, kazi za hotelini, na kazi za uani. Alipohitimu, alianzisha huduma, lakini wakati mwingine alikuwa anafanya kazi za kupaka nyumba rangi au kufanya matengenezo ya nyumba kwa sababu huduma yake ilikuwa haina uwezo wa kumlipa. Wakati wote alijitahidi kufanya majukumu ya huduma na maendeleo binafsi kuwa ni vipaumbele vyake badala ya kufanya faida kuwa ndiyo kipaumbele chake, ingawa alikuwa na mke na mtoto aliopaswa kuwatunza. Hatimaye ilifika kipindi ambacho huduma yake iliweza kumsaidia kabisa.

### Ukomavu na Tabia

► Wanafunzi wanapaswa wasome 1 Timotheo 4:12 na Maombolezo 3:27 kwa ajili ya kikundi.

Waraka wa 1 Timotheo uliandikwa kwenda kwa kijana ambaye alikuwa na majukumu ya kusimamia makanisa kadhaa. Katika 1 Timotheo 4:12 tunaona kwamba Mungu hutegemea vijana waliookoka kuwa vielelezo katika tabia zao na mienendo yao. Wanapaswa kuifanya kuwa kipaumbele kuanzishwa katika mafundisho ya Kikristo. Wanapaswa wadhihirishe usafi na upendo usio na ubinafsi kwenye kila mwingiliano na watu wengine. Tabia zao na maneno yao yanapaswa yamheshimu na kumletea Mungu utukufu.

Vijana walioamini/waliookoka wanapaswa waishi maisha ya uangalifu na yenye malengo. Hawapaswi kutumia vibaya nguvu walizopewa na Mungu kwenye hatua hii ya maisha. Hawapaswi kupoteza fursa za kujifunza, kuendeleza ujuzi wao, kuwahudumia watu

wengine, na kuchukua majukumu. Miaka ya ujana na utu uzima haipaswi itumike kwenye matamano ya mambo ya kibinafsi. Ni miaka iliyo bora kwa ajili ya kukua na kuhudumia. Mungu anaweza akawawezesha vijana waliookoka kujifunza kujitawala binafsi ili waweze kuzaa matunda kwa ajili yake.<sup>46</sup>

## **Kazi**

### **Mitazamo juu ya Kazi**

Katika tamaduni nyingine, ni jambo la kawaida kuwaona watu wakiwa wamekaa na hawafanyi kazi, ingawaje wanaweza kuwa ni vijana wadogo na wenye afya nzuri. Ingawa wanayo mahitaji na wanawajibika kwa watu wengine, hawana motisha wa kufanya kazi. Wanadai kwamba wangeweza kufanya kazi endapo wangeajiriwa kwa malipo mazuri. Hawako tayari kufanya kazi kwa malipo kidogo au kufanya kazi ambazo zinaonekana kuwa ni za hali ya chini ya kiwango. Hawataki kufanya kazi kuboresha mazingira yao hata kama wanufaika hawatakuwa ni wao wenyewe.

Wakati mwingine watu walioajiriwa wanafurahia kwa kuwa na ajira. Labda wanaishi katika nchi ambayo asilimia kubwa ya watu hawana uwezo wa kupata ajira iliyo nzuri.

Wanafurahia wanapokuwa wamevalia sare za kampuni na wanajivunia viwango vya hadhi walizo nazo katika hizo ajira zao. Lakini wakati wakiwa wanafurahia viwango na hadhi zao katika kazi hawafikirii sana jinsi ya kumhudumia mwajiri au kuwahudumia wateja. Wanajivunia kuwa sehemu ya jamii ya kampuni, lakini hawatambui ni kwa nini walijiriwa.

Tofauti na watu wanaokataa kufanya kazi, baadhi ya watu wamejielekeza kwenye kupata kazi au jinsi ya kupata fedha. Labda waliohamia kwenye eneo ambalo ajira inalipa mshahara mkubwa zaidi kuliko maeneo ya vijijini walikotoka. Wanataka wafanye kazi na kujipatia fedha za kutosha kwa kadri inavyowezekana. Wanapuuzia maeneo mengine muhimu ya maisha, kama vile kustawisha mahusiano yao na Mungu pamoja na familia zao.

Watu katika jamii wanaweza wakafanya mambo haya, lakini waamini hawapaswi kufanya yale mambo ambayo ni ya kawaida tu katika utamaduni wao. Badala yake, ni lazima watafute Mungu anasema nini, na kisha wamtii. Biblia ina mambo mengi ya kusema kuhusu kazi, bidii, na tija.<sup>47</sup>

### **Asili ya Kazi**

Mungu ni muumbaji (Zaburi 104:24). Mungu ni mzalishaji (Zaburi 104). Mungu kwa wakati wote anatenda kazi, akihusika na maisha ya kila mtu binafsi na katika mambo yote ya dunia kwa wakati wote (Yohana 5:17). Wakati Mungu alipoumba watu, aliwaumba kwa sura yake,

---

<sup>46</sup> Kupata zaidi kuhusu somo hili, ona somo la 12 katika kitabu cha *Muundo wa Kiroho Spiritual Formation*, kinachopatikana kutoka Shepherds Global Classroom.

<sup>47</sup> Kupata zaidi kuhusu somo hili, ona somo la 3 katika kitabu cha *Kuishi Maisha ya Kikristo kwa Vitendo* kinachopatikana kutoka Shepherds Global Classroom.



kwa mfano wake mwenyewe. Alihitaji watu wawe wabunifu na wasimamizi wenye kuleta tija katika uumbaji wake. Mungu aliwapa wanadamu mamlaka juu ya wanyama wa dunia, viumbe wa baharini na angani (Mwanzo 1:26). Aliwafanya watu kuwa wasimamizi na watumishi wa rasilimali zote za dunia (Mwanzo 1:28-30).

Kazi ni sehemu ya mpango wa Mungu kwa ajili ya maisha ya mwanadamu. Tangu mwanzo, Mungu aliwapa watu wajibu mkubwa wa kufanya. Kila mmoja wetu atamjibu iwapo tumefanya kwa uaminifu kazi aliyotuachia.

### **Kanuni kutoka katika kitabu cha Mithali**

Kitabu cha Mithali kiliandikwa mahususi kwa ajili ya vijana, kuwafundisha jinsi ya kufikiri na kutenda kwa hekima. Kitabu cha Mithali kina mambo mengi ya kusema kuhusu kazi:

► Wanafunzi wanapaswa wasome kila kifungu cha andiko kwenye Mithali kwa ajili ya kikundi.

### **Mithali 6:6-11, Mithali 10:5.**

Mchwa ni mfano mzuri wa kuangaliwa kwa ajili ya wanadamu.

- **Wanafanya kazi kwa bidii sana ingawa hakuna anayewalazimisha kufanya kazi.** Hakuna anayewaambia wanachopaswa kufanya au ni kwa jinsi gani wanapaswa kufanya, lakini bado wanafanya kwa tija kubwa. Kutokana na mchwa, tunajifunza kwamba hatupaswi kulazimishwa kufanya kazi. Tunapaswa **tupende** kufanya kazi kwa sababu hivyo ndivyo Mungu anavyotupatia mahitaji yetu.
- **Wanafanya kazi wakati wa kufanya kazi.** Kuna wakati wa kufanya kazi, na kuna wakati wa kufanya shughuli nyingine, na kuna wakati wa kupumzika. Inaweza kusaidia kuuliza, "Je, ninapaswa niwe ninafanya nini kwa sasa hivi?"
- **Wanafanya kazi wakati kukiwa bado kuna fursa za kufanya kazi.** Misimu inabadilika, na fursa za kupata rasilimali zinaweza zikapita. Fursa zetu pia huja na kutoweka. Ni lazima tutumie fursa tulizo nazo kwa sasa, au itapotea bure.
- **Wanafanya kazi ili baadaye wapate chakula wanachohitaji.** Hatupaswi kulala au kupumzika wakati wa kufanya kazi. Kama tutakuwa wavivu katika wakati ambao tunapaswa tuwe tunafanya kazi nzuri, mahitaji yetu ya baadaye hayatapatikana. Tunapaswa tufanye kazi **leo** ili kuweza kupata mahitaji yetu ya **kesho**.

**Mithali 19:15, Mithali 20:4, Mithali 12:24.** Mungu ameiweka dunia katika namna ambayo uchaguzi wetu una matokeo halisi (Wagalatia 6:7).

Ikiwa tutendelea kuchagua kuwa wavivu kupitia miili yetu, tutakuwa wadhaifu kimwili. Kama tutaendelea kuchagua kwa wavivu katika mawazo yetu, uwezo wetu wa kujifunza, kufikiri na kuwaza utapungua.

Kama tutakataa kufanya kazi wakati tukiwa na uwezo, Mungu anasema tunastahili tukae bila ya chakula (Soma 2 Wathesalonike 3:6-12).

Ikiwa tutafanya kazi kwa bidii, mara nyingi Mungu atatupa thawabu ya kuongezeka kwa fursa na wajibu mkubwa.

Mungu ameweka matokeo ya ujumla kawa ajili ya chaguzi zetu. Hatuwezi kuchagua matokeo yetu, lakini tunaweza kuchagua ni kitu gani tutafanya!

**Mithali 14:23, Mithali 20:6.** Watu wengine wanajiona kwamba wana akili sana, lakini wanakataa kufanya kazi. Wanapenda kuota ndoto na kuzungumzia jinsi ambavyo mambo yanaweza kuwa, lakini wao wenyewe hawanyi jambo lolote. Kwa hakika, Mungu anatutaka tufanye kazi, na siyo kuzungumzia tu kuhusu jambo hilo. Anatutaka tuwajibike na kuwa waaminifu katika mambo tuliyosema kwamba tutafanya.

**Mithali 15:19.** Wakati mwingine watu huwa wavivu kuhusu jinsi wanavyofanya jambo fulani. Wanapenda kuchagua njia iliyo rahisi, hata kama haitakuwa na matokeo mazuri. Labda watafanya kitu ambacho hakina gharama, lakini kile wanachofanya hakitadumu baada ya muda fulani. Labda njia yao inahitaji juhudi kidogo sana, lakini umaliziaji wa pale mwishoni utakuwa wa thamani kidogo sana. Inawezekana wanakubali shinikizo kutoka kwa watu wengine badala ya kuwa tayari wao wenyewe kufanya kazi kupitia changamoto na kufanya kitu kilicho sahihi.

► Ni mifano gani unaweza kufikiria ambapo watu ni wavivu katika mbinu zao za kufanya jambo fulani?

Mithali hii inatufundisha kwamba tutakapokuwa wavivu katika kufanya yale tunayopaswa kuyafanya, itatuletea matatizo kwetu sisi na kwa watu wengine baadaye. Lakini tutakapofanya jambo ambalo ni sahihi, tutapata thawabu ya matokeo mazuri. Tunapaswa tuwe waangalifu na tulio wazi sasa, ili tuweze kufurahia matokeo mazuri baadaye.

► Je, ni mifano gani unaweza kufikiria ambayo uvivu umesababisha matatizo na migogoro mikubwa ya baadaye? Je, ni mifano gani unaweza kufikiria ambayo wakati kulipokosekana uaminifu na bidii kulisababisha kutokuwepo na matokeo mazuri?

**Mithali 12:11, Mithali 21:20, Mithali 28:19.** Kwenu ninyi vijana, Mungu hakukupa nguvu na afya uliyo nayo ili uweze kuzipoteza bure kwa kufuatilia mambo yasiyofaa. Amekuamini uwe msimamizi mzuri wa uwezo wako wa kimwili na kiakili. Amekupa fursa ya kumtumikia yeye. Kuwa mtumishi mzuri kunakuhitaji wewe uweze kujidhibiti mwenyewe. hautaweza kutimiza mambo yote kwa ajili ya furaha. Utalazimika uelekeze nguvu zako, rasilimali, na muda wako kwa ajili ya kutimiza makusudi ya Mungu.

Mungu anakutarajia utoe mahitaji yako mwenyewe, mahitaji ya familia yako (1 Timotheo 5:8), na kwa ajili ya mahitaji ya wale wote ambao wanahitaji msaada na hawana mtu mwingine wa kutoa kwa ajili yao (1 Timotheo 5:3-16, Waefeso 4:28, Yakobo 1:27, Yakobo 2:15-16).

1 Wathesalonike 4:11-12 inasema,

...Tena mjitahidi kutulia, na kutenda shughuli zenu, na kufanya kazi kwa mikono yenu wenyewe, kama tulivyowaagiza; ili mwenende kwa adabu mbele yao walio nje, wala msiwe na haja ya kitu chochote.

Haya ni mapenzi ya Mungu kwa ajili ya watu wote ambao wameokoka/wameamini.

► Je, aina gani za kazi ambazo watu waliookoka/walioamini wanapaswa kuwa tayari kuzifanya? Je, kuwa na hadhi kuna umuhimu? Kama ni ndivyo, ni kwa njia gani au kwa kiwango gani?

Tutajenga juu ya mada ya kazi kwa kujadili fedha. Tumetoka tu kuzungumzia sababu muhimu sana ambazo Mungu anatutaka sisi tufanye kazi, ikiwa ni pamoja na kutupa sisi mahitaji yetu na mahitaji ya watu wengine. Kazi ni njia ya kawaida ya Mungu kwetu ya kutupa mahitaji yetu muhimu – chakula na mavazi (1 Timotheo 6:8). Katika maeneo mengi, watu hupata fedha kwa kufanya kazi, na kisha kuzitumia katika kupata mahitaji ya kimwili. Katika maeneo mengine, watu wanalipwa kwa kupewa chakula, mali, au kupatiwa huduma nyingine badala ya fedha. Kwa njia yeyote ile, Mungu anatoa kwa ajili ya mahitaji ya watu kupitia kazi zao.

### **Kuhusu Fedha**

Vifungu vingi vya Maandiko vinazungumzia mada ya fedha. Jinsi tunavyofikiri na kushughulika na fedha huathiri sana uhusiano wetu na Mungu na watu wengine. Kwa kuwa ni jambo muhimu sana, Mungu anatutaka sisi tuwe na ufahamu sahihi kuhusu fedha na matumizi yake.<sup>48</sup>

### **Kanuni kutoka katika kitabu cha Mithali**

► Wanafunzi wanapaswa wasome kila kifungu cha andiko kwenye Mithali kwa ajili ya kikundi.

Je, ni nini chanzo cha usalama wetu?

1. Mungu ndiye mtoaji wa mwisho kwa wenye haki (Mithal 10:3).
2. Hatupaswi kupenda na kutumaini utajiri, kwa sababu una mipaka katika uwezo wake na ni wa muda kwa kipindi fulani (Mithali 11:4, 28).

► Je, ni mawazo gani, mitazamo, na matendo gani yanayoonyesha kumtumaini Mungu kuwa mpaji na usalama wa mtu?

Kuna mambo mengi yaliyo muhimu zaidi kuliko utajiri; kwa mfano:

1. Kuwa na mahusiano mazuri na watu wengine (Mithali 15:17).

---

<sup>48</sup> Kupata zaidi kuhusu somo hili, ona somo la 9 katika kitabu *Kuishi Maisha ya Kikristo kwa Vitendo*, kinachopatikana kutoka Shepherds Global Classroom.

2. Kuwa na maarifa na hekima (Mithali 8:10-11).
3. Kuwa na hofu ya Mungu na kuwa katika uhusiano sahihi na yeye (Mithali 15:16).
4. Kuwa na heshima kwa sababu ya kuwa na tabia njema (Mithali 11:16).
5. Kuwa mwaminifu, mpole na mwenye upendo (Mithali 19:22).

► Je, ni kitu kipi katika haya ambacho kina changamoto zaidi kwako kwa ajili ya mazingira yaliyopo?

Kanuni za kusimamia fedha kwa usahihi:

1. Kupata fedha kupitia kazi ya bidii na uaminifu (Mithali 10:4).
2. Kusanya pesa kwa uvumilivu na kwa muda (Mithali 13:11).
3. Mheshimu Mungu kwa kumpa fungu la kumi la mapato yako ya kwanza. (Mithali 3:9-10).
4. Kuwa mkarimu kwa maskini (Mithali 11:24-25, Mithali 14:21, Mithali 19:17, Mithali 21:13).

► Je, ni kitu kipi katika haya ambacho kinakufanya uhangaika zaidi?

Maonyo dhidi ya kuwa na matumizi mabaya ya fedha:

1. Kamwe usiliasi Neno la Mungu kwa ajili ya fursa ya kupata fedha (Mithali 10:2, Mithali 15:27).
2. Usifanye maamuzi ya haraka au ya kizembe (Mithali 21:5).
3. Usiahidi kulipa madeni ya watu wengine (Mithali 6:1-5; Mithali 17:18).

► Je, ni kanuni ipi kati ya hizi za Mithali ambayo imepuuzwa sana katika utamaduni wako?

### **Marafiki wa Karibu**

► Wanafunzi wanapaswa wasome Mithali 13:20 na 1 Wakorintho 15:33 kwa ajili ya kikundi.

Urafiki wa karibu ni mojawapo ya ushawishi mkubwa zaidi katika maisha ya kijana mkomavu. Kwa kawaida watu hufanyika kuwa marafiki wa karibu na wale wanaoshirikishana maadili yao. Lakini urafiki humbadilisha kila mtu aliyeko kwenye urafiki, kwa mazuri au mabaya. Kuendelea kuwa marafiki wa karibu na mtu baada ya muda kutakushawishi. Mtazamo wako, falsafa zako, vipaumbele vyako, tabia yako, chaguzi zako na mwenendo wako vitaathirika. Marafiki wako wa karibu watakushawishi kwa mifano yao ya maisha, kwa wao kuidhinisha au kutoidhinisha chaguzi zako na kwa maneno yao ya kuvutia na au kushawishi.

► Kila mwanafunzi anapaswa kuandika majina 1-5 ya watu mahususi katika kujibu kila moja ya maswali haya:

- Je, kwa kawaida ni nani namtegemea ili kupata kibali na uthibitisho?

- Je, huwa ninazungumza na nani kuhusu matatizo yangu ya maisha?
- Je, ninatafuta ushauri wa nani ninapokuwa nataka kufanya uamuzi?
- Je, ni tabia ya nani inayoleta ushawishi kwenye tabia yangu?
- Je, ninashirikishana na nani falsafa zangu?

Fikiria juu ya watu ambao umeandika majina yao. Tabia zao zikoje? Mazungumzo yao yakoje? Kama utafuata mfano wao, je utakuwa unamfuata Kristo? (1 Wakorintho 11:1).

Je, ni watu walio na sifa hizi?

- Wenye kuwa na hofu ya Mungu (Kumbukumbu la Torati 10:12, 20, Zaburi 112:1).
- Wanaimarishwa na Neno la Mungu (Yohana 17:14-17).
- Wanafanya kipaumbele cha kwanza ni kumpendeza na kumtii Bwana katika kila kitu (2 Wakorintho 5:9-10).

Je, wanakushawishi wewe kutembea na Mungu kwa ukaribu na utiifu? Je, wanakuambia yaliyo kweli (yale yanayopatana na Neno la Mungu), au je, wanakuambia lililo rahisi kusikia? Je, wanakutia moyo kufanya jambo ambalo ni sahihi mbele za Mungu hata inapokuwa ni katika hali ya matatizo?

Wakati fulani kulikuwa na kijana ambaye alikuwa na ushawishi sana. Vijana wengine walimtegemea sana kwa ajili ya kupata kibali cha tabia zao. Walipotaka kuongea kitu ambacho ni cha kejeli au chenye maneno machafu, walikuwa wanamtazama ili kuona kama alikuwa anacheka. Walipofanya jambo la uasi walimwangalia kama atapepesa jicho lake, kuonyesha kukubaliana nao. Walikuwa wanataka wamfurahishe. Lakini hakuna hata mmoja wao aliyeacha kufikiria na au kujiuliza maswali haya: Je, kwa nini ninahitaji kibali **chake**? Je, yeye ni mtu ambaye ninapaswa niwe najaribu kumfurahisha? Je, tabia na mwenendo wake ni kielelezo kizuri kwa ajili yangu?

Inahitaji juhudi kufikiria kuhusu masuala haya. Waumini wanapaswa wawe na kusudi ambalo litawafanya watake kuchagua marafiki wa karibu na wenye ushawishi mkubwa. Bila shaka, Mungu anataka watu wake wawe wanawashawishi watu wengine ambao hawajakomaa kiroho au ambao bado hawajaokoka, lakini watu hao hawana sifa ya kuwa marafiki wetu wa karibu, washauri, au watu wa kutushawishi. Hatupaswi tuwe tunatafuta kibali kutoka kwao.

► Mwanafunzi anapaswa asome Zaburi 101 kwa ajili ya kikundi.

Zaburi hii iliandikwa na mfalme Daudi. Alikuwa na hofu ya Mungu. Alijikabidhi kabisa kwa Bwana kwamba angeishi maisha ya uadilifu. Alijua kwamba watu aliowaruhusu wawe kishawishi kwake aidha watamsaidia kukamilisha ahadi yake au wangemzuia asiifanye. Kwa sababu hiyo, alidhamiria kuchagua watu wachache tu walio waaminifu na wenye kumcha Mungu wawe washawishi wake.

Sisi siyo mfalme kama Daudi alivyokuwa na kwa kawaida hatuna mamlaka au wajibu wa kuwaadhibu watenda maovu kama Daudi alivyokuwa ameahidi kufanya. Hata hivyo,

tunapaswa kufuata mfano wa Daudi kwa namna nyingine. Ni lazima tujitolee kabisa kuishi maisha ya uadilifu. Ni lazima tuamue kwamba tutachagua watu wacha Mungu tu kama marafiki wetu wa karibu na washawishi wakubwa zaidi.

## Kufanya Maamuzi

Utu uzima wa mapema ni wakati ambao unafaa kwa kufanya maamuzi mengi, ambayo baadhi yao yatakuwa na matokeo ya maisha yote (yumkini hata ***milele***).<sup>49</sup> Yafuatayo ni baadhi ya maswali machache ambayo tunapaswa tuyazingatie katika akili zetu wakati tunapofanya chaguzi zetu mbalimbali:

- **Je, kitendo hiki kinalingana na jinsi Mungu anavyotaka niwe?** Jamii inatuambia kwamba, "Kuwa wewe mwenyewe." "Kuwa mkweli wewe mwenyewe." "Fuata moyo wako mwenyewe." Lakini tumeitwa kuwa waaminifu kwa Kristo, siyo kwa ajili yetu wenyewe. Kwa hakika, anatuambia sisi tuseme, "Hapana" kwa matamanio yetu wenyewe yanapokuwa yanapingana na utii wetu kwake (Mathayo 16:24-26). Mungu anaituambia tuishi katika kiwango chake cha haki. Anaelezea kuhusu watu ambao watabarikiwa, wenye hofu na utii kwenye kila jambo (Zaburi 15, Zaburi 112, Mathayo 5:3-11). Jinsi tutakapokuwa tunamfuata kwa uaminifu, ndivyo tutakavyokuwa tunafanyika kuwa watu wa Mungu kama anavyotutaka tuwe.
- **Je, kitendo hiki kitaathirije sifa yangu?** Kwa kila uchaguzi tunaoufanya, tunajijengea sifa yetu wenyewe. (Mithali 20:11). Ni kweli kwamba tunapaswa tujali zaidi kuhusu kile ambacho Mungu anatuwazia sisi. Lakini tutakapokuwa tumefahamika kama ni watu wenye uadilifu, tunawashawishi watu wengine kwa mambo yaliyo sahihi na kuwa mashahidi waaminifu kwa ajili ya Kristo. Mithali 22:1 inatuambia kwamba tunapaswa kutanguliza kuwa na jina jema kuliko mali nyingi.
- **Je, ni matokeo gani yatafuata uchaguzi huu?** Andiko la Mithali 22:3 linatuonyesha kwamba tunapaswa tujiandae kwa ajili ya baadaye kwa kufanya maamuzi mazuri leo. Tunapokuwa tunatafakari kuhusu chaguzi zetu, ni lazima tuzingatie yanayoweze kutokea kwa kila moja. Je, ni kwa jinsi gani chaguzi zetu zinaweza kuathiri maisha yetu wenyewe na maisha ya watu wengine?

Andiko la Mithali 4:23 linatuambia kwamba chaguzi na tabia zetu zinatokana na misukumo iliyoko ndani ya mioyo yetu. Kama tunataka tufanye chaguzi zilizo nzuri na zinazompendeza Mungu, ni lazima tuhakikishe kwamba tunakuwa waaminifu kwake (Kumbukumbu la Torati 6:2, 5-6, Kumbukumbu la Torati 13:4).

---

<sup>49</sup> Kupata zaidi kuhusu somo hili, ona somo la 5 katika kitabu cha *Kuishi Maisha ya Kikristo kwa Vitendo* kinachopatikana kutoka Shepherds Global Classroom..

## Afya ya Kimwili

Vijana wakomavu wanawajibika kwa ajili ya chaguzi binafsi, ikiwa ni pamoja na zile zinazohusiana na vile wanavyokula, shughuli zao za kimwili na ratiba za mazoezi yao ya mwili, na tabia zao za kulala. Kujidhibiti binafsi ni muhimu sana kwenye haya maeneo yote (1 Wakorintho 9:27). Watu waliookoka/waumini wanapaswa kutambua kwamba miili yao ni hekalu la Roho Mtakatifu na kwamba Tumekombolewa kwa damu ya Yesu (1 Wakorintho 6:19-20). Kwa kuwa pia sisi ni watumishi wa Mungu, tunapaswa tuitunze miili yetu na kujitia katika nidhamu ya kufanya chaguzi zilizo nzuri katika kila moja ya shughuli hizi, ili tuwe katika ubora wetu kwa ajili yake.<sup>50</sup>

► Wanafunzi wanapaswa wasome 1 Wakorintho 6:12-13, 19-20, na 1 Wakorintho 10:31 kwa ajili ya kikundi.

Fikiria kuhusu uchaguzi wako wa chakula na kiasi cha chakula kwa wiki zima iliyopita. Inawezekana ulikuwa na chakula kingi cha kutosha na chaguzi nyingi kuhusu kile ambacho ulikuwa unataka kula. Labda ulikuwa na chakula kidogo, ukiwa na uchaguzi mdogo wa vyakula utakavyokula. Kwa namna yeyote ile, kula na kunywa kwako kunapaswa kumpe Mungu utukufu. Kama kungekuwa na uwezekano wa Yesu kukaribishwa aje anywe na kula pamoja na wewe, je, ungechagua vyakula vilevile na kiasi kilekile unachochagua katika hali ya kawaida?

Swali hili linawezekana kuonekana kama ni lisilokuwa na maana, lakini labda linaweza kutumika kama ukumbusho wa kufikiria, kumshukuru, na kujidhibiti wakati wa kula chakula.

Usingizi ni eneo lingine ambalo waumini wanapaswa kudhihirisha jinsi ya kujidhibiti. Hatupaswi kuwa wavivu na kulala sana (Mithali 6:10-11, Mithali 20:13), wakati bado Mungu ameumba miili yetu katika uhitaji wa mapumziko ya mara kwa mara na yanayotosheleza (Zaburi 3:5). Watu wazima wenye afya njema wanahitaji masaa 6-8 ya kulala kwa kila usiku mmoja.

Katika Mhubiri 5:12 tunaelezwa kwamba usingizi ni zawadi kwa wale wanaofanya kazi kwa bidii. Mithali 3:24 na Zaburi 4:8 inazungumza juu ya usingizi mtamu, wa amani ambao Mungu huwapa watoto wake. Huu ni aina ya usingizi ambao unarejesha miili yetu. Kukiwepo na amani ya Mungu, tunawekwa huru kutokana na mashaka na mahangaiko ya siku, tukijua kwamba Mungu aliye mwaminifu anatuangalia sisi. Usingizi wenye utulivu huleta nguvu na akili kwa ajili ya miili yetu, na kututayarisha kwa ajili ya majukumu na huduma nyingine zinazofuata.

Mithali 3:24 inapatikana ndani ya sehemu ya kitabu cha Mithali inayojumuisha maagizo ya kuishi maisha yaliyojaa hekima, ufahamu, na busara za kuamua. Kama utataka kuwa na

---

<sup>50</sup> Kupata zaidi kuhusu somo hili, ona somo la 13 katika kitabu cha *Kuishi Maisha ya Kikristo kwa Vitendo* kinachopatikana kutoka Shepherds Global Classroom..

usingizi mtamu, unapaswa ufanye maamuzi ya busara kwenye maeneo mengine ya maisha yako, ikiwa ni pamoja na muda wako unaoutumia wa kuangalia runinga, au picha za video, kuperuzi mitandao ya intaneti, au matumizi ya simu, na kutumia muda mwingi pamoja na marafiki.

Usingizi unaweza kuharibiwa na chaguzi zako za vyakula na kiasi cha upatikanaji wake kwa siku, kiasi cha mazoezi ambayo umekuwa nayo, jinsi ulivyokabiliana au navyoshughulika na mambo magumu, na jinsi ambavyo unatumia fedha zako. Usingizi unaweza kuwa mtamu wakati mahusiano yetu na watu wengine yanapokuwa yamejazwa na tabia ya tunda la Roho yaliyoorodheshwa katika Wagalatia 5:22-23.

► Chukua muda kusoma Maandiko yaliyorejewa katika sehemu hii hapo juu.

Fanya tathmini kuhusu usingizi wako wa mujibu wa kanuni zinazopatikana katika maandiko haya. Je, unaupa mwili wako mapumziko yanayohitajika ili uweze kufanya kazi vizuri kama Mungu alivyokusudia?

Jaribu kuchunguza muktadha wa Aya zinazotoka katika kitabu cha Zaburi: Daudi anaziandika katika hali zenye mfadhaiko sana na bado anashuhudia uaminifu wa Mungu katika kumsaidia kurejesha hali ya mwili wake kupitia usingizi.

### **Kushughulika na Mfadhaiko**

Kwa utaratibu wa Mungu, miaka ya mwanzo ya mtu mzima imejaa majukumu na mambo mengi ya kuhudumia ambayo yanahitaji umakini mkubwa na yanayosababisha mfadhaiko (Maombolezo 3:27). Mtu anaweza akawa anajaribu kumaliza elimu yake ya shahada, aanzishe biashara, na kuwa anafanya kazi au kazi nyingine kadhaa. Kuna mahusiano mengi mchanganyiko ambayo yanahitaji umakini wa mwelekeo wa kimakusudi kutoka kwa kijana. Mambo ya fedha, mahitaji ya usafiri, na kuwa na nyumba yote haya yanahitaji umakini wa mtu, lakini yanaleta mfadhaiko mkubwa.

Mfadhaiko umefafanuliwa kama ni “mwitikio wa kimwili na mhemuko kutokana na matukio ambayo yanatutisha au kutupa changamoto.”<sup>51</sup> Jaribu kufikiria jinsi unavyoziangalia hali unazopitia. Je, akili yako inafanyaje kazi katika hali unayopitia sasa?

Kunapokuwa na Jambo mbele yako, ni kwa jinsi gani unakuwa ukilifikiria? Unaruhusu ujisikie mihemuko ya aina gani kuhusu uwezekano? Je, ni mtazamo gani unaoathiri jinsi ya kukabiliana na hali hiyo? Kwa ujumla silika na hulka yako ni nini? (Mithali 15:15)?

Mtazamo, silika, na hulka yako vyote vina vinagusa jinsi unavyokabiliana na hali za maisha unazopitia na kiwango cha mfadhaiko utakachokuwa nacho. Wakati mfadhaiko ni sehemu ya kawaida ya maisha, namna ya kukabiliana na mfadhaiko huo ni jambo binafsi. Wakati mwingine wasiwasi husababisha maumivu ya kichwa, maumivu ya misuli, magonjwa, shinikizo la damu, vidonda vya tumbo, na matatizo mengine mbalimbali ya kiakili,

---

<sup>51</sup> Robert S. Feldman, *Discovering the Lifespan*, 2nd ed. (Upper Saddle River, NJ: Pearson, 2012), 317.



kimhemuko, na kimwili (Mithali 12:25). Upokeaji mbaya wa mfadhaiko unaweza kuzuia sana huduma yako kwa ajili ya Kristo. Kwa sababu hiyo, siyo jambo la kushangaza kwamba Neno la Mungu linatuambia kwamba hatupaswi kuwa na wasiwasi au kuwa watu wenye dukuduku.

► Wanafunzi wanapaswa wasome Mathayo 6:34, 1 Petro 5:7, na Zaburi 105:4 kwa ajili ya kikundi.

Tunapokabiliwa na hali nzito zenye kutuelemea, ni lazima tuchague kumtumaini na kumtegemea Mungu, yeye peke yake asiyekuwa na mipaka. Yeye ni mkamilifu katika nguvu, hekima, na wema. Anawajali watoto wake kikamilifu. Anatutaka tutambue utegemezi wetu kwake, tumpelekee haja zetu zote, na tutafute nguvu zake kutoka kwake. Tutakapokuwa tunafanya hivyo, anaweza kutupa amani, pumziko, na mambo yote tunayohitaji kutoka kwake. Tukiwa katika ujana wetu, ni lazima tujifunze kuwa watulivu na wakimya mbele za Mungu na tumngojee yeye kwa ajili ya kutuongoza (Zaburi 46:10, Maombolezo 3:25-27).

► Orodhesha hali za mfadhaiko unazokabiliana nazo kwa sasa. Je, uwajibikaji wako unapaswa uweje kwa mujibu wa Neno la Mungu?

#### **Kwa ajili ya Majadiliano ya Kikundi**

► Katika somo hili, je, ni mawazo au kanuni gani ambazo zimekuwa mpya kwako? Je, ni kanuni gani nyingine za kibiblia ambazo umezifikiria kwamba zinahusiana na maeneo haya ya maisha ya kijana mkomavu?

► Je, maisha yako binafsi yataguswaje na kile ambacho umejifunza katika somo hili?

► Katika kanisa lako, ni mada zipi katika hizi zinazohitajika kushughulikwa zaidi miongoni mwa waumini vijana wkomavu?

► Unawezaje kuwashawishi vijana wa Kikristo ambao unawajua waweze kufikiri na kuishi kibiblia katika haya maeneo ya maisha?

## **Maombi**

Baba wa Mbinguni,

Asante kwa ajili ya Neno lako ambalo linatufundisha jinsi ya kuishi kwa ajili yako katika kila hatua ya maisha yetu. Asante kwa kutuandaa tuweze kuishi maisha yenye matunda na tija katika miaka yetu ya ujana mkomavu.

Tusaidie tukutukuze wewe kwa kuwa watumishi waaminifu wenye nguvu rasilimali, na fursa unazotupa. Tusaidie tuwe mvuto wa kimungu kwa wengine na kuchagua marafiki ambao ni washauri na wacha Mungu.

Tuwezeshe tufanye maamuzi ya busara na kukuheshimu wewe kwa miili yetu, akili zetu, na roho zetu.

Ameni

## **Kazi za Kufanya**

(1) Katika 1 Timotheo 4:12, Paulo alimwagiza Timotheo kwamba alipaswa awe mfano kwenye maeneo mahususi. Kwa kuandika, Fafanua kila moja ya maeneo haya. Kisha elezea jinsi kila kimoja katika haya kinavyowezezekana kwa kijana mkomavu kuishi. Toa angalau mfano mmoja wa vitendo kwa kila kipengele kimoja.

(2) Chagua mojawapo ya mada zilizopo katika somo hili:

- Ukomavu na tabia
- Tabia
- Fedha
- Marafiki wa karibu
- Kufanya maamuzi
- Afya ya mwili
- Mfadhaiko

Andika angalau aya zisizopungua tatu kuhusiana na mada uliyochagua:

- Tengeneza muhtasari wa kanuni zote za kibiblia zinazohusiana na mada hiyo.
- Elezea baadhi ya matukio chanya yanayotokana na kuwa mtiifu kwa hizo kanuni.
- Elezea baadhi ya matukio hasi yanayojitokeza wakati kanuni hizi zinapokuwa zimepuuzwa.

Utakapokuwa unaandika kuhusu haya matokeo chanya na hasi, hakikisha kwamba unafikiria kuhusu athari za chaguzi binafsi za mtu kwa ajili ya watu tofauti: mtu huyo mwenyewe, familia yao, jumuiya yao, na kanisa lao.

# Kiambatanisho “A”

## Heshima kwa Wanawake

### Mfano wa Yesu Kuhusiana na Heshima kwa Wanawake

Wanawake walichukuliwa kuwa ni watu duni sana kwenye karne ya kwanza ya ulimwengu wa Kirumi na katika Uyahudi. Mtazamo finyu wa wanawake bado umeenea katika tamaduni nyingi duniani kote, na nyumbani kwa watu wengi. Wanawake hawaheshimiwi, wanatumiwa kama vyombo vya kujamiiana na wananyanyaswa. Lakini heshima kubwa ya Yesu aliyokuwa nayo kwa wanawake inapaswa iwe mfano wetu.

Kwa Kristo, wana heshima kubwa na thamani ya asili sawa na ile ya mwanaume. Yesu alisema, “yeye aliyewaumba mwanzo, aliwaumba mtu mume na mtu mke” (Mathayo 19:4, Mwanzo 1:27). Mwanamke ameumbwa kwa sura ya Mungu kama vile nao wanaume walivyo. Kama vile wanaume, wana kujitambua binafsi, wana uhuru wa kibinafsi, wana majukumu binafsi kwa matendo yao. Wanawake wanaonekana na Yesu kama watu halisi, sio kama vyombo vya tamaa ya wanaume tu. Aliwaona kama watu ambao alikuja kwa ajili yao ulimwenguni (Luka 8:1-3).

Yakobo Borland, Yohana Piper na Wayne Grudem, wanatoa mifano hii iliyo wazi kabisa ya mtazamo wa hali ya juu wa Yesu na heshima yake kwa ajili ya wanawake kama inavyopatikana kutoka katika vitabu vyote vinne vya Injili:

#### **(1) Yesu alizungumza moja kwa moja na wanawake alipokuwa katika hadhara.**

Hili lilikuwa ni jambo lisilokuwa la kawaida kwa nyakati zile za Yesu duniani. (Yohana 4:27). Wanafunzi walishangaa walipomwona Yesu akizungumza na yule mwanamke Msamaria pale kwenye kisima cha Sikari. (Yohana 4:7-26). Yesu alizungumza kwa uhuru na mwanamke aliyekamatwa kwenye uzinzi. (Yohana 8:10-11). Luka anabainisha kwamba Yesu alikuwa anaongea hadharani na mjane wa mji mmoja mdogo uitwao Naini (Luka 7:12-13), Yesu anaongea na mwanamke mmoja, ambaye ametokwa na damu muda wa miaka kumi na miwili, (Luka 8:48, Mathayo 9:22, Marko 5:34), Aliongea na mwanamke aliyemwita kutoka kwenye umati wa watu (Luka 11:27-28). Yesu alizungumza na mwanamke aliyekuwa amepindana, hawezi kujinyosha kabisa kwa miaka 18 (Luka 13:12). Yesu aliongea na kundi la wanawake akiwa njiani kuuendea msalaba (Luka 23:27-31).

#### **(2) Yesu alionyesha heshima yake na thamani kubwa kwa wanawake kwa jinsi alivyokuwa anazungumza nao.**

Yesu alizungumza nao katika hali kuzingatia na kuwajali. Mathayo, Marko na Luka waliandika kwamba Yesu alimwita yule mwanamke aliyekuwa akitokwa na damu kuwa ni “binti” na akarejea kumtaja yule mlemavu kuwa ni “binti wa Abrahamu” (Luka 13:16). Kwa

kuwaita “binti wa Abrahamu” Yesu anawaweka kwenye hadhi moja sawa ya kiroho na “wana wa Abrahamu.”

### **(3) Yesu anaonyesha thamani ya asili ya wanawake kwa kuwawajibisha kibinafsi kwa ajili ya dhambi zao.**

Hali hii inaweza kuonekana katika kushughulika kwake na yule mwanamke pale kisimani (Yohana 4:16-18), mwanamke mzinzi (Yohana 8:10-11), na mwanamke mwenye dhambi aliyempaka mafuta ya marhamu kwenye miguu yake (Luka 7:44-50). Dhambi zao hazikupuuzwa bali zilishughulikwa. Kitendo chake kilionyesha kwamba kila mwanamke alikuwa na uhuru binafsi, alikuwa na maamuzi yake mwenyewe, na kila mmoja kwa binafsi yake ni lazima ashughulikie masula ya dhambi, toba, na msamaha.

### **Jinsi thamani ya Yesu kwa wanamke itakavyoweza kuliongoza Kanisa Leo.**

Jukumu halisi la mwanamke katika huduma na nyumbani linajadiliwa katika makanisa na madhehebu mengi kwa sasa, jinsi litakavyokuwa, lakini bado thamani na usawa wa mwanamke kama watu kamili walioumbwa kwa sura ya Mungu **kamwe** halihitaji maswali. Yesu aliendelea kuonyesha thamani na hadhi ya mwanamke kama watu. Yesu aliwaagiza wanawake wawe watangazaji wa kwanza wa kufufuka kwake. (Yohana 20:17). Kutoka kwao alithamini ushirika wao, maombi, huduma ya Kikristo, msaada wa kifedha, ushuhuda na ushahidi. Yesu aliwaheshimu wanawake, aliwafundisha wanawake, na aliwahudumia wanawake kwa kuwafikiria.

### **Heshima ya Mwanamke inayoonyeshwa kwenye Agano Jipya.**

Mfano wa Yesu wa heshima kwa mwanamke unaonekana katika maisha ya Roho Mtakatifu. Siku ya Pentekoste, Roho Mtakatifu alimwagwa juu wana na mabinti na watumishi wa kiume na wa kike (Matendo 2:17-18). Roho Mtakatifu hakuonyesha upendeleo kwa yeyote.

Katika Warumi 16: Paulo anamsifia mwanamke aitwaye Fibi kama mtumishi wa Kanisa. (Aya ya 1), Priska na Akila kwa pamoja kama watumishi wenzake katika Kristo Yesu (Aya ya 3-4), Mariamu kama aliyekuwa akifanya kazi kwa juhudi sana (Aya ya 6), Junia kama mtu ajulikanaye sana na mitume (Aya ya 7), na wanawake wengine pia.

Katika 1 Wathesalonike Paulo anasifia upole na upendo wa kinamama walioumbiwa na Mungu wakati alipoandika, “bali tulikuwa wapole katikati yenu, kama vile mlezi awatunzavyo watoto wake mwenyewe” (1 Wathesalonike 2:7). Katika Waefeso anawaamuru wanaume kuwapenda wake zao “kama Kristo naye alivyolipenda Kanisa, akajitoa kwa ajili yake; na kama miili yao wenyewe (Waefeso 5:25, 28). Petro anawasihi wanaume, “kaeni na wake zenu kwa akili; na kumpa mke heshima (1 Petro 3:7).

Kwa uwazi kabisa, wanawake walionekana wenye thamani kwenye kanisa la mwanzo, na wanaume walifundishwa kuwa na heshima kwa wanawake. Ni wakati sasa kwa viongozi wa kiroho popote walipo kusimama kidete na kuwatetea wanawake na kusimama dhidi ya unyanyasaji wa aina yeyote katika kila tamaduni. Ni wakati wetu wa kuwathamini

wanawake kama watu walioumbwa na Mungu kwa njia ya kipekee katika sura yake. Mafundisho ya aina yeyote ya tofauti za majukumu kwa ajili ya wanaume na wanawake katika kanisa na majumbani ni lazima yaanze na msingi huu au kama sivyoy, mafundisho yetu yatakuwa ni njia ya kuelekeza kwenye unyanyasaji.

### **Kwa ajili ya Majadiliano ya Kikundi**

- Elezea tofauti kati ya wanaume na wanawake ambazo zinafuata utamaduni wao. Je, ni kwa jinsi gani tofauti hizo zinaweza kufanyiwa maboresho kwa kutumia kwa uangalifu matumizi ya ukweli ulioko kwenye Biblia?
- Je, makanisa kwenye nchi yako yanawachukuliaje wanawake tofauti na wanaume? Je, kuna tofauti gani zilizopo kati ya makanisa na tamaduni?
- Kwa kuzingatia msingi wa Yesu, je, ni desturi gani zinapaswa kubadilika?



# Kiambatanisho “B”

## Kudhibiti Uzazi

### Njia za Kuzuia Mimba

Sayansi ya matibabu imebuni njia za kuzuia mimba kwa watu wanaotaka kufanya tendo la ngono lakini hawataki kupata watoto. Neno linalotumika kwenye njia za kuzuia mimba ni “uzazi wa mpango.” Kuna njia kadhaa za kufanya uzazi wa mpango:

1. Kutumia vidonge vinavyozuia kabisa mwili wa mwanamke kutoa yai kwa ajili ya kuweza kurutubishwa.
2. Kutumia vidonge vinavyosababisha yai lisiwe na uhai baada ya kupokea mbegu za kurutubisha.
3. Kutumia vifaa vya kukaa mwilini ambavyo vinazuia mbegu za kiume (manii) kuingia kwa mwanamke.

Kuna kipindi cha siku chache kila mwezi mwanamke anarutubisha. Wenzi wanaweza wakajifunza ratiba ya mwili wa mwanamke ili waweze kujizuia kujamiiana wakati ambapo mwanamke anaweza akapata mimba. Njia hii ya nne haijulikani kama ni uzazi wa mpango.

### Sababu za Watu kutumia Uzazi wa Mpango

Baadhi ya mashirika yanapendekeza matumizi ya kondomu ili kupunguza kuenea kwa magonjwa na kuzuia mimba miongoni mwa watu ambao hawajizuii kufanya ngono na wenzi wa ndoa pekee. Matumizi ya uzazi wa mpango nje ya ndoa hayatajadiliwa hapa. Biblia inakataza kujamiiana nje ya ndoa. Wakristo wote wa Kiinjili wanaamini kwamba njia sahihi ya kuepuka magonjwa na kuzuia mimba nje ya ndoa ni kutojamiiana kabisa hadi wakati wa kuingia kwenye ndoa.

Kuna sababu kadhaa ambazo baadhi ya wanandoa huzitumia kwa ajili ya uzazi wa mpango:

- Wataalamu bingwa wa tiba katika maeneo mbalimbali wanahimiza matumizi ya vifaa vya kuzuia mimba kwa ajili ya uzazi wa mpango kwa familia maskini ambazo zinahangaika kuwahudumia watoto wengi, ili waweze kuzaliwa watoto wachache.
- Wakati mwingine wanandoa wanahitaji kusubiri kwa muda baada ya kuoana kabla ya kupata watoto kwa sababu aidha ya kuweka akiba ya fedha au kuboresha aina yao ya kuishi kwa njia nyingine.
- Wanandoa wanaweza wakatumia vifaa vya kuzuia mimba kwa ajili ya uzazi wa mpango kwa madhumuni ya kurefusha muda wa kuzaliwa kati ya watoto wanaotarajiwa kuzaliwa.

- Wakati mwingine wanandoa wanatumia uzazi wa mpango kwa sababu wanajiona tayari wanayo idadi ya watoto ambao waliwahitaji na kwamba hawataki kuongeza wengine tena.
- Wakati mwingine, mwanamke hujikuta ana matatizo ya afya, na daktari anamshauri atumie uzazi wa mpango kwa sababu kwa wakati huo mimba inaweza ikawa ni hatari kwake na kwa mtoto wake.

### **Midahalo kati ya Mekanisa kuhusiana na Uzazi wa Mpango**

Biblia haizungumzii mahususi kuhusu aidha ni sahihi au siyo sahihi kujaribu kuzuia mimba. Kanisa Katoliki linalaani matumizi ya uzazi wa mpango lakini linaruhusu njia za kupanga ratiba za jinsi ya kuepuka kubeba mimba. Baadhi ya viongozi wa Kanisa la Othodoksi la Mashariki linapanga kuzuia mimba, lakini siyo wote. Miongoni mwa mekanisa ya Kiprotestanti na ya Kiinjili, kuna aina mbalimbali za mafundisho ya imani kuhusiana na suala hili.

Dondoo zifuatazo zinatumiwa na baadhi ya mekanisa kama sababu za kupinga na kukataza matumizi ya uzazi wa mpango. Baada ya kila mada ya majadiliano kuna nyongeza ya mtazamo.

(1) Watoto ni baraka kutoka kwa Mungu na ndilo kusudio la ndoa.

Somo kuhusu kukosa watoto linaelezea baraka za Mungu kwa watoto. Baadhi ya mekanisa wanaamini kwamba thamani ya Mungu kwa watoto ndiyo sababu ya kukataza na kupinga uzazi wa mpango. Waumini wengine wanasema kwamba kama watakuwa na watoto, siyo jambo baya kuzuia mimba za ziada, hasa kama kuna tatizo la ugonjwa au changamoto za kiuchumi.

(2) Uzazi wa mpango hutumiwa kulinda matendo machafu ya kujamiiana na madhara yake.

Ukweli kwamba zinaweza kutumiwa kwa ajili ya makusudi yasiyo na uadilifu, hauna uhusiano wowote na suala la matumizi yake na wanandoa.

(3) Uzazi wa mpango hulifanya tendo la ndoa kuwa la kibinafsi zaidi na lisilokuwa safi kwa kuondoa uhalali wa kusudi la kujamiiana, ambao ni kupata mimba na kuzaa watoto.

Wakati ni kweli kwamba tendo la ngono linaweza likawa la ubinafsi au lisilokuwa safi, ni sehemu ya mahusiano ya ndoa, na linaweza lisiwe kwa ajili ya kupata watoto (1 Wakorintho 7:3-5). Biblia inatuambia kwamba waume kwa wake watahudumiana wenyewe katika njia hii.

(4) Uzazi wa mpango hufanya mimba iwe ni uchaguzi wa wanadamu na siyo uchaguzi wa Mungu.

Baadhi ya mekanisa yanaamini kwamba wanandoa wanapaswa wamwamini Mungu katika kuwapa watoto wanaopaswa wawe nao, bila ya kujaribu kudhibiti muda au idadi ya watoto.



Baadhi ya Wakristo wengine husema kwamba sisi tuna wajibu wa kufanya maamuzi kuhusu vipengele vyote ya maisha yetu, na tunaweza kufanya maamuzi kuhusu kuzuia kupata mimba kama tutataka kufuata vipaumbele vya Kibiblia.

### **Jambo la Dhamiri**

Kwa kuwa: (1) Biblia haijatoa tamko rasmi kuhusu uzazi wa mpango, na (2) Kwa kuwa waumini wa Kiinjili wanayo maoni yao mbalimbali kuhusiana na suala hili, waumini wanapaswa waheshimu maamuzi ya waumini wengine. Wanandoa wanapaswa wahakikishe kwamba wamejitoa kabisa kwa Mungu na wanafuata vipaumbele vya kibiblia, kisha waombe kwa ajili ya kupata hekima kutoka kwa Mungu wanapokuwa wanataka kufanya uamuzi huu.

Wakati mimba inapotokea hakuna maamuzi mengine ya kujadiliana kuhusu aidha mtoto awepo au asiwepo. Maandiko yako dhahiri kwamba ni kosa kubwa kukatiza uhai wa mtoto ambaye yuko tumboni hajazaliwa bado. Kwa sababu uhai wa binadamu unaanzia pale mimba inapotunga, vidonge vinavyozuia yai lisirutubishwe na kuishi baada ya uhai kuanza ni makosa. Wanandoa wanaochagua kutumia uzazi wa mpango wanapaswa wahakikishe kwamba wanatumia kitu ambacho kitazuia mimba na sio kitu ambacho kitasababisha kifo cha yai lililorutubishwa.



# Vyanzo Vilivyopendekezwa

## Maandalizi kwa ajili ya Harusi

Drescher, John. *For Better, For Worse*. Morgantown, PA: Masthof Press, 2012.

Thomas, Gary. *Sacred Marriage*. Grand Rapids: Zondervan, 2000.

## Ndoa

Eggerichs, Emerson. *Love and Respect*. Nashville: Thomas Nelson, 2004.

Thomas, Gary. *Sacred Search*. Colorado Springs: Daudi C Cook, 2013.

## Ujinsia

Ferrer, Hillary. *Mama Bear Apologetics Guide to Sexuality: Empowering Your Kids to Understand and Live Out God's Design*. Eugene: Harvest House Publishers, 2021.

Sprinkle, Preston. *People to Be Loved: Why Homosexuality is not Just an Issue*. Grand Rapids: Zondervan, 2015.

Yuan, Christopher. *Holy Sexuality and the Gospel: Sex, Desire, and Relationships Shaped by God's Grand Story*. New York: Multnomah, 2018.

Shimer, Ted. *The Freedom Fight: The New Drug and the Truths That Set Us Free*. Houston: High Bridge Books, 2020.

## Kulea

Brown, Nadine M. *How to Have Kids with Character (Even if Your Kids are Characters)*. Wheaton: Tyndale House Publishers, Inc., 1990.

Chapman, Gary and Ross Campbell. *The Five Love Languages of Children*. Chicago: Northfield Publishing, 1997.

Dobson, James. *Bringing up Boys*. Wheaton: Tyndale House Publishers, Inc., 2001.

Friedeman, Matt. *Discipleship in the Home: Teaching Children*. Changing Lives. Wilmore: Francis Asbury Society, 2010.

Hubbard, Ginger. *Don't Make Me Count to Three!* Wapwallopen, PA: Shepherd Press, 2003.

Mulvihill, Josh. *Biblical Worldview: What It Is, Why It Matters, and How to Shape the Worldview of the Next Generation*. Roanoke: Renewanation, 2019.

Tripp, Tedd. *Shepherding a Child's Heart*. Wapwallopen: Shepherd Press, 1995.

**Familia**

Garland, David and Diana Garland. *Flawed Families of the Bible*. Grand Rapids, MI: Brazos Press, 2007.

Mally, Sarah and Stephen Mally and Grace Mally. *Making Brothers and Sisters Best Friends*. Marion, IA: Tomorrow's Forefathers Inc, 2002.

# Kumbukumbu ya kazi zilizofanywa

Jina la Mwanafunzi \_\_\_\_\_

Kwenye jedwali iliyopo hapa chini, onyesha ni lini kazi za kufanya ulizopewa zilipomalizilika. Kazi zote za kufanya zilizotolewa zinatakiwa zimalizike kwa ukamilifu ili kuweza kupata Cheti cha ufaulu kutoka Shepherds Global Classroom.

Somo	Kazi ya kufanya 1	Kazi ya kufanya 2	Kazi ya kufanya 3	Kazi ya kufanya 4
1				
2				
3				
4				
5				
6				
7				
8				
9				
10				
11				
12				
13				
14				
15				

Maombi kwa ajili ya kupewa Cheti cha Kufuzu kozi kutoka Shepherds Global Classroom yanaweza kukamilishwa kupitia ukurasa wetu wa wavuti [www.shepherdsglobal.org](http://www.shepherdsglobal.org). Vyeti vitatumwa kwa mfumo wa kidigitali kutoka kwa Raisi wa SGC kwenda kwa wakufunzi na wawezeshaji ambao watakamilisha maombi hayo kwa niaba ya mwanafunzi (au wanafunzi).